

1 NOVEMBA, 2023

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TATU**

**Kikao cha Pili – Tarehe 1 Novemba, 2023**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Maelezo ya Waziri wa Afya kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

**1 NOVEMBA, 2023**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

### **MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza maswali ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anatropia.

Na. 7

**Wanawake waliokuwa Wabunge na Madiwani  
katika chaguzi tatu mfululizo**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza: -

Je, Wanawake wangapi wamekuwa Wabunge wa Majimbo na Madiwani katika chaguzi tatu mfululizo zilizopita?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU  
(MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu Swalii la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia 2010 hadi 2020 zilifanyika chaguzi tatu katika ngazi ya Ubunge na Udiwani.

Katika chaguzi hizo, jumla ya Wabunge Wanawake 73 walishinda chaguzi hizo na kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Majimbo. Aidha, kwa upande wa Madiwani Jumla ya wanawake 654 waliweza kuchaguliwa na hivyo kuwa Madiwani katika Kata husika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kutokana na majibu aliyonipatia ni wastani wa wanawake 24 huwaguliwa kila baada ya Uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo, naona kwamba ongezeko ni dogo wanawake 24 kila baada ya miaka mitano ni wachache sana kuwakulisha licha ya Serikali kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa kuongeza ushiriki wa wanawake. Swali langu ni mkakati gani mahususi unaopaswa kuwa revised ili kuongeza idadi ya wanawake kwenye siasa? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Mkakati gani wa Serikali wa kubadilisha *Political Parties Act* ili kuweka kifungu kitakachovilazimisha vyama vya siasa kuwa na idadi maalumu ya wanawake watakaokuwa wagombea kwenye chaguzi mbalimbali kwenye hii nchi. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwanza nisema Serikali inatambua na kuthamini sana sana ushiriki wa wanawake katika shughuli za kisiasa na lakini na maeneo mengine. Niseme tu katika eneo hili mkakati uliopo ndani ya msajili wa vyama vya siasa ni kuendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wanawake kuendelea kujiamini na waweze kuijandaa kugombea nafasi hizo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, tutaleta Bungeni mabadiliko ya Sheria ya vyama vya siasa ili kuvitaka vyama sasa

**1 NOVEMBA, 2023**

kuwa na Sera ambayo itaweka mwongozo mahususi wa kujumuisha wanawake kwenye kugombea nafasi mbalimbali. Kwa hiyo, niwaondoe shaka wanawake wenzangu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anawajali anawathamini na tutaendelea kufanya vizuri kwenye eneo hili la kuhakikisha tunawajumuisha wanawake kwenye ngazi zote za maamuzi, ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Dkt. Ntara.

Na. 8

**Mkataba Na.189 Wafanyakazi wa Majumbani**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itathibitisha Mkataba Na. 189 wa Wafanyakazi wa Majumbani?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kuridhia Mkataba Na. 189 ulianza mwaka 2011 hadi 2016 ambapo ulifika hatua ya kuridhiwa kwa kuwasilishwa Bungeni. Hata hivyo, kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi na utekelezaji wa Mkataba tajwa, iliamuliwa kuwa wadau waendelee kupewa elimu kuhusu Mkataba huo kabla ya hatua za uridhiaji kuendelea. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi wa Majumbani CHODAWU imetoa elimu kuhusu Mkataba husika kuitia Makongamano na vikao 90 ambao

**1 NOVEMBA, 2023**

ni wafanyakazi wa majumbani, Viongozi wa vyama vyatatu na waajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeanza hatua ya uchambuzi wa Mkataba Na. 189 kwa kupitia Sheria na Kanuni zinazosimamia wafanyakazi wa majumbani. Baada ya hatua hizo na mapitio kukamilika, hatua inayofuata ni ya kushirikisha wadau kwa lengo la kupokea maoni yao kuhusu maeneo ambayo Serikali inapendekeza kuridhia katika mkataba husika. Aidha, Serikali itazingatia umuhimu wa vipengele vyatatu na waajiri ambavyo vitazingatia mila, desturi na uwezo wa nchi katika kutekeleza Mkataba husika, ahsante. (Makofisi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Waziri kwa ushirikiano katika eneo hilo nimekuwa nikisaidia sana. Lakini swali langu la kwanza swala la wadau kutoa maoni pamoja na elimu limefanyika kwa muda mrefu sana.

Je, Serikali kupitia comissionar wa kazi haioni iko haja sasa ya kuharakisha kuridhia mkataba huo angalau wawe parcial ili wafanyakazi hao wawe rasmi? (Makofisi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, baada ya Serikali kupitia VETA na CVM kuzindua mitaala ya wafanyakazi wa majumbani, je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza udahili wa wanafunzi hao kwa sababu sasa hivi hata wanafunzi kutoka Vyuo Vikuu na Vyuo vingine wanaajiriwa kufanya kazi majumbani. Ni mpango gani sasa Serikali inafanya ili wanafunzi wawe wengi katika hivyo Vyuo vyatatu na waajiri? Ahsante. (Makofisi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, AJIRA, VIJANA NA  
WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** Mheshimiwa Naibu

## 1 NOVEMBA, 2023

Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Thea Medard Ntara kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mkataba huu wa kimataifa tayari Serikali ilikwisha kuanza kuchukua hatua toka mwaka 2021 lakini kwa sehemu kubwa kama Mheshimiwa Mbunge anavyoelewa na nampongeza sana amekuwa akipambana sana amekuwa akipambana sana kuhusiana na swala hili. Katika mikataba ya kimataifa ina hatua za msingi tatu, hatua ya kwanza ni ya ku-sign pale ambapo wanachama wa umoja huo wanapokutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili ni *reservation* na ya tatu ni *lactification*. Kwenye *reservation* ni pale ambapo nchi inaruhusiwa kutokukubaliana na baadhi ya matakwa ambayo yameelezwa lakini, katika *ratification* ni pale ambapo tayari mme-sign na badee mnaingia kwenye *ratification* kwamba mnaamua kuzi-domesticate hizo sheria ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo pamoja na uchambuzi ambao umeeleza na wadau ambapo tuliwashirikisha tulibaini kwamba sisi tulikuwa mbele kidogo ya mkataba huu wa kimataifa wa mwaka 2011 kwenye masuala ya kazi, Sheria tayari sisi tunazo nchini ambazo zinaleza utaratibu wa kazi lakini pia masuala ya mkataba na hatua nyingine maswala ya mishahara lakini pia masuala ya afya na usalama mahali pa kazi na masuala ya ifadhi ya jamii. Haya yote yapo yameelezwa kwenye mkataba lakini sisi tulikuwa tumekisha kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kuangalia sasa yale ambayo yatakuwa yanautofauti na ambayo yatakuwa na tija kwa upande wetu. Kwa kweli kundi hili ni muhumu na tunaendelea kulihudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalilake la pili la kuhusu mtaala wa wafanyakazi. Ni kweli Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu

**1 NOVEMBA, 2023**

Hassan iliona umuhimu wa wafanyakazi wa ndani kuwa wananyanyasika sana na kwa Sheria tuliyonayo katika Kifungu cha tano cha Sheria ya Ajira na mahusuano kazini, Kifungu cha sita, cha saba lakini pia kifungu cha 11, vyote hivi vinaeleza kuhusu haki na wajibu wa wafanyakazi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sababu tumeanzisha hiyo program kwenye Vyuo vya VETA wewe mwenyewe utakuwa shahidi na Waheshimiwa Wabunge kwamba wafanyakazi wa ndani wananyanyasika sana kwenye maeneo mengi. Sasa tumeona kuanzisha utaratibu huo wa taaluma na kutangaza zaidi ili udahili uongezeke lakini pia kuhakikisha wanafanya kazi kimikataba na watambue na hata sisi kama wawakilishi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante umejibu vizuri sana ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Mwijage.

Na. 9

**Hitaji la Fibre Speed Boat kwa ajili ya kubeba wagonjwa**

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka Fibre Speed Boat mbili zilizofunikwa kama ambulance ili kusaidia Wananchi wa Visiwa 39 vya Wilaya ya Muleba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri atajibu swalii namba tisa, 10, 12.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la

**1 NOVEMBA, 2023**

Mhe Charles John Mwijage, Mbunge wa Jimbo la Muleba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeandaa mpango mkakati utakaowezesha maeneo magumu kufikika kama visiwani na maeneo mengine kupata huduma za usafiri wa dharura pindi utakapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango huo umeainisha vifaa vya usafiri vitakavyotumika kusafirisha wagonjwa ikiwemo usafiri wa anga yaani *air ambulance* na usafiri wa maji yani *boat ambulance*. Aidha, Mpango huo unatarajiwa kukamilika Disemba 2023 na kuanza utekelezaji katika mwaka wa fedha 2024/2025 na Wilaya ya Muleba itapewa kipaumbele, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES JOHN P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nisikitike kwa majibu ya Serikali. Serikali imegawa ambulance lakini sisi Wilaya ya Muleba ambayo 70% ni maji na kuna visiwa 38 hatuna kifaa sio dharura yaani ndiyo maisha yetu visiwa 38 vinahitaji vesal *reliable vesal* ya ku-move. Serikali hamuoni kwamba mchukue jithada za Mheshimiwa Rais ku-copy ile vesal mliyopeleka Mafia na sisi mtununulie kama hiyo kusudi wananchi waweze kufika katika sehemu za huduma kwa sababu eneo hilo lina watu wengi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba tu nimuhakikishie Mheshimiwa Mwijage kwamba Serikali ya awamu ya Sita inatia kipaumbele cha hali ya juu sana katika maeneo ambayo hayafikiki kuhakikisha kwamba huduma za rufaa zinatekelezwa ipasavyo. Ndiyo maana sasa imeandaa mpango makakati wa kuainisha maeneo yote ambayo

**1 NOVEMBA, 2023**

ni magumu kufikika yale ambayo yanahitaji *boat ambulance* ikiwemo Halmashauri ya Muleba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie kwamba tayari tupo hatua nzuri na mwaka ujao wa Fedha 2024/2025 tunaanza kutenga fedha kwa ajili ya kupata hizo *boat ambulance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

Na. 10

### **Kugawa Kata za Wilaya ya Mbanga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itagawa Kata za Matiri, Litumbandyosi, Linda, Mkumbi, Litembo, Nyoni, Maguu na Langiro Wilayani Mbanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Jimbo la Mbanga Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kuanzisha maeneo mapya ya utawala upo kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na mwongozo wa uanzishwaji wa maeneo ya utawala wa mwaka 2014, Hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga inashauriwa kuanzisha mchakato wa maombi ya Kata za

**1 NOVEMBA, 2023**

Matiri, Litumbandyosi, Linda, Mkumbi, Litembo, Nyoni, Maguu na Langiro kwa kufuata utaratibu ulioainishwa kwa kuanza na vikao vya ngazi za vijiji, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Kamati ya Ushauri ya Mikoa (RCC) kisha kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa tathimini ya vigezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa sasa Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu msingi kwenye maeneo yakiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadae kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia hii ya kugawa kata tuna nia pia ya kugawa vijiji na mwaka unaokuja ni mwaka wa uchaguzi. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Halmasahuri ya Wilaya ya Mbinga ambayo vijiji vingi vimeleta maombi ya kugawanywa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kauli ya Serikali ni kwamba taratibu za kisheria za maombi ziendelee, na Serikali itapokea maombi hayo kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, itafanya tathimini ya vigezo lakini kipaumbele cha kwanza kwa sasa ni kuboresha kwanza maeneo ya kiutawala yaliyopo. Lakini hili halizuij kuendelea na taratibu katika ngazi ya halmasahuri, ahsante. (Makofii)

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunakwenda swalii namba 12. Mheshimiwa Ally Mhata.

Na. 12

**Benki kuwa Wakala wa Ukopeshaji na Ukusanyaji  
Madeni wa Halmashauri**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali italeta Sheria ya kuruhusu halmashauri kutumia benki kama wakala wa ukopeshaji na ukusanyaji madeni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua ufanisi wa kutumia benki kama wakala wa ukopeshaji na ukusanyaji wa mmadeni kwa kuzingatia kuwa benki zina miundombinu na utaalamu wa kutoa huduma hizo. Hata hivyo, ili kutumia benki katika kutekeleza jukumu la mikopo ya asilimia 10, maandalizi na utafiti unapaswa kufanyika ili kuendana na lengo kusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliunda Kamati ya Kitaifa ambayo ilichambua na kuandaa mapendekezo ya uendeshaji wa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha, timu imeshakamilisha kazi hiyo na kuwasilisha maoni na mapendekezo ambapo Serikali inaendeleia kuifanya kazi na baada ya kukamilisha itatoa utaratibu, ahsante.

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata majibu ya Serikali. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali kwa kipindi hiki imesimamisha utoaji wa mikopo ili kupisha kuandaa utaratibu mzuri wa utoaji mikopo hiyo.

Je, Serikali haioni haja kuwa na mpango wa dharura wa kutoa mikopo wakati tunasuburi utaratibu huo mpya kwa sababu wananchi wnhitaji sana mikopo hiyo hasa kipindi hichi cha kilimo? (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, lengo la Serikali kusitisha utoaji wa mikopo hii ilikuwa ni kuhakikisha kwamba fedha zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu zinawafikia walengwa lakini pia zinatumika kwa tija na kurejeshwa ipasavyo. Hiyo ndiyo ilikuwa changamoto kubwa iliyopelekea kusitisha utoaji wa mikopo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendanalo hili jambo kwa kasi ili mapema iwezekanavyo utaratibu rasmi uwezekutolewa na mikopo ianze kutolewa kwa wananchi badala ya kuwa na utaratibu wa dharura ambao utakuwa hauna tija sana kwa sababu bado utakuwa na mapengo mengi. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba si muda mrefu sana Serikali itatoa utaratibu na mikopo ya 10% itanza kutolewa kwa wananchi wetu, ahsante. (Makofij)

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunarudi swalii namba 11, Mheshimiwa Mariki.

Na.11

**Hitaji la Vifaa vya Maabara Shule za Mkoa wa Katavi**

**MHE. MARTHA F. MARIKI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa kwa maabara ya sayansi katika shule za Mkoa wa Katavi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Martha Festo Mariki, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mpango wa kuboresha elimu ya sekondari katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga shilingi bilioni 5.148 kwa ajili ya kununua vifaa vya maabara ili viweze kusambazwa katika shule za sekondari kote nchini ikiwemo shule za Mkoa wa Katavi. Ununuzi wa vifaa hivyo upo katika hatua za mwisho kulingana na taratibu za manunuzi.

Aidha, katika Mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka vifaa vya Maabara katika Shule za Mbende, Usevya, Mizengo Pinda, Mamba, Chamalendi, Kasansa, Kabungu, Karema, Mpandandogo, Kandamilumba, Mwese, Kapalambsenga na Homera zilizopo kwenye Mkoa wa Katavi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki.

**1 NOVEMBA, 2023**

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kutenga bilioni tano kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivi, lakini, pamoja na jitihada za Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha elimu nchini hususan elimu ya sekondari kwa upande wa sayansi. Nidhahiri kabisa katika Mkoa wetu wa Katavi bado kuna upungufu mkubwa sana wa walimu hususan walimu wa kike na walimu wa sayansi. (Makofij)

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na Mkoa wa Katavi ambao una upungufu mkubwa, ikiwepo shule ya Mwangaza ina mwalimu mmoja tu wa sayansi na Shule ya Rungwa ambayo ina zaidi ya wanafunzi 1500 lakini haina kabisa walimu wa sayansi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Je, Serikali inaongeza jitihada gani kuhakikisha kwamba ina boresha elimu ya sayansi hususan kuhakikisha watoto wa kike wanakwenda kuongezeka na kupata elimu ya sayansi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Martha Mariki na hili la kwanza la upungufu wa walimu Mkoani Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika kuhakikisha inaondoa upungufu wa walimu katika maeneo yote nchini ikiwemo Mkoa wa Katavi; na katika Mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali iliajiri jumla ya walimu wa sayansi 6,949.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka huu ambayo inatekelezwa ya 2023/2024 Serikali imetenga ajira kwa ajili ya

**1 NOVEMBA, 2023**

kupunguza upungufu wa walimu wa sayansi. Tunaendelea kuratibu na wenzetu wa Ofisi ya Rais, Utumishii li kuweza kupata vibali vya kuweza kuajiri walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swalii la pili la Mheshimiwa Martha Mariki linalohusu jitihada za Serikali; Serikali hii, hasa utashi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, alihakikisha kwamba tunakwenda kujenga shule za wasichana za sayansi katika kila mkoa. Awamu ya kwanza, Mheshimiwa Rais alitoa fedha kwa ajili ya kujenga shule kumi kwenye mikoa kumi na awamu ya pili kuna fedha bilioni 48 imekwenda kwenye mikoa 16. Hii yote ni kuhakikisha kwamba watoto wa kike wanapata elimu iliyobora na elimu ya sayansi katika mikoa yote. Hivyo, awamu ya kwanza jumla ilienda bilioni 40 na awamu ya pili bilioni 48.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Eliadory Felix.

Na. 13

### **Kutangaza Maeneo ya Uwekezaji Kigoma**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufungua na kutangaza maeneo ya uwekezaji Mkoani Kigoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI,  
OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo: -

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali ni kuendelea kuzitangaza fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini zikiwemo zinazopatikana Mkoani Kigoma. Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuandaa makala maalum (*documentary*) ya kutangaza maeneo ya uwekezaji katika Mkoa wa Kigoma, pia, kufanya makongamano ya kimataifa ya biashara na uwekezaji, ambapo kongamano la kwanza lilifanyika mwaka 2019 na la pili lilifanyika mwaka 2022. Aidha, mwezi Mei, 2024, Mkoa wa Kigoma unatarajia kufanya Kongamano la tatu la Kimataifa la Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutangaza maeneo ya uwekezaji kupitia ziara za viongozi wa Kitaifa ndani na nje ya nchi na kupitia ofisi zetu za balozi zetu, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, ni maeneo yapi ambayo Serikali imeyaainisha katika Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya uwekezaji?

(ii) Je, ni shughuli zippi za kipaumbele zilizoainishwa kutangazwa katika maeneo hayo? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza. Mkoa wa Kigoma ni moja ya Mikoa ya kimkakati hapa nchini, hivyo maeneo ambayo tunaaazimia kuyawekea uwekezaji wa kutosha ni kwenye uongezaji thamani katika mazao ya kilimo.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, azma hiyo, inadhihirika pale ambapo Mheshimiwa Rais wetu Mpwendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameendelea kuboresha miundombinu wezeshi ikiwemo barabara za lami lakini pia, kupeleka umeme wa Gridi ya Taifa ili kuona namna gani tunaweza kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari pale Kigoma tumeshaweka kiwanda kikubwa cha kuchakata chikichi lakini pili, kuna kiwanda kikubwa kinaenda kujengwa cha kuchataka sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli muhimu ambazo zinaweza kufanya katika Mkoa wa Kigoma, mahsus Buhigwe ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka, na kwa kuwa tunajua wako mpakani na kuna masoko ya DRC na Burundi, kwa hiyo, tunataka tuone mazao ya tangawizi, kahawa, ndizi, parachichi na mazao mengine yanastawishwa na kuwekezwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba Halmashauri zote katika Mkoa wa Kigoma kutenga maeneo ya uwekezaji ili kuweza kufanikisha lengo na azma ya Mheshimiwa Rais wetu Mpwendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuweka Mkoa wa Kigoma kuwa Mkoa wa kimkakati, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunakwenda Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ng'wasi Damasi Kamani.

Na. 14

### **Kigezo cha uzoefu wa kazi kwa wahitimu**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza: -

Je, Serikali haioni kigezo cha uzoefu katika kuomba kazi ni ubaguzi dhidi ya vijana waliohitimu vyuo wanaolenga kuingia katika soko la ajira?

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA  
UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, naomba kujibu swali liloulizwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ajira za Serikali zinatekelezwa kwa kuzingatia Sera ya Menejimenti na Ajira ya mwaka 2008. Kwa mujibu wa Aya ya 4.2(i) ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma inaelekeza kuwa Ajira kwa mara ya kwanza (*entry point*) hususan kwa wale wanaojiriwa kwa cheo cha kuanzia kwenye miundo itafanyika kwa kuzingatia vigezo vya utaalam bila kujali uzoefu, isipokuwa kama kazi husika itahitaji kuwa na uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uzoefu huwekwa kwenye nafasi ambazo si madaraja ya kuingilia kazini mfano nafasi za waandamizi, viongozi au kada ambayo uzoefu ndio sifa ya msingi ya kuingilia kama vile kada ya udereva ambapo lazima mtumishi huyu ajue kuendesha gari kwa viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa Muundo wa Utumishi wa Kada hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali ya nyongeza;

- (i) Je, nini kauli ya Serikali juu ya waajiri wa sekta binafsi ambao bado wanatumia kigezo hiki cha uzoefu kwenye kutangaza ajira?
- (ii) Je, Serikali iko tayari kufufua ule utaratibu maalum uliokuwepo mwanzo na kuutengenezea sera ambao utawatambua na kuwapa

kipaumbele wahitimu ambao wanajitolea kwenye ofisi mbalimbali za umma kwa ajili ya kupata uzoefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imekuwa inafanya jithada kubwa hasa kuitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuhakikisha kwamba wale waajiri wanazingatia vigezo ambavyo vinatakiwa katika ukuzaji au uenezaji au ule usimamizi wa soko la ajira. Mojawapo ni katika eneo la watu binafsi ambako nako mara kwa mara tunawaelekeza kwamba lazima vigezo vyta kuingia viangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwenye sekta binafsi, pamoja na utaratibu ambao sisi kwenye soko la ajira tumeuzoea lakini ni kweli kwamba kwenye sekta binafsi kinachoangaliwa zaidi ni tija ili kuweza kusaidia mtu aweze kupata faida katika jambo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge tunayachukua na tutaendelea kuyasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo la pili; kwa wale wahitimu ambao wanaomba kazi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inawatambua; na sasa tuko katika hatua za mwisho, kama nilivyowahi kueleza mwanzo, ya kukamilisha ule muundo mzima au taratibu nzima za jinsi wao pia tunawaingiza katika soko la ajira kwa kuzingatia vigezo. Vigezo hivyo ni pamoja na kigezo cha kuwajengea uwezo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa maana ya lugha ya *internship*, lakini pia, kuweka vigezo vingine ambavyo vitawasaidia vijana waweze kuingia katika soko la ajira kirahisi, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mafuwe.

**1 NOVEMBA, 2023**

Na. 15

**Serikali Kununua Vipuri na Vyuma katika Kiwanda cha  
Kilimanjaro Machine Tools**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuelekeza taasisi zake kununua mashine na vipuri katika kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imekifanya ukarabati mkubwa Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools* (KMTC) ikiwa ni pamoja na kujenga tanuri la kuyeyushia chuma (*Foundry*), ukarabati wa miundombinu ya kiwanda na utengenzaji wa mtambo wa kuweka utando katika bidhaa za chuma ili kuzuia kutu (*hot dip galvanizing plant*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa taasisi zake zinazotumia bidhaa na vipuri vinavyozalishwa na KMTC zinaingia mikataba ya kununua mashine na vipuri kutoka KMTC, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, na ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sasa Serikali imeridhia kwamba taasisi zake zikanunue vyuma pamoja na vipuri kwenye kiwanda hicho;

Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuweka mpango mzuri wa kutumia chuma cha Liganga ambacho Serikali inaendelea na mchakato wa kuzalisha ili chuma hicho kitumike kuzalisha vyuma kwa ajili ya taasisi zetu za Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Halmashauri ya Wilaya ya Hai imepeleka maombi ya kupewa eneo kwa ajili ya kuanzisha Mji Mdogo wa Kibishara Njia Panda ya kwenda Machame. Ninaomba kufahamu, Serikali imefikia wapi katika mpango huo wa kutupa eneo la kibishara Njiapanda ya Machame?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni kweli moja ya mikakati ya Serikali ni kuona rasilimali zetu nchini zinatumika kuzalisha bidhaa ambazo tunahitaji kuzitumia na hasa kwenye hizi bidhaa za chuma ambazo tunatumia fedha nyingi sana kuagiza chuma kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Serikali tunavyoendelea kutimiza na kukamilisha uanzishwaji na utekelezaji wa Mradi wa Liganga na Mchuchuma tunaamini hii ndio itakuwa malighafi itakayotumika na kiwanda hiki cha KMTC.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kuna hatua zimeshafanyika ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kule Mchuchuma na Liganga, na sasa tunakamilisha majadiliano na wawekezaji ili tuanze kuchimba chuma na kuhakikisha inatumika katika viwanda vyetu kikiwemo KMTC.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali la pili; ni kweli Mheshimiwa Mbunge amekuwa akifuatilia sana kuhakikisha eneo hili la KMTC ambalo ni eneo kubwa wenzetu wa Halmashauri ya Hai wanapata eneo la kujenga Mji Mdogo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali tumeshaanza kujadiliana na kupitia NDC ambao wameshaweka *master plan* ili kuona namna ya kua-accommodate maombi hayo ya Mheshimiwa Mbunge na wana Hai. Katika mpango huo tutaona nini tutawapa na wafanye shughuli gani zinazoendana na mahitaji mahsusii ya Kiwanda hiki cha KMTC, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mtenga.

Na. 16

#### **Kulipa Fedha Kampuni za Mbolea na Viuatilifu Mtwara**

**MHE. HASSAN S. MTENGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazilipa fedha Kampuni za Usambazaji wa Mbolea na Viuatilifu Mtwara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasan Seleman Mtenga, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kulipa madai ya Kampuni na Mawakala wa pembejeo yaliyotokana na usambazaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbolea na viuatilifu kwa wakulima hapa nchini. Madai hayo ni pamoja na madai ya Kampuni na

**1 NOVEMBA, 2023**

Mawakala waliosambaza pembejeo kwa mfumo wa ruzuku katika msimu wa 2015/2016 katika Mikoa 24 ya Tanzania Bara ukiwemo Mkao wa Mtwara. Madai hayo yalifanyiwa uhakiki na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG). Hadi kufikia Septemba, 2023 kiasi cha shilingi 42,440,275,705.00 kimelipwa kwa Kampuni na Mawakala 307 wanaostahili kulipwa. Kati ya kiasi hicho, shilingi 679,750,000 zimelipwa kwa kampuni zinazohudumu Mkao wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika msimu wa 2021/2022 na msimu wa 2022/2023, Serikali iliratibu usambazaji wa tani 28,576.70 za sulphur, lita 4,181,824.50 za viuatilifu vya maji na mabomba 1,337 yenye thamani ya shilingi 156,325,550,300.00 kwa ajili ya wakulima wa korosho katika maeneo ya uzalishaji ikiwemo Mtwara. Kati ya kiasi hicho, Serikali imewalipa wazabuni kiasi cha shilingi bilioni 112.7, na deni lililobaki ni shilingi bilioni 43.5. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha malipo ya madeni hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, ngoja. AG, ultaka kusimama? Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina swali moja la nyongeza;

Je, ni lini mfuko wa pembejeo utarejeshwa ili Serikali iweze kumaliza haya matatizo yote ya ulipaji wa madeni ya watu ambao wanaleta mbolea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba, jambo hili liko katika mchakato na sisi kama Wizara ya Kilimo tunalipitia upya ili kuhakikisha tunaondokana na hizi changamoto, kwa hiyo tutakapolimaliza tu, tutalirudisha kwa wananchi mara moja kama ilivyokuwa hapo awali ili kuondokana na kero hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jambo hili tumelipokea.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Felista Njau.

Na. 17

**Kutoa elimu ya kilimo salama kwa kutumia Televisheni  
ya Taifa na Redio**

**MHE. FELISTA D. NJAU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Televisheni ya Taifa na Redio katika kutoa elimu ya kilimo salama na chenye tija?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Deogratius Njau, Mbunge wa Viti Maalum kama kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo inaendelea kutoa elimu katika mnyororo wa thamani wa uzalishaji wa mazao nchini kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo matumizi ya vyombo vyahabari kupitia televisheni na redio; mikutano; mafunzo rejea kwa nadharia na vitendo; na mifumo ya kidijitali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kilimo cha mbogamboga pembezoni mwa mito na mifereji inayotiririsha maji machafu kutoka viwandani katika majiji makubwa hasa Dar es Salaam.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kwa wananchi hawa ili waweze kukiuka athari ambazo zinaweza kutokea kiafya?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amesema wanatoa elimu kwa njia ya nadharia na vitendo. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa mwaka huu wametoa elimu mara ngapi na maeneo gani? Ahsante. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, hili swali la pili ni la takwimu kama huna takwimu zake unaweza ukaliacha ukajibu la kwanza tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ni kweli nikianza na swali la pili, takwimu kwa hapa siwezi kuwa nazo niwe mkweli nitalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Jibu la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo suala la pili, ni kwamba tutaendelea kutoa elimu. Vilevile, katika maeneo ambayo yana athari, kuna kanuni ziko katika ngazi za halmashauri ambazo zinapaswa kusimamiwa ili kuondoa kero hii ambayo Mheshimiwa Mbunge umeainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu kwamba, sisi kama Wizara ya Kilimo tutaendelea kuelimisha wananchi wetu na vile vile

**1 NOVEMBA, 2023**

tutazihamasisha halmashauri ziweze kutekeleza sheria na kanuni za halmashauri kwenye kusimamia yale maeneo ambayo yako katika mito na vile viwanda vinavyotiririsha majitaka katika maeneo ya wananchi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Kassinge.

Na. 18

**Fidia kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fidia kwa wananchi 438 Waliofanyiwa uthamini kupisha upanuzi wa Kiwanja cha ndege Kilwa – Masoko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha robo ya mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikamilisha zoezi la Uwekaji Wazi Daftari la Fidia (*valuation report disclosure*) kwa wananchi 438 waliofanyiwa uthamini ili kupisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hiyo, mnamo mwezi Agosti, 2023 Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara ya Uchukuzi, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Lindi, walifanya na kukamilisha zoezi la uhakiki wa daftari la fidia.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hizi, zoezi la ulipaji wa fidia litaanza mara baada ya Wizara ya Fedha kukamilisha taratibu zote za kifedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali na nina maswali mawili ya nyongeza. Mchakato wa uboreshaji na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Kilwa Masoko ni wa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; nataka Mheshimiwa Naibu Waziri, awahakikishie Watanzania, Wanakilwa na Bunge hili, je, mpango wa Serikali wa uboreshaji na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kilwa Masoko bado uko pale pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amefika Kilwa Masoko mara kadhaa. Alifika mwezi Juni akiwa Mwenyekiti wa Kamati na akafika mwezi Agosti akiwa Naibu Waziri katika Sekta hii ya Uchukuzi na alikuja mahususi kwa ajili ya masuala haya ya kiwanja cha ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale kuna changamoto kadhaa, kwa wananchi wangu hawa 438 mpaka sasa bado hawajalipwa fidia. Je, yuko tayari sasa baada ya Bunge hili kwenda Kilwa Masoko akiambatana nami ili kwenda kusikiliza kero za hawa wananchi wangu 438?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. DAVID M. KIHENZILE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe uhakika Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kusini kwamba, Serikali ya Awamu ya Sita inayo dhamira ya dhati ya kuboresha Uwanja wa Ndege wa Kilwa Masoko. Pia, hiyo inakwenda sambamba na uwekezaji mkubwa unaofanyika pale wa kujenga bandari kubwa kwa ajili ya uvuvi.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia kwamba mpango wa Serikali uko pale pale, mara baada ya wenzetu wa Wizara ya Fedha kukamilisha taratibu za ndani, fidia hiyo kwa wananchi hao itaanza kulipwa. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili anauliza je, niko tayari kuambatana naye baada ya kumaliza Bunge hili. Amekiri mwenyewe nilikwenda pale pamoja na wenzangu nikiwa Mwenyekiti wa Kamati Kilimo na Mifugo. Vile vile, nimekwenda hapo juzi kukagua bandari hiyo na uwanja huo. Niko tayari kwenda pamoja naye ili tukawape uhakika wananchi hao ambao wanamwamini Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ili waendelee kujenga imani naye.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan.

Na. 19

### **Ujenzi wa Gati la Abiria la Kisasa Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Ghati la Kisasa la Abiria kwenye Bandari ya Dar es Salaam?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. DAVID M. KIHENZILE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha huduma kwa wananchi wake katika maeneo mbalimbali ya nchi, likiwemo Jiji la Dar es Salaam. Ili kuendeleza juhudhi hizo, Serikali kupitia TPA inakamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa gati la kisasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ambao hadi sasa upo katika hatua za mwisho na unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kwa kuendelea kufuutilia kero za wananchi katika maeneo yao. Serikali itaendelea kuboresha huduma hizo ili kuwawezesha wananchi kufanya kazi zao bila kikwazo chochote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri mwenyewe kwamba, upembuzi yakinifu utakamilika Desemba, je, ni lini ujenzi utaanza rasmi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, ujenzi huo utazingatia kwa kiasi gani kuweka vifaa vyta kisasa ili abiria wasikaguliwe na mbwa kama inavyofanyika sasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. DAVID M. KIHENZILE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan kama nilivyo sema hapo awali. Hatua ya kwanza ambayo Serikali inafanya ni kufanya uthamini au upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao utaweza kutusaidia kujua nini kinapaswa kufanyika. Pia, mara baada ya kukamilisha hatua hiyo, hatua itakayofuatia itakuwa ni kuanza kufikiria au kuanza mchakato kwa ajili ya ujenzi. Kwa sababu, Serikali

**1 NOVEMBA, 2023**

imeendelea kufanya maboresho makubwa sana kwenye bandari zetu nchini ikiongozwa na Bandari yetu kubwa ya pale Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili; kama nilivyojibu swalii la kwanza, katika usanifu huu unaoendelea kwa ajili ya ghati letu jipya la Dar es Salaam, utaambatana pamoja na ufungaji wa mashine ya ukaguzi wa kisasa ambao utatumia teknolojia ya kisasa ya ukaguzi kwa ajili ya abiria na mizigo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi, Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 20

**Majeshi ya Ulinzi na Usalama kulinda miradi mikubwa ya kimkakati**

**MHE. ESHTER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kuhusisha Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alljibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Jeshi la Ulinzi la

**1 NOVEMBA, 2023**

Wananchi wa Tanzania limeendelea kulilinda Taifa letu pamoja na Miradi Mikubwa ya Kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuitia Makao Makuu ya Jeshi imekuwa ikitoa wataalam mbalimbali wanaoungana na wataalam wa vyombo vingine vya Usalama ili kuhakikisha miradi ya kimkakati inakuwa salama wakati wote, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza au kuajiri vijana wengi zaidi na kuwapa mafunzo hayo ili waweze kusimamia ile miradi mikubwa inayotolewa kwenye mikoa na wilaya, kwa sababu mingi imeonekana ikihujumiwa sana? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni kama aliyoyaeleza Mheshimiwa Mbunge Malleko, ni kweli kwamba Serikali ina dhamira na imekuwa ikiajiri vijana kwa ajili ya kuijunga na vyombo vyetu vingi vya usalama ikiwemo Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, Fire na Uokozi pamoja na Magereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vyote hivi hushiriki katika shughuli za ulinzi na usalama wa miundombinu inayoendelezwa kwenye maeneo yetu kuitia Kamati za Usalama za Wilaya na Kamati za Usalama za Mikoa, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**1 NOVEMBA, 2023**

Na. 21

**Kutumika kwa Sheria za Ardhi kwenye Miji**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, kwa nini Sheria za Ardhi zinazokusudiwa kutumika kwenye miji zinatumika maeneo ya vijiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa kisheria wa usimamizi wa ardhi nchini umegawa ardhi katika makundi matatu ambayo ni Ardhi ya Kijiji, Ardhi ya Hifadhi na Ardhi ya Jumla. Kwa kuzingatia mgawanyo huo, Ardhi ya Vijiji inasimamiwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 na maeneo ya miji yanasisimamiwa na Sheria ya Ardhi, Sura 113. Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo ndani ya mipaka ya vijiji yanayosimamiwa na Sheria ya Ardhi, Sura 113 kutokana na kumilikishwa kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114 au kuhawilishwa. Aidha, baadhi ya maeneo ya vijiji yametangazwa kuwa ya kuendelezwa kimji (*Planning Area*) na kuandaliwa Mpango Kabambe (*Master Plan*) na hivyo kuyafanya yasisimamiwe na Sheria ya Ardhi, Sura 113.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri, nakushukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, uhalisia uliopo ni kwamba, kuna mkanganyiko mkubwa sana kwenye halmashauri za miji ambazo

zina vijiji. Sasa, Waziri atakubaliana nami kwamba, ni wakati sasa wa kutoa maelekezo kwa sababu sheria inataka utayari wa eneo kabla halijawa declared planning area. Maeneo mengi yamekwenda kuwa declared planning area kabla hayajawa tayari na ni maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yuko tayari kutoa maelekezo ili kufanyike marekebisho ya kutangaza upya maeneo ya vijiji yasitawaliwe na Sheria za Miji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, kwa kuendelea kufuatilia maslahi ya wananchi wake wa Jimbo la Njombe Mjini. Ni kweli Sheria ya Mipango Miji, Sura ya 355 kifungu cha 77(1)(b) kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Ardhi, kutoa Kanuni zinazoongoza upangaji wa miji (*Planning Space Standard*). Vilevile mwaka 2018 Kanuni hiyo ilitolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilithibitishie Bunge lako kwamba Kanuni hii tumeisimamisha na tumetoa maelekezo kwa wataalam wa ardhi wa Wizara ya Ardhi, kuipitia upya na kutoa Kanuni ambayo itaendana na hali halisi ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni hii ndiyo inayohusika kwenye ujenzi wa vituo vya mafuta vile vyenye ardhi ndogo, inahusika kwenye mashamba ya mijini ya ekari tatu na ukiangalia hali halisi ya Mji wa Njombe kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mji wa kilimo. Pia kilimo kinacholimwa pale ni kilimo cha parachichi na sisi Wizara ya Ardhi hatuwezi kuwa kikwazo cha kuendeleza zao la parachichi ambalo linalimwa kwenye Wilaya ya Njombe.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuirejea Kanuni hiyo na tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge wa Njombe na Wabunge wengine wenye maeneo ya vijiji ambayo na sura ya kijiji, ili Kanuni itakayotoka iweze kuendana na mazingira ya wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Aleksia Kamguna.

Na. 22

### **Ujenzi wa uzio Hospitali ya Mkoa wa Morogoro**

**MHE. ALEKSI A. KAMGUNA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga uzio katika Hospitali ya Mkoa wa Morogoro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huu utaanza mwezi Januari, 2024 na kukamilika mwezi Septemba, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia.

**1 NOVEMBA, 2023**

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, Mkoa wa Morogoro katika hospitali ya rufaa kuna matatizo ya majengo. Pale ndani majengo yake yako scattered. Sasa inakuwa ni vigumu sana kutoa huduma kwa wakati mmoja.

Je, Serikali imejipangaje kujenga jengo la kuinuka juu (ghorofa) ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wake? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; katika Kituo cha Afya cha Ifakara, kuna matatizo ya kpimo ambacho kinaitwa *fetal monitors* ambacho kinahusika kwa ajili ya wanawake.

Je, Serikali imejipangaje kupeleka vifaa hivyo ili wale akinamama waweze kupata huduma stahiki? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mazuri ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, suala la kwamba majengo yako mbalimbali (*scattered*), lakini pia eneo la Hospitali ya Morogoro ni dogo kwa maana ya ukubwa wa eneo lile. Mheshimiwa Waziri wa Afya amekwishaelekeza kwamba, Hospitali zote za Mikoa, Kanda na Taifa wasijenge tena bila kuwa na *plan* ya hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hospitali zote zimeelekezwa kuchora na kuhakikisha wanakuwa na *plan* ya ujenzi ambayo inatatua matatizo aliyoyasema na wataleta *plan* na majengo ya ghorofa yatakwenda juu na sasa ndiyo yatakuwa yanajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mheshimiwa Mbunge swali la la Kituo cha Afya, naomba aje sasa hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kama alivyoona pale Dar es Salaam

**1 NOVEMBA, 2023**

alipozindua vifaa mbalimbali, tuwasiliane na Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, tuone kifaa hicho, halafu aandike mara moja na aweze kupelekewa kifaa hicho kwenye eneo husika. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Fedha. Mheshimiwa Condester.

Na. 23

### **Uhitaji wa Huduma za Forodha Kakozi Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICALWE** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuweka Kituo cha Forodha Kakozi Momba ili kuunga mkono jitihada za kujenga Soko la Mazao la Kimataifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sicalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania ina utaratibu wa kupitia na kufanya tathmini ya sehemu zote ambazo zinaweza kujengwa ofisi kwa ajili ya ukusanyaji kodi. Utaratibu huu unazingatia uwiano wa gharama za ukusanyaji wa mapato na kiwango cha kodi kinachotarajiwa kukusanywa pindi ofisi hizo zitakapofunguliwa kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mwenendo wa kukua kwa biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya kina katika maeneo mbalimbali ikiwemo Kakozi

Momba na mipaka mbalimbali hapa nchini. Aidha, maeneo yatakayokidhi vigezo vya kujengwa ofisi za forodha kulingana na tathmini hiyo, taratibu za uanzishwaji wa ofisi hizo zitaanza kwa kuzingatia upatikanaji wa rasilimali watu na fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, kwa kuwa Julai, 2021 Waziri wa Fedha na Mipango alifanya ziara na kutembelea Kituo hicho cha Forodha na majibu ya Serikali yanasema kwamba, wanafanya tathmini kwa kina.

Je, tathmini hiyo ya kina itachukua muda gani kukamilika (*time frame*)?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kutokana na umuhimu wa Kituo chenyewe cha Forodha cha Tunduma, kwa sababu kimebeba nchi nyingi za Kusini mwa Afrika - SADC na kituo kile kuonekana kuzidiwa katika kutoa huduma za forodha. Je, Serikali haioni kuna haja na uharaka sana wa kuongeza Kituo kingine cha Forodha kwenye ule mpaka ambako ni Kakozi, kwa ajili ya kunusuru mapato yanayopotea na kuongeza mapato kwa Taifa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester. Hata hivyo, kabla ya kujibu naomba nimpongeze sana kwa namna anavyofuatilia kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini itakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali iko kazini na atapata mrejesho.

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba nimwelekeze Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, aangalie uharaka wa ujenzi wa kituo hicho huko Kakozi – Momba, endapo atajiridhisha kutokana na tathmini yake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Antipas, kwa niaba yake Mheshimiwa Ng'wasi Kamani.

Na. 24

### **Elimu ya Kujikinga na Majanga ya Moto**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI**  
aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa idhini kwa Makampuni binafsi kutoa elimu ya kujikinga na majanga ya moto kwa Wananchi na Taasisi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Antipas Zeno Mgungusi, Mbunge wa Malinyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa makampuni binafsi kushiriki katika shughuli za huduma ya zimamoto na uokoaji nchini, kama vile ufungaji wa mifumo ya kuzima moto, usambazaji na matengenezo ya vifaa vya kuzima moto kwa wananchi na taasisi. Serikali itafanya marekebisho madogo ya kanuni ya ukaguzi, tozo na cheti ya mwaka 2008 ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kutambua na kujumuisha makampuni binafsi katika utoaji wa elimu ya kinga na tahadhari dhidi ya majanga ya

**1 NOVEMBA, 2023**

moto kwa masharti na vigezo vitakavyowekwa na Serikali, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali na pamoja na kwamba focus ya Serikali sasa hivi ni kufanya kazi na sekta binafsi kwa mfumo wa PPP. Je, ni lini sasa uhuishwaji huu wa hizi kanuni utakamilika ili kuweza kuwezesha sekta binafsi kuingia na kutoa elimu ya majanga haya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuharakisha hili jambo ambalo amelipendekeza Mheshimiwa Kamani, ni jambo jepesi kwa sababu Kanuni zinaishia kwa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wataandaa mapendekezo ya namna ya kuzingatia kwenye Kanuni zilizopo ili kuhuisha na kujumuisha hili suala kwenye utendaji wa Zimamoto na Uokozi, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

Na. 25

### **Ujenzi wa Chuo cha VETA Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Wilayani Kakonko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundji Stadi (VETA) katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya VETA katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Aidha, Wilaya ya Kakonko ni miiongoni mwa wilaya hizo 64 ambazo zinajengewa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali imeshapeleka kiasi cha shilingi 228,000,000 pamoja na vifaa vya ujenzi ikiwemo nondo na sementi kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Kakonko ambapo ujenzi upo katika hatua ya kujenga misingi ya majengo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kamamba.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri, niliomba kujengewa chuo na sasa ujenzi umeanza, naishukuru sana Serikali. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, majengo ambayo yameanza kujengwa katika chuo kile ni majengo Tisa kati ya majengo mengi ambayo yatajengwa katika eneo hilo; Je, ni lini majengo hayo ambayo yapo katika mpango huo yataanza kujengwa?

Swali la pili; ni lini ujenzi sasa utakamilika ili wananchi wa Wilaya ya Kakonko ambao wanasubiri chuo hiki kwa hamu sana utakamilika na mafunzo yaweze kuanza? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kamamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ujenzi wa vyuo hivi unagharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu, kwa awamu ya kwanza tumetenga zaidi ya bilioni 1.5 kwa ajili ya majengo ya awamu ya kwanza ambayo ni majengo tisa na ujenzi huo umeanza mwezi wa Nane mwaka huu na ni ujenzi ambao tunatarajia utachukua kati ya miezi nane mpaka 12. Kwa hiyo, ni matarajio yetu ifikapo mwezi wa Sita au wa Saba mwakani majengo haya Tisa ya awamu ya kwanza yatakuwa yamekamilika na yatakapokamilika kwa sababu tumejenga kimkakati, tutahakikisha kwamba majengo haya yatakapokamilika chuo kiweze kuanza kutoa huduma hapohapo wakati tunaendelea na ujenzi wa awamu ya pili. kwa hiyo ujenzi wa awamu ya kwanza unatarajiwa kunako mwezi wa Sita, ama mwezi wa Saba mwakani utakuwa umekamilika *then* tutaanza ujenzi wa awamu ya pili kwa kadri ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu. Nakushukuru

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunakwenda Wizara ya Maji Mheshimiwa Sillo.

Na. 26

### **Mradi wa Maji Darakuta Hadi Minjingu – Babati**

**MHE. DANIEL B. SILLO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza mradi wa maji wa Darakuta – Magugu - Mwada hadi Minjingu – Babati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Darakuta-Magugu ndio unoendelezwa kwa awamu ya pili mpaka Minjingu ambapo utagharimu shilingi bilioni 5.672 na kazi zinazotarajiwa kufanyika ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu umbali wa Kilometra 46, ujenzi wa tenki la lita 250,000 na ufungaji wa pampu za kusukuma maji. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwezi Juni, 2022 chini ya Mzabuni *Plasco Limited* na kazi hiyo ilitarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 3 Julai, 2023, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (*BAWASA*) ilivunja Mkataba na *Plasco Limited* baada ya kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati. Kwa sasa, Serikali imeanza ununuzi wa mabomba kupita mfumo mpya wa Ununuzi wa *NEST*, na ifikapo mwezi Desemba 2023, Mzabuni wa mabomba atakuwa ameshapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utatekelezwa kwa muda wa miezi sita na unatarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2024 na utanufaisha wananchi zaidi ya 23,000 wa Kata za Mwada na Nkaiti.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Serikali napenda kujibu swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapita miaka miwili sasa toka Serikali ipeleke mabomba katika Miji Midogo ya Dareda na Galapo kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji chakavu.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukarabati miradi hii chakavu katika Miji hii ya Galapo na Dareda?

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Daniel Sillo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu chakavu katika maeneo aliyoyataja tayari Mamlaka ya BAWASA inashughulikia na imeomba fedha milioni 511 ya kufanya kazi hii ambayo imekatishwa watu wa Plasco lakini vilevile kuhakikisha maeneo chakavu yanafanyiwa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Kiteto tumekosa vyanzo vya uhakika vya maji, ni lini Serikali itatuletea mradi wa Simanjiro ufile Kiteto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Olelekaita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Simanjiro kuelekea Jimboni kwake taratibu zinaendelea uhakikisha mara tukipata fedha tutaweka mkakati maalum kuhakikisha tunapeleka kule maji ya uhakika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Rweikiza.

**1 NOVEMBA, 2023**

Na. 27

### **Mradi wa Maji Kata Sita - Bukoba Vijijini**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Je, lini mradi wa kupeleka maji katika Kata Sita za Izimbya, Kyaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja kutoka Ziwa Ikimba utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi wa maji wa Ziwa Ikimba uliopangwa kunufaisha Kata Sita za Izimbya, Kyaitoke, Mugajwale, Ruhunga, Katoro na Kaibanja zenyе jumla ya Vijiji 17. Utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2024. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 inaendelea na uchimbaji wa visima katika Wilaya ya Bukoba Vijijini ambapo uchimbaji wa visima virefu Sita utafanyika katika Kata za Ruhunga, Kaibanja, Mgajwale, Izimbya, Katoro na Kyaitoke. Kwa ujumla uchimbaji huo umefikia asilimia 60 na unatarajiwa kukamilika Mwezi Novemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali inatarajia kutekeleza mradi wa maji mwingine katika Kata ya Katoro utakaohusisha, ukarabati wa tanki la lita 150,000, Ujenzi wa vituo vyia kuchotea maji 35, ulazaji wa miundombinu ya kusambaza maji kilometra 37, kujenga nyumba ya pampu, kufunga umeme na Kununua na kufunga pampu ya kusukuma maji. Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo anatarajiwa kupatikana mwezi Januari, 2024.

**1 NOVEMBA, 2023**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rweikiza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kusema kweli napongeza kwa hatua ambazo zimefikiwa katika mradi huo, tunachosubiri ni utekelezaji hapo mwakani mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mwingine wa maji pale Kemondo, Mradi wa Maji Kemondo umechukua miaka mitatu, karibia minne bila kukamilika. Kwa nini unachelewa hivyo? (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii moja la nyongeza na nipokee pongezi zake, ninakushukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kupokea namna ambavyo taratibu tumeendelea kuzifanya na kwa ushirikiano wako Mheshimiwa Mbunge ninakuhakikisha mradi huu utaenda kuanza mara moja kadri tulivyosema.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mradi wa Kemondo umechelewa kwa sababu ya kusubiria pampu ambazo zilikaa muda mrefu pale bandarini kupia michakato mbalimbali ya kiutaratibu, lakini mpaka hivi ninavyoongea tayari zile pampu zimeshachukuliwa, anazo Mkandarasi, kuitia Bunge lako Tukufu naomba nimuagize huyu Mkandarasi mwenye pampu za mradi wa Kemondo mara moja kufika mwisho wa wiki hii lazima pampu hizo ziweze kufika kwenye mradi. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kujua mradi mkubwa wa maji kutoka Momba kwenda Tunduma mpaka Mbozi umefikia hatua gani?

**1 NOVEMBA, 2023**

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stella Fiyao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mkubwa anaouongelea ni mradi wetu wa kimkakati kama Wizara, tukitambua changamoto kubwa ya maji katika Mji wa Tunduma vilevile Mji wa Mombasa. Mradi huu tayari utekelezaji unaendelea na tutahakikisha unakwisha kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Madini Mheshimiwa Tunza.

Na. 28

### **Utafiti wa Madini – Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Serikali imefanya utafiti kuhusu uwepo wa Madini Mkoani Mtwara?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia GST imefanya utafiti wa awali na kuainisha madini yapatikanayo katika Mkoa wa Mtwara. Miiongoni mwa madini hayo ni kinywe, vito aina ya ruby, sapphire, rhodolite, amazonite na green tourmaline. Pia madini ya

metali aina ya dhahabu, shaba, manganese na chuma. Vilevile madini ya viwanda kama marble na chokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, madini mengine ni mchanga wenye madini mazito (*heavy minerals*) kama rutile, titanium, ilmenite, zircon na magnetite, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua baada ya utafiti huo wa awali kuna muendelezo gani katika ugunduzi huo wa madini?

Swali langu la pili, ni kwa kiasi gani wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanafahamu maeneo hayo yenyе madini ili waweze kuitumia fursa hiyo kujipatia kipato? Nakushukuru.(Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hatua zinazochukuliwa baada ya madini kutambulika maeneo yenyе madini hayo, Afisa Madini ya Mkoa anao wajibu wa kupeleka taarifa hizo kwa Mkuu wa Mkoa na Wakuu wa Wilaya, aidha kupitia machapisho ambayo GST wanaandaa. Mwaka huu mwezi wa Tano waliandaa kitabu cha madini yapatikanayo katika Wilaya zote za Tanzania, wananchi hufikishiwa taarifa pia kupitia mafunzo mbalimbali ambayo Wizara inatoa na kupitia utaratibu huo wananchi wengi wamejitokeza kwenda kukata leseni za utafiti na uchimbaji wa madini yaliyobainika katika hayo maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali lake la pili kwamba wanayafahamu maeneo hayo? Jibu ni ndiyo kwa sababu ya taarifa ambazo Wizara inasambaza kupitia GST na taasisi zingine za Wizara na ndiyo maana sasa hivi madini ya graphite yameanza

**1 NOVEMBA, 2023**

kuchimbwa na wachimbaji wadogo ambao wamepata leseni na wanaendelea na utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika maeneo yenyeye dhahabu kama Nanyumbu na Masasi wachimbaji wadogo wameendelea kufaidika na Wizara sasa hivi iko katika mchakato wa kufanya utafiti wa kina zaidi ili wajue kiasi na aina ya madini na ubora wa madini yanayopatikana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Kamonga.

Na. 29

### **Elimu ya Mikopo ya Vifaa vya Uvubi - Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, lini elimu ya uvubi na mikopo ya vifaa vya kisasa vitatolewa kwa wananchi wa Manda, Ruhuhu, Iwela, Lupingu, Lifuma, Makonde, Kilondo na Lumbila?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUBI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvubi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu ya kwanza ya mradi wa kuwawezesha wavubi boti za kisasa, Wizara ya Mifugo na Uvubi imetoea jumla ya boti nne za kisasa kwa wavubi wa Ziwa Nyasa. Kati ya boti hizo, boti mbili zimetengwa kwa wanufaika wa Halmashauri ya Ludewa ambazo nitazikabidhi kwa wanufaika hao hivi karibuni. Aidha, katika hatua za awali za upatikanaji wa wanufaika wa

**1 NOVEMBA, 2023**

mikopo hiyo, wavuvi wa Ludewa Kata za Manda, Ruhuhu, Lumbila, Lupingu na Ludewa walipatiwa elimu na mafunzo ya uvuvi endelevu na utaratibu, upatikanaji na urejeshaji wa mikopo yaliyofanyika Tarehe 16 - 25 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuwawezesha wavuvi boti za kisasa ambazo zitatolewa kwa wavuvi wa maeneo yeny shughuli za uvuvi hapa nchini ikiwemo Halmashauri ya Ludewa. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, Wizara itaendelea kutoa elimu na mafunzo ya uvuvi endelevu, ujasiriamali katika uvuvi na namna ya kunufaika na fursa za mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha ikiwemo TADB kwa wananchi wa maeneo ya uvuvi ikiwemo Ludewa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nimshukuru Mheshimiwa kwa majibu mazuri, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Kata hizo Nane zina jumla ya wananchi 26,582. Je, kwa idadi hiyo ya boti mbili Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba Serikali inatakiwa iongeze boti?

Swali la pili, wavuvi wa Jimbo lile wana changamoto nyingi na wana maoni mengi ambayo wangetamani wakae na Mheshimiwa Waziri. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kutangulizana na mimi baada ya Bunge hili kwenda kukaa na wavuvi wa Jimbo la Ludewa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ugawaji wa boti lilianza kwa zoezi la awali Mheshimiwa Rais amekwishatoa maelekezo kwamba tuangalie maeneo yote yeny

**1 NOVEMBA, 2023**

uhitaji wa kuongeza boti hizo na tayari tumeshaainisha maeneo ambayo yana umuhimu wa kuongeza boti na sasa Wizara iko tayari kuongeza boti kulingana na mahitaji ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu kuwatembelea, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Kamonga kwa jinsi ambavyo anaafuatilia sana shida za wananchi wake na kuwatatulia, kwa kadri hiyo na sisi Wizara tuko tayari kufika katika eneo lake kwenda kuzungumza na wavuvi hao kuona namna sahihi ya kutatua changamoto wanazopitia wavuvi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha na maswali ya jana ambayo yalibaki tumeyaongezesa leo na tutayaongezesa wiki nzima mpaka yote yapate nafasi ya kuulizwa.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni 21 wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya amba ni viongozi na wataalam kutoka Wizara ya Afya amba ni Dkt. John Jingu - Katibu Mkuu, Dkt. Grace Magembe - Naibu Katibu Mkuu, Profesa Tumain Nagu - Mganga Mkuu wa Serikali, Bernad Konga - Mkurugenzi Mkuu NHIF, Dkt. Beghato Saqware - Kamishina wa Bima amba wameambatana na Watendaji Waandamizi wa Wizara ya Afya, pamoja na taasisi zake, karibuni sana na hongereni kwa kazi nzuri. (*Makofii*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni 48 wa Mheshimiwa Mathayo David - Wajumbe wa Baraza la Wazazi kutoka Wilaya ya Same Mkoa wa Kilimanjaro. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata amba ni walimu wa Sekondari Kyela Mkoa wa Mbeya. (*Makofii*)

## **1 NOVEMBA, 2023**

Mgeni wa Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ambaye ni jamaa yake kutoka Dar es Salaam Ndugu Ally Hassan Illanga. (Makofii)

Mgeni wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhani, Katibu wa CCM Kata ya Merya kutoka Jimbo la Singida Kaskazini Ndugu Abel Isango. (Makofii)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Yustina Rahhi, ndugu zake kutoka Mwanza amba ni Ndugu Yusta Arcadius Rahhi na Ndugu Appolon John Array, karibuni (Makofii)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 20 kutoka TUDARCO Jijini Dar es Salaam na watumishi 27 kutoka Halmashauri ya Mji wa Bariadi, karibuni sana. (Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Sekretariati ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendesha mafunzo kuhusu mfumo wa uwasilishaji tamko kwa njia ya mtandao (*Online Declaration System*) mafunzo haya yatafanyika siku ya Alhamisi tarehe mbili Novemba, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhudhuria mafunzo hayo muhimu ili tupate uelewa wa utendaji kazi wa mfumo huo wa uwasilishaji tamko kwa njia ya mtandao.

Katibu.

**1 NOVEMBA, 2023**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada ya Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa Mwaka 2022**

(Kusomwa Mara ya Pili)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye Muswada sasa namuita Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu. (Makofii)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (Na. 8) wa Mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na shupavu kwa nchi yetu katika Nyanja zote. Sisi katika sekta ya Afya tunajivunia mageuzi makubwa anayofanya Rais Samia katika kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana kwa Watanzania wote bila vikwazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Rais Samia ameendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuboresha huduma za afya ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaatiba vya kisasa vya uchunguzi na kutibu magonjwa, kuongeza bajeti ya dawa na bidhaa nyingine za afya, sambamba na kuimarisha upatikanaji wa wataalam wa afya katika ngazi zote. Hakika jitihada za Rais Samia zinaonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake alizozianzisha mwaka 2018 ambazo zimewezesha nchi yetu kupunguza vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kwa asilimia 35 kutoka vifo 67 hadi vifo 43 kwa kila vizazi hai mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa asilimia 80 kutoka vifo 530 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104 katika kila vizazi hai mwaka 2020. Hakika hii ni rekodi ya kutukuka kwa nchi yetu. Vilevile, tunampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson kwa kuteuliwa kuwa Rais wa 31 wa Mabunge Duniani na Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika. Katika hili, hii ni fahari na heshima kubwa sana kwa nchi yetu, kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi duniani wanayo juu ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupongeze wewe pamoja na Wenyeviti wa Kamati ya Bunge. Kipekee nimpongeze Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo na Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndungulile kwa ushirikiano mzuri ambao walitupatia katika kuitia Muswada huu mbele ya Kamati. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana ya kuchambua Muswada huu kwa umakini, weledi na umahiri mkubwa na kusikiliza na kupokea maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, naomba kutoa chimbuko la kuandaliwa kwa Muswada huu kuwa ni kutimiza wajibu wa Serikali wa Kikatiba wa kuhakikisha wananchi wote wanapata

huduma bora za afya bila vikwazo. Aidha, kuwasilishwa kwa Muswada huu ni utekelezaji wa maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 83 (e) inayotaka kuimariswa kwa Mfumo wa Bima ya Afya nchini ili kufikia lengo la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya kwa Wote ni sehemu ya kufikia malengo ya Huduma za Afya kwa Wote (*Universal Health Coverage*). Dhana ya huduma za afya kwa wote imejengeka katika Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la Mwaka 1948; Katiba ya Shirika la Afya Duniani na kuwekewa viwango vya Kimataifa katika Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Na. 102 wa mwaka 1952 pamoja na pendekozo Na. 202 kuhusu Hifadhi ya Jamii la Mwaka 2012. Pia, Azimio la Alma-Ata la Mwaka 1978 (*Alma-Ata Declaration of 1978*) ambalo limeeleza wazi kwamba, upatikanaji wa huduma za afya ya msingi na zenyе ubora ni haki ya kila mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya huduma za afya kwa wote imejengeka katika nguzo kuu tatu ambazo ni:-

- (i) Uwezo wa kuwafikishia wananchi huduma za afya;
- (ii) Upatikanaji wa huduma bora za afya; na
- (iii) Mfumo madhubuti wa ugharamiaji wa huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, naomba tuwe na utulivu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, toka uhuru Serikali za awamu zote zimewekeza katika sekta ya afya kwa kiasi kikubwa ili kuwezesha wananchi wengi kuzifikia huduma za afya, ambapo sasa huduma zinapatikana kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za halmashauri, hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za rufaa za kanda, hospitali maalum na Hospitali ya Taifa. Kutokana na

uwekezaji huo, upatikanaji wa huduma za afya nchini umeendelea kuimarika katika ngazi zote za msingi, kati na huduma za kibingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa ugharamiaji huduma za afya ulianza na Sera ya Serikali ya Huduma bila Malipo mwaka 1960 hadi mwaka 1990 ambapo utaratibu wa wananchi kuchangia huduma za afya ulianza kutumika. Utaratibu huu ulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na wananchi wengi kukosa huduma za afya kutokana na kukosa fedha za kugharamia matibabu papo kwa papo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utaratibu huu unawaingiza wananchi wengi hususan wasio na uwezo katika umaskini kutokana na gharama kubwa za matibabu. Kutokana na changamoto hizo, kuanzia miaka 2000 Serikali ilianzisha utaratibu wa bima ya afya kwa Mifuko ya Bima ya Afya ya Umma na kampuni binafsi za bima ya afya. Hata hivyo, bado wananchi wengi takribani asilimia 85 wapo nje ya utaratibu huu wa bima ya afya kutokana na uhiari wa kuijunga na bima za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa hadi Septemba, 2023 ni asilimia 15.3 tu ya Watanzania wote ndio wapo katika Mfumo wa Bima ya Afya (*NHIF 8%; CHF 6%, NSSF-SHIB 0.3% na Bima Binafsi 1%*). Hivyo, Muswada ninaouwasilisha mbele yako, unalenga kuimarisha mfumo wa ugharamiaji huduma za afya kupitia Bima ya Afya kwa Wote ili kufikia lengo la huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya awali, sasa naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022. Kwanza, lengo la kutungwa kwa sheria inayopendekezwa ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote kupitia Mfumo wa Bima ya Afya na kuweka mfumo wa ushiriki katika skimu za bima za afya kwa raia na wakazi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu unaopendekezwa utamwezesha mwananchi kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi anapozihitaji huduma hizo kwa kuwa ugonjwa hauji kwa kutoa taarifa kusema nitaumwa kesho au kesho kutwa, lakini tunaamini utaratibu wa bima ya afya utawawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika za maendeleo na hivyo kuwaepusha kuingia katika janga la umaskini, maradhi zaidi, ulemavu wa kudumu pamoja na vifo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tisa. Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambapo kuna Kifungu cha 1, Kifungu cha 2, 3 na cha 4. Katika utangulizi Kifungu hiki kimempa Waziri mamlaka ya kubainisha tarehe za kuanza kutumika kwa vifungu mbalimbali vyatya sheria hii. Kifungu cha 2 kinaainisha mipaka ya matumizi ya sheria hii, na Kifungu cha 3 kinaweka masharti kuhusu tafsiri ya misamiati

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza Kifungu cha 3 kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa na kuongeza misamiati kama tulivyobainisha katika aya C ya jedwali la marekebisho. Kifungu cha 4 kimeainisha malengo ya sheria hii ambayo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote. Lengo la kifungu hiki ni kuweka misingi ya kuzingatiwa wakati wa usimamizi na utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili inaweka masharti kuhusu Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote. Kifungu cha 5 kinaweka wajibu wa ushiriki wa kila mtu katika Mfumo wa Bima ya Afya. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa lengo la kuhakikisha kila mtu anajiunga na Bima ya Afya kama inavyoainishwa katika aya D ya jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 6 kinapendekeza kuanzisha Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo makundi mbalimbali yatajumuishwa na kushiriki katika Skimu za Bima ya Afya. Makundi hayo ni pamoja na waajiri, watumishi wa umma,

wafanyakazi walioajiriwa katika sekta rasmi binafsi, waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi na wananchi wasio na uwezo. Washiriki wengine katika Mfumo wa Bima ya Afya nchini ni Skimu za Bima ya Afya, vituo vya kutolea huduma za afya na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (*Tanzania Insurance Regulatory Agency*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7 kinaainisha majukumu ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania katika kudhibiti na kusimamia Mfumo wa Bima ya Afya. Kifungu hiki tunapendekeza tusianzishe mamlaka nyingine ya kusimamia bima ya afya bali tutumie Mamlaka ya Usimamizi wa Bima ya Afya ndiyo iwe mamlaka ya kusimamia pia bima ya afya. Mamlaka hii tumeonyesha mambo ambayo itakuwa na wajibu wa kuyafanya. Pia tumependekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki katika aya E ya jedwali la marekebisho, tumeonesha maeneo ambayo tunapendekeza kufanya marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu inaweka masharti kuhusiana na Skimu za Bima ya Afya. Kifungu cha 8 kinatambua uwepo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kama Skimu ya Bima ya Afya ya Umma. Kifungu hiki kimempa mamlaka Waziri kuboresha Skimu ya Bima ya Afya ya Umma. Lengo la kifungu hiki ni kuendelea kuboresha huduma za bima ya afya katika Skimu ya Bima ya Afya ya Umma kwa kuzingatia matokeo ya tafiti na tathmini mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9 kinaweka utaratibu wa kampuni binafsi kusajiliwa kama Skimu za Bima ya Afya Binafsi baada ya kutimiza vigezo na masharti. Madhumuni ya Kifungu hiki ni kuwawezesha wananchi kuwa na uhuru wa kuchagua aina ya skimu ambazo watapenda ziwahudumie na kupanua wigo wa uwepo wa skimu za bima ya afya. Kupitia kifungu hiki, wananchi watachagua kujunga na bima ya afya ya umma au bima ya afya binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 10 kama inavyoonekana katika aya F ya jedwali la marekebisho. Kifungu cha 11 kinaweka katazo la uendeshaji wa Skimu za Bima ya Afya bila kusajiliwa. Kifungu cha 12 kinaipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima jukumu la kutunza rejestra ya Skimu za Bima ya Afya zilizosajiliwa chini ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 kinaweka utaratibu ambaao Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itaifuata ikiwa inataka kufuta usajili wa Skimu ya Bima ya Afya na hatua zitakazochukuliwa iwapo skimu ya bima ya afya itataka kujiondoa katika utoaji wa huduma za bima ya afya. Aidha, Serikali katika aya G ya jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa kuongeza utaratibu wa kuzingatiwa kabla ya skimu ya bima kufutiwa usajili kwa lengo la kulinda masilahi ya mwanachama na watoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne inaweka masharti kuhusu vitita vya mafao. Kifungu hiki cha 14 kinaweka ulazima kwa Skimu za Bima ya Afya kutoa kitita cha mafao ya huduma muhimu (*Standard Benefit Package*) kwa wanufaika. Maana yake kampuni za bima za afya za umma na binafsi zinazotaka kutoa mafao ya bima ya afya watapaswa kuzingatia kitita cha mafao ya huduma muhimu. Pia, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kama ilivyobainishwa katika aya ya kwanza ya jedwali la marekebisho. Lengo la Kifungu hiki ni kuhakikisha kila mwanachama anapata huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa usawa na kutoa fursa ya upatikanaji wa huduma za ziada pale ambapo mwanachama atahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumependekeza kufuta kifungu cha 15 kama tulivoonesha katika aya J ya jedwali la marekebisho na kukiandika upya kwa kuainisha huduma za afya zilizojumuishwa katika kitita cha mafao ya huduma muhimu. Hata hivyo, Waziri anayo mamlaka ya kufanya marekebisho ya kitita hicho kwa

kuzingatia matokeo ya tathmini na uendelevu wa Skimu za Bima ya Afya

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Wote na kwa kutambua uzoefu na uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*), Serikali inapenda kufanya marekebisho kama inavyobainishwa katika aya K ya jedwali la marekebisho kwa kuanzisha Kitita cha Bima ya Afya cha Jamii (*Community Health Insurance Package – CHIP*) ikiwa ni mpango mbadala wa Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*). Lengo la kufanya mabadiili kaya ni kuhakikisha wananchi wote wanajumuishwa katika utaratibu wa bima ya afya ili kupata huduma bora za afya pasipo vikwazo wanavyokutana navyo sasa kuitia utaratibu wa *CHF*. Vikwazo hivyo ni pamoja na:-

- (i) Wananchi chini ya *CHF* kutopata huduma za afya wanapokuwa nje ya maeneo yao waliyojiandikisha, yaani katika halmashauri zao na mikoa yao. Sasa hivi Bima ya *CHIP* endapo itapitishwa na Bunge lako tukufu, mwananchi mwenye *CHF* atawezekana kupata huduma za afya popote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Haitaishia katika halmashauri yake, haitaishia katika mkoa wake, atapata huduma zote muhimu katika vituo vyote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
- (ii) *CHF* inatoa wigo mdogo wa kuchangiana kati ya mikoa na halmashauri zenyewe uchumi mkubwa na mdogo, wananchi wenye kipato kikubwa na kidogo na wagonjwa na wasio wagonjwa kutokana na kusimamiwa katika ngazi za halmashauri;
- (iii) Bima ya *CHF* inatoa ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao na kukosekana kwa huduma muhimu, kwa mfano huduma za afya ya kinywa na meno, kutojumuishwa kwa baadhi ya dawa na hivyo kumlazimu mwanachama kulipia.

- (iv) Muundo wa CHF haukidhi misingi na kanuni za uendeshaji wa bima ya afya mathalan kutotenganisha kwa majukumu kati ya mnunuzi na mtoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16 kinaweka utaratibu wa utoaji wa kitita cha mafao ya ziada kama itakavyoainishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima. Pia tumeomba tufanye marekebisho katika kifungu cha 17 kama tulivyoonyesha katika aya M na aya N ya jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada huu inaweka masharti kuhusu uanachama na uchangiaji katika Skimu za Bima ya Afya. Kifungu cha 18 kinaainisha watu wanaopaswa kujejunga na Skimu za Bima ya Afya na kuweka wajibu wa kila mtu kujejunga. Katika kifungu cha 20 tumebainisha utaratibu wa usajili wa wanachama ambapo waajiri katika sekta za umma na binafsi watatakiwa kuwasajili waajiriwa wao ndani ya siku 30 toka kuanza kwa mkataba wa ajira. Kila mtu katika sekta rasmi na isiyo rasmi atatakiwa kujejunga na Skimu ya Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 21 kinaweka viwango vya uchangiaji kwa wanachama kutoka sekta ya umma, sekta rasmi binafsi na isiyo rasmi. Tunapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu hiki kwa kubainisha kwamba mchango wa asilimia sita wa mshahara utakuwa ni kwa ajili ya mwajiri wa sekta ya umma na mwajiri wa sekta binafsi atakayeamua kusajili wanachama wake katika bima ya afya ya umma, lakini sekta binafsi hawalazimishwi kusajili waajiriwa wao katika mfuko wa umma. Kwa hiyo, wanaweza wakasajili katika mifumo binafsi na watazingatia sheria zinashughulikia au zinazosimamia vitita vya sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumeweza kupokea ushauri wa sekta binafsi, tusiwalazimishe kuchangia asilimia sita ya mishahara yao na ya watumishi wao kuchangia bima ya afya. Kwa hiyo, watachagua wenyewe utaratibu utakaowapendeza. Sharti ni kuwa na bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kifungu cha 22 kinaweka utaratibu wa kutambua na kusajili kundi la watu wasio na uwezo kwa lengo la kuhakikisha wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu hiki kama inavyobainishwa katika aya P ya jedwali la marekebisho. Ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa watu wasio na uwezo, Serikali inapendekeza kuanzisha mfuko wenyewe lengo la kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mfuko utaweza kutumika kugharamia huduma za matibabu kwa magonjwa sugu na magonjwa ya muda mrefu kama vile saratani na magonjwa ya figo na huduma za dharura zitokanazo na ajali kama inavyobainishwa katika aya Q. Tumepokea malalamiko mengi kuhusu watu wenyewe changamoto za magonjwa ya figo, magonjwa ya saratani na hivyo kushindwa kupata huduma za matibabu kwa sababu ya kukosa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia ni sikivu imewasiliza Watanzania. Kwa hiyo sambamba na kugharamia wasio na uwezo, pia tutagharamia sehemu ya matibabu kwa magonjwa sugu na magonjwa ya muda mrefu kama saratani na magonjwa ya figo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale ambapo palitukwamisha mwanzoni, vyanzo vya Mfuko huu kipekee kabla sijashukuru niseme, vyanzo vya Mfuko huu kutokana na maamuzi ya Waziri wa Fedha ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye carbon (carbonated drinks), vinywaji vikali (*liquor*), bidhaa za vipodozi (cosmetic products), kodi ya michezo ya kubahatisha, ada ya bima za vyombo vya moto na mapato yatokanayo na ushuru wa miamala ya electronic (electronic transaction levy) kwa kadiri

itakavyompendeza, kadiri itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo hivi siyo vipya lakini Waziri wa Fedha amekuwa msikivu kwa kuamua kutoa sehemu ya mapato yanayotokana na vyanzo hivi kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo. Pia fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko na zawadi na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa misaada tayari kwa mfano tunao wadau wetu wanaolipia bima za afya kwa wanawake wajawazito katika mikoa ya Mtwara, Tanga na Mbeya. Kwa hiyo, tunaamini wadau wa maendeleo watatuunga mkono kulipia bima za afya kwa watu wasio na uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuhakikisha kuwa watu wasio na uwezo wanapata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha. Hakika, historia ya Tanzania, historia ya dunia itamkumbuka Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kufuta utaratibu wa misamaha ambayo kwa uhalisia wananchi hawapati misamaha, ipo kwenye karatasi lakini akienda hospitali hakuna dawa, hakuna vipimo. Kwa mara ya kwanza Rais Dkt. Samia anaweka historia na msingi wa kuhakikisha Watanzania wasio na uwezo takribani milioni 15.8 sawa na kaya milioni 3.6 watapewa Bima ya Afya bila malipo ili kuweza kumudu gharama za matibabu. (Makofi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee tunaishukuru pia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kuweka msisitizo wa umuhimu wa kuwa na mfuko wa kugharamia Bima ya Afya kwa wasio na uwezo. Tunashukuru Bunge, kwa kweli na nyie

mliweka msukumo mkubwa wa kuhakikisha tunakuwa na vyanzo mahususi na siyo maneno ya kwenye makaratasi ya kuhakikisha tunalipia Bima za Afya kwa watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali tutalisimamia kikamilifu suala hili kuhakikisha kwanza tunawatambua watu wasio na uwezo na pa kuanzia tunapo, kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi (*Household Budget Survey – HBS*) wa mwaka 2017/2018. Zinaonyesha kuwa 26.4% ya watu wote Tanzania ni wananchi wasio na uwezo na ndiyo wale milioni 15.8 lakini kuna wasio na uwezo zaidi ambao wanaishi katika absolute tunasema umasikini uliokithiri ni milioni nne; kwa hiyo, hawa pia tutawapa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 23 kinaweka sharti kwa skimu za Bima ya Afya kuweka na kutunza amana lakini pia tumependekeza kufanya marekebisho kama inayoonekana kwenye aya (r) ya jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya sita, inaweka masharti kuhusu udhibiti ubora wa huduma. Kifungu cha 26 kina lengo la kuhakikisha skimu za Bima ya Afya zinazingatia ubora katika utoaji huduma. Kifungu cha 27 kinaipa wizara jukumu la kuhakikisha ubora wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya saba ya Muswada huu inaweka masharti mengineyo kwa namna moja au nyingine. Kifungu cha 28 kinaitaka kila skimu ya Bima ya Afya ya Umma na Binafsi kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wake kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote itakavyoelekezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima. Kifungu cha 29 kinaruhusu skimu za bima ya afya za umma na binafsi kufanya uwekezaji kwa lengo la kukuza mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa haki za wanufaika na watoa huduma katika mfumo wa Bima ya Afya

zinalindwa, kifungu cha 31 kinaweka utaratibu wa namna ambavyo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itakavyoshughulikia malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine kubwa, Serikali ni sikivu. Tumepokea maoni na ushauri wa wadau mbalimbali pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, kuhusu kufungamanisha Bima ya Afya na huduma muhimu mbalimbali za kijamii. Serikali yenu sikivu imesikia na imekubali maoni na ushauri wa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia aya (w) ya jedwali la marekebisho tunapendekeza kukifuta kifungu cha 32 kilichokuwa kinafungamanisha huduma mbalimbali za kijamii na Bima ya Afya. Huduma zilizokuwa zimefungamanishwa ni pamoja na leseni ya udereva, bima za vyombo vyta moto, VISA za kuingilia nchini, utambulisho wa mlipakodi, usajili wa laini za simu, hati za kusafiria, uandikishaji wa wanafunzi kidato cha tano na kidato cha sita na utoaji wa Kitambulisho cha Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia maoni na ushauri wa Wabunge na Watanzania. Sisi kama Serikali tutajikita katika kutoa elimu na hamasa kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa Bima ya Afya ili kuhakikisha wananchi wengi wanajunga na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuwaepusha wananchi kuingia katika umasikini, maradhi zaidi au ulemavu wa kudumu. Tunayo mifano iliyo hai ya wananchi ambao walilazimika kuuza mali zao ikiwemo mashamba yao, mifugo yao, vyombo vyta usafiri, vifaa vyta ndani, magodoro, vitanda na kuweka rehani mali zao ili kugharamia matibabu yao au ya wapendwa wao. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo sambamba na kuwa tumeridhia kutofungamanisha Bima ya Afya na huduma mbalimbali za kijamii, bado tunaona ni muhimu kila mtu kuwa na Bima ya Afya lakini tutawekeza zaidi katika elimu na hamasa kwa jamii. Kifungu

cha 33 kinampa mamlaka Waziri ya kutunga kanuni kwa masuala mbalimbali kwa lengo la kutekeleza Sheria inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tumeondoa kutofungamanisha lakini sheria lazima iwe na sanctions. Sasa ili tusifungamanishe lakini pia ionekane Bima ya Afya ni lazima, tunapendekeza katika jedwali la marekebisho kufanya marekebisho kwa kuweka adhabu ndogo ya 10% ya mchango wa kila mwaka kwa mtu yeyote ambaye hatajiunga na Bima ya Afya kwa kipindi cha miaka mitatu tangu Sheria ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Waziri mwenye mamlaka ya Afya amepewa mamlaka ya kutoa msamaha wa ulipaji wa adhabu ya 10% kwa kuzingatia maslahi ya umma au sababu nyiningine yoyote. Kama nilivyosema tutawekeza zaidi kwenye elimu na hamasa kwa jamii. Lakini pia tutajitahidi kuboresha huduma za afya ili wananchi wengi waweze kuvutiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 35 kinaweka utaratibu wa kushughulikia madai ya skimu za Bima ya Afya ambapo Mahakama ndiyo ina uwezo wa kuamuru ulipwaji wa fidia lakini pia tumepokea maoni na ushauri kuhakikisha pia tunatoa adhabu, utaratibu wa uwajibishwaji wa chombo hodhi pamoja na watendaji kwa makosa yatakayofanywa chini ya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, tunaainisha masharti kuhusu Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii CHF ambayo kama nilivyosema tunaianzisha upya chini ya Sheria hii, tumebainisha katika aya (b, d) ya jedwali la marekebisho na ababu za kubadilisha au kuobresha (CHF) tayari nimezitaja. Sheria hii inapendekeza kuwepo kwa masharti kuhusiana na kipindi cha mpito kisichozidi miaka 12 tangu kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inabainisha Sheria mbalimbali zitakazofanyiwa marekebisho baada ya Muswada huu kupita. Tumezitaja kwa mfano ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima

ya Afya, Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sheria ya Mtoto, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria ya Udhibiti wa Hospitali Binafsi na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulitokea pia maoni na ushauri kuhusu mapendelekezo ya Muswada huu kufuta fao la matibabu liliokuwa linatolewa na NSSF kupitia SHIB. Baada ya kufanya uchambuzi, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya kutofuta fao hili kwa sababu tumeona fao hili la NSSF linaweza kuendelea kama fao la afya na siyo fao la bima ya afya; kwa hiyo linaendelea kutumika kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio mambo makubwa ambayo nimeyaeleza katika Muswada, naomba Muswada ambao nimeuwasilisha usomwe sambamba na jedwali la marekebisho liliotolewa na Serikali ili kuzingatia maoni na ushauri wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza; viyi kama Serikali tumejipanga ili kuhakikisha kwamba Sheria hii inaanza kutumika? Kwanza kama nilivyosema tutaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu dhana na umuhimu wa Bima ya Afya. Tumeandaa mkakati wa utoaji wa elimu utakaokuwa na jumbe mahususi, tutashirikisha wadau mbalimbali, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini pamoja na viongozi katika ngazi zote. Elimu itatolewa kabla na wakati wa utekelezaji wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa huduma za afya. Tunaamini kabisa huduma bora za afya ndizo zitakazovutia wananchi wengi kuijunga na skimu mbalimbali za Bima ya Afya. Kwa kutambua hilo, Serikali itaendelea kuhakikisha tunaboresha huduma za afya katika ngazi zote na kwa mfano ikiwemo ujenzi wa vituo vya kutoa huduma za afya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu, tumeongeza vituo vya kutoa huduma za afya kutoka 8,449 mwaka 2019 hadi kufikia vituo 11,630 mwezi Septemba, 2023 sawa

na ongezeko la vituo 3,181. Kazi ya kujenga vituo vya afya ni kazi endelevu, itaendelea. Tunatambua bado kuna vijiji havina zahanati, bado kuna baadhi ya kata hazina vituo vya afya; kwa hiyo, kazi hii itaendelea ya kuboresha. Tutaendelea kuboresha upatikanaji wa dawa; kwa mfano dawa muhimu upatikanaji wake umeimarika kutoka 62% mwezi Agosti, 2022 hadi 73% Agosti, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunamshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kufanya uwekezaji mkubwa katika vifaatiba vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa ikiwemo x-ray 199, CT scan 30 ambazo tumezisambaza katika mikoa yote ya Tanzania bara na zimeanza kufanya kazi kasoro mikoa miwili (Songwe na Mkoa wa Mara).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumeweza kuweka *MRI machine* katika Hospitali za Rufaa za kanda, vifaatiba vingine ikiwemo *Ultrasound* katika ngazi ya hospitali za halmashauri na vituo vya afya. Tumeendelea kuajiri au kuongeza rasilimaliwatu katika Sekta ya Afya. Tumeonyesha watumishi ambao tumewaa jiri; kwa mfano mwaka wa fedha 2021/2022 tumeajiri watumishi zaidi ya 10,000; 2022/2023 watumishi 8,800. Tutaendelea kusomesha watumishi hususani katika fani za ubingwa na ubingwa bobesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendeleza jitihada za kuhakikisha watumishi wa afya wanatoa huduma za afya kwa kuzingatia weledi (*professionalism*) na maadili (*ethics*) ya utoaji huduma za afya. Tutaendelea kuhakikisha tunaimarisha matumizi ya TEHAMA ili kuwezesha sheria hii itekelezwe kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha maelezo yangu kuhusu Muswada huu, naomba kutoa kwa ufupi manufaa ya kutungwa kwa Sheria hii ambayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza; Sheria hii endapo itapitishwa na Bunge Waheshimiwa Wabunge, tutawahakikishia kundi kubwa la

Watanzania kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila ya kikwazo cha fedha. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Waheshimiwa Wabunge, tunaomba mtafakari. Tukipitisha Muswada huu tunaweka msingi wa matibabu bora kwa Watanzania milioni 15.8 wasio na uwezo. Tunaweka msingi na kuandika historia ya matibabu ya uhakika kwa Watanzania wenzetu milioni 15.8. Pia Sheria hii ikipita itaweza kuimarisha uhai, uhimilivu na ustahimilivu wa skimu za Bima ya Afya kwa kuwa sasa hivi Bima ya Afya siyo lazima, matokeo yake wanaojunga wengi kwa uhiari ni wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano wa *Toto Afya Card*, 99% ya watoto waliokuwa wameandikishwa katika utaratibu wa *Toto Afya Card*, watoto 200,000; 99% wanasa jiliwa wakiwa tayari ni wagonjwa; hii siyo Bima ya Afya. Maana ya Bima ya Afya ni kuchangiana wagonjwa na wasio wagonjwa. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, mko watu 100, katika watu 100 wataumwa watu 20, 80 watalipia wenzao. Utaratibu wa Bima ya Afya ya asilimia zaidi ya 90 ni wagonjwa; hiyo siyo Bima ya Afya labda tufikirie kuwa na Mfuko wa Kutibu watoto wagonjwa lakini siyo Bima ya Afya. Kwa hiyo, tunaamini Muswada huu unakwenda pia kutibu kwa sababu sasa itakuwa kila mtu atahimizwa, watoto wote wale wataandikishwa wataweza kuchangiana na kulipiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaimarisha usimamizi na udhibiti wa utoaji huduma za afya kwa sababu tumeamua sasa hivi kuna malalamiko naletewa. *NHIF* anamkata mtoa huduma hospitali anasema hapa umeiba, hapa umetoa, umenikata hela. Waziri wa Afya nina maslahi na *NHIF* tumeona tusianzishe utaratibu mpya, tuitumie *TIRA* (Mamlaka ya Taifa ya Usimamizi wa Bima) kuwa ndiyo mdhibiti wa skimu zote za Bima ya Afya za Serikali na binafsi. Kwa hiyo, kama ni kupelekwa kwenye Baraza la Maamuzi na sisi twende tukajieleze *TIRA* badala ya kuwa na maslahi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, athari tusipopitisha Muswada huu. Wananchi watajiunga kwa hiari tayari wakiwa ni wagonjwa na hivyo kuondoa dhana ya kuchangiana għarama za matibabu lakini tutadhoofisha uhai na uendelevu wa skimu za Bima ya Afya. Kundi kubwa la wananchi kuwa nje ya mfumo wa Bima ya Afya amba ni 85% lakini wananchi wasio na uwezo kushindwa kupata huduma bora za matibabu, wananchi kushindwa kumudu għarama za matibabu kutokana na ongezeko kwa magħoñja yasiyo ja kuambukiza (*non-communicable diseases*), kukosekana kwa udhibit madhubuti wa utoaji huduma katika soko la bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; lakini siyo kwa umuhimu; naomba nisistize kuwa Bima ya Afya ndiyo mfumo bora, rahisi na endelevu amba imethibitika katika nchi mballimbali duniani kuwawezesha wananchi wengi hususani wa kipato cha chini kupata huduma bora za afya pindi wanapozihitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi tunafahamu kuwa pale familia inapokuwa na mgħoñja, basi huuza mali zao ili kupata fedha za kulipia għarama za matibabu. Hata hii changamoto mara Waziri tumezuiwa maiti Muhibbili shilingi milioni nne, shilingi milioni tano hatuna; Sheria hii inakwenda kutatua changamoto ya kuzuiwa maiti katika hospitali zetu. Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote kuijunga na Bima ya Afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ja kuugua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani; nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya kwa uhirikiano mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nawashukuru watumishi wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkoo Dkt. John Jingu amba wamekuwa wakifanya shughuli hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkoo Sera Bunge na Uratibu kwa uratibu na uhirikiano wake katika maandalizi ja Muswada huu. Kipekee

nitambue mchango mkubwa wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wake mkubwa katika kipindi chote cha maandalizi ya Muswada huu, hususan katika kuwezesha upatikanaji wa vyanzo mahususi vya fedha kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee namshukuru Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ndugu Onorius Njole Mwandishi Mkuu wa Sheria na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa wakati wa maandalizi ya Muswada huu. Vilevile, nawashukuru wataalam kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI na wadau wote wa sekta ya afya waliota maoni na mapendekozo yaliyowezesha maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na si kwa umuhimu nitambue taasisi zifuatazo; TASAF, APHTA, TEA, kampuni binafasi za bima ya afya, TIRA, NHIF, NBS na NSSF. Kipekee kukamilika na hadi kufika hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amekuwa ni nguvu na msukumo mkubwa wetu ndani ya Serikali katika kutuongoza na kutusimamia, vilevile utashi wa kisiasa wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan umetuwezesha leo kufikia hatua hii, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaitendea haki endapo sitaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya Mheshimiwa Stansalaus Haroon Nyongo Mbunge wa Maswa na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya. Nikushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kutupa fursa hii ya kuwasilisha Muswada huu. Hakika Bunge la 13 linaenda kuandika historia katika maisha ya Watanzania kuwa na uhakika wa kupata huduma bora za afya, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nachukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kuliomba Bunge lako Tukufu liujadili

**1 NOVEMBA, 2023**

Muswada huu wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa Mwaka 2022 pamoja na marekebisho ambayo tunayapendekeza na hatimaye kuupitisha katika hatua ya kusomwa kwa mara ya tatu na hatimaye sheria inayopendekezwa kuwa sehemu ya sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofij)

**MAELEZO YA MHESHIMIWA UMMY ALLY MWALIMU (MB), WAZIRI WA AFYA AKIWASILISHA MUSWADA WA KUTUNGA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE NA.8 WA MWAKA 2022 KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 01 NOVEMBA 2023 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maelezo kuhusu Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (Na.8) wa Mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na shupavu kwa nchi yetu katika Nyanja zote. Sisi katika sekta ya Afya tunajivunia mageuzi makubwa anayofanya katika kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa watanzania wote bila vikwazo vyovyyote. Vilevile, ameendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuboresha huduma za afya nchini hususani katika ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi na kutibu magonjwa, kuongeza bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa na bidhaa nyingine za afya na kuimarisha upatikanaji wa wataalam wa afya katika ngazi zote. Hakika jithada za Rais Samia zinaonekana katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kipekee tunampongeza **Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa jithada zake alizozianzisha mwaka 2018 ambazo zimewezesha nchi yetu kupunguza Vifo vya Watoto wa umri chini na

miaka mitano kwa asilimia 35 kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2022. Aidha, Vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kwa asilimia 80 kutoka vifo 530 katika kila vizazi hadi 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104 katika kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022. Hakika hii ni rekodi ya kutukuka kwa nchi yetu. Vilevile, nawapongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. Aidha, nichukue fursa hii kumpongeza **Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb)** kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa **Rais wa 31 wa Mabunge Duniani (Inter Parliamentary Union)** na **Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika** kushika wadhifa huo. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi Duniani wanayo juu ya nchi yetu na wewe mwenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, niendelee kukupongeza kwa kuongoza vyema Bunge letu na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Aidha, nawapongeza **Mheshimiwa Naibu Spika** na **Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge** kwa kukusaidia vyema katika kuliendesha Bunge letu. Vilevile, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga Sheria pamoja na kusimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI inayoongozwa na **Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo** - Mwenyekiti wa Kamati, na **Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndungulile** - Makamu

Mwenyekiti, kwa ushirikiano na ushauri mzuri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu mbele ya Kamati hiyo. Kamati hii ilifanya kazi kubwa ya kuchambua Muswada huu kwa makini, weledi na umahiri mkubwa na kusikiliza na kuchambua maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati hiyo na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, naomba kutoa Chimbuko la kuandaliwa kwa Muswada huu wa Bima ya Afya kwa Wote kuwa ni kutimiza wajibu wa Serikali wa Kikatiba wa kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora za afya bila vikwazo. Aidha, kuwasilishwa kwa Muswada huu ni Utekelezaji wa Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 83 (e) inayotaka kuimarishwa kwa mfumo wa Bima ya Afya nchini ili kufikia lengo la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote.

**Mheshimiwa Spika**, Bima ya Afya kwa Wote ni sehemu ya kufikia malengo ya **Huduma za Afya kwa Wote (Universal Health Coverage)**. Dhana ya huduma za afya kwa wote imejengeka katika Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa la mwaka 1948; Katiba ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya mwaka 1948; na kuwekewa viwango vya Kimataifa katika Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Na. 102 wa mwaka 1952 pamoja na pendekezo Na. 202 kuhusu hifadhi ya jamii la mwaka 2012. Pia, Azimio la Alma Ata la mwaka 1978 (Alma-Ata Declaration of 1978) ambalo limeeleza wazi kwamba, upatikanaji wa huduma za afya ya msingi na yenye ubora ni haki ya kila mtu. Dhana ya Huduma za Afya kwa Wote imejengeka katika nguzo kuu tatu ambazo ni; uwezo wa kuwafikishia wananchi huduma za afya, upatikanaji wa huduma bora za afya na mfumo madhubuti wa ugharamiaji wa huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Tangu uhuru Serikali za awamu zote sita zimewekeza katika sekta ya afya kwa kiasi kikubwa ili kuwezesha wananchi wengi kuzifikia huduma za afya ambapo kwa sasa

huduma zinapatikana kuanzia ngazi ya Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya/Halmashauri, Hospital za Rufaa za Mikoa, Hospital za Rufaa za Kanda, Hospital Maalum na Hospitali ya Taifa. Kutokana na uwekezaji huo, upatikanaji wa huduma za afya nchini umeendelea kumeimarika kuanzia ngazi ya msingi, kati na huduma za kibingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuchochaea tiba utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa ugharamiaji huduma za afya ulianza na Sera ya Serikali ya huduma bila malipo mwaka 1960 hadi mwaka 1990 ambapo utaratibu wa wananchi kuchangia huduma za afya ulianza kutumika. Utaratibu huu ulikua na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na wananchi wengi kukosa huduma za afya kutokana na kukosa fedha za kugharamia matibabu papo kwa papo. Aidha utaratibu huu unawaingiza wananchi wengi hususani wasio na uwezo katika umaskini kutokana na gharama kubwa za matibabu. Kutokana na changamoto hizo, kuanzia mwaka 2000 Serikali ilianzisha utaratibu wa bima ya afya kwa Mifuko ya bima ya afya ya Umma na Kampuni binafsi za bima ya afya. Hata hivyo, bado wananchi wengi takribani asilimia 85 wapo nje ya utaratibu huo kutokana na uhiari wa kuijunga na Bima za afya. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia Septemba 2023 ni asilimia 15.3 tu ya wananchi wote ndio wapo katika mfumo wa bima ya afya (NHIF 8%; CHF 6%, NSSF-SHIB 0.3% na Bima Binafsi 1%). Hivyo, Muswada ninaouwasilisha unalenga kuimarisha mfumo wa ugharamiaji huduma za afya kupitia bima ya afya kwa wote ili kufikia lengo la huduma bora za afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu **Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022**. Lengo la kutungwa kwa Sheria inayopendekezwa ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote kupitia mfumo wa bima ya afya na kuweka mfumo wa ushiriki katika skimu za bima ya afya kwa raia na wakazi wote. Utaratibu unaopendekezwa utawezesha mwananchi kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi anapohitaji huduma hizo na

kumwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na hivyo kumuepusha mwananchi kuingia katika janga la umaskini.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa. **Sehemu ya Kwanza** inahusu masharti ya utangulizi ambapo **Kifungu cha Kwanza** kinahusu Jina na kuanza kutumika kwa Sheria. Kifungu hiki kimempa Waziri Mamlaka ya kubainisha tarehe za kuanza kutumika kwa Vifungu mbalimbali vyta Sheria ili kutekeleza mfumo wa Bima ya Afya kwa wote. **Kifungu cha Pili** kinaainisha mipaka ya matumizi ya Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 3** kinaweka masharti kuhusu tafsiri ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Sheria kwa lengo la kuweka maana iliyokusudiwa na kuondoa utata wa tafsiri unaoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii. Aidha, Serikali inapendekeza kifungu hicho kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa na kuongeza misamiati kama inavyobainishwa katika **Aya C** ya Jedwali la Marekebisho. **Kifungu cha 4** kimeainisha Malengo ya Sheria hii ambayo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote. Lengo la kifungu hiki ni kuweka misingi ya kuzingatiwa wakati wa usimamizi na utekelezaji wa Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Pili** inaweka masharti kuhusu Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote. **Kifungu cha 5** kinaweka wajibu wa ushiriki wa kila mtu katika Mfumo wa Bima ya Afya. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa lengo la kuweka ulazima wa kila mtu kuijunga na Bima ya Afya kama inavyoainishwa katika **Aya D** ya Jedwali la Marekebisho. **Kifungu cha 6** kinapendekeza kuanzisha Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo makundi mbalimbali yatajumuishwa na kushiriki katika Skimu za Bima ya Afya. Makundi hayo ni pamoja na Waajiri, Watumishi wa Umma, Wafanyakazi walioajiriwa katika sekta binafsi, waliojiajiri wenyewe katika sekta isiyo rasmi na wananchi wasio na uwezo. Washiriki wengine katika mfumo wa bima ya afya ni skimu za bima ya afya, vituo vyta kutolea huduma za afya na **Mamlaka ya**

**Usimamizi wa Bima Tanzania (Tanzania Insurance Regulatory Agency - TIRA).**

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7** kinaainisha majukumu ya Mamlaka ya

Usimamizi wa Bima Tanzania (Tanzania Insurance Regulatory Authority TIRA) katika kudhibiti na kusimamia mfumo wa bima ya afya nchini. Kwa mujibu wa kifungu hiki, Mamlaka hiyo, pamoja na mambo mengine, itakuwa na wajibu wa kusajili na kudhibiti skimu za bima ya afya; kuhakikisha kuwa kila skimu ya bima ya afya inatoa **kitita cha mafao ya huduma muhimu** (Standard Benefit Package) kwa mujibu wa Sheria hii; na kutoa miongozo kuhusiana na uendeshaji wenye tija na ufanisi wa shughuli za skimu za bima ya afya. Lengo la usimamizi na udhibiti wa bima ya afya ni kuhakikisha ufanisi wa utoaji wa huduma za bima ya afya. Serikali inapendekeza marekebisho katika kifungu hiki kama ilivyoainishwa katika **Aya E** ya Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu** inaweka masharti kuhusiana na skimu za bima ya afya. **Kifungu cha 8** kinatambua uwepo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kama skimu ya bima ya afya ya umma. Aidha, kifungu hiki kimempa mamlaka Waziri kuboresha skimu ya bima ya afya ya umma. Lengo la kifungu hiki ni kuendelea kuboresha huduma za bima ya afya katika skimu ya bima ya afya ya Umma kwa kuzingatia matokeo ya tafiti na tathmini mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9** kinaweka utaratibu wa kampuni binafsi kusajiliwa kama skimu za bima ya afya binafsi baada ya kutimiza vigezo na masharti yatakayoainishwa katika Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria inayopendekezwa. Dhumuni la kifungu hiki ni kuwawezesha wananchi kuwa na uhuru wa kuchagua aina ya Skimu ambazo watapenda zi wahudumie na kupanua wigo wa uwepo wa skimu za bima ya afya ili kuongeza fursa ya ushiriki kwa lengo la kukuza ushindani na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inapendekeza kufutwa kwa **kifungu cha 10** kama inavyoonekana katika **Aya F** ya jedwali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 11** kinaweka katazo la uendeshaji wa skimu za bima ya afya bila kusajiliwa. Lengo ni kuhakikisha kuwa skimu zote za bima ya afya za umma na binafsi nchini zinasajiliwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria inayopendekezwa. **Kifungu cha 12** kinaipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima jukumu la kutunza Rejesta ya Skimu za Bima ya Afya zilizosajiliwa chini ya Sheria inayopendekezwa ili kuwezesha uratibu na usimamizi wa Skimu hizo.

Aidha, **Kifungu cha 13** kinaweka utaratibu ambao Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itaifuata ikiwa inataka kufuta usajili wa skimu ya bima ya afya na hatua zitakazochukuliwa iwapo skimu ya bima ya afya itataka kujiondoa katika utoaji wa huduma za bima ya afya. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha kuwa watoa huduma za bima ya afya wanafuata utaratibu wa kujiondoa au kuondolewa katika shughuli ya utoaji wa huduma za bima ya afya ili kulinda haki na maslahi ya wanachama na watoa huduma za afya. Aidha, Serikali katika **Aya G** ya Jedwali la Marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa kuongeza utaratibu wa kuzingatiwa kabla ya skimu ya bima ya afya kufutiwa usajili kwa lengo la kulinda maslahi ya wanachama na watoa huduma za afya.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne** inaweka masharti kuhusu vitita vya mafao. **Kifungu cha 14** kinaweka ulazima kwa skimu za bima ya afya kutoa kitita cha mafao ya huduma muhimu (Standard Benefit Package) kwa wanufaika. Aidha, kifungu hiki kinatoa fursa kwa wanachama kupata kitita cha mafao ya ziada kinachojumuisha huduma zaidi ya zilizomo katika kitita cha mafao ya huduma muhimu. Lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha kuwa kila mwaniachama anapata huduma za kitita cha mafao ya huduma muhimu kwa usawa, na kutoa fursa ya upatikanaji wa huduma za ziada pale ambapo mwaniachama atahitaji. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kama inavyobainishwa katika **Aya I** ya Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoainishwa katika **Aya J** ya Jedwali la marekebisho, **Kifungu cha 15** kimefutwa na kuandikwa upya kwa kuainisha huduma za afya zilizojumuishwa katika kitita cha mafao ya huduma muhimu. Vilevile, kifungu hiki kinampa Waziri mamlaka ya kufanya marekebisho ya kitita hicho kwa kuzingatia matokeo ya tathmini na uendelevu wa Skimu za bima ya afya. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za afya kwa wanachama wote.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufikia lengo la Bima ya Afya kwa Woe na kwa kutambua uzoefu na uwekezaji uliofanywa na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kama inavyobainishwa katika **Aya K** ya Jedwali la marekebisho kwa **kuanzisha kitita cha bima ya afya cha jamii (Community Health Insurance Package – CHIP)** ikiwa ni mpango mbadala wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ambapo Sheria iliyoanzisha Mfuko huo inapendekezwa kufutwa na kuianzisha upya chini ya sheria hii. Lengo la kuanzishwa kwa kitita hicho ni kuhakikisha wananchi wote wanajumuishwa katika utaratibu wa bima ya afya ili kupata huduma bora za afya pasipo vikwazo wanavyokutana navyo sasa. Vikwazo hivyo ni pamoja na: **(i)** Wananchi kutopata huduma za afya wanapokuwa nje ya maeneo waliyojiandikisha na hivyo kulazimu kulipia huduma za afya kwa utaratibu wa papo kwa papo hali inayoathiri shughuli za kijamii na kiuchumi; **(ii)** Wigo mdogo wa kuchangiana kati ya Mikoa na Halmashauri zenye uchumi mkubwa na mdogo, wananchi wenyewe kipato kikubwa na kidogo na wagonjwa na wasio wagonjwa kutokana na kusimamiwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa; **(iii)** Ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao kinachotolewa na hivyo kukosekana kwa huduma muhimu mathalani huduma za afya ya kinywa na meno, kutojumuishwa kwa baadhi ya dawa na hivyo kumlazimu mwanachama kulipia **(iv)** Muundo wa CHF kutokidhi misingi na kanuni za uendeshaji wa bima ya afya mathalani kutotenganisha kwa majukumu kati ya mnunuzi na mtoa huduma za afya; na **(v)**

Uhiari wa wananchi kujeungu unaosababisha wananchi kujeungu wakiwa wagonjwa.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 16** kinaweka utaratibu wa utoaji wa kitita cha mafao ya ziada kama itakavyoidhinishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima kwa kuzingatia uhitaji. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho kupitia **Aya M** ya Jedwali la marekebisho kwa kufuta **Kifungu cha 17** na maudhui ya kifungu hicho kuwekwa katika kifungu kipyaa kama inavyobainishwa katika **Aya N** ya Jedwali la marekebisho. Lengo la kifungu hiki ni kutoa wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mkataba na skimu za bima ya afya kwa lengo la kuhakikisha wanufaika wanapata huduma kwa utaratibu utakaowekwa.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano** inaweka masharti kuhusu uanachama na uchangiaji katika skimu za bima ya afya. **Kifungu cha 18** kinaainisha watu wanaopaswa kujeungu na skimu za bima ya afya na kuweka wajibu wa kila mtu kujeungu. **Kifungu cha 19** kinabainisha aina na idadi ya watu wanaoweza kujumuishwa katika skimu za bima ya afya kama wategemezi wa mwanachama mchangiaji. **Kifungu cha 20** kinaweka utaratibu wa usajili wa wanachama ambapo waajiri katika sekta za umma na binafsi watatakiwa kuwasajili waajiriwa wao ndani ya siku 30 toka kuanza kwa mkataba wa ajira. Aidha, kila mtu katika sekta rasmi na isiyo rasmi atatakiwa kujeungu na skimu ya bima ya afya kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 21** kinaweka viwango vya uchangiaji kwa wanachama kutoka sekta ya umma, sekta rasmi binafsi na sekta isiyo rasmi. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu hiki kwa kubainisha kuwa mchango wa asilimia sita wa mshahara utakuwa kwa ajili ya mwajiri wa sekta ya umma na mwajiri wa sekta rasmi binafsi atakayechagua kuwasajili waajiriwa wake katika skimu ya bima ya afya ya umma kama ilivyoainishwa katika mapendekezo ya mabadiliko katika **Aya O** ya

Jedwali la marekebisho. **Kwa muktagha wa Sheria hii mshahara wa sekta ya Umma na sekta rasmi binafsi, umetafsiriwa kwa maana sawa na ile inayotumika na mifuko ya hifadhi ya jamii** kwa sekta zote mbili mtawalia. Dhumuni la kifungu hiki ni kuwa na maana zinazofanana na kuhakikisha uwepo wa uwiano katika uchangiaji wa Kitita cha mafao ya Huduma Muhimu. Vilevile, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hiki kwa kutoa uhuru kwa waajiri wa sekta rasmi binafsi kuchagua skimu ya bima ya afya ya umma au binafsi kuwasajili waajiriwa wao.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 22** kinaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa kundi la watu wasio na uwezo kwa lengo la kuhakikisha wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali, ambapo kundi hili litajumuishwa chini ya skimu ya bima ya afya ya Umma kwa namna itakavyoainishwa kwenye kanuni. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu hiki kama inavyobainishwa katika **Aya P** ya Jedwali la marekebisho. Ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa kundi hilo, Serikali inapendekeza kuanzishwa Mfuko wenyewe lengo la kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo. Aidha, Mfuko utaweza kutumika kugharamia huduma za matibabu kwa magonjwa sugu na ya muda mrefu kama vile saratani na magonjwa ya figo na huduma za dharura zitokanazo na ajali kama inavyobainishwa katika **Aya Q. Vyanzo vyatoku huo ni pamoja na sehemu** ya mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kaboni (carbonated drinks), Vinywaji vikali (Liqour), bidhaa za vipodozi (Cosmetic Products), Kodi ya michezo ya kubahatisha, Ada ya bima za vyombo vyatoku huo ni pamoja na sehemu ya mapato yatokanayo na ushuru wa miamala ya kielektroniki (Electronic Transaction Levy) kwa kadri itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, fedha zitakazotengwa na Bunge, mapato yatokanayo na uwekezaji wa mfuko; na zawadi na misaada kutoka kwa wadau mbalimbali.

Kipekee nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati **Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan,**

kwa uwamuzi wake wa kuhakikisha kuwa watu wasio na uwezo wanapata huduma bora za afya bila kikwazo chochote, hakika historia ya Tanzania na Dunia itamkumbuka.

**Mheshimiwa Spika**, Kipekee tunaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI, kwa kuweka msisitizo wa umuhimu wa kuwa na Mfuko kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo. Hili tutalisimamia kikamilifu kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha wananchi wasio na uwezo wanapata huduma bora za afya. Katika kuwatambua watu wasio na uwezo mapendekezo ya Serikali ni kuboresha mifumo ya utambuzi wa watu kwa kutumia Mamlaka zilizopo. Takwimu za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey – HBS) wa mwaka 2017/18 zinaonyesha kuwa asilimia 26.4 ya watu wote Tanzania Bara ni wananchi wasio na uwezo. Kwa kuzingatia utafiti huo asilimia 26.4 ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 (59,851,347) **idadi wa wananchi wasio na uwezo ni 15,800,756** sawa na **kaya 3,637,121**. Aidha wananchi wasio na uwezo na ambao wanaishi katika **umaskini uliokithiri ni 4,044,843** ambao ni asilia 8 sawa na **kaya 1,113,513**.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 23** kinaweka sharti kwa skimu za bima ya afya kuweka na kutunza amana katika Benki Kuu ya Tanzania ambayo itatumika kwa ajili ya kuhakikisha kuwa wanachama waliosajiliwa chini ya skimu husika hawaathiriki endapo skimu hizo zitashindwa kuendelea kutoa huduma kwa wanufaika wake kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, Serikali inawasilisha mapendekezo yaliyoainishwa katika **Aya R** ya Jedwali la Marekebisho yanayobainisha jukumu hili kutekelezwa kupitia Sheria ya Bima, Sura ya 394. **Kifungu cha 24** kinaweka utaratibu wa utambuzi wa wanachama na wanufaika kwa lengo la kupata taarifa zitakazowezesha uhakiki wa wanachama na kudhibiti udanganyifu. **Kifungu cha 25** kinaweka masharti kuhusiana na ukomo wa uanachama ambapo uanachama utafikia ukomo iwapo mwanachama atafariki au ataacha kuchangia katika skimu ya bima ya afya. Hata hivyo, kifungu kinabainisha kuwa wategemezi

wa mwanachama aliyefariki, wataendelea kupata huduma kwa kipindi kitakachobainishwa na Waziri mwenye dhamana katika Kanuni. Dhumuni la kifungu hiki ni kulinda haki za wategemezi wa mwanachama. Vilevile, Serikali inapendekeza kuongeza sababu za ukomo wa uanachama kama ilivyoainishwa katika **Aya S** ya Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita** inaweka masharti kuhusu udhibiti ubora wa huduma zitolewazo na vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya. **Kifungu cha 26** kina lengo la kuhakikisha skimu za bima ya afya zinazingatia ubora katika utoaji wa huduma za bima ya afya kulingana na miongozo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima. **Kifungu cha 27** kinaipa Wizara jukumu la kuhakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba na skimu za bima ya afya za umma na binafsi vinatoa huduma bora za afya kwa wanufaika kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyotolewa na Wizara kama inavyopendekezwa katika **Aya T** ya Jedwali la marekebisho. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha vituo vinatoa huduma bora za afya kwa wananchi kupitia mfumo wa Bima ya Afya.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba** inaweka masharti mengineyo ambayo kwa namna moja au nyingine yatahusika katika utekelezaji wa masharti ya Sheria hii. Kwa kuwa uendeshaji wa skimu utazingatia kanuni za uendeshaji wa bima za afya, **Kifungu cha 28** kinaitaka kila skimu ya bima ya afya ya umma na binafsi kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wake kila baada ya miaka mitatu au wakati wowote itakavyoelekezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima na taarifa ya tathmini kuwasilishwa kwa Mamlaka hiyo pamoja na Waziri. Kifungu hiki kinaipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima uwezo wa kuchukua hatua dhidi ya skimu kutokana na upungufu utakaobainishwa na taarifa ya tathmini ya uhai na uendelevu. Dhumuni la kifungu hiki ni kuhakikisha skimu za bima ya afya zinakuwa na ukwasi na uendelevu wa kutoa huduma kwa wanufaika.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 29** kinaruhusu skimu za bima ya afya za umma na binafsi kufanya uwekezaji kwa lengo la kukuza mtaji na hivyo kuimarisha uhai na uendelevu wake. Aidha, **Kifungu cha 30** kinaipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima jukumu la kutoa miongozo kuhusiana na ukomo wa għarama za uendeshaji wa skimu za bima ya afya ili kuhakikisha skimu hiso zinakuwa na uwezo wa kuijendesha na kusimamia utekelezaji wa majukumu yake bila kuathiri utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wanachama wake.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa haki za wanufaika na watoa huduma katika mfumo wa bima ya afya zinalindwa, **Kifungu cha 31** kinaweka utaratibu wa namna ambavyo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itakavyoshughulikia malalamiko.

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, Serikali, kupertit **Aya W** ya Jedwali la Marekebisho, **inapendekeza kukifuta kifungu cha 32 kilichokuwa kimefungamanisha huduma mbalimbali za kijamii na bima ya afya**. Huduma zilizokwu zimefungamanishwa ni pamoja na leseni ya udereva, bima za vyombo vya moto, viza ya kuingilia nchini, utambulisho wa mlipa kod, Usajili wa Laini za Simu, hati ya kusafiria, uandikishaji wa wanafunzi kidato cha tano na cha sita na utoaji wa kitambulisho cha Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo ni lengo ya Serikali kuwa kila mtu nchini awe na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua. Baada ya Sheria hii kupertishwa, Serikali itaendelea kutoa elimu na hamasa kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya lengo likiwa ni kuwaepusha wananchi kuingia katika umaskini. Tunayo mifano iliyoi hai ya wananchi ambao walilazimika kuza mali zao ikiwemo mashamba, mifugo, vyombo vya usafiri, vifaa vya ndani na kuweka rehani mali zao ili kugharamia matibabu yao au ya wapendwa wao. Aidha Seerikali itaendelea kuboresha huduma za afya katika ngazi zote ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora za afya.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 33** kinampa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni kwa masuala mbalimbali kwa lengo la kutekeleza sheria inayopendekezwa kwa ufanisi. Aidha **Kifungu cha 34** kinaweka katazo kwa wanufaika, vituo vya kutolea huduma za afya na skimu za bima ya afya na mtu yeyote kutoa taarifa za uongo na kuweka adhabu iwapo watathibitika kufanya hivyo. Dhumuni la kifungu hiki ni kulinda uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya kwa kuzuia masuala ya udanganyifu na ubadhirifu wa pesa za wanachama ili kuhakikisha huduma za bima ya afya zinazotolewa zinakidhi vigezo na ni endelevu. Aidha, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu hicho kwa kutenganisha adhabu ya Skimu ya Bima ya afya na vituo vya kutolea huduma za afya, kuongeza kiwango cha kulipa faini, kuongeza sharti la ulipaji wa fidia kwa hasara iliyosababishwa na kuweka adhabu kwa wataalam, kama inavyobainishwa katika **Aya Y** ya Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maoni ya kutokufungamanisha huduma za kijamii na bima ya afya na katika kuhakikisha ulazima wa kuwa na bima ya afya unatekelezwa, Serikali katika **Aya Z** ya Jedwali la marekebisho inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuweka adhabu ya asilimia 10 ya mchango wa kila mwaka kwa mtu yeyote ambaye hatajiunga na bima ya afya kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuanza kutekelezwa kwa Sheria inayopendekezwa. Hata hivyo, Waziri amepewa mamlaka ya kutoa msamaha wa ulipaji wa adhabu ya asilimia 10 kwa kuzingatia maslahi ya umma au sababu nyingine yoyote.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 35** kinaweka utaratibu wa kushughulikia madai ya skimu za bima ya afya ambapo mahakama ina uwezo wa kuamuru ulipwaji wa fidia iwapo kosa litathibitika kutendwa na mwanachama au mtu yoyote. Vilevile, **Kifungu cha 36** kinatoa adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahsusii haijatolewa chini ya Sheria inayopendekezwa. Dhumuni la kifungu hiki ni kuweka utaratibu wa kushughulikia makosa yote ambayo hayajawekewa adhabu mahsusii katika Sheria. Serikali inapendekeza

kufanya marekebisho ya kutenganisha adhabu kati ya mtu binafsi na taasisi kama inavyobainishwa katika **Aya AA** ya Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37** kinaweka utaratibu wa uwajibishwaji wa chombo hodhi pamoja na watendaji kwa makosa yatakayofanywa chini ya Sheria inayopendekezwa kwa lengo la kuweka utii wa Sheria. **Kifungu cha 38** kinaweka ukuu wa Sheria inayopendekezwa na sheria nyingine katika masuala yanayohusu uendeshaji na usimamizi wa mfumo wa bima ya afya nchini. Lengo la kifungu hiki ni kuondoa ukinzani wa sheria baina ya Sheria hii na sheria nyingine yoyote inayohusiana na masuala ya bima ya afya.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane** inaanisha masharti kuhusu Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii, masharti ya mpito na masharti yanayoendelea. **Kifungu cha 39** kinafuta Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii na wanufaika wataendelea kupata huduma kuitia **kitita cha bima ya afya cha Jamii (Community Health Insurance Package – CHIP)** kama inavyobainishwa katika **Aya BB** ya Jedwali la Marekebisho. Kifungu hiki pia kinabainisha masharti yatakayoendelea kutekelezwa baada ya kufutwa kwa Sheria ya Mfuko wa Afya ya Jamii ili kulinda haki za wanufaika wake.

**Mheshimiwa Spika**, sababu kubwa ya kuchukua hatua hii ni Muundo wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kutokidhi misingi na kanuni za uendeshaji wa bima ya afya mathalani, Mfuko wa Afya ya Jamii una wigo mdogo wa kuchangiana kati ya Mikoa na Halmashauri zenyetechu na mkubwa na mdogo, wananchi wenyewe kipato kikubwa na kidogo na wagonjwa na wasio wagonjwa kutokana na kusimamiwa katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa, wanufaika kutoweza kupata huduma za afya nchi nzima isipokuwa katika Halmashauri walizojiandikisha tu.

**Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine ni ufinyu wa huduma katika kitita cha mafao kinachotolewa na hivyo kukosekana kwa huduma muhimu mathalani huduma za afya ya kinywa na meno,

kutojumuishwa kwa baadhi ya dawa na hivyo kumlazimu mwanachama kulipia. Vilevile, wananchi kutopata huduma za afya wanapokuwa nje ya maeneo waliyojiandikisha na hivyo kulazimu kulipia huduma za afya kwa utaratibu wa papo kwa papo hali inayoathiri shughuli za kijamii na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 40** kinaweka masharti kuhusiana na kipindi cha mpito kisichozidi miezi kumi na miwili tangu kuanza kutumika kwa Sheria inayopendekezwa ambapo wadau wote watapaswa kutekeleza masharti ya Sheria hiyo. Vilevile, Kifungu hicho kinampa Waziri mamlaka ya kuongeza kipindi cha ziada cha mpito kisichozidi miezi sita baada ya kipindi cha awali cha mwaka mmoja kupita. Lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha uendelevu wa huduma kwa wanachama walio kwenye skimu mbalimbali na kuwawezesha wadau mbalimbali kufanya maandalizi na kukamilisha taratibu za utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa.

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa** inabainisha Sheria mbalimbali zitakazofanyiwa marekebisho baada ya Muswada huu kupita. Sheria hizo ni Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura ya 395; Sheria ya Hifadhi ya Jamii, Sura ya 135; Sheria ya Bima, Sura ya 394; Sheria ya Mtoto, Sura ya 13; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366; Sheria ya Udhhibit wa Hospitali Binafsi, Sura ya 151; na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii, Sura ya 50.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kutoa ufanuzi kuhusu sababu za kufanya marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Sura ya 50. Marekebisho haya yanalenga kuendelea kutoa fao la matibabu kwa wanufaika wake kama fao la afya na sio bima ya afya.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha Sheria inayopendekezwa inatekelezwa kwa ufanisi Serikali imejipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya. Utoaji wa elimu kwa umma utatekelezwa kuititia Mkakati wa Utoaji wa Elimu kwa Umma unaobainisha jumbe mahususi zinazotakiwa kutolewa, ushirikishaji

wa wadau mbalimbali hususan viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini, pamoja na viongozi katika ngazi ya Taifa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Elimu kwa umma itatolewa kabla na wakati wa utekelezaji wa Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, tunatambua pia kuwa utekelezaji wa Sheria inayopendekezwa na utayari wa wananchi kujunga na Skimu za Bima ya afya unategemea kwa kiasi kikubwa **upatikanaji wa huduma bora za afya** zinazotolewa kwa wananchi wenyе bima ya afya. Hivyo huduma za afya zikiwa bora zitawavutia wananchi wengi kujunga na skimu za bima ya afya. Katika kutambua hilo, Serikali itahakikisha huduma bora za afya zinapatikana katika ngazi zote. Kwa mfano katika kipindi cha takriban miaka mitatu vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo **8,449 mwaka (2019) hadi kufikia vituo 11,630 mwezi Septemba, 2023**, sawa na ongezeko la Vituo 3,181. Vilevile, **upatikanaji wa dawa** katika vituo vya kutolea huduma za afya umeimarika kutoka **asilimia 62 mwezi Agosti, 2022 hadi kufikia asilimia 73 (mwezi Agosti, 2023)**.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha awamu ya sita chini ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhi Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umefanyika uwekezaji mkubwa katika vifaatiba vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa na matibabu ikiwemo **X-rays (199), CT-Scan (30), MRI (4)** ikiwa ni pamoja na **Ujenzi wa Idara ya Wagonjwa wa Dharura (EMD) (111) na Wodi za Wagonjwa Muhtuti (ICU) (73)** hadi katika ngazi ya Hospitali za Halmashauri. Uwepo wa hatua hii katika vituo vya kutolea huduma za afya kumesogeza huduma za kiuchunguzi karibu zaidi na wananchi na kuwapunguzia gharama waliyokuwa wakitumia kufuata huduma hizo katika Hospitali za Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali pia imeendelea kuongeza rasilimali watu katika sekta ya Afya, ambapo Mwaka **2020/2021** iliajiri **watumishi wa afya 3,347, Mwaka 2021/2022** **watumishi 10,285 na mwaka 202/23** **watumishi 8,8277** walijiriwa. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha **Shilingi bilioni tisa (9)** zimetengwa kwa ajili ya

ufadhili wa mafunzo ya Ubingwa na Ubingwa Bobezi kwa watumishi wa Afya wa Serikali. Aidha, tutaendeleza jitihada za kuhakikisha watumishi wa afya wanatoa huduma kwa kuzingatia Weledi na Maadili.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuwezesha utoaji wa huduma bora za bima ya afya kwa wananchi, Serikali pia itaendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA. Ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii, tutazitaka skimu za bima ya afya kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za bima ya afya ikiwemo usajili na utambuzi wa wanachama na vituo vya kutolea huduma za afya na utekelezaji wa majukumu ya skimu hizo. Hatua hii pia itasaidia kudhibiti udanganyifu na vitendo vya ubadhirifu ambapo fedha nyingi hupotea na hivyo kuzifanya skimu za bima ya afya kutokuwa endelevu. Serikali itahakikisha kwamba mfumo wa bima ya afya unasihamiwa ipasavyo, kuitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) ambayo itahakikisha haki na wajibu wa mwanachama, mtoa huduma na skimu za bima ya afya zinatikelezwa kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuhitimisha maelezo yangu kuhusu Muswada huu, naomba kutoa kwa ufupi manufaa ya kutungwa kwa sheria hii ambayo ni pamoja na; **Kundi kubwa la wananchi** kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha; kuimarisha **Uboreshaji wa huduma** katika Vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma na binafsi, ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba; kuimarika kwa **Uhimilivu na ustahimilivu** wa Skimu za bima ya afya kutoa huduma kwa kuwa wananchi watapaswa kuijunga na Skimu za Bima ya Afya kabla ya kuwa ni wagonjwa; **Kuimarika kwa usimamizi na udhibiti** katika utoaji wa huduma za Bima ya Afya zitolewazo na Mifuko na Kampuni Binafsi za Bima ya Afya; **Kuboreshwa kwa vitita vya mafao** vinavyotolewa na skimu za bima ya afya na **Kuimarisha hali ya kipato kwa wananchi**.

**Mheshimiwa Spika**, athari zitakazoendelea kujitokeza endapo Sheria hii haitatungwa ni pamoja na; Wananchi kijiunga kwa hiari na wakiwa tayari ni wagonjwa na hivyo kuondoa dhana ya kuchangiana gharama za matibabu; Kudhoofisha uhai na uendelevu wa skimu za bima ya afya zilizopo; Kundi kubwa la wananchi kuwa nje ya mfumo wa bima ya afya (asilimia 85) hivyo kuwa katika hatari ya umaskini; Wananchi kushindwa kumudu gharama za matibabu kutokana na kuongezeka kwa magonjwa yasiyoambukizwa (NCDs); Kukosekana kwa Udhibiti Madhubuti wa utoaji wa huduma katika soko la bima ya afya na Serikali kushindwa kufikia lengo la Afya Bora kwa Wote.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, naomba nisisitize kuwa, Bima ya Afya ndio mfumo bora, rahisi na endelevu ambao umethibitika katika nchi mbalimbali duniani kuwawezesha wananchi wengi hususani wa kipato cha chini kupata huduma bora za afya pindi wanapozihitaji. Wengi tunafahamu kuwa pale familia inapokuwa na mgonjwa basi huuza mali zao ili kupata fedha za kulipia gharama za matibabu. Nitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote kijiunga na Bima ya Afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua.

### SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana **Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano anaoendelea kunipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu hasa katika kipindi cha maandalizi ya Muswada huu. Aidha, ninawapongeza watumishi wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na **Dkt. John A.K. Jingu**, Katibu Mkuu, **Dkt. Grace E. Magembe**, Naibu Katibu Mkuu na **Prof. Tumaini J. Nagu**, Mganga Mkuu wa Serikali. Kwa mara nyingine tena nimshukuru **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kutuongoza vyema katika mchakato huu, **Mhe. Jenista J. Mhagama (Mb)**, **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)** kwa uratibu na ushirikiano wake katika maandalizi ya Muswada huu.

**1 NOVEMBA, 2023**

Kipekee nitambue mchango wa **Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.)**, Waziri wa Fedha, kwa ushirikiano wake katika kipindi chote cha maandalizi ya muswada huu hususan katika kuwezesha upatikanaji wa vyanzo vya fedha kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo. Kwa namna ya pekee pia ninamshukuru **Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi**, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, **Ndugu Onorius Njole**, Mwandishi Mkuu wa Sheria na watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa wakati wa Maandalizi ya Muswada huu. Vilevile, niwashukuru wataalam kutoka ofisi ya Rais TAMISEMI na Wadau wote wa sekta ya afya waliota ushauri, maoni na mapendeleko yaliyowezesha maandalizi ya Muswada huu.

Mwisho na si kwa umuhimu nitambue taasisi zifuatazo: - **TASAF, APHTA, TEA, Kampuni binafasi za Bima ya Afya, TIRA, NHIF, NBS na NSSF.**

**Mheshimiwa Spika**, naomba nirudie tena kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI. Nimalizie kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Muswada huu na nichukue nafasi hii kuliomba Bunge lako Tukufu liujadili Muswada huu wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (Na.8) wa Mwaka 2022 na kuupitisha katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Tatu na hatimaye Sheria inayopendekezwa kuwa sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Ummy Ally Mwalimu (Mb.)

**WAZIRI WA AFYA**

01 NOVEMBA, 2023

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Si kwa ulichokisema lakini ni kwa namna ulivyo sema, umeweka passion, umeweka utu kwa Watanzania, hongera sana. Waheshimiwa Wabunge kwa Muswada huu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia apewe maua yake. (Makofii)

Kuna wageni 25 wa Mheshimiwa Suma Fyandomo ambao ni Madiwani kutoka sehemu mbalimbali za nchi wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mary Mwamfupe, Diwani wa Viti Maalum Manispaa ya Ubungo. Hawa wamekuja kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, Spika na Rais wa Mabunge ya Duniani na wametoka Arusha, Mwanza, Tanga, Iringa na Dar es Salaam na wanaongozwa na Mheshimiwa Mwamfupe pamoja na Florance Masanja Mkurugenzi, hongereni sana na karibuni Dodoma. (Makofii)

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati muhimu iliyosimamia Muswada huu, Mheshimiwa Nyongo, Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Huduma za Jamii, karibu.

**MHE. STANLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na kabla sijasoma maoni ya Kamati nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuuleta Muswada huu kupitia Serikali yake kwa manufaa ya wananchi, tunashukuru sana. Niendelee kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa usimamizi wake na maelekezo yake ikiwa ni pamoja na kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza sana Kamati yangu kwa jinsi walivyotoa ushirikiano na kusimamia kuhakikisha tunafika hapa na Kamati hii imefanya kazi kubwa. Lakini kipekee niwapongeze na kuwashukuru sana wajumbe wa Kamati iliyopita, Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambao tulianza nao

**1 NOVEMBA, 2023**

kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba Muswada huu unakwenda kusimama na unakuwa na manufaa kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulisomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Nane wa Bunge la 12 (tarehe 23 Septemba, 2022) kwa mujibu wa Kifungu cha 97 (1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020. Baada ya hatua hiyo, Muswada huu ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia misingi ya Kanuni za Bunge, Kamati ilianza kushughulikia Muswada huu katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 17 hadi 21 Oktoba, 2022. Baada ya hatua ya uchambuzi kukamilika, Serikali iliuondoa Muswada huu kabla ya kusomwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mswada huu uliletwa kwa mara nyingine katika Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambapo Kamati iliendelea na vikao vya uchambuzi tarehe 30/01/2023 na tarehe 7 hadi 8/02/2023. Hata hivyo, baada ya hatua ya uchambuzi kukamilika, Serikali iliuondoa Muswada huu kabla ya kusomwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu, umeletwa kwenye Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na kuchambuliwa tarehe 31/10/2023 ili kukamilisha hatua zake muhimu katika Mkutano wa Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Kamati kufanya uchambuzi wa Muswada huu ni kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali kuzingatia ahadi zake kwa wananchi pamoja na misingi ya

uendeshaji wa sekta ya afya nchini kwa namna inayozingatia maendeleo ya ustawi wa jamii na taifa. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linatarajiwa kuupitia Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa namna inayozingatia maslahi ya umma na uhai endelevu wa taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanya kazi Muswada huu, matokeo ya uchambuzi ambayo yanajumuisha maoni na ushauri kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi. Hivyo, taarifa inajumuisha maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kama inavyoonekana katika taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia mbalimbali zilitumika; njia na mbinu zilizotumika. Uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1)(b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Aidha, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, imewekewa misingi inayoitaka Taarifa ya Kamati ioneshe namna jambo lililoripotiwa liliyofanyiwa kazi. Vilevile, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (*reliability*) na ustahiki (*validity*), naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanya kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia zilizotumika kuufanya kazi Muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya taarifa hii, Kwa manufaa ya Bunge lako tukufu naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo: -

- (a) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu Mbunge tarehe 19 Oktoba, 2022. Lengo ni

kupata mantiki ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inayopendekezwa.

- (b) Kufanya mapitio ya Maudhui ya Muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa katika usimamizi wa Bima ya Afya kwa Wote. Madhumuni ni kutathmini kufaa au kutokufaa kwa sheria inayopendekezwa.
- (c) Kuoanisha mapendeleko ya Muswada wa Sheria inayojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za umma chini ya sekta hii. Kusudio ni kuzingatia hali halisi katika kutathmini na mapendeleko yanayotolewa na mtoa hoja.
- (d) Kujadili dhana kuu (*key concept*) ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Lengo ni kujenga mtazamo mpana unaosaidia kuhakiki maudhui ya Muswada kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi; na
- (e) Kupokea na kusikiliza Maoni ya Wadau kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 97(2) pamoja na masharti ya Kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020. Nia ni kuwa na maoni jumuifu kutoka kwa wananchi na kuliwezesha Bunge kuendelea kuzingatia mtazamo wao katika utungaji wa Sheria, Maoni ya Wadau (*Public Hearing*) yaliyopokelewa katika kikao kilichofanyika tarehe 20 Oktoba, 2022.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati pia ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao. Kamati inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliowasilisha maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya uchambuzi wa maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kulisaidia Bunge lako tukufu kutunga sheria yenye manufaa na inayozingatia maslahi ya sekta hii,

Kamati ilitumia mbinu mbalimbali kuuelewa Muswada huu. Naomba kubainisha mbinu hizo kwa kutaja zifuatazo: -

- (a) Kubaini nia ya mapendekezo kwa kusoma jina refu la Muswada na Sheria iliyopendekezwa kutungwa, pamoja na kupitia maelezo ya sababu na madhumuni ya Muswada huu.
- (b) Kupambanua mambo makuu yanayotunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote katika mfumo wa kisheria na usimamizi wa masuala ya Afya.
- (c) Kuainisha nia, mambo yanayopendekezwa kutungwa kwa Kanuni na Sheria zilizopo pamoja na ahadi iliyotolewa kwa wananchi katika llani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; na
- (d) Kupima mapendekezo ya utungaji wa Sheria ya Bima ya Afya katika muono mpana wa Afrika na Dunia kwa ujumla. Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine kufanya uchanganuzi linganifu (*comparative analysis*) kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa na Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa, ambazo uwezo wake umetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi matarajio ya wananchi. Nikiri kuwa njia na mbinu hizo zimeiwezesha Kamati kupata kwa undani wa Sheria inayopendekezwa kufanyika katika mfumo wa kisheria kwenye kusimamia masuala ya bima kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Muswada, maelezo ya awali. Muswada huu umegawanyika katika Sehemu kuu Tisa zenye jumla ya Ibara 74 ambapo unapendekeza kutungwa kwa Sheria Mpya ya Bima ya Afya kwa Wote kwa lengo la kuanzisha

skimu za huduma za afya kwa wananchi ili kuwapatia uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki na kupembua maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Uchambuzi huo ulijumuisha mapitio ya jumla ya maudhui na baadaye upembuzi kwa ibara za Muswada huo ili kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria yanayopendekezwa. Lengo ni kujiridhisha na masuala makuu manne ya uchambuzi, ambayo ni: -

- a) Iwapo kuna mahitaji ya sheria inayopendekezwa.
- b) Iwapo pendekezo katika Muswada huu linaendana na ahadi za mwelekeo wa jumla wa nchi, kanda na dunia.
- c) Iwapo pendekezo linakidhi haja ya sheria iliyobainishwa; na
- d) Iwapo misingi ya utungaji wa sheria imezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, taarifa hii inabainisha uchambuzi katika Sehemu kuu Tisa. Sehemu hizo ni Masharti ya Utangulizi, Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, Skimu ya Bima ya Afya, Vitita vya Mafao, Uanachama na Uchangiaji katika Skimu ya Bima ya Afya na Udhibiti wa Ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilipata ufanuzi kuhusu maudhui ya Muswada wa Sheria na Uchambuzi wa ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vya Sheria inayotungwa. Mtiririko huo unaweza kulisaidia Bunge kufanya uamuzi unaotokana na tatizo au ombwe la sheria inayopendekezwa, utakaotatua au kuziba ombwe ipasavyo na unaozingatia misingi ya utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upembuzi wa Maudhui ya Muswada (*thematic review*). Madhumuni ya kupembua maudhui ya Muswada huu ni kubaini uthabiti wa utungaji wa Sheria inayopendekezwa ili

kulishauri Bunge inavyopaswa. Kwa ujumla utaratibu wa kibunge wa hoja kuwasilishwa, kuungwa mkono, kujadiliwa na kuamuliwa, unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki, upembuzi wa kina na hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio kimaudhui ya Muswada huu ili kulibainishia Bunge mambo yatakayolisaidia kuamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya jumla yanaonesha kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kutungwa ni bima ya afya kwa wote (*Universal Health Insurance*). Msingi wa kutungwa kwa sheria hii ni kuwezesha raia na wakazi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha. Kwa maana hiyo, Muswada huu unahu kutungwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya mwaka 2022 ambapo unaweka mfumo wa usimamizi na udhibiti wa utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya miongozo, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kamati ilichambua Muswada huu kwa muktadha wa ahadi walizopewa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sababu ya kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Kamati ilibaini kwamba, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoongoza Serikali, kiliwaahidi wananchi kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini pamoja na kuhakikisha lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote linafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria hii imeelezwa kuwa ni kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha pindi anapohitaji huduma hizo kuitia mfumo wa bima ya afya. Nia hiyo inaendana na ahadi waliyopewa wananchi kama inavyotolewa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 Ibara ya 9(d)(iv) “Kutoa huduma za afya kwa Wote” na ibara ya 83(e) “Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ikiwemo mifuko ya bima za afya (*NHIF* na *CHF*) ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Afya. Wakati wa uchambuzi wa mapendelekezo ya Serikali, Kamati iliona umuhimu wa kuoanisha Sheria inayopendekezwa kutungwa na mtazamo wa nchi kisera. Hii ni kutokana na ukweli usiopingika kuwa, Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007, imekuwa ndiyo nyenzo kuu ya kimkakati katika suala la kusimamia afya ambapo dira yake inajielekeza katika kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo ya mtu binafsi na hata taifa kwa ujumla. Aidha, imewekwa wazi kuwa madhumuni ya sera hii ni kuinua hali ya afya ya wanachi wote kwa kuweka mfumo wa huduma ya afya utakaokidhi mahitaji ya wananchi na kuongeza umri wa kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Kikanda wa Kimataifa. Sheria inayopendekezwa pia ina lengo la kuendana na mabadiliko ya mifumo ya kikanda kimataifa ambapo imeweka mkazo katika kuhakikisha kunakuwepo na mfumo wa huduma za afya kwa wote, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (*World Health Organisation- WHO*). Mfumo huu wa huduma za afya kwa wote una jukumu la kuwaunganisha watu wote kupata huduma za afya katika hali ya usawa kwa dhumuni la kuwezesha afya bora kwa wananchi na kuongeza uwezo wa kuishi kwa watu wote kama ilivyo katika takwa la *Universal Declaration of Human Right (UDHR)* la haki ya kuishi. Hii inamaanisha kuwa na uwezekano wa kupata huduma za afya kwa wakati na mahali zinapotakiwa bila kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zinaeleza kwamba, watu wanaoishi katika mazingira hatarishi katika nchi zenyе kipato cha chini na cha kati wanakabiliwa na viwango vinavyoongezeka vya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na kuongeza gharama za huduma ya afya. Takwimu za Shirika la Afya Duniani na Benki Kuu za mwaka 2021, zinaeleza kwamba takriban watu milioni 100 bado wanaendelea kusukumwa katika umasikini mkubwa, yaani wanaishi kwa dola 1.9 au chini yake kwa siku kwa sababu ya kulazimika kulipia huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu zaidi ya milioni mia nane ambao ni takriban asilimia 12 ya idadi ya watu ulimwenguni wanatumia angalau asilimia 10 ya mapato yao kwa ajili ya kugharamia matibabu ya kwao binafsi au familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote Wanachama wa Umoja wa Mataifa ziko katika mchakato wa kuhakikisha zinawawezesha wananchi wao kuwa na bima ya afya ambayo inaruhusu kupata huduma ya afya wakati wowote, popote na kwa kila mtu bila kuwa na kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hizo zimekubaliana kufaulisha Mpango wa Afya kwa Wote (*Universal Health Coverage*) itakapofika mwaka 2030 kama sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Namba Tatu yaani *Sustainable Development Goal – Number Three*. Lengo hili linadhadhuria kuhakikisha watu wote wana afya njema na ustawi wa watu wa umri na rika zote. Pia, limeweka msisitizo katika kuwawezesha watu wote kuishi maisha yenye afya bora hatimaye kuongeza umri wa kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba miongozo mbalimbali ya Taifa na Kimataifa inaanishi maudhui ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa kutungwa hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu uzoefu wa nchi zingine. Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ilipitia machapisho mbalimbali yaani *literature review* ya tafiti zilizofanyika kuhusu bima ya afya kwa wote ili kupata uelewa wa ndani kuhusu Nchi za Afrika zinazofanya vizuri katika Bara la Afrika ili kuweza kujifunza kutoka kwao. Mionganini mwa nchi zilizoonekana kufanya vyema katika bima ya afya kwa wote Barani Afrika ni nchi ya Ghana na Rwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hiyo ilipata nafasi ya kujifunza namna nchi zingine hususan Ghana, Rwanda na Misri zinavyotekeliza mfumo wa bima ya afya kwa wote, ikijumuisha

mafanikio na changamoto na namna nchi hizo zinavyokabiliana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa nchi ya Ghana; katika ziara yake nchini Ghana Kamati ililenga kujifunza mambo makuu manne kama ifuatavyo: -

- (i) Utaratibu wa kuwatambua na kusajili wanachama katika mpango wa Bima ya Afya kwa Wote;
- (ii) Upatikanaji wa Fedha na ulipaji wa rasilimali fedha katika Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote;
- (iii) Mchakato wa kuhakiki madai ya watoa huduma za Bima ya Afya kwa Wote; na
- (iv) Wajibu wa Serikali katika Mpango wa kuwa na Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuweka dodoso hizo ni kutaka kujenga msingi wa kuiwezesha Kamati kupata uzoefu na uelewa wa kina kuhusu utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, mafanikio na changamoto, hivyo kuliwezesha Bunge kutunga sheria itakayokuwa bora zaidi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Nchi ya Ghana, fedha kwa ajili ya Bima ya Afya kwa wote hupatikana kwa njia kuu tano ambazo ni, ruzuku ya kiasi cha asilimia 2.5 ya kodi ya ongezeko la thamani yaani VAT inayotokana na bidhaa zinazoingizwa au kuuzwa ndani ya nchi; Michango ya wanachama walioajiriwa na wasioajiriwa; Mapato yatokanayo na ukataji wa bima za ajali yaani Road Accident Fund na faida inayotokana na uwekezaji wa mapato yanayopatikana na misaada kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utambuzi wa kaya masikini, Ghana wanatumia taasisi ya *Livelihood Empowerment*

Against Poverty (LEAP) ambayo tafsiri yake kwa Kiswahili kisicho rasmi ni Uwezeshwaji wa Kimaisha Dhidi ya Umaskini. Kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na mambo ya Afya, skimu hii ina ofisi katika matawi yote 172 katika wilaya 172 na ofisi katika mikoa yote 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi ya Ghana ina aina mbili za Wanachama ambao ni; wanachama waajiriwa na wanachama wasioajiriwa. Walioajiriwa hutambuliwa, husajiliwa na kuchangishwa kutokana na ajira zao. Aidha, walioko nje ya ajira hutambuliwa kwa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Bima ya Afya nchini humo na taasisi mbalimbali za Serikali kutoka katika ngazi ya Serikali za Mitaa hadi kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Nchi ya Ghana imefanikiwa kuanzisha skimu za Bima ya Afya kwa wote, imekutana na ugumu wa kutekeleza mpango huu kwa ufanisi kwa kutegemea michango ya wanachama peke yake. Aidha, hadi kufikia Mwaka 2021 ni asilima 56 tu ya wananchi wa Ghana waliojiunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Uzoefu wa Nchi ya Rwanda tumeuona, Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakapitia wakuona. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kidogo katika historia ya Bima ya Afya hapa Tanzania. Mheshimiwa Waziri ameeleza na sisi katika Kamati tunatambua kabla ya uhuru, huduma za afya nchini zilikuwa zinatolewa zaidi kwenye maeneo ya shughuli za kiuchumi kama mijji na mashamba makubwa. Baada ya uhuru, Serikali iliweka msukumo zaidi katika kupanua huduma za afya ili kuwafikia wananchi wengi hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma hii, Serikali iliweka mfumo wa rufaa wa huduma za afya. Kwa mfumo huu, Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa, Maalum, Kanda na Taifa zilianzishwa. Aidha, Serikali ilihamasisha na kuwezesha hospitali za Mashirika ya Kidini kushirikiana nayo kutoa huduma kwa wananchi. Kipaumbele kilikuwa katika utoaji wa huduma za tiba zaidi kuliko kinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi chote hicho hadi miaka ya 1990, huduma za afya zilitolewa bila malipo. Hii ilichagizwa zaidi na falsafa ya Azimio la Arusha la Mwaka 1967 iliyoweka msingi wa usawa wa huduma zote za kijamii. Sera ya Afya, 2007 ambayo imeandikwa na Bwana Kumburu mwaka 2015. Kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, Mwaka 1993, Serikali ilianzisha mabadiliko katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuanzisha sera inayotaka kuwashirikisha wananchi katika kuchangia ghamama za huduma za afya na utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Afya ya Mwaka 1993, Bunge lilitunga Sheria ya uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya yaani NHIF Namba Nane ya Mwaka 1999. Awali Mfuko huu ulilenga kuwanufaisha watumishi wa umma pekee, lakini baadaye Kanuni za uendeshaji wa mfuko ziliboreshwaa na kuruhusu uandikishwaji wa wanachama kutoka kwa watu binafsi na sekta binafsi. Katika Mfuko huu watumishi wa umma walikuwa wakilipa mchango wa lazima yaani asilimia tatu ya mshahara wa mwanachama kwa mwezi. Kwa ujumla hadi sasa Tanzania ina skimu mbalimbali ambazo zimeorodheshwa katika taarifa hii ikiwemo TIKA, NHIF, CHF na TIRA.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Sheria hii; Sheria inayopendekezwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutungwa kwa Sheria hii kutawezesha: -

- (i) Wananchi wote yaani raia na wasio raia wanaoishi nchini kufaidika na utoaji wa huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya mahali popote nchini bila kuwa na kikwazo cha fedha;
- (ii) Kuongeza kiwango cha kuishi yaani *life expectancy* kwa kuweka masharti yatakayowezesha utolewaji wa huduma bora na udhibiti wa uendeshaji wa mfuko, kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa wote; na

- (iii) Kuchochaea ushindani wa uanzishwaji na uendeshaji wa skimu za huduma za afya kwa wote kwa kuweka masharti ya kupanua wigo wa huduma mbalimbali za afya kwa kutumia mfumo wa bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya uchambuzi kwa kila Ibara. Mheshimiwa Waziri ameleeza kwa maana ya sehemu ya kwanza tumefanya uchambuzi na tunashukuru sana Serikali imekuwa siku sana. Namshukuru sana Waziri wa Afya na Waziri wa Fedha kwa kutoa ushirikiano kwa kila Ibara. Waheshimiwa Wabunge mtapitia na kwenye lile jedwali la marekebisho tumeeleeza. Tumekwenda katika Sehemu ya Kwanza tumefanya marekebisho, tumekwenda Ibara ya 3 tumefanya marekebisho, tumekwenda Sehemu ya Pili ya Muswada ambapo tumefanya marekebisho mbalimbali. Sehemu ya Tatu tumefanya marekebisho, Sehemu ya Nne ya Muswada tumefanya marekebisho ikiwemo Ibara ya 15 na Sehemu ya Tano tumefanya marekebisho ambayo yalikuwa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hii ya 5 inahusu wanachama na uchangiaji katika skimu ya Bima ya Afya. Ibara ya 22 inaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa kundi la watu wasiokuwa na uwezo kwa lengo la kuhakikisha wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha. Kamati ilitaka kujiridhisha ikiwa Serikali ina vyanzo mahsus na vya uhakika vya fedha kwa ajili ya kugharamia watu wasiokuwa na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandika upya Kifungu hiki na kuanisha vyanzo vya mapato kama inavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho na Mheshimiwa Waziri amevitaja vyanzo hivyo. Kamati pia imeonyesha uthibitisho wa vyanzo vya kugharamia Mfuko huo kutoka Serikalini. Hivyo, Kamati inasisitiza Mfuko huu ulindwe kwa kuwekewa utaratibu mzuri wa usimamizi ili uweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 inahusu uwekaji wa amana kwa Skimu ya Bima, sawa na kiasi kinachotosha kutoa huduma kwa kipindi cha miaka miwili, kabla ya kusajiliwa. Kamati imetathmini na kuona kuwa kiwango cha amana kitajwe kwenye Sheria na kiwe kiasi cha wastani ambacho hakitakwamisha uendeshaji wa skimu za Bima ya Afya. Kiwango hicho kiwe ni asilimia ya mtaji kutokana na tathmini ya ukwasi na uendelevu wa skimu. Lengo ni kuviweka wazi viwango hivyo na kuondoa uwezekano wa kudhoofisha na kupunguza uwezo wa skimu kujiedesha kwani fedha hiyo ni sehemu ya mtaji ambayo itakuwa haitumiki. Serikali imekubali kufanya marekebisho ya Ibara hii kwa kuihusisha na Sheria ya Bima ambapo dhamana ni asilimia ya mtaji uliolipiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya marekebisho mengi na ambayo kwa kweli yataendelea kuja katika lile jedwali la marekebisho. Naomba sasa kwa sababu ya muda niende kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni ya jumla na mapendekezo mahsusini ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa Sheria hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua kuandaa na kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa wote wa mwaka 2022, ambao kimsingi unalenga kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha kwa kupitia mfumo wa bima ya afya. Huu ni msingi mzuri wa kuhakikisha kwamba raia wote wanakuwa na afya njema kwani wataweza kupata matibabu kwa wakati pale watakapohitaji na hivyo kujenga Taifa la watu wenye afya njema na wenye mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya mtu mmoja mmoja na hata taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika kuhusu maoni na mapendekezo mahsus. Pamoja na uchambuzi na marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada huu, Kamati inaisisitiza Serikali katika mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la fedha, Serikali ina dhamira ya kutambua na kugharamia huduma za Bima ya Afya kwa watu wasio na uwezo kama ilivyo katika Ibara ya 22 ya Muswada huu. Awali, Kamati inashauri Serikali kuanzisha Mfuko Maalum yaani *Equity Fund* ambao utakuwa na vyanzo mahsus vya fedha na vyenye uhakika ambavyo vitaainishwa kwenye Sheria hii kama ilivyo katika Sheria zingine, mfano, Sheria ya Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (*REA*) Na. 8 ya Mwaka 2005 na Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Sura 272 ya mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa Serikali imeridhia kuanzisha Mfuko kwa ajili ya kugharamia Bima ya Afya kwa watu wasio na uwezo na kuthibitisha vyanzo vya Mfuko huo kama itakavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. Kamati inasisitiza Serikali kubainisha utaratibu wa uendeshaji wa Mfuko huo ili kuulinda na uweze kuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vitita vya mafao, Serikali imeboresha vitita kwa kuongeza kitita kingine chenye gharama ya chini ambacho ni kitita cha Bima ya Afya ya Jamii. Hata hivyo, Kamati bado inaona upo umuhimu wa kuongeza kitita kingine chenye gharama za kati ili kumpatia mwananchi machaguzi zaidi au kuchagua kitita anachoona kinamfaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipindi cha msamaha (*grace period*); Kamati inaona ipo haja ya kuwa na kipindi cha msamaha yaani (*grace period*) cha miezi mitatu kutoka kuisha kwa kitita pale mchangiaji anapofariki. Hii ni kwa ajili ya kumpa mjane au mgane au mtegemezi aliyebakia nafasi ya kulipia malipo ya bima kwa mwaka unaofuata au kujisajili na mfumo wa watu wasio na uwezo kutohana na madhara ya kifo cha mchangiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti wa kina (*actuarial study*). Kamati inaona kuwa ni muhimu kufanyika kwa utafiti wa kina (*actuarial study*) mahsus i kwa ajili ya Bima ya Afya kwa wote kwani itasaidia mambo mbalimbali ya msingi kama vile kubainisha viwango vya uchangiaji wa bima na kiasi cha fedha zitakazohitajika kwa ajili ya watu wasiokuwa na uwezo; Uboreshaji wa huduma za afya ili kufanikisha malengo mapana ya sheria hii; Serikali kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vingi zaidi katika maeneo yenye upungufu wa vituo vya afya; Kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na kuongeza watumishi wa kada ya afya. Aidha, kuhakikisha watumishi wa afya wanazingatia maadili ya kazi yao. Haitakuwa vema watu wanakwenda kutibiwa kwa bima, halafu wanakuta lugha mbovu ya watumishi wa sekta ya afya. (Makofsi)

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa umma; Serikali iweke juhudini katika kutoa elimu bora mara kwa mara kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuijunga na skimu za Bima ya Afya, utaratibu wa ugharamiaji wa huduma za afya kwa kutumia Bima ya Afya na upatikanaji wa huduma mbalimbali za afya kwa raia aliyejiunga na Bima ya Afya. Hii itasaidia kuondoa upotoshaji katika jamii na kuelewa umuhimu wa mfumo mzima wa Bima ya Afya, jambo ambalo litasababisha wananchi wengi kuijunga na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati, lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Naibu Waziri kwa ushirikiano wanaotupa katika Kamati yetu. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Grace Maghembe; Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu; pamoja na

**1 NOVEMBA, 2023**

watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia wakati tunapambana na jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Ndugulile ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri wanaonipa. Naomba majina haya yaingie kwenye Hansard, nilitamani niyataje lakini nawashukuru sana Wajumbe hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc na kwa kipekee Sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa shughuli hii. Hawa Makatibu wamekesha hata leo hawajalala wakiendelea kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote (Na.8) wa mwaka 2022 pamoja na marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofij)

1 NOVEMBA, 2023

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA  
YA UKIMWI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA  
WOTE WA MWAKA 2022 KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

[Yanawasilishwa kwa Mujibu wa Kanuni ya 99 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu ulisomwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Nane wa Bunge la 12, tarehe 23 Septemba, 2022 kwa mujibu wa Kifungu cha 97 (1) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Baada ya hatua hiyo, Muswada huu ulipelekwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa mujibu wa Kanuni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia misingi ya Kanuni za Bunge, Kamati ilianza kushughulikia Muswada huu katika vikao vilivyofanyika kuanzia tarehe 17 hadi 21, Oktoba 2022. Baada ya hatua ya uchambuzi kukamilika, Serikali iliuondoa Muswada huu kabla ya kusomwa kwa mara ya pili.

**Mheshimiwa Spika**, Mswada huu uliletwa kwa mara nyingine katika Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambapo Kamati iliendelea na vikao vya uchambuzi tarehe 30/01/2023 na tarehe 7 hadi 8/02/2023. Hata hivyo, baada ya hatua ya uchambuzi

kukamilika, Serikali iliuondoa Muswada huu kabla kabla ya kusomwa kwa mara ya pili.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu, umeletwa kwenye Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI na kuchambuliwa tarehe 31/10/2023 ili kukamilisha hatua zake muhimu katika Mkutano wa Kumi na Tatu.

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya Kamati kufanya Uchambuzi wa Muswada huu ni kuliwezesha Bunge kuishauri Serikali kuzingatia ahadi zake kwa wananchi pamoja na misingi ya uendeshaji wa Sekta ya Afya nchini kwa namna inayozingatia maendeleo ya ustawi wa jamii na taifa. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi linatarajiwa kupitia Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa namna inayozingatia maslahi ya umma na uhai endelevu wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inalijulisha Bunge kuhusu jambo lililofanyiwa kazi na Kamati, njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu, matokeo ya uchambuzi ambayo yanajumuisha maoni na ushauri kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufanya maamuzi. Hivyo, taarifa inajumuisha Maoni na Ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kama inavyoonekana katika Taarifa iliyowekwa mezani mapema leo hii.

## 1.2 Njia na Mbinu zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Miswada ya Sheria ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Aidha, Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka msingi unaotaka Taarifa ya Kamati ioneshe namna jambo linaloripotiwa lilivyofanyiwa kazi. Vilevile, ili kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (*reliability*) na ustahiki (*validity*), naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kuufanyia kazi Muswada huu.

### 1.2.1 Njia zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, njia zilizotumika kufanya kazi Muswada huu zimechangia kufanikisha uchambuzi na hatimaye maandalizi ya Taarifa hii. Kwa manufaa ya Bunge lako Tukufu naomba kuzitaja njia zilizotumika na madhumuni ya kila moja kama ifuatavyo:-

- (a) Kupokea maelezo ya mtoa hoja kuhusu mapendekezo ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb) tarehe 19 Oktoba, 2022. Lengo ni kupata mantiki ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote inayopendekezwa;
- (b) Kufanya mapitio ya Maudhui ya Muswada na kubaini mambo yanayopendekezwa katika usimamizi wa Bima ya Afya kwa Wote. Madhumuni ni kutathmini kufaa au kutokekfaa kwa Sheria inayopendekezwa;
- (c) Kuoanisha mapendekezo ya Muswada wa Sheria inayojadiliwa na miongozo mingine katika shughuli za umma chini ya sekta hii. Kusudio ni kuzingatia hali halisi katika kutathmini mapendekezo yaliyotolewa na mtoa hoja.
- (d) Kujadili dhana kuu (*key concept*) ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Lengo ni kujenga mtazamo mpana unaosaidia kuhakiki maudhui ya Muswada kwa kulinganisha na matarajio ya wananchi; na
- (e) Kupokea na kusikiliza Maoni ya Wadau kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 97(2) pamoja na masharti ya Kanuni ya 136(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Nia ni kuwa na maoni jumuifu kutoka kwa wananchi na kuliwezesha Bunge kuendelea kuzingatia mtazamo wao katika utungaji wa Sheria. Maoni ya Wadau (*Public Hearing*) yalipokelewa katika kikao kilichofanyika tarehe 20 Oktoba, 2022. Aidha, Kamati pia ilipokea na kujadili maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa njia ya mtandao.

Kamati inatoa shukrani za dhati kwa wadau wote waliowasilisha maoni yao, ambayo kwa kiasi kikubwa yameongeza mawanda ya uchambuzi wa maudhui ya Muswada huu.

### 1.2.2 Mbinu zilizotumika

**Mheshimiwa Spika**, ili kuweza kulisaidia Bunge lako tukufu kutunga Sheria yenye manufaa na inayozingatia maslahi ya sekta hii, Kamati ilitumia mbinu mbalimbali kuuelewa Muswada huu. Naomba kubainisha mbinu hizo kwa kutaja zifuatazo:-

- (a) Kubaini nia ya mapendekezo kwa kusoma Jina Refu la Muswada na Sheria inayopendekezwa kutungwa, pamoja na kupitia maelezo ya sababu na madhumuni ya Muswada huu;
- (b) Kupambanua mambo makuu yanayotunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote katika mfumo wa kisheria na usimamizi wa masuala ya Afya;
- (c) Kuoanisha nia, mambo yanayopendekezwa kutungwa kwa Kanuni na Sheria zilizopo pamoja na ahadi iliyotolewa kwa wananchi katika llani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020; na
- (d) Kupima mapendekezo ya utungaji wa Sheria ya Bima ya Afya katika muono mpana wa Afrika na Dunia ujumla. Kamati ilifanya rejea katika nyaraka mbalimbali pamoja na uzoefu katika nchi nyingine ili kufanya uchanganuzi linganifu (*comparative analysis*) kwa lengo la kuboresha masharti yanayopendekezwa na Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitumia njia na mbinu zilizobainishwa, ambazo uwezo wake umetoa manufaa ya uchambuzi unaoliwezesha Bunge kukidhi matarajio ya wananchi. Nikiri kuwa njia na mbinu hizo zimeiwezesha Kamati kupata kwa undani wa Sheria inayopendekezwa kufanyika katika mfumo wa kisheria Kwenye usimamizi wa masuala ya Bima ya Afya kwa wote.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

#### 2.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tisa (9) zenyе jumla ya Ibara Sabini na Nne (74), ambapo unapendekeza kutungwa kwa Sheria Mpya ya Bima ya Afya kwa Wote kwa lengo la kuanzisha skimu za huduma za afya kwa wananchi ili kuwapatia uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ulifanyiwa uchambuzi kwa kuhakiki na kupembua maudhui, masharti, mpangilio na dhamira kwa ujumla. Uchambuzi huo ulijumuisha mapitio ya jumla ya maudhui na baadaye upembuzi wa Ibara za Muswada huo ili kupata picha halisi ya maudhui na msingi wa masharti ya Sheria yanayopendekezwa. Lengo ni kujiridhisha na masuala makuu manne ya kiuchambuzi, ambayo ni:

- (a) Iwapo kuna mahitaji ya sheria inayopendekezwa;
- (b) Iwapo pendeleko katika Muswada huu linaendana na ahadi na mwelekeo wa jumla wa nchi, kanda na dunia;
- (c) Iwapo pendeleko linakidhi haja ya sheria iliyobainishwa; na
- (d) Iwapo misingi ya utungaji wa sheria imezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kubaini mambo hayo, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika sehemu kuu Tisa. Sehemu hizo ni: Masharti ya Utangulizi, Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, Skimu ya Bima ya Afya, Vitita vya Mafao, Uanachama na uchangiaji katika Skimu ya Bima ya Afya na Udhibiti wa Ubora. Aidha, Kamati ilipata ufanuzi kuhusu maudhui ya Muswada wa Sheria na

Uchambuzi wa Ibara za Muswada ikilinganishwa na vifungu vyatia Sheria inayotungwa. Mtiririko huo unaweza kulisaidia Bunge kufanya uamuzi unaotokana na tatizo au ombwe la sheria inayopendekezwa, unaotatua au kuziba ombwe ipasavyo na unaozingatia misingi ya utungaji wa sheria.

## **2.2 Upembuzi wa Maudhui ya Muswada (*thematic review*)**

**Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya kupembua maudhui ya Muswada huu ni kubaini uthabiti wa utungaji wa Sheria inayopendekezwa ili kulishauri Bunge inavyopaswa. Kwa ujumla utaratibu wa kibunge wa hoja kuwasilishwa, kuungwa mkono, kujadiliwa na kuamuliwa, unahitaji misingi inayofanikisha uhakiki na upembuzi wa kina wa hoja inayojadiliwa. Kwa sababu hiyo, Kamati imefanya mapitio ya kimaudhui ya Muswada huu ili kulibainishia Bunge mambo yatakayolisaidia kuamua.

Mapitio ya jumla yanaonesha kuwa dhana kuu katika sheria inayopendekezwa kutungwa ni Bima ya Afya kwa Wote (*Universal Health Insurance*). Msingi wa kutungwa kwa Sheria hii ni kuwezesha raia na wakazi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha. Kwa maana hiyo, Muswada huu unahu kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2022 ambapo unaweka mfumo wa usimamizi na udhibiti wa utoaji wa huduma za bima ya afya kwa wote.

## **2.3 Mapitio ya Miongozo**

**Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM).** Kamati ilichambua Muswada huu kwa muktadha wa ahadi walizopewa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Sababu ya kufanya hivyo ni kupima kama matarajio ya Wananchi yanazingatiwa katika Muswada huu. Kamati ilibaini kwamba, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoongoza Serikali, kiliwaahidi wananchi kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini pamoja na kuhakikisha lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi

wote linafikiwa. Nia ya mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria hii imeelezwa kuwa ni kuweka utaratibu utakaowezesha mwananchi kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha pindi anapohitaji huduma hizo kuitia mfumo wa bima ya afya. Nia hiyo inaendana na ahadi waliyopewa wananchi kama inavyotolewa katika llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020 Ibara ya 9 D (iv) "**Kutoa huduma za afya kwa Wote**" na Ibara ya 83(e) "**Kuimarisha mfumo wa bima ya afya nchini ikiwemo mifuko ya bima za afya (NHIF na CHF) ili kufikia lengo la Serikali la kuwa na bima ya afya kwa wananchi wote**".

**Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Afya.** Wakati wa uchambuzi wa mapendekezo ya Serikali, Kamati iliona umuhimu wa kuoanisha Sheria inayopendekezwa kutungwa na mtazamo wa nchi kisera. Hii ni kutohana na ukweli usiopingika kuwa, Sera ya Taifa ya Afya ya Mwaka 2007, imekuwa ndiyo nyenzo kuu ya kimkakati katika suala la usimamizi wa afya ambapo dira yake inajielekeza katika kuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo ya mtu binafsi na hata taifa kwa ujumla. Aidha, imewekwa wazi kuwa madhumuni ya sera hii ni kuinua hali ya afya ya wanachi wote kwa kuweka mfumo wa huduma za afya utakaokidhi mahitaji ya wananchi na kuongeza umri wa kuishi.

**Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Kikanda na Kimataifa.** Sheria inayopendekezwa pia ina lengo la kuendana na mabadiliko ya mifumo ya kikanda na kimataifa ambayo imeweka mkazo katika kuhakikisha kunakuwapo na mfumo wa huduma za afya kwa wote. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (*World Health Organisation- WHO*), mfumo wa huduma za afya kwa wote una jukumu la kuwaunganisha watu wote kupata huduma za afya katika hali ya usawa kwa dhumuni la kuwezesha afya bora kwa wananchi na kuongeza uwezo wa kuishi kwa watu wote (kama ilivyo katika takwa la *Universal Declaration of Human Right – UDHR* la haki ya kuishi). Hii inamaanisha kuwa na uwezekano wa kupata huduma za afya kwa wakati na mahali zinapotakiwa bila kikwazo cha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa zinaeleza kwamba, idadi ya watu wanaoishi katika mazingira hatarishi katika nchi zenyenye kipato cha chini na cha kati wanakabiliwa na viwango vinavyoongezeka vya magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na kuongeza gharama za huduma ya afya. Takwimu za Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia za mwaka 2021, zinaeleza kwamba takriban watu milioni mia moja (milioni 100) bado wanaendelea kusukumwa katika umasikini mkubwa yaani wanaishi kwa dola 1.90 au chini yake kwa siku kwasababu ya kulazimika kulipia huduma za afya. Watu zaidi ya milioni mia nane (milioni 800) ambao ni takriban asilimia kumi na mbili (12%) ya idadi ya watu ulimwenguni wanatumia angalau asilimia kumi (10%) ya mapato yao kwa ajili ya kugharamia matibabu ya kwao binafsi au familia.

**Mheshimiwa Spika**, nchi zote wanachama wa Umoja wa Mataifa ziko katika mchakato wa kuhakikisha zinawawezesha wananchi wao kuwa na bima ya afya ambayo inaruhusu kupata huduma ya afya wakati wowote, popote na kwa kila mtu bila kuwa na kikwazo cha fedha. Nchi hizo zimekubaliana kufaulisha mpango wa afya kwa wote (*Universal Health Coverage-UHC*) kufikia mwaka 2030 kama sehemu ya Malengo ya Maendeleo Endelevu Namba Tatu, (*Sustainable Development Goals – SDGs Three*). Lengo hili limedhamiria kuhakikisha watu wote wana afya njema na ustawi wa watu wa umri na rika zote, na pia limeweka msisitizo katika kuwawezesha watu wote kuishi maisha yenye afya bora hatimaye kuongeza umri wa kuishi.

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba miongozo mbalimbali ya Taifa na Kimataifa inaakisi maudhui ya Muswada wa Sheria inayopendekezwa kutungwa.

## 2.4 Uzoefu wa Nchi zingine

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Huduma na Maendeleo ilipitia machapisho mbalimbali (*literature review*) ya tafiti zilizofanyika kuhusu bima ya afya kwa wote ili kupata uelewa wa ndani kuhusu

nchi za Afrika zinazofanya vizuri katika Bara la Afrika ili kuweza kujifunza kutoka kwao. Miongoni mwa nchi zilizoonekana kufanya vyema katika bima ya afya kwa wote Bara la Afrika ni Ghana na Rwanda.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hiyo ilipata nafasi ya kujifunza namna nchi zingine hususan Ghana, Rwanda na Misri zinavyotekeleza mfumo wa bima ya afya kwa wote, ikijumuisha mafanikio na changamoto na namna nchi hizo zinavyokabiliana na changamoto hizo.

#### **2.4.1 Uzoefu wa nchi ya Ghana**

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara yake nchini Ghana Kamati ililenga kujifunza mambo makuu manne kama ifuatavyo:-

- i) Utaratibu wa kuwatambua na kusajili wanachama katika mpango wa Bima ya Afya kwa wote;
- ii) Upatikanaji wa Fedha na ulipaji wa rasilimali fedha katika Mpango wa Bima ya Afya kwa wote;
- iii) Mchakato wa kuhakiki madai ya watoa huduma za Bima ya Afya kwa wote; na
- iv) Wajibu wa Serikali katika Mpango wa kuwa na Bima ya Afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kuweka dodoso hizo ni kutaka kujenga msingi wa kuiwezesha Kamati kupata uzoefu na uelewa wa kina kuhusu utekelezaji wa bima ya afya kwa wote, mafanikio na changamoto, hivyo kuliwezesha Bunge kutunga sheria itakayokuwa bora Zaidi kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, katika nchi ya Ghana fedha kwa ajili ya bima ya afya kwa wote hupatikana kwa njia kuu tano ambazo ni, ruzuku ya

kiasi cha asilimia **2.5** ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) inayotokana na bidhaa zinazoingizwa au kuuzwa ndani ya nchi; michango ya wanachama walioajiriwa na wasio ajiriwa; mapato yatokanayo na ukataji wa bima za ajali (*Road Accident Fund*); na faida inayotokana na uwekezaji wa mapato yanayopatikana na misaada kutoka kwa watu na taasisi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utambuzi wa kaya masikini, Ghana wanatumia taasisi ya *Livelyhood Empowerment Against Poverty (LEAP)* ambayo tafsiri yake kwa Kiswahili kisicho rasmi ni Uwezeshwaji wa Kimaisha Dhidi ya Umasikini; kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana na mambo ya Afya. Skimu hii ina ofisi katika matawi yote 172 katika wilaya 172 na ofisi katika mikoa yote 76.

**Mheshimiwa Spika**, nchi ya Ghana ina aina mbili za wanachama ambao ni; wanachama waajiriwa na wanachama wasioajiriwa. Walioajiriwa hutambuliwa, husajiliwa na kuchangishwa kutokana na ajira zao. Aidha, walioko nje ya ajira hutambuliwa kwa ushirikiano kati ya Mamlaka ya Bima ya Afya nchini humo (*National Health Insurance Authority*) na taasisi mbalimbali za Serikali kutoka katika ngazi ya Serikali za mitaa hadi kitaifa. Vilevile, Ghana imanzisha Mfuko mmoja wa umma ambao unatoa huduma za Bima, kudhibiti ubora wa huduma, kupanga bei ya huduma, kudhibiti bima binafsi za afya, kusimamia kampuni binafsi zinazotoa huduma za bima ya afya na kutatua migogoro. Aidha, kwa nchi ya Ghana vitita vya mafao hupangwa na skimu kwa kuzingatia malengo ambapo hutofautiana kulingana na mahitaji ya soko.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba nchi ya Ghana imefanikiwa kuanzisha skimu za bima ya afya kwa wote, imekutana na ugumu wa kutekeleza Mpango huu kwa ufanisi kwa kutegemea michango ya wanachama peke yake. Aidha, hadi kufikia Mwaka 2021 ni asilima 56 tu ya wananchi wa Ghana waliojunga na Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote.

## 2.4.2 Uzoefu wa Nchi ya Rwanda

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwengine, nchi ya Rwanda ni mionganoni mwa nchi ambayo imefanikiwa katika mpango wa bima ya afya kwa wote. Hivyo, baada ya kupitia tafiti mbalimbali za nchi hiyo Kamati Huduma na Maendeleo ya Jamii iliona ni vema kutembelea nchini Rwanda ili kujifunza zaidi kuhusiana na mafanikio pamoja na changamoto inazopitia katika utekelezaji wa bima ya afya kwa wote. Shauku hii imechochewa na hasa baada ya kuona kuwa nchini Rwanda huduma za afya zimeongezeka kutoka **asilimia 35** mwaka 2000 hadi kufikia **asilimia 90.7** mwaka 2015, baada ya kuanzishwa kwa bima ya afya kwa wote.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipotembelea nchini Rwanda ilikuwa na hadidu za rejea takriban 20 zilizotaka kujua uanzishwaji, uimairishwaji, uendelezaji na usimamizi wa skimu za bima ya afya pamoja na huduma ili kuiwezesha Kamati kutoa maoni stahiki na kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutunga Sheria bora ya Bima ya Afya kwa Wote.

**Mheshimiwa Spika**, vyanzo vya fedha nchini Rwanda vinatokana na; michango ya wanachama; (waajiriwa, ikiwa ni pamoja na watumishi wa umma; na wasio waajiriwa); ruzuku ya Serikali (Serikali hutenga Dola za Kimarekani milioni sita, sawa na Shilingi za Tanzania bilioni 14.4); pamoja na fedha kutokana na makato ya huduma mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Rwanda ina aina tano za skimu ambazo ni; Skimu ya Mfuko wa bima ya Afya ya Jamii (*Community Based Health Insurance - CBHI*); Skimu ya Afya kwa ajili ya watumishi wa sekta ya umma na sekta rasmi binafsi (RAMA); Skimu ya Vikosi vya Jeshi; Skimu za bima ya afya za binafsi (*Commercial Health Insurance*); na Mifuko Maalum ya Bima ya Afya. Skimu zote hizo zimewekewa utaratibu wa vyanzo vyake vya fedha kwenye sheria.

**Mheshimiwa Spika**, nchini Rwanda utambuzi wa wananchi wasio na uwezo unafanyika katika ngazi za vijiji kwa kushirikiana na Local Organization Development Agency (LODA)

**Mheshimiwa Spika**, kwa uzoefu huo, Sheria ya Tanzania, pamoja na mambo mengine inatarajiwa kubainisha utaratibu wa upatikanaji wa fedha, ruzuku kutoka Serikalini, kuwa na mfuko maalum (*equity fund*), pamoja na namna ya kuwatambua wasio na uwezo.

## 2.5 Historia ya Bima ya Afya Nchini Tanzania

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uhuru, huduma za afya nchini zilikuwa zinatolewa zaidi kwenye maeneo ya shughuli za kiuchumi kama miji na mashamba makubwa. Baada ya uhuru, Serikali iliweka msukumo zaidi katika kupanua huduma za afya ili kuwafikia wananchi wengi hasa walioko vijijini. Ili kufanikisha azma hii, Serikali iliweka mfumo wa rufaa wa huduma za afya. Kwa mfumo huu, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za mikoa, maalum, kanda na taifa zilianzishwa. Aidha, Serikali ilihamasisha na kuwezesha hospitali za mashirika ya kidini kushirikiana nayo kutoa huduma kwa wananchi. Kipaumbele kilikuwa katika utoaji wa huduma za tiba zaidi kuliko kinga.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi chote hicho hadi miaka ya 1990, huduma za afya zilitolewa bila malipo. Hii ilichagizwa zaidi na falsafa ya **Azimio la Arusha (Arusha Declaration Philosophy)** la mwaka 1967 iliyoweka msingi wa usawa wa huduma zote za kijamii (Sera ya Afya, 2007; Kumburu, 2015). Kutokana na hali mbaya ya kiuchumi, mwaka 1993 Serikali ilianzisha mabadiliko katika sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuanzisha Sera inayotaka kuwashirikisha wananchi katika kuchangia gharama za huduma za afya na utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha na kuimarisha utekelezaji wa sera ya Afya ya Mwaka 1993, Bunge lilitunga Sheria ya uanzishwaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*National Health Insurance Fund*)

Namba Nane ya Mwaka 1999. Awali mfuko huu ulilenga kuwanufaisha watumishi wa umma pekee lakini baadaye Kanuni za uendeshaji wa mfuko ziliboreshwa na kuruhusu uandikishwaji wa wanachama kutoka kwa watu binafsi na sekta binafsi. Katika mfuko huu watumishi wa umma walikuwa wakilipa mchango wa lazima wa asilimia tatu (3) ya mshahara wa mwanachama kwa mwezi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hadi sasa Tanzania ina skimu nne za bima za utoaji wa huduma za afya ambazo ni; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*National Health Insurance Fund - NHIF*), (*Social Health Insurance Benefit*) unaomilikiwa na NSSF, Community Health Fund (*CHF*) na Tiba kwa Kadi (*TIKA*). Kwa mujibu wa Kumburu, 2019 taarifa zilizopatikana TIRA zinaonesha kuwepo kwa taasisi binafsi saba (7) zinazotoa huduma za bima ya afya. Aidha taasisi nyingine zinatoa huduma za bima ya afya kwa kutumia kitita cha bima ya maisha.

## **2.6 Umuhimu wa Sheria Inayopendekezwa**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria inayopendekezwa ni muhimu sana kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutungwa kwa Sheria hii kutawezesha:-

- i. Wananchi wote (raia na wasio raia wanaoishi nchini) kufaidika na utoaji wa huduma za afya katika vituo vyote vya kutelea huduma za afya mahala popote nchini bila kuwa na kikwazo cha fedha;
- ii. Kuongeza kiwango cha kuishi (*life expectancy*) kwa kuweka masharti yatakayowezesha utolewaji wa huduma bora na udhibiti wa uendeshaji wa mfuko, kuanzisha mfumo wa bima ya afya kwa wote; na
- iii. Kuchochea ushindani wa uanzishwaji na uendeshaji wa skimu za huduma za afya kwa wote kwa kuweka masharti ya kupanua wigo wa huduma mbalimbali za afya kwa kutumia mfumo wa bima ya afya kwa wote.

## 2.7 Uchambuzi Kuhusu Ibara za Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huu unahusu maeneo ambayo Kamati imeona haja ya kufanya marekebisho kwa ajili ya kuboresha Muswada. Wakati wa kufanya uchambuzi, Kamati ilibaini mambo mbalimbali. Baadhi ya mambo hayo ni kama ifuatavyo: -

### 2.7.1 Sehemu ya Kwanza ya Muswada

**Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza** ya Muswada inaweka Masharti ya Utangulizi na inajumuisha Jina la Sheria, Tarehe ya Kuanza Kutumika, Mipaka ya Matumizi, pamoja na kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitoa maoni ya kulifanyia marekebisho jina refu la Muswada huu. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake kuhusu jina refu la Muswada, kama inavyoonekana kwenye Jedwali la marekebisho la Serikali.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 3** ya Muswada, Kamati inaona ni muhimu kuwekwa tafsiri ya neno "**ndugu wa damu**" ili kuondoa mkanganyiko kwa wategemezi wanaotakiwa kwa mujibu wa sheria hii. Hali kadhalika, Kamati inapendekeza kuongezwe tafsiri ya "**Mtu asiyé na uwezo**" ili kuhakikisha makundi yote muhimu yamezingatiwa na kuepusha mgongano wa tafsiri. Vilevile Kamati inashauri kuwepo na tafsiri ya neno Skimu.

**Mheshimiwa Spika**, mapendekezo hayo ya tafsiri za maneno yamekubaliwa na Serikali.

### 2.7.2 Sehemu ya Pili ya Muswada

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu hii inahusu masharti ya mfumo wa bima ya afya kwa wote. Katika **Ibara ya 7** Kamati imeona kwamba upo umuhimu wa kuwa na uendelevu wa mfumo wa Bima ya afya, hivyo kupendekeza kuongeza **Ibara ndogo ya 2 (m) inayohusu utafiti na**

**uvumbuzi (research and development).** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia maoni hayo.

### 2.7.3 Sehemu ya Tatu ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaweka masharti kuhusiana na skimu za bima ya afya. **Ibara ya 10** inatambua skimu maalum za bima ya afya ambazo ni tofauti na bima ya afya ya umma na binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona hakuna sababu ya kuwa na aina ya tatu ya skimu kwa waajiriwa pekee ilhali zipo skimu za umma na binafsi zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria zikilenga kundi hilo hilo. Baada ya majadiliano ya kina kuhusu Ibara hii Serikali imekubali kuyazingatia katika jedwali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13** inahusu kufuta usajili wa skimu, Kamati inashauri haki za wanachama ziwekwe wazi kwenye Sheria katika mazingira ambapo skimu itakuwa imefutiwa usajili. Lengo ni kuhakiksha mwanachama haathiriki na ufutaji wa skimu ya bima ya afya. Serikali imezingatia na kuongeza ibara ndogo kwenye ibara ya 13.

### 2.7.4 Sehemu ya Nne ya Muswada

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inaweka masharti kuhusu utoaji wa kitita cha mafao ya msingi kwa wanufaika wa skimu za bima ya afya. **Ibara ya 15** inampa Waziri mamlaka ya kuainisha katika Kanuni kitita cha mafao ya msingi kitakachotolewa na skimu za bima za afya ambapo kila skimu itatakiwa kutoa kitita hicho. Kamati inapendekeza marekebisho kwenye neno "**kitita cha mafao ya msingi**" na badala yake iwe "**kitita cha mafao ya huduma zote muhimu**" ili kuakisi maudhui yaliyokusudiwa.

**Ibara ya 15 (1)** Kamati inaona ni muhimu sana kwa Serikali kuainisha huduma zote muhimu zitakazotolewa kwenye kitita cha mafao ya huduma muhimu ili kuepusha mkanganyiko katika utekelezaji wa

Sheria hii. Serikali imekubali kuyazingatia mapendekezo ya Kamati kwa kuanisha kwenye sheria huduma zitakazotolewa na watoa huduma wa afya kwenye kitita badala ya kuweka kwenye Kanuni kama ilivyokuwa awali. Aidha, Serikali imeongeza kitita kingine cha bima ya afya ya jamii kinachotarajiwa kuwa na gharama ya chini.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17** inahusu wigo wa upatikanaji wa huduma za afya. Kwa tathmini ya Kamati, Ibara hii irekebishwe ili kuepusha wanachama kukimbilia kutibiwa katika hospitali kubwa pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekubali kuifuta ibara hii na kuhamisha maudhui yake kwa kuiandika upya katika Ibara ya 19.

#### **2.7.5 Sehemu ya Tano ya Muswada**

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inahusu uanachama na uchangiaji katika skimu ya bima ya afya. **Ibara ya 22** inaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa kundi la watu wasiokuwa na uwezo kwa lengo la kuhakikisha wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha. Kamati ilitaka kujiridhisha ikiwa Serikali ina vyanzo mahsus na vya uhakika vya fedha kwa ajili ya kugharamia watu wasio na uwezo. Serikali imeandika upya kifungu hiki na kuainisha vyanzo vya mapato kama itakavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. Kamati pia imeoneshwa uthibitisho wa vyanzo vya kugharamia mfuko huo kutoka serikalini. Hivyo, Kamati inasisitiza mfuko huu ulindwe kwa kuwekewa utaratibu mzuri wa usimamizi.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 23** inahusu uwekaji wa amana kwa Skimu ya Bima, sawa na kiasi kinachotocsha kutoa huduma kwa kipindi cha miaka miwili, kabla ya kusajiliwa. Kamati imetathmini na kuona kuwa kiwango cha amana kitajwe kwenye Sheria na kiwe kiasi cha wastani ambacho hakitakwamisha uendeshaji wa skimu za bima ya afya. Kiwango hicho kiwe ni asilimia ya mtaji kutoptana na tathmini ya ukwasi na uendelevu wa skimu. Lengo ni kuviweka wazi viwango hivyo na kuondoa uwezekano wa kudhoofisha na

kupunguza uwezo wa skimu kuijendesha kwani fedha hiyo ni sehemu ya mtaji ambayo itakuwa haitumiki. Serikali imekubali kufanya marekebisho ya ibara hii kwa kuihusisha na Sheria ya Bima ambapo dhamana ni asilimia ya mtaji uliolipiwa.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 25** inahusu utaratibu wa ukomo wa uanachama ambapo ukomo huo utafikiwa pale ambapo mwanachama amefariki au anaacha kuchangia katika skimu ya bima ya afya. Kamati imetathmini na kuona katika kifungu hiki ibara ndogo ya 2, imezingatia zaidi mwanachama kupoteza maisha ndipo wategemezi wake waendelee kunufaika na huduma za bima pasipo kuangalia madhara mengine ambayo yanaweza kusababisha ukomo wa uanachama. Hivyo, kwa kuzingatia umuhimu wa hoja ya Kamati, Ibara hii isomeke kama ifuatavyo: -

"25. (2) Iwapo mwanachama anayechangia kupitia makato ya mshahara wake atafariki, **kupata ulemavu wa kudumu** au **kuachishwa kazi**, wategemezi wake wataendelea kunufaika na huduma kwa kipindi kitakachoainishwa katika kanuni". Ushauri huu umezingatiwa na Serikali katika Jedwali la Marekebisho

## 2.7.6 Sehemu ya Saba

**Mheshimiwa Spika, Sehemu hii** inahusu masharti mengineyo. **Ibara ya 32** inaweka masharti ya zuio la kupata baadhi ya huduma pasipo kuwa na bima ya afya. Kamati imefanya tathmini ya kina na kuona kwamba Ibara hii inakiuka haki za msingi za watu na kuleta usumbufu. Serikali imezingatia na kukifuta kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 34** inahusu katazo kwa wanufaika, vituo vya kutolea huduma za skimu ya bima ya afya na skimu za bima ya afya kutoa taarifa za uongo na kuweka adhabu ikiwa watathibitika kufanya hivyo. Kwa makosa yanayofanywa na watu binafsi, Kamati inapendekeza kupunguza adhabu ya kifungo kisizidi miezi sita.

**Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36** inahusu makosa ya jumla ambapo inaweka utaratibu wa kushughulikia makosa yote ambayo hayajawekewa adhabu mahsus i katika Sheria hii. Kamati inaona ni muhimu adhabu hizi zitofautishwe kwa wanachama na skimu za watoa huduma za afya. Serikali imezingatia ushauri huu kama inavyoonekana katika jedwali la marekebisho ya Serikali.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 Maoni na Mapendeleko ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi wa maudhui na masharti mbalimbali katika Muswada huu, Kamati inayo maoni ya jumla na mapendeleko mahsus i ambayo yakizingatiwa yatarahisisha mchakato wa utekelezaji wa Sheria hii kama ifuatavyo: -

#### 3.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuchukuwa hatua kuandaa na kuleta Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022, ambao kimsingi unalenga kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi kupata huduma bora za afya bila kikwazo cha fedha kwa kuitia mfumo wa bima ya afya. Huu ni msingi mzuri wa kuhakikisha kwamba raia wote wanakuwa na afya njema kwani wataweza kupata matibabu kwa wakati pale watakapohitaji na hivyo kujenga Taifa la watu wenye afya njema na wenye mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya mtu mmoja mmoja na hata taifa kwa ujumla.

#### 3.2 Maoni na Mapendeleko Mahsus

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchambuzi na marekebisho ya Ibara mbalimbali za Muswada huu, Kamati inaisisitiza Serikali katika mambo muhimu yafuatayo;

### 3.2.1 Fedha

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inadhamira ya kutambua na kugharamia huduma za bima ya afya kwa watu wasio na uwezo kama ilivyo katika ibara ya 22 ya Muswada. Awali, Kamati ilishauri Serikali kuanzisha mfuko maalum (*equity fund*) ambao utakuwa na vyanzo mahsusini vya fedha na vyenye uhakika ambavyo vitaainishwa kwenye Sheria hii kama ilivyo katika Sheria zingine mfano, Sheria ya Wakala wa Usambazaji wa Umeme Vijiji (REA) Na. 8 ya Mwaka 2005 na Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Sura 272 ya Mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako kuwa Serikali imeridhia kuanzisha Mfuko kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo na kuthibitisha vyanzo vya mfuko huo kama itakavyoonekana kwenye jedwali la marekebisho. Kamati inasisitiza Serikali kubainisha utaratibu wa uendeshaji wa mfuko huo ili kuulinda na kuwa endelevu.

### 3.2.2 Vitita vya Mafao

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imeboresha vitita kwa kuongeza kitita kingine chenye gharama ya chini ambacho ni kitita cha bima ya afya ya jamii. Hata hivyo, Kamati bado inaona upo umuhimu wa kuongeza kitita kingine chenye gharama za kati ili kumpatia mwananchi machagua zaidi ya vitita.

### 3.2.3 Kipindi cha Msamaha (*Grace Period*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ipo haja ya kuwa na kipindi cha msamaha (*Grace Period*) cha miezi mitatu (3) kutoka kuisha kwa kitita pale anapofariki mchangiaji. Hii ni kwa ajili ya kumpa mijane/mgane au mtegemezi aliyebakia nafasi ya kulipia malipo ya bima kwa mwaka unaofuata au kujisajili na mfumo wa watu wasio na uwezo kutokana na madhara ya kifo cha mchangiaji.

### 3.2.4 Utafiti wa Kina (*Actuarial study*)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa ni muhimu kufanyika kwa utafiti wa kina (*Actuarial study*) mahsus i kwa ajili ya bima ya afya kwa wote kwani itasaidia mambo mbalimbali ya msingi kama vile kubainisha viwango vya uchangiaji wa bima na kiasi cha fedha zitakazohitajika kwa ajili ya watu wasio na uwezo.

### 3.2.5 Uboreshaji wa Huduma za Afya

**Mheshimiwa Spika**, ili kufanikisha malengo mapana ya sheria hii, Serikali kuendelea kuboresha huduma za afya kwa kujenga vituo vingi zaidi katika maeneo yenye upungufu wa vituo vya afya, kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja kuongeza watumishi wa kada ya afya. Aidha, kuhakikisha watumishi wa afya wanazingatia maadili ya kazi.

### 3.2.6 Elimu kwa Umma

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iweke juhudini katika kutoa elimu mara kwa mara kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuijunga na skimu za bima ya afya, utaratibu wa ugharamiaji wa huduma za afya kwa kutumia bima ya afya na upatikanaji wa huduma mbalimbali za afya kwa raia aliyejiunga na bima ya afya. Hii itasaidia kuondoa upotoshaji katika jamii na kuelewa umuhimu wa mfumo mzima wa bima ya afya, jambo ambalo litasababisha wananchi wengi kuijunga na bima ya afya.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wanani. Naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb	-	<b>Mwenyekiti</b>
2. Mhe. Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, Mb	-	<b>M/Mwenyekiti</b>
3. Mhe. Aysharose Ndagholfi Mattembe, Mb	-	- Mjumbe
4. Mhe. Bernadeta Kasabango Mushashu, Mb	-	- Mjumbe
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb	-	"
6. Mhe. Christopher Olenyokie Ole Sendeka, Mb	-	"
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb	-	"
8. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb	-	"
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb	-	"
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb	-	"
11. Mhe. Hassan Haji Kassim, Mb	-	"
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb	-	"
13. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	-	"
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb	-	"
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb	-	"
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb	-	"
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb	-	"
18. Mhe. Seif Salum Seif, Mb	-	"
19. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	-	"
20. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb	-	"
21. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb	-	"
22. Mhe. Jacqueline Andrew Kainja, Mb	-	"

**1 NOVEMBA, 2023**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ndc na kwa kipekee sekretarieti ya Kamati kwa uratibu wa shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

#### **4.1 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Ukimwi, inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha **Muswada wa Sheria ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa Mwaka 2022** pamoja marekebisho yake, kama ulivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),

**MWENYEKITI KAMATI YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**

1 NOVEMBA, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti kwa kusoma vizuri sana. Naipongeza Kamati yako kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza mjadala, tunaanza na Mheshimiwa Askofu Gwajima. Mheshimiwa Mushashu na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrew wajiandae.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia huu Muswada wa Bima ya Afya kwa Watu Wote. Wewe kama Mwalimu wangu wa mambo ya siasa na kiongozi wangu, naomba nikubaliane na maneno uliyoyasema kwamba kwa habari ya Muswada wa Bima ya Afya kwa Watanzania wote, Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi apewe maua yake.

Asiyemba maua yake basi ana fitina binafsi, lakini kwa habari ya Muswada huu nasema tena Mama Samia Suluhu Hassan apewe maua yake. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikubali kwamba upatikanaji wa dawa nchini umekuwa sana kutoka asilimia 62 mwezi Agosti, 2022 mpaka asilimia 72 mwezi Agosti, 2023. Kwa hiyo, upatikanaji wa dawa umekua sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubali jambo moja kwamba tumeongeza pia uhaba wa watumishi wa Wizara ya Afya, mpaka sasa hivi tumefikia *almost* asilimia 50.4, hii ndiyo sababu ninaendelea kusema katika suala hili la afya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Waheshimiwa Mawaziri wake wapewe maua yao.(Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisema jambo moja, asilimia 26.4 ya Watanzania ambao ni kama Watanzania milioni 15.8 wako kwenye umaskini wa kutupwa na hii ni sawa na kaya milioni tatu na laki sita. Hawa wote kwa namna ya kawaida, hawana uwezo kabisa wa kugharamia huduma za afya mahala wanapokaribia kwenda katika vituo vya afya au zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia asilimia nane ya Watanzania ambao ni *almost* milioni 4 ya watanzania wote ni watu walio kwenye ule umaskini uliokithiri. *Almost* kaya milioni moja na laki moja ni Watanzania ambao wako kwenye umaskini uliokithiri, hawana uwezo kabisa wa kulipa, kugharamia huduma za afya wao wenyewe. Kwa hiyo, naweza kusema asilimia 85 ya Watanzania hawawezi kupata huduma ya afya inavyotakiwa kwa sababu ya vikwazo vya kifedha walivyonavyo. Naomba ku-declare *interest*, mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020, Ibara ya 83(e) inazungumza kuisimamia Serikali ili kuwapa Watanzania wote Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo, nataka kuishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan na Waheshimiwa Mawaziri wake, Mheshimiwa Waziri Ummy na Msaidizi wake Mheshimiwa Godwin Mollel kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili tuupitishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shakespeare aliwahi kusema; "mto hauwezi kunywa maji yake wenyewe wala mti hauwezi kukaa chini ya kivuli chake wenyewe." Ndivyo walivyo Watanzania walio maskini wasioweza kumudu afya, wanahitaji kusemewa na sisi, hawawezi wakajisemea wao wenyewe. Nataka kusema kwa uwazi kabisa hatuwezi kuchelewa hata kwa dakika moja kujadili na kupitisha huu Muswada wa Afya ili Watanzania wote, wanawake kwa wanaume, vijana kwa watoto wapate Bima ya Afya na wao waweze kutibiwa.(Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu ni maskini sana. Wananchi wetu wengi wanapoteza maisha kwa magonjwa ambayo yanaweza kutibika. Unakuta mtu anaumwa ugonjwa wa kawaida lakini hawezi kumudu matibabu na matokeo yake anapoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ukifungua simu za Waheshimiwa Wabunge, Mbunge ye yote hapa lazima kwenye simu yake utakuta ujumbe au meseji anaambiwa na wapiga kura wa Jimboni kwake nisaidie fedha nikalipe dawa au nisaidie fedha nikalipe hospitali au nina maiti hospitalini nimeshindwa kuitoa kwa sababu za huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu leo bila kufumba macho, bila kupoteza muda tupidishe na tuujadili huu Muswada wa Bima ya Afya ili akina Mama wa Tanzania watibiwe, vijana watibiwe, wazee watibiwe na Watanzania wote kutoka Mashariki, Magharibi, Kaskazini wapate Muswada wa Bima ya Afya na Tanzania iendelee sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimehudhuria misiba minne tofauti iliyobadili mtazamo wangu juu ya Bima ya Afya. Msiba wa kwanza nilihudhuria mahala fulani kule Bunju, nilikuta Balozi mmoja amefariki, Balozi wetu wa Shina, Mwenyekiti wa Shina. Nilipouliza kwa nini alifariki, wanasema alikuwa hana uwezo akaenda kwenye maabara kupima akaonekana ana malaria, lakini akakosa shilingi elfu tatu ya kununua dawa ya malaria. Alikuwa ana shilingi elfu moja ya kupima kuona ana malaria, hakuwa na shilingi elfu tatu ya kununua dawa ya malaria, akarudi nyumbani. Akakaa baada ya muda akazidiwa akapoteza maisha yake. Ni watu wengi wa namna hii nchi yetu ya Tanzania kutoka mashariki mwa Tanzania mpaka magharibi mwa Tanzania, kusini mpaka kaskazini, wanaopoteza maisha kwa magonjwa ambayo yanaweza yakatibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni saa ya wakati wetu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tupitishe Muswada wa Bima kwa Watanzania Wote, ndugu zetu watibiwe na Tanzania yetu isonge mbele. Falsafa ya bima ni watu wachache wenyewe uwezo wa kulipa bima walipe bima na hao wachache wanaolipa bima wawafanye watu wengi wasio na uwezo wa kulipa bima wapate faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea wagonjwa wote wanakwenda kukata bima, hiyo siyo bima tena. Ninawaomba Watanzania wenyewe uwezo wa kulipa bima tulipe bima kwa uaminifu kwa ajili ya ndugu zetu wengine ambao wao hawana uwezo wa kulipa bima ili tuwabebe na kwa pamoja mfuko wetu uwe imara na tusonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri nilionao, kwa sababu kuna baadhi ya vijiji havina zahanati kabisa, ukienda kule vijijini kuna baadhi ya vijiji havina zahanati kabisa. Hao wananchi na wenyewe ili waweze kutibiwa watalazimika kulipa Bima ya Taifa, Bima ya Afya wakati huohuo hawana mahala pa kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali sana ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Waheshimiwa Mawaziri wake, wajitahidi sana maeneo ya vijiji ambavyo hakuna zahanati, wapeleke zahanati ili ile maana ya hawa wananchi na wao kulipa bima walipe bima na wapate mahala pa kutibiwa kuliko walipe bima halafu hawana mahala pa kutibiwa.(Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rwanda ni nchi ndogo sana, hawana rasilimali kama zetu, hawana madini kama yetu lakini wana Bima ya Afya. Hawana milima kama yetu lakini wana Bima ya Afya, hawana mito kama yetu lakini wana Bima ya Afya kwa watu wao. Hawana maziwa kama yetu lakini wanatibu watu wao, hawana bahari kama yetu lakini wanatibu watu wao. Hawana watu wengi kama sisi lakini wanatibu watu wao, hawana ardhi kama ya kwetu lakini wanatibu watu wao, hawana dhahabu, almasi na madini kama ya kwetu lakini wanatibu watu wao. Sisi sasa ni wakati muafaka wa Taifa letu la Tanzania tuwatibu watu wetu wawe na afya njema na naam! Tanzania mpya inakuja. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ninaunga mkono hoja na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuupitishe Muswada huu wa Sheria ya Bima ya Taifa kwa Watu Wote kwa kishindo na nguvu ili ndugu zetu wote watibiwe. Nakushukuru kwa kunipa nafasi. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namuita Mheshimiwa Mushashu, jiandae Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia huu Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI, vilevile nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ambao tulianza kuuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kazi kubwa imefanyika, naipongeza Wizara, wameweza kuyachukua maoni mengi yaliyotolewa na wadau na yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Kwa sasa hivi Muswada ulivyo ni Muswada mzuri na sheria itakayotokana na Muswada huu inaweza kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha bora yanategemea na afya bora. Huu Muswada Watanzania wengi wameusubiri kwa muda mrefu. Walikuwa wanauleta mbele ya Kamati tunaurudisha kwa sababu tulitaka tuone kwamba kila Mtanzania sasa anaenda kushughulikiwa, anaweza akahudumiwa, ndiyo maana kila ulipokuwa unaletwa tunaleta maoni, sasa hivi tumefikia mahali tunaona maoni yamezingatiwa na huu Muswada sasa unaenda kuwajali Watanzania wote kwa hiyo naomba muupitishe. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunajua kwamba gharama za matibabu ni kubwa, vipimo, madawa, ukihitaji upasuaji, kwa bahati mbaya ukiugua haya magonjwa yasiyoambukiza au ya muda mrefu kama presha au kisukari, wewe unakua ni mgonjwa wa kudumu, ni mtu ambae unahitaji matibabu kila siku ni gharama kubwa ambayo Watanzania wengi hawawezi kuimudu, inabidi wafe kwa sababu wanakosa matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya ukiugua figo ndugu zangu, unatakiwa kusafisha figo mara mbili mara tatu kwa wiki moja ambapo gharama zake ni shilingi laki mbili na nusu hadi laki tatu. Ni Watanzania wangapi wanaweza kumudu kulipa shilingi laki saba na nusu hadi laki tisa kwa wiki moja ili waweze kusafishwa figo? Utakuta ni wale wenye fedha tu wanaendelea kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia sheria hii ikishatungwa, ina maana kwamba hata hawa watu wanaenda kutibiwa. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kwamba huu mchakato wa kuleta Bima ya Afya kwa wote uanze ili kusudi

hata wale Watanzania ambao walikuwa wanakufa kwa sababu ya kukosa fedha za matibabu waweze kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu nimeupenda sana kwa sababu unajali na umezingatia hali ya Mtanzania wa kawaida. Unaangalia kwamba kama kuna mwanachama wamemruhusu aweze kuwa na wategemezi wengine wanne pamoja na mwenza kwa hiyo, ni wewe na mwenzi wako ambaye anaweza akawa ni mke au mume, akapata huduma lakini unaruhusiwa vilevile na wategemezi ambao wanaweza kuwa wazazi wako wewe mwenyewe lakini kwa mara ya kwanza hata wazazi wa mke wako au wazazi wa mume wako na wenyewe watahudumiwa na huu Mfuko wa Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile unaruhusiwa kupata huduma kwa ajili ya mtoto uliyemzaa, mtoto uliyemuasili na mtoto hata wa kambo na yenyewe inaruhusiwa ilimradi awe na chini ya umri wa mika 21. Vilevile ndugu zako wa damu ambao bima nyingi zilikuwa hazizingatii hiki kitu, anaruhisiwa sasa, ataruhusiwa kwa sheria hii ikishapita. Unaweza ukamuhudumia hata ndugu yako wa damu ilimradi awe na umri wa chini ya miaka 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 17 kinatoa wigo mpana kwamba sasa ukikatia hata Bima ya Afya Dar es Salaam, ukaikatia hata Tanga, ukaikatia hata Bukoba unaruhusiwa kwenda kuhudumiwa kwenye kituo chochote kinachotoa huduma ya afya katika Mkoa wowote ule ilimradi unazingatia yale masuala ya rufaa na masharti mengine yatakayokuwa yamewekwa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32 cha Muswada ule uliowasilishwa kilikuwa kinaleta vikwazo kwa huduma nyingi za kijamii. Kilikuwa kinasema kwamba huwezi kupata leseni ya biashara mpaka uwe na Bima ya Afya, huwezi kupata *tin* au namba ya mlipa kodi mpaka uwe na Bima ya Afya. Huwezi kupata hata *passport* ya kusafiria, uwe na Bima ya Afya, huwezi kumuandikisha mwanafunzi wa Kidato cha Tano na cha Sita hadi awe na Bima ya Afya, kwa

hiyo, ilikuwa inaleta vikwazo kwa watu kupata huduma mbalimbali za kiafya lakini sasa hivi naipongeza Serikali kwa kuwa wasikivu, hiki kipengele kimefutwa na kimeondolewa kabisa kwenye Muswada. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 inawatambua watu wasiokuwa na uwezo ili mtanzania yeyote yule aweze kupata matibabu bila kikwazo cha kutokuwa na fedha. Sensa imeshabainisha kwamba kuna watanzania wangapi au asilimia ngapi ni watu ambao ni maskini. Naomba kuweka hapa angalizo. Hapa ukishasema watu ambao hawana uwezo wanaenda kupata matibabu bure, kila mtu atajitokeza kwamba ni maskini, lazima Serikali hapa tuwe waangalifu, tuweke vigezo mahsusvi vyatambua mtu ambaye hana uwezo ni nani ndani ya Tanzania, la sivyo kila mtu atasema hana uwezo, huu mfuko utaelemewa na Bima ya Afya ita-collapse.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza vilevile wakati wanatambuliwa watu ambao hawana uwezo, hata watu wenye ulemavu ule ulemavu mkubwa, watambuliwe kama watu ambao hawana uwezo. Nampongeza tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwajali watu wote, hataki mtu yeyote, mtanzania yeyote afe kwa sababu ya kukosa pesa za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa kukubali kuanzisha Mfuko wa Matibabu, Mfuko wa Bima ya Afya. Mojawapo ya kitu kilichokuwa kinakwamisha Muswada usisonge mbele, tulikuwa tunajiuliza hawa watu ambao hawana uwezo wanaenda kutibiwaje? Serikali imekubali kwamba itaanzisha huo Mfuko. Vilevile wameianisha vyanzo mahsusvi vyatambua kuingiza hela kwenye huu Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendeleko langu ni kwamba tunaomba huu Mfuko sasa ukatungiwe sheria ili uwepo kisheria, mtu yeyote asije akaamka akaamua kuufuta. Nakuomba Mheshimiwa

Mwigulu huu mfuko ukatungiwe sheria tuhakikishe kwamba hivi vyanzo viwe *sustainable*, tuhakikishe kwamba hizi hela zinazoingia kwenye huu Mfuko zinakuwa *ring fenced* kusudi ziweze kufanya kazi moja ya kutoa huduma ya Bima ya Afya kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, baada ya Muswada huu kupita, ninaomba sasa elimu itolewe kwa ukubwa, uhamasishaji ufanywe mkubwa kama tulivyofanya kwenye Sensa kusudi Watanzania waweze kuelewa maana na umuhimu wa Bima ya Afya na wakubali kuingia. Serikali iendelee kuboresha mazingira, ninajua mmejenga zahanati nyingi, vituo vya afya vimejengwa, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hospitali zimejengwa, tunaomba sasa muhakikishe kwamba kwenye hizo hospitali kuna vifaatiba, vitendanishi, kuna dawa, kuna watumishi ili kusudi hata watakaoanza kuingia kwenye huo Mfuko waende kuwaambia wenzao kwamba tukienda kwenye hivyo vituo tunatibiwa, tukienda kwenye hivyo vituo tunawakuta Madaktari, tunawakuta Manesi, kwa hiyo, tuendelee kuboresha mazingira na kwa kufanya hivyo tutawahamasisha watu wengi watashawishika kuingia kwenye huo Mfuko wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa sasa uhamasishaji umetosha ninaomba tuanze na wale amba wana mishahara kama kawaida, wale amba wapo kwenye *private sector* lakini wana vipato, kwa sababu sasa Sensa imeshatusaidia kutambua asilimia ngapi ya watu amba hawana uwezo, tuanze kuchukua wachache wachache, tuanze kuwaingiza kwenye Bima. Kamati yetu ilienda Rwanda, Kamati yetu ilienda mpaka Ghana na wao hawajafikia 100 percent. Wameanza polepole, wanaendelea kuboresha kadri uchumi unavyokuwa na vile vyanzo vinavyozidi kuongezeka watu wanaendelea kuongezeka. Msiogope nenda muanze, ni kitu kizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuwashawishi Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hapa Muswada huu ulipofikia ukiulinganisha na Muswada ulioletwa hapa mwanzo, huu ni

Muswada mzuri sana, wamezingatia mawazo ya Waheshimiwa Wabunge yaliyotolewa humu ndani na yaliyotolewa ndani ya Kamati kwa hiyo tukubali tuupitishe kusudi uweze kutunga sheria ya kwenda kumsaidia kila Mtanzania. Nawaomba Watanzania, sheria ikishatoka basi tuingie kwenye hii Bima ya Afya kwa sababu ndiyo mkombozi wa kutuwezesha kupata huduma bora za kiafya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jacqueline, jiandae Mheshimiwa Francis Mtinga, jiandae Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami niweze kuchangia katika Muswada huu wa Bima ya Afya kwa Wote. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake Tukufu kwa kazi nzuri anayofanya kwa jitihada njema zinazoonekana katika nchi yetu na kwa wananchi wote kwa ujumla. Muswada huu umeshaletwa mara mbili lakini haukuweza kutekelezeka lakini leo hii Muswada huu umeletwa na Wizara ya Afya na tumeendelea kuujadili Muswada huu hapa kwenye Bunge lako Tukufu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza pia Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Fedha wote kwa pamoja kwa kukaa na kuja na vyanzo vya fedha vya kuwezesha Mfuko huu wa Bima ya Afya kwa watu wote kwa watu ambaao ni maskini ambaao hawatojiweza. Tunaipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kuona kwamba karibia takribani watu Milioni 15.8 wasiojiweza wataingia katika Mfuko huu wa Bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa inaonekana watu wengi wanashindwa kupata matibabu sawia kutokana na uchumi mbovu na magonjwa hayana hodi. Kamati tumeridhia Muswada huu uweze kujadiliwa na tuweze kuupitisha, tuunge mkono hoja ya Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vya mapato kwa watu wasiojiweza vimeainishwa hapo, amevisoma ikiwemo vinywaji ambavyo ni vikali, vinywaji ambavyo vina carbon, michezo ya betting na vitu vingine ambavyo vimeainishwa na Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatusomea Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutoa ushauri kwenye hili suala la watu wasiojiweza, kuangalia utaratibu mzuri ambao utatuletea takwimu zote za watu wote ambao kweli hawajiwezi. Tumeangalia mfumo mzima wa TASAF bado una changamoto zake. Baadhi ya maeneo tunashindwa kupata *figures* za watu wote ambao hawajiwezi. Naomba waboreshe kwa sababu watatumia mfumo wa TASAF kuweza kugundua watu ambao hawajiwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi tuone wauboreshe tuweze kupata *figures* ambazo zitakuwa zinaenda sawa na tunachokitegemea. Vilevile kuna jambo ambalo tunahitaji uboreshaji wa huduma za afya bado tuna changamoto nyingi. Kuna maeneo kutoka eneo moja, Kata moja kwenda Zahanati ni takribani kilometa 25, 28, 30 na kuendelea, tunaomba Serikali iongeze huduma za afya kwa kuhakikisha vituo vinaongezeka vya afya na watumishi wa afya pamoja na upatikanaji wa dawa ili wananchi hawa ambao wote waingie kwenye Mfuko wa Bima kwa Wote anapofika hospitali aweze kupata huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba Serikali iweze kuangalia namna njema na nzuri ya uhamasishaji kila mwananchi aone anawiwa kujunga katika Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote ili tuweze kupata tija na kiu ya Mheshimiwa Rais iweze kukatika na aweze kuona matunda kuitia Mfuko huu wa Bima ya Afya kwa Wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa aweze kutufafanulia; amesema kuna makundi ya watu wasiojiweza, watu ambao wako Serikalini, na vilevile kuna watu ambao hawajaajiriwa popote, ni vijana ambao

hawana ajira, au kijana ambaye hana mzazi wa kumlipia. Kuna mwingine yawezekana akawa hana ajira lakini anaingia kwenye bima ya familia; mwingine hana baba wala mama, hivyo hataenda kujiingiza kwenye bima ya mjomba, wala shangazi kwa sababu kule nako patakuwa pamejaa. Hawa watu wataingiaje? Watasaidiwaje? Kwa sababu hawana ajira, na vijana ambaao hawana ajira ni wengi sana, ndiyo maana tunasikia malalamiko ya ajira kwa sababu vijana hawana ajira. Je, hao watu mmewaingiza kwenye kundi lipi? mtawajua?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri tunaomba utueleze, mme pangaje kuhusu watu ambaao hawatakatwa fedha kila mwezi kwa ajili ya bima kama watu ambaao ni wafanyakazi wa Serikali, mashirika binafsi na taasisi; watu ambaao hawana ajira rasmi kama wafanyabiashara, na wengine: Je, watachangia kwa kila mwezi au kwa mwaka? Yaani ije ionekane, na kiwango chake tunaomba kiwe ni reasonable ambapo kila mtu atakuwa na uwezo wa kukimudu, yaani kuwepo na vigezo vyote vinavyoweza kum-favor huyo mwananchi wa namna hiyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono na niwaombe Wabunge wote tuunge mkono hoja ya Bima ya Afya kwa Wote, iweze kutusaidia tuondokane na zile message za Mheshimiwa kuna mgonjwa au shangazi anaumwa, nakadhalika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Francis Mttinga, jiandae Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Muswada huu ambaao unaleta jambo zuri sana kwa Watanzania. Nami nimshukuru sana Rais wangu kwa kuleta jambo hili ambalo ni suluhisho kwa

wanyonge walio wengi katika suala zima la huduma. Rais wetu amekuwa mtu msikivu na mvumilivu sana. Muswada huu umerudi mara nyingi, lakini naye amekuwa bado na moyo wa kuhakikisha anarudisha tena na tena na kuboresha mpaka sasa jambo hili zuri linaenda kutimia kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa kwa wananchi ni huduma bora na za uhakika katika suala zima la afya, hilo ndiyo jambo kubwa ambalo wananchi wanalitegemea. Jambo hili limebebwaa na mambo kama matatu; kwanza, miundombinu kwa maana ya majengo na vitu vingine, vilevile vifaa tiba na dawa, la mwisho, watoa huduma wenyewe pamoja na wataalamu wa afya kwa ujumla. Mambo haya matatu ndiyo yanabeba suala zima la kufanikiwa vizuri sana kwa sheria hii na wananchi kuona faida ya jambo hili kuja kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa miundombinu, Serikali yetu imefanya makubwa sana. Tunayo majengo mengi ya kutosha, zahanati zimejengwa za kutosha na vituo vya afya. Japo bado changamoto zipo, lakini kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mwanzo, angalau sasa tunaweza kusema kwamba miundombinu ipo kule kwa wananchi wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vifaa tiba vimekwenda vya kutosha katika hospitali zetu za wilaya. Mama yetu ametulea vifaa ambavyo tulikuwa tunaviona tu, tunavisikia viko Muhimbili, viko Bugando lakini leo katika hospitali zetu za wilaya tuna huduma za kutosha; x-ray, *ultra-sound*, na kadhalika. Vitu ambavyo vilikuwa ni anasa katika huduma za afya leo vinapatikana katika wilaya zetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo napenda sana kuiomba Serikali ni suala zima la wataalamu na wahudumu wa afya. Tuna miondombinu tayari, tuna vifaa tiba, tuna dawa, lakini yote haya lazima awepo mtu wa kuhakikisha vinafanya kazi kwa maana ya wataalamu na watoa huduma. Kwa bahati nzuri tunao wa

kutosha mtaani. Nchi yetu ime-train madaktari wa kutosha, manesi wa kutosha, wapo mtaani. Leo ukitangaza ajira hapa hata hiyo jinsi ya ku-file mafaili inakuwa ni shida jinsi ya maombi yatakavyokuwa. Naomba Serikali yangu ifanye maamuzi magumu katika kuajiri ili wahudumu hawa waende kwenye vituo ambavyo tumevijenga ili wawepo. Wananchi watakapokwenda na bima zao, wakute wahudumu wapo, vifaa viro na dawa zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili suala la kuajiri, najua ni suala la kibajeti, lakini naiomba Serikali yangu, imefanya mambo makubwa sana ambayo pengine hatukuwahi kutegemea kama yangefanyika, lakini leo yanafanyika katika nchi hii. Kwa hiyo, hili suala la kuajiri watoa huduma wa afya, naomba Serikali yangu ifanye maamuzi magumu ili jambo hili la Muswada wa Bima ya Afya liweze kwenda vizuri kama tunavyotarajia kwa kuwepo wataalamu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo pia katika hili yakifanyika yanaweza kusaidia. Kwa mfano, kiwango cha malipo ya bima kwa daktari anayehudumu kwenye zahanati ni kidogo sana. Kiwango hiki kina-discourage madaktari wengi hata walioko mtaani hawana kazi kufanya kazi kwenye zahanati hata zile za binafsi. Kama kiwango hiki kikirekebishwa kidogo, nina uhakika wapo watu wenyе zahanati zao za binafsi wataingia mkataba na madaktari kwamba wewe fanya kazi ya kuhudumia wagonjwa hapa, malipo yote yale ya bima ya kumwona mgonjwa itakuwa posho yako, nami nitabaki na dawa na vipimo. Sasa kwa kiwango kile kwa sababu ni kidogo mno, kina-discourage na ndiyo maana madaktari wengi wanakimbilia mijini, hawawezi kwenda kufanya kazi kwenye vituo vya afya hata vile vya watu binafsi ambavyo viko kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana katika hili Mheshimiwa Waziri tufanye marekebisho ya bei ya mgonjwa kumwona daktari anapohudumiwa kwenye zahanati, kule ambako ndipo kuna wananchi wengi na magonjwa ya kawaida. Najua mnaweza mkadhani kwamba ooh, wataanza kuwaona tu

wagonjwa ovyo ovyo; Serikali ina mbinu nyingi za kufanya udhibiti na kukagua jinsi kama wameona wagonjwa kweli ama vipi? Hilo ni jambo dogo sana kuliko jambo kubwa la madaktari kuwepo huko kwenye zahanati kwa sababu wako wengi. Kwanza tutawasaidia hata wao, wakati wanasubiri ajira rasmi hizi kubwa anaweza kwenda kwenye zahanati, akaendelea kutoa huduma na wananchi wetu wakaendelea kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kile kiwango naomba mkitazame upya, ni kidogo mno, kina-discourage madaktari kwenda kwenye zahanati kwa sababu kwa kiwango kile cha kumwona mgonjwa kimewekwa kidogo sana. Tuangalie ile professional yake, tusiangularie kwamba ile ni zahanati ili wagonjwa wetu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba pia TAMISEMI na Wizara ya Afya kwa pamoja ifanyike operation maalum ya kumalizia maboma ya zahanati ambayo wananchi wameyajenga kwa wingi sana katika nchi hii. Nina hakika kama ikifanyika operation maalum ya kumalizia yale maboma, vijiji vingi sana vitakuwa na zahanati, na jambo hili sasa litafika mahali pake, kwamba mwananchi wa kijiji ameuza mazao yake, amejiunga na bima ya afya, ana hakika akienda kwenye zahanati atamkuta Daktari, atakuta dawa na atapata huduma nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maboma yapo mengi, mama yetu Rais wetu ametusaidia sana kwenye madarasa, leo ametujengea mpaka shule nzima, unakuta inaanza mpaka inakamilika. Kwa hiyo, kuna mzigo mkubwa umepungua kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe TAMISEMI itoe maagizo maalum kwa halmashauri na yenyewe TAMISEMI na Wizara ya Afya kwa ujumla hebu tuiwekee mkakati maalum, operation maalum ya kumalizia maboma yote ya zahanati ambayo yamejengwa na wananchi mpaka hatua ya lenta. Yapo mengi!

Kwenye jimbo langu tu nikiamua kuyahesabu ni mengi. Nina uhakika pia Wabunge wote humu kwenye majimbo yao kuna maboma ya kutosha. Kwa hiyo, huu Muswada uende sambamba na umaliziaji wa hizi zahanati ili jambo hili liende vizuri, na ile hofu yetu ya mwanzo iliyofanya turudishe mara nyingi Muswada huu, itaweza kutibika kwa kiasi kikubwa kwa kumalizia haya maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naiomba Wizara ya TAMISEMI ikarabati vituo vya afya vikongwe ili vifanane kutoa huduma na vituo vya afya vya kisasa ambavyo mama yetu ametupatia. Vituo vya afya vya sasa ni kama hospitali kubwa. Yaani lile neno kituo cha afya ni utaratibu, lakini sisi tukiangalia huko na wananchi wetu wa vijijini, ni hospitali kubwa, inafanya operation inafanya kila kitu. Sasa kuna vituo vya afya vikongwe vya siku nyingi vimebakia majina tu. Sasa vile vikarabatiwe ili viende sambamba na vituo vya afya vipyta ili wananchi wa maeneo yote katika jimbo au katika eneo, wawe wanajua wakienda kwenye kituo cha afya wanapata huduma zinazofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, pale kwangu Kituo cha Afya Kinyangiri, Kituo cha Afya Mkalama, ni vya siku nyingi, ni vikongwe. Vikikarabatiwa vile, vinafanana na vituo vya afya vya kisasa ambavyo tumevipata leo, kama pale Bumanga na pale llunda. Basi vikifanana katika majimbo mengi kwa mfano huu ninaoutoa, nina uhakika basi hii bima ya afya na huu Muswada tunaoupitisha, vitakwenda mahali pake, na hivyo wananchi watafurahia huduma hii, na hofu yetu ile ya mwanzo ambayo tulikuwanayo, nina uhakika tutakuwa tumeitibu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba vituo vya huduma za afya vya binafsi, leo hii vinatumia zaidi Mfuko wa Bima ya Afya, lakini ukiangalia kikubwa wanachofanya ni uboreshaji tu wa mazingira yale. Kuna TV pale, sijui kuna nini, lakini watoa huduma ni wale wale madaktari wetu, tena wengine wanatoka kwenye kituo cha afya cha Serikali wanakwenda kufanya parttime kwenye kituo cha afya cha binafsi, lakini ni yule yule; lakini utakuta wananchi

wengi wanakimbilia kwenye vile vituo vya afya vya binafsi, kwa sababu tu ya mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, sasa tuna vituo vya afya vizuri, vya kisasa, lakini na wananchi pia wajue kwamba hata vituo vyetu vya afya vya Serikali ni vizuri. Pia na sisi wa Serikali tuendelee kuboresha yale mazingira; mgonjwa akifika pale aone kabisa hapa nimefika mahali pa kupona, yaani mazingira yenyewe yanaonesha nitapona, ili wananchi watumie hivi vituo vya afya vya Serikali na huu mfuko basi uweze kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake unakuta huduma ile ile ya Malaria unapimwa kwenye kituo cha afya cha kawaida cha Serikali kwa shilingi 1,000, lakini ukienda kituo cha afya cha binafsi kwa sababu ya zile TV na nini unaweza ukashangaa kipimo hicho hicho kimechajiwa shilingi 5,000. Sasa mfuko unaisha haraka. Basi na sisi tuboreshe vituo vyetu kwenye Serikali. Simaanishi vile vya private vikose huduma, Hapana, viendelee kutupa challenge lakini na sisi wa Serikali tuboreshe mazingira yafanane, mgonjwa akifika apate huduma nzuri, kauli nzuri, kuna TV pale, anaangalia program, anajua tayari mimi nikitoka hapa nimepona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa huu Muswada, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, hili jambo wananchi wetu wamelisubiri kwa muda mrefu, sisi ndio tulikuwa tuna hofu kama wananchi wakuu tunaowawakilisha, na tulikuwa tuna hofu kwa nia njema kwamba vitu viende huko chini. Kwa kiasi kikubwa, mama yetu, kupitia Wizara zake hizi ambazo zinasimamia mambo yamekwenda vizuri, vituo vya afya tunaviona, zahanati tunazona. Sasa tupitishe jambo hili ili tuendelee kujifunza na kuiboresha wakati tunalifanya, naamini baada ya siku moja litakuwa ni jambo bora na litakuwa la mfano katika dunia hii ambayo Mungu ametupatia. Maana Tanzania tumekuwa nchi ya mfano kwa mambo mengi. Nina hakika hili leo tunalianza, lakini baada ya siku chache litakuwa ni jambo bora, na watu wengi watakuja kujifunza katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashauri tupitishe kwa kauli moja ili jambo hili lianze haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mtinga. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, jiandae Mheshimiwa Dkt. Mnzava na Mheshimiwa Getere.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie katika wasilisho la Serikali kuhusiana na Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote. Tanzania ni sehemu ya dunia na sasa hivi duniani mambo makubwa yanayoongelewa ni malengo endelevu ya STG. Katika STG kuna STG Na. 3 ambayo inaongelea masuala ya afya bora kwa watu wote. Kutokana na hili, msingi mkuu wa afya kwa watu wote (*universal health coverage*) umetokana. Katika hili, msingi mkuu wa afya kwa watu wote ina mambo makubwa matatu. Kwanza upatikanaji wa huduma (*accessibility*); pili, inaongelea masuala ya ubora wa huduma za afya (*quality of care*) na la tatu ni kuhakikisha kwamba mwananchi haingii gharama kubwa kupata matibabu. Huu ndiyo msingi wa hili jambo ambalo tunalijadili siku ya leo, kwamba *affordability* na *universal health coverage*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu vilevile wakati tunaliangalia suala hili, kwa sababu msingi wake mkubwa ni afya kwa watu wote (*universal health coverage*), tukaangalia katika maeneo yote. Nikisikiliza mijadala hapa tunajikita katika eneo moja tu katika sekta ya afya, nalo ni katika suala la tiba, lakini tukumbuke afya kwa sasa hivi ina mihimili minne. Elimu ya afya (*health promotion*), suala la kinga (*prevention*), tiba (*curative*), na masuala ya huduma za utengamao (*rehabilitation*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ambayo tunayo sasa hivi katika sekta ya afya, mwenendo wetu tunahama kutoka katika

magonjwa ya kuambukiza, tunakwenda magonjwa yasiyoambukiza. Maana yake ni nini? Tofauti na miaka ya 1960, 1970, na 1980 ilikuwa ni kwamba mgonjwa anaugua ugonjwa, akienda hospitali anatibiwa, baada ya pale anapona, harudi tena katika mfumo wa afya. Sasa hivi mgonjwa akipata kisukari, akipata ugonjwa wa moyo, akipata magonjwa haya mengine kiharusi, hawa ni wagonjwa wa kudumu. Kwa hiyo, ni lazima sasa tujipange vizuri, na gharama za matibabu kwa wagonjwa hawa ni kubwa sana na wananchi wengi wanashindwa kumudu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya hili jambo ambalo tunalijadili sasa hivi pamoja na juhudi kubwa ambazo zimefanywa na Serikali; na katika hatua hii napenda sana kuwapongeza Serikali kwa kuwekeza katika miundombinu. Mmefanya kazi kubwa sana. Vilevile mmefanya kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba vifaa navyo vinapatikana. Hili jambo la kuhakikisha kwamba CT-Scan na MRI sasa hivi ziko katika ngazi ya mikoa, kwa kweli ni hatua kubwa sana Hili nataka niwapongezeni sana Serikali. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo ambalo tunahitaji tufanye vizuri zaidi, na hilo ni katika suala la rasilimali watu. Ni lazima mhakikishe kwamba tunakuja na njia zote na ubunifu wote ambao utafanya tupate rasilimali watu. Haiwezekani tukawa na miundombinu iliyokuwa bora, mmeweka vifaa vizuri lakini watumishi hakuna. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba rasilimali watu tunakwenda kufanya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo mmelifanya vizuri ni ongezeko la upatikanaji wa dawa. Naona trend inakwenda vizuri, na ninataka niwapeni hongera katika hilo. Sina shida kwenye hivi vifurushi kwa sababu kuna mambo makubwa ambayo nilikuwa nayaangalia, na hayo mmeyatimiza. Kwanza vitita kwa ajili ya katika mafao ya kijamii ambayo mmeliweka. Kwa sababu katika msingi wowote ni *primary health care*. Hiyo afya ya jamii ndiyo msingi mkuu. Kama tutaweka kitita kwa wale wananchi ambao wanapata huduma katika ngazi ya jamii, hilo ni jambo moja kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nawapongeza kwa usikivu wenu Serikali ni hili ambalo mmelifanya la kuhakikisha kwamba magonjwa sugu pamoja na huduma za dharura nazo zinakwenda kuwekewa mfuko. Hongereni sana katika eneo hili. Nimefarijika sana kwamba sasa Tanzania na sisi sasa tunaenda katika mwelekeo wa kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia yote sasa hivi kuna biashara, vyakula na vinywaji ambavyo vinaleta madhara kwa binadamu. Pombe, vinywaji vikali, hizi soda ambazo zina sukari nyingi na vyakula vingi. Sasa kule katika dunia tunaita ni syntaxes, kwamba ni vitu ambavyo vinasababisha magonjwa. Naipongeza sana Serikali kwa kuona sasa, hivi vitu tunaanza kuvitumia katika kusaidia katika tiba. Kwa hiyo, na hili nilipongeze kwamba tumekuja na hivi vyanzo ambavyo navyo vitakwenda kusaidia katika utoaji wa huduma za afya. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nitoe ushauri wangu. Kwanza, kabla ya utekelezaji, pamoja na kwamba sisi kama Wabunge tutaupitisha Muswada huu leo, nendeni mkajipe nafasi ya kuweka mifumo vizuri ya usimamizi, uendeshaji wa hii Sheria ya Bima ya Afya. Mtahitaji mambo mengi sana, tunapitisha mambo mengi sana hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kabla ya utekelezaji, kama tulivyofanya kwenye sensa, nendeni mkatoe elimu. Wekeni bajeti ya kutosha ya kutoa elimu na kufanya uhamasishaji katika jamii ili wananchi waelewe na waweze kuijunga katika Mfuko huu wa Bima ya Afya. Ingawa tumetoa ufungamanishaji, nimeona mmewe ka adhabu, tuwekeni motisha, kwa nini mtu aende akajiunge na huduma za afya? Kuna njia nyingi za kuweza kulifanya jambo hili na kuweza kumfanya mtu, pamoja na kumpa elimu, lakini akapata motisha ya kwenda kuijunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani kwa mfano huduma kwa mtu ambaye hana bima inaweza ikawa na gharama juu kiasi kuliko

yule mtu ambaye anakuwa na bima ili mtu nae aone kwamba kuna faida ya yeye kwenda kuijunga na bima. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nilikuwa nataka nilishauri pamoja na kwamba tumeanzisha Mfuko ni muhimu sana fedha hizi zikawa *ring fence* katika Mfuko huu, zikaelekezwa katika huduma ambazo zimechengwa. Lakini Serikali ijaribu kuangalia vilevile fedha zinazopatikana katika Sekta ya Afya badala ya kwenda katika Mfuko Mkuu zirudishwe kwenda kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya wananchi wengi yatakuwa akikata bima akienda hospitali akute Watumishi wa Afya, akute dawa zipo na apate vipimo ambavyo atakuwa anavihitaji. Tukienda kwa *style* hiyo nauhakika kwamba tutavuka hata yale malengo ambayo nchi nyingi wamekuwa *wana-struggle* nayo sisi tunaweza tukapiga hatua kubwa zaidi. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya yote nawapongezeni sana kwa hatua ambayo mmeifikia na mimi niwaombe Wabunge wenzangu tuwaunge mkono Serikali kwa kupitisha Muswada huu, nawashukuruni sana. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Daktari. Sasa namwita Dkt. Mnzava, jiandae Mheshimiwa Getere, jiandae Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa kuweza kuchangia katika Muswada muhimu sana wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya mwaka 2022. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mama Samia kwa kazi kubwa anazozifanya kwa kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kwa ufasaha na kwa umakini sana. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, bima kwa wote ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi katika Ibara yake ya 83E naomba kunukuu; “Kuhimarisha Mfumo wa Bima ya Afya Nchini ikiwemo Mfuko wa

Bima ya Afya NHIF na CHF ili kufikia lengo la Serikali na kuwa na Bima ya Afya kwa Wote," mwisho wa kunukuu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la Bima ya Afya kwa wote ni suala ambalo sisi kama Watanzania tumelisubiri kwa muda mrefu sana. kwa sababu kwanza ni takwa la Kikanda na takwa la Kimataifa lakini pia ni haki ya msingi ya kila Mtanzania kupata Bima ya Afya. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na sababu mbalimbali ambazo zilipelekea Muswada huu usisomwe mara ya pili, ninaishukuru sana Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuhakikisha kwamba zile changamoto ambazo kama Wabunge tuliziona na tukawa na mashaka, tukajadiliana kwa kina, tukafikia muafaka kwamba Wizara ya Afya ikayapitie yale ambayo tulikuwa tunaona kwamba ni kikwazo yalikuwa hayatubariki. Niwashukuru sana Wizara ya Afya kwa kuwa wasikivu. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yote ambayo Wabunge walikuwa na wasi wasi kwa sababu sisi Wabunge ndiyo wawakilishi wa Wananchi. Tulikuwa tunatazama kule nje itakuwaje? lakini Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imekwenda kutekeleza yale ambayo sisi kama wawakilishi wa wananchi tulikuwa tunaamani sana yawepo kwa kweli nawapongeza sana na hii ni juhudi ya Mheshimiwa Rais. Kwa sababu ana dhamira safi ya kuhakikisha kwamba Watanzania wote, Wananchi wake wote wanapata huduma ya afya. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiyopingika ukienda kwenye Wilaya, ukienda kwenye Mikoa, ukienda kwenye zahati, zahanati zimejengwa, Vituo vya Afya vimejengwa, hospitali kila halmashauri inayo, zipo ambazo zimekamilika, zipo ambazo zinaendelea kujengwa. Lakini haitoshi bado kuna vifaa ambavyo Serikali ya Mama Samia imevitoa angalia digital x-ray karibia 199, angalia CT scan 32 karibia kila Mkoa una CT scan lakini mashine za MRI na zenyewe zipo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nikijiuliza sana kwamba vitu vyote hivi miundombinu ambayo imetengenezwa. Mwanzoni tulikuwa tuna wasi wasi na idadi ya Watumishi lakini mpaka sasa hivi tunaona kwamba ni takribani asilimia 50.4 ya Watumishi, upungufu uliyokuwepo umeanza kutoweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa naijuliza vifaa vyote hivi ambavyo vipo kwenye Hospitali za Wilaya, zipo kwenye zahanati, zipo kwenye Hospitali za Rufaa ni ghamama kiasi gani? Je, ni Wananchi wangapi wanaweza wakaweza kupata huduma kwa kutoa fedha zao mikononi? Nikawa najua kabisa kwamba hapa Wananchi wengi wanakwenda kupata matatizo. kwa sababu ni wangapi ambao wanauwezo? tumeona katika Taarifa ya Mheshimiwa Waziri, asilimia 85 ya Watanzania wana kikwazo cha fedha kwenda kupata matibabu katika Vituo vya Afya, katika Zahati, katika Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maoni ya Wabunge ushauri uliyotolewa na Kamati, Wizara ya Afya ikakaa chini na Wizara ya Fedha ikatoa vyanzo vya uhakika kuhakikisha kwamba Wananchi ambao hawana uwezo wa kuchangia Huduma za Afya kuna Mfuko maalum ambapo Serikali itatoa fedha, itatenga fedha kwa ajili ya Wananchi wote kuweza kupata huduma kwa kujunga na Mfuko wa Bima ya Afya kwa watu wote. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi binafsi pamoja na Kamati ya Afya na Masuala ya Ukimwi tumeridhishwa na Mpango wa Serikali yetu wa bima kwa watu wote kila Mtanzania aweze kupata huduma ya afya. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nitoe angalizo kumekuwa na Bima ya Afya (NHIF). Tumeona mapungufu ambayo yalikuwa yakijitokeza na watu waliokuwa wanatibiwa na Bima ya Afya ya Taifa hawakuwa wengi kama ambavyo tunakwenda kuwapata wengi sasa Watanzania wote wataingia kwenye Mfumo wa Bima ya

Afya. Yale matatizo ambayo tulikuwa tunayaona ukosefu wa madawa, ukosefu wa Watumishi ambao wana weledi;

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Tamisemi kuhakikisha kwamba Wananchi wote watakao jiunga katika Mfumo wa Bima ya Afya kwa watu wote wanapokwenda kwenye Zahanati, wanapokwenda kwenye Kituo cha Afya, wanapokwenda kwenye Hospitali wapate huduma inayoridhisha, wapate huduma ambayo ni rafiki kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuwashawishi wananchi wote itakapofika wizara itaanza kutekeleza hii azima yake ambayo Chama cha Mapinduzi na Serikali yake inahitaji kuwashudumia wananchi tuwape ushirikiano. Lakini ushirikiano hauwezi ukatolewa kama hatutawaelimisha wananchi wetu, tutoe elimu ya kutosha, tuhamasishe na sisi Wabunge ni Mabalozi ikawe agenda yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda kwenye Mikutano yetu ya hadhara tuhakikishe kwamba inakuwa ni moja ya agenda ili Wananchi wetu waweze kujua manufaa ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa watu wote iwe rahisi kwa wananchi wetu kujunga na Mfumo wa Bima ya Afya kwa watu wote ili waweze kupata huduma ambazo zinastahili kuweza kuwashudumia katika matatizo ambayo wanakwenda kuyapata. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sitakuwa na mengi ya kusema; mambo yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi jamani mwenye macho haambiwi tazama, mwenye masikio haambiwi sikia. Tunasikia kila kunapokucha na leo limekuja hili la Bima ya Afya kwa watu wote haijawahi kutokea, tumekuwa tukisuasua, tumekuwa tukijivuta lakini sasa ubwabwa tumeishatengewa, kazi yetu sisi ni kunawa mikono na kula na kuhakikisha kwamba Wananchi wote wanapata huduma ya bima kwa watu wote. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja na ninaomba Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja. Kwa sababu zile message

za kuambiwa naomba fedha ya matibabu, naomba limefanyaje zitapungua kwa sababu kila Mtanzania atakuwa na access ya matibabu bila kikwazo chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Boniphace Getere, jiandae Mheshimiwa Iddi Kassim, jiandae Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Bima ya Afya kwa Wote. Cha kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais kwa utulivu wa nchi yetu kafanya kazi nzuri heshima tunayo baraka na neema ya nchi tunayo kila kitu kinawezekana hata jana nimeona nchi nyingi zinafika kwenye nchi yetu zinapongeza demokrasia ya nchi yetu. Kwa hiyo, haya yote anafanya vizuri Mama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme neno moja tu kabla sijaendelea. Huu Mfuko kwa akili yangu na matamanio yangu napenda uwe Mfuko wa heshima kwenye nchi yetu na Mfuko wenyе heshima kwa Mama. Usiwe mfuko wa majanga kwa Mama narudia usiwe Mfuko wa majanga kwa Mama, uwe Mfuko wenyе heshima kwa Mama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme neno kidogo tu maneno machache tu ambayo Wabunge wengi wamechangia. Leo nchi yetu ina miundombinu mingi sana ina Vituo vya Afya siyo vingi lakini asilimia 90 au 85 ina Zahanati hata siyo nyingi lakini zipo. Ina Hospitali za Wilaya lakini leo ukienda Bunda Hospitali ya Wilaya ya Bunda ina majengo mazuri sana, ina Madaktari wawili tu hakuna tiba, kuna Kituo cha Afya Mgeta kimejengwa 2017 kina *ultrasound* na majengo mengine ya *mortuary, mortuary* tu jokofu halijawahi kuwekwa mpaka leo. Nimetembea TAMISEMI, nimetembelea Wizara ya Afya hakuna majokofu kituo kipo kina daktari mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najiuliza, Mheshimiwa Ummy nakupenda, najua unachapa kazi, huu Muswada ukija nao utajiandaa, utawaamrishaje Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya, utaamrishaje Daktari Mfawidhi wa Zahati wakati yuko Tamisemi? Wewe uko Wizara ya Afya? Leo nchi yetu katika tiba imegawinyika kwenye maeneo mawili, eneo zuri zaidi ni eneo la Hospitali za Rufaa, eneo la Hospitali za Kanda na Hospitali za Mikoa ziko vizuri sana kwa sababu ziko Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Hospitali za Wilaya Vituo vya Afya, Zahanati Mganga mmoja, uwajibikaji mdogo, madawa kidogo. Sasa niombe kwenye hili kama kweli tunataka kwenda kwenye Mfuko wa Afya kwa wote tuijandae. Nimuombe Mheshimiwa Rais, Wizara ya TAMISEMI ibaki na majengo, Watumishi wote wa Wizara ya Afya kutoka Zahanati mpaka juu waende kwenye Wizara ya Afya tuondoe hii *D by D* katika suala la uzima ambao siyo lazima sana. Watumishi wote wa chini wa Zahanati wa Vituo vya Afya wa Wilaya waende Wizara ya Afya, TAMISEMI ibaki na majengo. Tutafaulu kwa eneo kubwa kujenga hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wakati fulani hili jambo siyo hela ni uwajibikaji, uwajibikaji ni mdogo sana kwenye jambo hili chini Zahanati na Vituo vya Afya. Kwa hiyo, hilo niseme kwamba, hilo tulichukue tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa na mambo ya kushauri la kwanza tunaenda kuchambua maskini ambayo ni asilimia 20 milioni kumi na tano ama nyingine milioni nane, tunaenda kuwatambua ni utaratibu gani utatumika kuwatambua hawa masikini? Lazima tutengeneze utaratibu mzuri wa kuwachambua hawa masikini ili kuwalipia na kiwango cha kuwalipia kiwe *affordable* kiwe kiasi ambacho masikini wa Tanzania anaweza kulipa lazima hilo nalo tuwaelimishe Watanzania wajue. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumesema tukiingia Mfuko wa Afya Watanzania watapata huduma bora ya afya na anauwezo wa

kupata huduma maeneo yote. Ni kweli kwa Bima ya Afya ya sasa hivi iliyopo inawezekana asipate huduma kwenye Wilaya ya Ukerewe na Wilaya nyingine. Lakini hilo ni jambo moja kwamba atapata huduma je, Bima ya Afya kwa Wote inatoa huduma kwa vigezo vyote? Au huduma ya afya mtakuja mtuambie ukiwa na bima hii utapata huduma hii. Ili wazo la kuleta generally kwamba Bima ya Afya ikitokea yote mtu atapata huduma bila vikwazo vy a fedha nayo tuiondoe. Lazima tuonyeshe Watanzania kwamba huduma ipi anapata kwa Bima ya Afya aliyonayo? na siyo kwamba, kila mahali atapata Bima ya Afya yeyote. Kwa hiyo, nalo tulitazame vizuri Mheshimiwa Ummy ulieleze vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilikuwa nalisema ni Watanzania kwa ujumla. Hata sisi Wabunge tumekuwa mafundi wa kukodi ndege kwenda vilioni, tumekuwa mafundi wakukodi magari kwenda vilioni lakini hatukuwa mafundi wa kulipia watu Bima ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wamekuwa mafundi wa kuzika watu siyo kuwahudumia, sasa tujiondoe kwenye hilo tuwe mafundi wa kulipa Bima ya Afya tuokoe watu kabla ya kwenda vilioni lazima tuwe na hali hiyo. Mtu akisikia fulani amefariki anakodi ndege, anakodi magari, maturubai, vitu gani anaonekana fundi kuzika mtu lakini siyo fundi kumuhudumia na hilo nalo tuliangalie sana tuone namna gani tunaenda kuokoa hiyo hali ambayo siyo nzuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Ummy nimesikia unazungumza Mkoa wa Mara ambao ni Mkoa wenyewe watu wengi sana milioni mbili na ushee una CT scan ambazo zimekaa pale mieze sita hazijafungwa na hilo nalo ndiyo tumetoka kuzungmza vifaa tunanunua lakini kufunga hatufungi. Sasa itakuaje? Niombe Mkoa wa Mara tuone muazibike nataka kutokupata tamko kutoka leo kwamba hiyo CT scan itafungwa lini? au ndiyo watu waendelee kufa na Mfuko wa Afya unakuja na watu wanaenda kufa na vifaa tunavyo. Kwa hiyo, nalo tulizungumze na wewe kwa

**1 NOVEMBA, 2023**

sababu umelisema wewe hapa ndiyo maana kwamba linafanyikaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho nikuombe Majokofu ya Zahanati ya Kituo cha Afya Mgeta lakini upeleke kwa Waganga wa Hospitali ya Wilaya Halmashauri ya Bunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema siku ya leo kuweza kutoa mchango wangu kwenye Huduma ya Bima ya Afya kwa wote. Moja kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya kwenye nchi yetu hii ya Tanzania na hasa kwenye Mkoa wa Shinyanga Wilaya ya Kahama Halmashauri ya Msalala. Mheshimiwa Rais ametufanyia mambo makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Afya Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan ametuletea fedha nyingi sana ambazo zimeenda kujenga Miundombinu ya Afya na Naibu Waziri, Daktari Mollel atakuwa shahidi alipokuja kutembelea kwenye Jimbo la Msalala na tukafanya ziara ambapo alishuhudia Ujenzi wa Zahati zaidi ya thelathini na nne zikiwa zimekamilika kwenye Jimbo la Msalala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kumpongeza sana Dada yangu Ummy anafanya kazi kubwa sana. Nichukue fursa hii kukupongeza Dkt. Mollel unaafanyakazi kubwa sana na wewe utakuwa shahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Msalala Halmashauri ya Msalala tumeweza kupatiwa fedha za kujenga Vituo vya Afya zaidi ya vinne. Hivyo kupelekea kuwa na jumla ya Vituo vya Afya kumi kwenye Jimbo la Msalala. Mheshimiwa Rais kwa kushirikiana na Mgodi wa Barrick wameweza kutupatia fedha, tukaweza kukamilisha Zahati ishirini na nne na zingine tukaongeza Zahanati kumi na kwa sasa tumekamilisha zaidi ya Zahati thelathini na nne. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwanza kabisa ninaunga mkono, tunaunga mkono sisi Wanamsalala ni wahitaji wa Bima ya Afya kwa Wote ni wahanga. Kwa hiyo Dada yangu Ummy Mwalimu tambua ya kwamba, Jimbo la Msalala tuko pamoja na wewe tuko pamoja na Mheshimiwa Rais. Tunaunga mkono, mwenyewe Mbunge nimefanya ziara tayari nimewaelimisha wananchi na sasa tunasubiria usichelewe, tunahitaji Huduma ya Afya kwa Wote iweze kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Msalala kwa sasa kila Kijiji takribani Zahati zimekamilika na Zahati zote hizi ishirini na nne zimekamilika sasa baadhi ya Zahati bado hatujazifungua kwa nini hatujazifungua? ni kwa sababu ya kukosa Watumishi na kukosa Vifaa tiba. Hivyo niombe, tunapoenda kupilisha sheria hii basi Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana mkatupa jicho la pekee kwenye Jimbo la Msalala. Kwa sababu tayari Zahati ishirini na nne zimekamilika na hazijafunguliwa, zinahitaji Watumishi, zinahitaji Vifaa Tiba hivyo tunaomba basi muende mkahakikishe ya kwamba vifaa tiba na Zahati hizi zinaenda kufunguliwa na zinafanya kazi ili ziweze kutoa huduma kwenye maeneo yale. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwenye Jimbo la Msalala tuna Vituo vya Afya ambavyo vinafanya kazi. Nichukulie mfano vituo viwili tu ambavyo vimeduwa na changamoto kubwa sana ya juu ya upatikanaji wa Bima za Afya na huduma kwenye maeneo yale. Tuna Kituo cha Afya Bugarama, tuna Kituo cha Afya Runguya kumeduwa na changamoto nyingi na kubwa sana ya upatikaji

wa huduma kwa wananchi wetu, hasa wale wenye bima zile za awali. Hivyo naamini baada ya kuwa tumeenda kupidisha huduma hii ya afya kwa wote itaenda kuondoa tatizo la rushwa kwenye maeneo yale, itaenda kuondoa tatizo la kutopatiwa huduma kwa wakati, kwa wananchi wetu kwenye maeneo yale. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwani tumepata changamoto kubwa sana na haya ndiyo malalamiko ya sisi wananchi wetu kwa Wabunge kwenye maeneo yetu yale kumekuwa na huduma mbovu. Kwa sababu tu mtu akienda na fedha yule mwenye bima haudumiwi kwa wakati, anawahudumia kwanza mwenye fedha na ile fedha namna ya kuweza kui-manage inakuwa ni kazi ngumu sana matokeo yake ile fedha inaingia mifukoni mwa watu na haiendi kutatua tatizo la kununua dawa. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe ninaamini kabisa Uanzishwaji wa Huduma ya Bima hii itaenda kusaidia upatikanaji wa madawa, itaenda kusaidia upatikanaji wa huduma kwa wakati. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilifanya ziara siku moja kwenye Kituo cha Afya Runguya, nikawaeleza wahudumu na madaktari kwenye eneo lile, nikasema, ni lazima ifikie wakati sasa watumishi na Madaktari kwenye maeneo yale wanaofanya kazi kwenye Vituo vya Afya na Zahanati zetu waondoe mentality za kufanya kazi Kiserikali na wafanye kazi Kibiashara kwani huduma zinazotolewa kwenye maeneo yale ni huduma za kibiashara. Hivyo, ni bora wakaka wakatengeneza mpango kazi mzuri utakaowawezesha kukusanya mapato vizuri, kutoa huduma zilizokuwa bora na upatikanaji wa dawa kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto dada yangu Ummy uende ukazifanyie kazi, hasa katika kuboresha upatikanaji wa dawa na hii MSD.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo yetu hasa ya vijijini na hasa sisi kwenye maeneo ya wachimbaji kumekuwa na changamoto kubwa gari za MSD zinapoleta dawa. Unakuta gari kubwa limeleta dawa lakini linapofika pale linatushushia mipira mingi ya kujikinga kuliko dawa. Niombe, tunapokwenda kutekeleza huduma hii na mpango huu, kuhakikisha kwamba madawa yanaenda kupatikana. Shirika hili liende likaboreshwé na waache kutuletea mipira ya kinga kwa wingi, walete dawa ambazo zitasaidia wananchi wetu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ummy. Lakini niombe, Mheshimiwa Mollel unafahamu, tumeanzisha chuo ambacho tumepewa fedha na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Mgodi wa Barrick tumemaliza Chuo cha Afya. Niombe Mheshimiwa Waziri uje tuweze kukifungua chuo kile ili mwaka kesho kianze kutoa huduma ili tupate watumishi waende wakahudumie kule na huduma za afya kwa wote zinapokuja kuanzishwa basi ziende zikatoe huduma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi, naomba niwapongeze sana. Usichelewe dada yangu Ummy, anza kutekeleza mapema. Wananchi wa Msalala tuko nyuma yako Mheshimiwa, tunahakikisha ya kwamba huduma hii inaenda kufanya kazi vizuri. Kwani, mnafahamuu mimi mwenyewe maombi niliyokuwa nayo, kuna watu wako ndani wana magonjwa sugu hatuwezi kuwahudumia. Leo hii Mbunge nimekuwa nikipokea maombi mengi, watu wanataka fedha za operesheni, wanataka fedha za kwenda kufanyiwa *ultrasound*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Siluhu Hassan, ametuletea fedha zaidi ya milioni 750 tumeleta vifaa, *ultrasound*, X-ray ziko kwenye maeneo yale. Sasa ziende zikafanye kazi, tuleteeni wataalamu wa kutosha ili huduma ya Bima ya Afya kwa wote hii itakapoanza basi iweze kuhakikisha kwamba inatoa huduma...

**1 NOVEMBA, 2023**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## **TAARIFA**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Msalala. Pamoja na kupewa hizo fedha za vifaa tiba na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, leo halmashauri zote tumepewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa Hospitali zetu za Wilaya, ahsante sana. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa taarifa, haya tunaendelea.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapokea taarifa hii kwa mikono miwili kwani ndio utaratibu wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha ya kwamba anatuletea fedha kuweza kukamilisha miundombinu ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kukushukuru sana Mheshimiwa Ummy, chapa kazi. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100, wana-Msalala tuko pamoja na wewe. (Makofij)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. Kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, kipekee kwa kuruhusu huu Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote kuingia hapa Bungeni, kwa kweli sisi watanzania tunamshukuru sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Waziri wetu wa Afya pamoja na timu yake yote. Kwanza, najua amehangaika sana na

huu Muswada umeingia mara nyingi Bungeni, lakini hatimaye leo tunaenda kuupitisha; nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina sababu kubwa tatu za kwa nini naunga mkono hoja ya bima ya afya kwa wote. Sababu ya kwanza, tuliahidi katika llani yetu ya 2025, tutahakikisha wananchi wetu hawapati shida wakiwa wanatafuta matibabu, wananchi wetu watapata bima ya afya kwa wote. Kwa hiyo, ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia la pili ni kwamba na nchi mbalimbali, sisi wenyewe Tanzania tumeridhia makubaliano ya kimataifa na ya kikanda ikiwepo masuala ya *sustainable development goals* na *declaration* mbalimbali kwamba, tutahakikisha kunakuwa na usawa katika utoaji wa huduma za afya. Mojawapo ya eneo la kuahakikisha kwamba tunatoa usawa katika huduma ya afya ni kuhakikisha kwamba kila mtu anakuwa na access, anapata huduma ya afya kwa wakati, kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ambalo Rais amelileta leo ni utekelezaji wa maagizo ya kimataifa, *commitment* za kimataifa ambazo tuliziingia sisi ambazo hatutakiwi kujitenga na dunia, hilo la pili. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tunatambua asilimia 26 ya Watanzania ni masikini na ni takribani Watanzania milioni 15. Leo hii asubuhi wakati nakuja nilipigiwa simu na mwananchi anaitwa Jeremiah Samwel, anayetoka Kijiji cha Chilejeo Kata ya Chikuyu Manyoni. Amenipigia simu ana binamu yake alikuwa anajifungua kwa *complications*, amefanyiwa scissor katika Hospital ya St. Gaspar Itigi na amefariki akaacha mtoto ni mzima. Huyu ndugu anadaiwa 1,700,000. Nilimpigia simu akamuone Mkuu wa Wilaya, hapa sasa hivi nimeongea naye ameniambia kwamba anaelekea Itigi lakini bado hana matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu kama hawa ndio wanaohitaji bima ya afya kwa wote. Mzazi kama huyu badala ya kuhangai kumzika binamu yake anahangaika kutafuta fedha ya kupewa maiti akazike. Lakini lingine yule mtoto ni mzima. Sasa, ili apewe mtoto anadaiwa 100,000. Tunahitaji bima ya afya kwa wote. Kwa hiyo, mimi niliona nitoe sababu hizo tatu kwa nini tunahitaji bima ya afya kwa wote? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Kama nilivytangulia kusema tumechelewa nchi nyingi kama vile Ghana, Nigeria, mtani wangu pale amesema kuhusu Rwanda wameshafika mbali kwenye bima ya afya kwa wote. Sisi tumechelewa, Mheshimiwa Rais ameshafanya mambo makubwa. Sasa hivi huko tuna shule nyingi zimejengwa, zahanati nyingi zimejengwa, hospitali nyingi zimejengwa, sasa tuelekee kwenye bima ya afya kwa wote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni nini, la kwanza, Mheshimiwa Waziri tunakuamini sana na timu yako. Unapoenda kutengeneza kanuni za utekelezaji wa hii sheria tunatakayoipitisha leo hakikisha iwe shirkishi ili zile kero ambazo wananchi wanazisema zikawekwe vizuri. Lengo letu wale masikini wapate huduma ya afya, kama huyu masikini wa leo ambaye sasa hivi anahangaika kutafuta 1,700,000 ili akachukue maiti aende akazike kwao pale Chilejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho tumekuwa na mfuko wetu wa bima ya afya (*National Health Insurance Fund*). Tunapokwenda kuanzisha hii Bima ya Afya kwa Wote nadhani ni muda muafaka ku-transform hii *National Health Insurance Fund*, tunahitaji kuja na lidude kubwa, kwa nini tusije na Mamlaka? Kenya, Nigeria na Ghana wana Mamlaka. Nadhani ni muda mwafaka sasa tuibadilishe na hii *National Health Insurance Fund* tuje na *National Health Insurance Authority*, ambayo ita-cut across na kusimamia utoaji wa Bima ya Afya kwa wote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo tena nishukuru sana pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwetu kule Manyoni amefanya mambo makubwa sana. Tulipewa bilioni nne ya ujenzi wa shule ya sekondari ya wasichana, juzi hapa ametupa bilioni 1.4 ya kukarabati hospitali ya wilaya; na sasa hivi mimi kata zangu zote tuna sekondari. Kwa kweli, sisi tunamshukuru sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kusema mimi ni muumini wa bima ya afya na naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, sasa Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono kwa asilimia 100 Muswada huu ambao umefikishwa hapa leo. Pongezi zangu nyingi ziende kwa Mheshimiwa Waziri wetu Ummy Mwalimu, Naibu Waziri Dkt. Mollel, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Bima ya Afya na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kutuletea huu Muswada ili tuweze kuujadili hapa Bungeni. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kweli ameweke uwekezaji mkubwa sana kuboresha miundombinu katika hospitali zetu nchi nzima ukiwemo Mkoa wetu wa Iringa, hasa katika miundombinu, vifaa tiba, dawa na watumishi. Kwa kweli maua yake mengi sana apatiwe Mheshimiwa Rais wetu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto kwa asilimia 80, kutoka vifo 530 mpaka vifo 104 kwa vizazi

100,000 hii siyo kazi ndogo. Kazi hii aliianza tangu akiwa Makamu wa Rais; amefanya kazi nzuri sana Mheshimiwa Rais wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu tuliusubiri kwa muda mrefu sana. Mara nyingi sana umekuja hapa Bungeni tunaurudisha. Naomba niwapongeze sana hata Kamati hii ambayo imeufanyia kazi Muswada huu. Kwanza umekuja vizuri sana na mambo mengi sana mimi naona yamezingatiwa; kwa kweli nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza Serikali kwa kuwa chanzo cha uhakika cha kugharamia watu wasio na uwezo na matibabu. Hapo kwa kweli nimuunganishe hata Waziri wetu wa Fedha kwa kuona umuhimu sasa wa kuwa na chanzo cha uhakika ili watu wasio na uwezo waweze kugharamiwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt. Mwigulu, hongera sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, ambaye kwa kweli amejonesha kwamba ni Rais wa Wanyonge. Tunaona asilimia 26 ya Watanzania ambao ni kama milioni 15.8 wanakwenda sasa kuguswa na matibabu. Muswada huu leo tukiupitisha tutaweka msingi wa huduma za matibabu kwa watu wasio na uwezo; hii kazi si ndogo, Watanzania wote tunajisifu kwa kazi nzuri hii ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu sasa, wakati tunaupitisha Muswada huu, kuwepo sasa na mfumo mzuri sana wa kuwatambua watu wasio na uwezo kweli. Tusije tukaupitisha Muswada wakawa watu ambao wana uwezo tukawaweka katika mfumo huo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mfuko huu utumike kulipia wajawazito na watoto ambao wako chini ya umri wa miaka mitano. Kwa sababu tunaona ile Bima ya Afya kwa Watoto ilikuwa

imesaidia, lakini kukawa na malalamiko makubwa sana, watoto wengi walikuwa hawatibiwi wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo na mpango mzuri kwa ajili ya wazee, kwenye vituo vya watoto yatima na watu wenye ulemavu wasiojiweza ili waweze kufaidika na Muswada huu. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naomba nongoose marekebisho ya CHF kuweza sasa kutumika nchi nzima kwa sababu watanzania walikuwa wanapata shida sana na CHF. Mtu anakata CHF lakini ukienda Mkoa mwingine hautibiki, ukienda wilaya nyingine hautibiwi. Sasa hivi tumeambiwa kwamba itatibu nchi nzima. Kwa hiyo, ni kitu kizuri sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kugharamia bima kwa wananchi wasiokuwa na uwezo hasa kwa magonjwa sugu kama figo, sukari na kadhalika. Hii ni kazi nzuri sana. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa niombe sasa, kwa kweli katika Mkoa wetu wa Iringa tumekuwa na tatizo la muda mrefu sana la daktari wa mifupa. Wananchi wanapata shida sana, siku zote wamekuwa wakija huku Dodoma, hata ambulance haitoshi kwa sababu mara kwa mara kuna ajali nyingi hata za watu wa boda boda na za gari; hatuna daktari wa mifupa kwa muda mrefu. Sasa niombe, wakati tunapitisha Muswada huu, basi iangalie vitu ambavyo vinawagusa watu kama hivyo ili kuweza kukamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mwisho kabisa niombe; katika vijiji vyetu kuna baadhi ya vituo vya afya ambavyo bado havina madaktari na wafanyakazi ni wachache. Hivyo maboresho yafanyike ili kuhakikisha kwamba kila kata inakuwa na zahanati au kituo cha afya ili wananchi waweze kufaidika. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, na nampongeza Mheshimiwa Rais wetu. (Makofii)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa bado tuna muda, kwa hiyo namuita sasa Mheshimiwa Mohamed Said Issa, amalizie sehemu ya mchana.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika Muswada huu, ambao kwa mimi binafsi naunga mkono kuletwa hapa Bungeni leo na kuweza kuujadili ili kwenda kumsaidia Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kama walivyotangulia kusema wenzangu, ni Muswada ambao umekuja Bungeni mara nyingi lakini tukawa tunaurudisha kutokana na mapungufu mengi yaliyokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naipongeza Wizara pamoja na Kamati hii ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kuweza kupitia Muswada huu vizuri na kuweza kuuleta sasa ukiwa walau una sura nzuri, ambao utakwenda kumkomboa mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi nimefarijika sana kuja kwa Muswada huu kwa sababu sasa Watanzania watakwenda kupata huduma ya afya ambayo ni ya uhakika. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupongeza Muswada huu lakini mimi ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Konde kuna mambo ningependa kushauri. Naona kuna baadhi ya sehemu hazijakaa sawa katika Muswada huu. Kwa mfano, katika ukurasa wa kumi pale namba 8(d) inayosema kwamba huduma za afya zitatolewa kulingana na michango; mimi ninaona suala hili la kusema kwamba zitatolewa kutokana na michango bado linaonekana kama kuna utofauti wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba huduma hii ya afya inatakiwa iende kwa wananchi wote bila kuleta ubaguzi, kusiwe na kwamba mwenye kutoa mchango mkubwa ndiye atapata huduma hii na mchango mkubwa hivi. Huduma za afya tunajua kwamba kuna viwango tofauti, hii ni namna ya utoaji wa huduma lakini siyo zile huduma za afya zenyewe; huduma za afya zenyewe kwa magonjwa yote ziwe ni kwa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, na huduma hii inapaswa kuwa siyo ya hiari, ni kwa wote, kwa sababu gani nasema hivyo? Ni kwa sababu, wananchi wote wanahitaji hii huduma. Sasa tukisema ni ya hiari itakuwa kwamba baadhi ya wananchi wanaweza kuamua wasiingie lakini wakakutana na hii shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napendekeza huduma hii ya kuingia kwenye bima ya afya iwe kwa wote na isiwe kwa hiari. Kwa nini nasema hivyo? Nasema kwa sababu ni jukumu la Serikali na Taifa kuweza kutoa huduma sahihi kwa wananchi wote kwa magonjwa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli nimeona hapa vyanzo vya kupata fedha kwa ajili ya kaya masikini. Kwa kweli, mimi bado haijaniingga vizuri, sijafahamu vizuri, naona kama jambo hili kweli wamejitätahidi kufikiri lakini wamezungumza fedha ambazo zitasaidia kaya maskini ni zile zinazotokana na kodi ambazo zitatozwa kwenye vinywaji vikali, michezo ya kubahatisha (*betting*) n.k.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwanza ni vya mapato vya nchi kwenye Bajeti yetu Kuu. sasa leo tunavipeleka moja kwa moja huku. Na tunapokuja na bajeti hapa huwa tunaona ndivyo vyanzo vya mapato. Kwa nini tunavipeleka kwenye mfuko huu? au tume-change gear sasa tunavipeleka moja kwa moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mapato haya hii ni njia moja ya kuwakataza watu wasifanye *betting*. Unapotoa kodi kubwa kwenye

*betting* maana yake unazuia *betting*. Unapotoa kodi kubwa kwenye vinywaji vikali maana yake unazuia. Je watu wakiacha kunywa pombe kali, wakiacha kucheza hii michezo, fedha hizi za mfuko zitapatikana wapi? (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwe ni chanzo cha fedha hizi. Mimi nimefuatilia kwa makini suala hili, nachukulia mfano wenzetu nchi ya Uingereza, kule ni watu wote wanatibiwa kwa Mfuko wa Afya. Mwenye kazi na asiyekuwa na kazi lakini michango yao inakuja pale mwenye kipato officially kinakatwa moja kwa moja, yule ambaye hana michango, hana kipato, ambaye anapokea fedha za msaada wa Serikali yeye anatibiwa bure na anapata huduma zile zile za yule mtu aliyechangia. (Makofij)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nashauri bima hii iwe kwa wote, kwa lazima lakini vyanzo hivi viwe ni vya uhakika; ikiwemo kuingizwa katika bajeti kabisa bila kuangalia kwanza tunakwenda kupata vyanzo hivi vya michezo ya *betting* na nini. Hilo ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri hapa kabla ya kuja na huu Muswada aliwahi kusema kwamba Mfuko wetu wa Bima ya Afya, umechoka. Sasa leo hakuja kutueleza kwa nini sasa unakuja kupata msuli?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili tulitakiwa tutafute kwanza tiba ya kwa nini huu mfuko ulichoka? Lakini hakuja kutueleza. Tuliangalia hapa Ripoti ya CAG ilisema kwamba fedha nyingi zimechukuliwa ndani ya mfuko huu kutokana na Hospitali za Binafsi. Fedha nyingi wamelipwa ambazo zimekuja kufanya mfuko huu kuwa dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri Serikali isiogope kazi yake ichukue bima hii ya afya kwanza kufanya pilot kwenye Serikali yenyewe bila kuingiza kwenye private. lende moja kwa moja kwa wananchi kwenye Shughuli za Serikali, halafu wakiona kwamba

**1 NOVEMBA, 2023**

imefanikiwa ndipo viingie vituo vya private kwa sababu tunaogopa tunaweza kuja kukwama tena. Hili jambo ni zuri ni jambo jema, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kulileta kwa wananchi. Kwa kweli huo ni ushauri wangu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mengine unaweza kumuandikia Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa nawashukuru kwa michango mizuri.

Waheshimiwa Wabunge, watakaochangia jioni ni Mheshimiwa Neema Mwandabila, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Engineer Samwelii Hhayuma, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Eric Shigongo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Tabasam.

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 Jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

1 NOVEMBA, 2023

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022**

(Majadiliano Yanaendelea)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia.

Tutaanza na Mheshimiwa Gerald Mwandabila, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Mhandisi Samwel Xaday Hhayuma ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kuweza kupata nafasi hii jioni hii kuweza kuchangia katika Muswada huu wa Bima ya Afya kwa watu Wote. Kabla sijaenda mbali zaidi natamani kutumia nafasi hii kujipongeza Serikali ya Dkt. Samia kwa kuona umuhimu wa jambo hili na kuona kulifanya haraka kabla ya uchaguzi wa 2025 haujafika, tuwe tumeweza kuwaangalia watu wetu katika eneo la suala la bima ya afya hii kwa watu wote. Pia, nitumie nafasi hii kujipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa sababu, wakati tunajadili wakati huu wao waliweza kuliona tangu hapo, hata wakaweza kuliweka kwenye ilani yetu pendwa ya Chama Cha Mapinduzi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni kweli bima hii ya afya ilikuwa na changamoto hata tukawa tunaweza kuirudisha mara nyngi. Ilikuwa iingie tangu mwezi Februari, lakini tunaona Wizara kwa kushirikiana na timu yake wakaenda kupambana kuhakikisha wanafanya marekebisho ya kutosha kulingana na ushauri wa Kamati, lakini na Wabunge wote kadiri ambavyo walikuwa wameshauriwa. Kwa hiyo, tunapongeza Mheshimiwa Ummy na timu yake yote kwa kuweza kufanya jitihada ya makusudi kubadilisha maeneo yote

ambayo tulikuwa tunaona yana changamoto hadi kuleta Muswada huu ambao una matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge ambaye niko kwenye Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii niseme tu ninayo furaha kubwa sana kuweza kushiriki katika kujadili mjadala huu kwani naona wale watu ambao ni makundi maalum wameweza kupewa kipaumbele na kuangaliwa kwa namna gani watasaidiwa, ili waweze kuwa na uhakika wa kuhudumiwa katika afya zao, hasa pale wanapokuwa wamepata changamoto. Kila mtu anahitaji kuwa na afya njema na tunajua kabisa Taifa lolote linategemea nguvukazi ambayo iko vizuri kiafya. Kwa hiyo, kwa hili naendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kuyaona makundi haya maalum. (Makof)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu bima ya afya imekuwepo, kumekuwa na skimu mbalimbali za bima ya afya. Nataka nijikite kwenye ile bima ya afya ya watu ambao tulikuwa tumewalenga watu wengi (*ICHF*) ambayo ni bima iliyoboreshwa. Tunafahamu bima hii ilikuwa ni nzuri na nia yake ilikuwa ni njema kwa wananchi. Wananchi walipewa dhamana ya kuchangia Sh.30,000 tu lakini tunatambua kwamba, kulikuwa na changamoto kubwa katika kuhakikisha wananchi wanaingia kwenye Mfuko huu wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kufeli kwa jambo lolote huwa hakutokei hivihivi, nina imani kwamba, Waziri na timu yake wamefanya utafiti wa kutosha kujua ni kwa nini hii bima iliyoboreshwa ilikuwa inawafanya wananchi washindwe kuijunga. Kwa hiyo, zile changamoto ambazo zilikuwepo wataenda kupambana kuhakikisha wananchi wengi wanajiunga, kwa sababu unapoongelea suala la afya, ukiwa mzima huwezi ukaona shida yake, lakini pale ambapo utaumwa, ambapo huwezi kwenda sehemu yoyote kutafuta chochote, ndipo ambapo unaanza kuona umuhimu wa bima ya afya. Kwa hiyo, nimwombe Waziri kwenye hili aweze kuwa na tafiti ya kutosha kuangalia ni namna gani bima ya

afya ile nyingine ambayo ilikuwa imelenga kundi kubwa la watu ya CHF ni kwa nini ilikuwa inafeli.

Mheshimiwa Spika, na kiukweli naamini bima hii ya afya kwa watu wote itaenda hata kunusuru ule mgogoro ambaa ulikuwepo kati ya watu wa TASAF na Maafisa wetu Maendeleo ya Jamii kwa sababu, walikuwa wanalazimishwa kuingia kwenye bima ya afya kwa kilekile kipato kidogo wanachopewa cha kujikimu maisha yao. Kwa hiyo, naamini kile kiwango cha TASAF wataendelea kukipata, lakini pia watasaidiwa kwa namna nyingine kuweza kupata bima ya afya. Kwa hiyo, hili pia linanipa faraja kuona kwamba, sasa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii watakuwa katika hali nzuri ya kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu inakuja hapa, Serikali inahitaji fedha kwa ajili ya kuendesha Mfuko huu wa Bima ya Afya kwa watu Wote. Katika kuendesha mfuko huu mimi natamani kabla ya kumterm mtu kwamba, ni maskini, iangalie kila mtu kwa kiwango chake anaweza kuchangia shilingi ngapi kwenye Mfuko huu. Najaribu kusema hivi kwa sababu, natambua makundi ya watu wanapishana; kuna mtu anaweza asiwe na uwezo wa shilingi 10,000 lakini uwezo wa shilingi 5,000 anao, lakini mwengine anaweza asiwe na uwezo wa shilingi 10,000 lakini shilingi 50,000 anayo. Kwa hiyo, natamani kabla ya kumpeleka mtu kwenye hali ya kimaskini waangalie je, huyu mtu anaweza kupata angalau hata shilingi 5,000 hata shilingi 10,000 ili tu awe sehemu ya kuchangia Mfuko wetu wa Bima ya Afya. Niseme tu kwa kufanya hivyo itakuwa chanzo cha mapato cha Mfuko huu kimeongezeka. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe angalizo moja kwa maana ya kwamba, lengo la bima ya afya sio kumwongezea mzigo mwananchi. Yeyote anayechangia si kwa maana yeye anakuwa na fedha nyingi kiasi kwamba, hana majukumu mengine. Nataka kuongelea kundi la watumishi na wale wote ambaa watakuwa wamepewa dhamana ya kuchangia ambaa wako kwenye mifumo isiyo rasmi wana uwezo wa kuchangia. wanapokuwa na watoto

ambao wako shulenii, tumeona hapa umri ambao umetajwa ni miaka 21, lakini uhalisia ni kwamba, kuna watoto wa vyuo vikuu ambao ni wa wazazi ambao ni watumishi, wanaenda chuoni zaidi ya umri huo, unakuta mtu anamaliza chuo ana miaka 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kwenye hii bima iweze kueleza au watakapotunga kanuni zao waweze kueleza wazi kwamba, mtoto yeote ambaye anaendelea kuwa kwenye mahitaji au ulezi wa mzazi wake asiweze kuingizwa kwenye kundi la kujilipia bima ya afya. Nasema hivi kwa sababu, tunaona watoto wanaenda vyuoni, kunakuwa na hela ambayo inachangiwa kama bima chuoni, wakati huo huo mzazi huku anaendelea kulipa na ile hela haitatoka kwenye mfuko mwingine zaidi ya mzazi yuleyule. Kwa hiyo, unakuta huku mzazi amejiandikisha yeye labda na mume wake tu, lakini anaenda kutoa fedha nyingine kwenda kuchangia kwenye Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya watoto wake ambao bado wanamtegemea ambao wako chuoni.

Mheshimiwa Spika, kwa hili wakiweza kutuangalia kwa namna moja au nyingine, watakuwa wamepunguza machungu ya Watanzania ambao wana mzigo mkubwa wa kuendesha maisha na kimsingi maisha kwa sasa hivi yamekuwa ni magumu sana na kila mmoja wetu hapa analifahamu hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa kuongelea katika Muswada huu, kumekuwa na mpango wa kuwashudumia wazee, ambao ndio lile lile kundi la wenyewe uhitaji, kiukweli huduma kwa wazee hazikuwa nzuri kwa kiwango hicho. Hazikuwa nzuri kwa kiwango hicho kwa sababu, kwanza hata maeneo waliyokuwa wanapewa huduma kulikuwa na hali fulani ya unyanyapaa.

Mheshimiwa Spika, sasa basi tunajua bima zinazoenda kutengenezwa zitakuwa na kiwango fulani cha huduma. Magonjwa makubwa yanapokuja, mfano magonjwa ambayo mtu labda anatakiwa kwenda hospitali kubwa kama Muhimbili, huko Mloganzila, sijui Jakaya Heart Institute kwa hiyo, unakuta kwamba,

wazee wengi hawatakuwa na uwezo wa kwenda huko na ni wazee wetu tunawapenda, tungependa waendelee kuishi na hawana uwezo. Nafahamu sio wazee wote ambao hawana uwezo, lakini wapo ambao specifically ni kweli hawana uwezo, wangeangaliwa au wangetengewa namna ya kuweza kusaidiwa mpaka huduma ya mwisho kabisa kwa sababu, tunapoongelea huduma ya bima ya afya kwa watu wote lengo ni kuweza kum-cover mtu katika hali zote.

Mheshimiwa Spika, najua kwamba, wana utaratibu mzuri wa kuweza ku-screen watu kutenganisha kwamba, huyu anaweza akahudumiwa kwenye *level* gani, huyu *level* gani na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kama wataweza kujiongeza na kufanya katika maeneo hayo, kweli, Watanzania wengi wataweza kupona na afya zao zitakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, pia hata wale wote watakaokuwa wamepewa zile bima za bure; sidhani kwamba, lengo lao ni kwamba, wakiumwa kichwa au wakaumwa tumbo ndio waweze kuhudumiwa, lakini watakapoumwa yale magonjwa magumu ambayo mtu hana chochote basi waangalie namna ya kuweza kuwasaidia. Natambua kumekuwa na utaratibu wa kutoa misamaha kuititia ofisi mbalimbali za Maafisa Ustawi wa Jamii, lakini kumpa Afisa Ustawi wa Jamii uwezo wa kutoa misamaha, wakati mwingine wamekuwa wakitoa misamaha *fake*, kitu ambacho kinakuwa kinaendelea kuipa Wizara mzigo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama watakuwa wanatengeneza kanuni zao, waangalie namna ya mambo yote haya watayawekaje ili kuweza kulisiaidia Taifa letu. tunajisikia vibaya kuona kwamba, mfuko wetu huu wa bima ya afya ya Taifa unatumia fedha nyingi wakati mwingine kwa hali za kisanii tu, inakuwa sio sawa. Kwa hiyo, kama watatengeneza udhibiti mzuri, naamini mambo mengi yataenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niweze kusema nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma na Mheshimiwa Festo Richard Sanga ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia muswada huu. Katika jambo ambalo limefanyika vizuri, yako mengi yaliyofanyika vizuri, lakini jambo hili haki ya Mungu, kwa kweli, tunampongeza sana Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa sababu, taarifa ambayo ametupa hapa kwamba, kwa kipindi hiki kifupi cha Serikali ya Awamu ya Sita vimeongezeka vituo vya afya vingi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukulie tu kwenye jimbo langu, vituo vilivyoongezeka ni vituo vine. Kwa hiyo, ukijumlisha na sehemu nydingine ni vituo vingi kama alivyosema. Kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameliona jambo hili kwa sababu, uhai wa binadamu ni afya. Tunapoteza baadhi ya watu wetu kwa sababu, hawana uwezo, wanashindwa kufanya matibabu. Sasa Wizara kupitia Rais wetu wameliona hili kwa kweli, sasa wananchi wetu wanakwenda kupona. Kwa hiyo, tunashukuru sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri hii waliyoiona kwamba, sasa tunakwenda kuwaponya Watanzania kwa kupitia Bima ya Afya kwa Wote. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, watu ambao wanakadiriwa kupewa, takribani watu 15,800,000 hivi, sio kitu kidogo ni watu wengi sana. Hapo ndio tunapozungumza kwamba, Rais amefanya mambo makubwa katika nchi hii. Ndio tunapojumlisha hapo tunaposema sasa Rais ametoa ma-bi na ma-bi na ma-bi, sio kitu kidogo hiki. Kwa hiyo, tunapongeza sana jambo hili la kuwapa watu wetu bima ya afya kwa wote. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ombi langu, leo sina mchango mkubwa sana mambo ni mazuri. Ombi langu, ni mawili, moja; Wizara ya Afya ihakikishe inaongeza viwanda kwa ajili ya dawa, ili kusudi viendane sasa na uhitaji wa dawa katika nchi yetu. Tunaishukuru Serikali kwa kutupa sisi pia, Mkoa wa Njombe, hususan Jimbo la Makambako, kujenga kiwanda cha dawa, tunasema tu hapa Makambako na Watanzania ahsante sana, waendelee kuhakikisha viwanda hivi vinakamilika. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, ombi la pili, *ambulance* katika kituo cha afya ambacho kiko mbali kidogo na hospitali yetu iliyoko pale Makambako. Kituo cha afya hiki kiko mbali kiko Kitandililo, kwa hiyo, tunaomba sana katika mgawo wa *ambulance* iandikwe moja kwa moja kwenda Kitandililo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la tatu; sasa tuone namna ambavyo hawa watu watakaokuwa wanapata, tusiingie kwa mfano kwenye TASAF, wako watu wanapewa zile fedha za kwamba, hawa ni wazee wakati watu wenyewe wana uwezo. Kwa hiyo, hili liangaliwe lisijirudie huku, wapewe watu ambao tunadhani huyu hana uwezo, ndio waweze kupewa kwa hiyo, litakuwa ni jambo zuri. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo sasa mimi kama mzee, Mheshimiwa Ummy pamoja na Naibu Waziri wake wanafanya kazi hii kwa maslahi ya Watanzania, wanatembea usiku na mchana wakitumwa na mama na Rais wetu. Wameacha pia, majimbo yao, ombi langu kwa Jimbo la Tanga na ombi kwa Jimbo la Mheshimiwa Naibu Waziri kwa sababu, anawaponya Watanzania, tunaomba ninyi wananchi wa Tanga wa Jimbo la Mheshimiwa Ummy Mwalimu wahakikishe wanafanye mambo mawili, moja, kumwombea kwa Mungu afike 2025. La pili, kuhakikisha 2025 wanatoa kura nyingi kwa Rais, pia wanatoa kura nyingi kwa Mheshimiwa Ummy Mwalimu na wanatoa kura nyingi kwa Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa sababu, anawatumikia Watanzania. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wako watu wanatembea wanasema wanasikiliza kero za wananchi. Niwaambie Watanzania wenzangu, kero za wananchi zitatolewa na Chama Cha Mapinduzi kupitia Serikali yake, hao wengine wanawadanganya. Kama hivi sasa, tayari kero hii ya watu ambao hawana uwezo, Serikali ya Mama Samia tayari inatoa bima kwa wote. Kwa hiyo, hawa watu wengine wanawadanganya, wanapita huko wanawaambia sisi tunasikiliza kero, thubutu, hamna kitu chochote, watakaowatolea kero ni Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru. Mwisho, ombi la Watanzania kupitia Bunge hili na Watanzania wenzako walioko Mbeya kwa namna ambavyo tulikuwa tunakuombea ili litimie hilo la kuwa Rais wa Dunia, tunakushukuru sana na Mungu akubariki. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Festo Richard Sanga na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu wa Bima ya Afya kwa Wote. Naomba nianze kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Mollel na watumishi wote wa Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, safari hii haikuwa nyepesi. Nilikuwa kwenye Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, tulivutana sana. Niwapongeze watu hawa hawakulala muda mwingi, wamepambana ili kufikisha Muswada huu hapa ambapo umefika. Hongereni sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pia, niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo inafanyika kwenye sekta ya afya. Mmetoa taarifa kwamba, angalau vifo vyatya akinamama vimepungua, vifo vyatya watoto chini ya miaka mitano navyo vimepungua. Naamini haya ni matokeo chanya ya

uwekezaji ambayo yamefanyika kwenye sekta ya afya kwa kujenga vituo vya afya, kwa kujenga zahanati, kwa kujenga hospitali za Wilaya, kwa kujenga hospitali za rufaa za mikoa, lakini pia kwa kujenga hospitali za kanda.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze kwa kazi kubwa ambayo imefanyika, hasa ndani ya Wizara, lakini nimpongeze sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, nakumbuka maneno yake wakati alipokuja Hanang, alisema yeye afya ni namba moja, elimu, masuala ya maji. Kweli hili tunaliona kwa maboresho ambayo yanafanyika kwenye sekta ya afya. Nampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo inafanyika, lakini pia, Mheshimiwa Waziri na timu yake niwapongeze sana, tulikuwa na mvutano kwenye maeneo kadhaa; moja ilikuwa yale maeneo ya kufungamanisha, hasa kifungu kile cha 32.

Mheshimiwa Spika, sisi tulikuwa tunasema ukifunga leseni za biashara, tunahimiza watu warasimishe biashara, tunahimiza kuongeza base ya walipa kodi lakini ukibana wewe maana yake ni kwamba hayo yote mengine yameshindikana, *ina-contradict* na mipango mingine ya nchi lakini mmekubali mmeliona hili.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la leseni. tulisema kwamba, suala la leseni ni suala la ajira kwa vijana wetu, ukisema kwamba unaibana kwenye eneo hili ni lazima mtu awe na bima kwanza, unaongeza gharama ya mtu kupata leseni. Sasa, hayo yote mmeyaona nawapongeza sana kwa akili chanya ya kuwasaidia Watanzania ambao walikuwa na changamoto kwenye eneo la afya.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umechelewa, ulikuwa unahitajika jana siyo leo, nawapongeza kwamba tayari angalau tumepiga hatua. Nafahamu kwa sababu mimi nilitoka sekta ya afya, nimekuja mara nyingi kwenye meza zenu kwa ajili ya kuleta malalamiko na namna ya kuwasaidia wananchi wangu. Wengine waliokwama kwa ajili ya kuwasaidia ndugu zao ambao wako

hospitalini wanataka msaada wa matibabu kwa sababu gharama zimekuwa kubwa. Hayo yalikuwa ni mengi lakini mara kadhaa mtu amefariki, watu wanalia nyumbani maiti imeshikiliwa hospitali, tungekuwa na mfumo huu wa Bima ya Afya kwa Wote, hizo changamoto tusingezipitia. Ninaamini huu ni mwarobaini na ni wakati sahihi.

Mheshimiwa Spika, niseme maeneo manne tu ambayo mimi napenda nishauri. Eneo la kwanza, kwenye eneo la elimu kwa umma ambalo ndiyo tumeshauriana kwamba ndiyo namna pekee ambayo tunaweza kuwasajili watu wengi, wajisajili kwa hiari bila kusukumana, bila Polisi, bila kukamatana.

Mheshimiwa Spika, tutumie mifumo ya kawaida ya kijamii, kwa sababu suala la afya ni suala la kijamii. Mtu akipata changamoto jamii inahusika. Kwenye utaratibu wetu wa kawaida wa maisha, maeneo mengi ukitoa mijini kidogo kuna utaratibu tofauti lakini sisi tunaotoka vijiini, kuna wale Wenyeviti wanaoshughulika na masuala ya kijamii sherehe, magonjwa, misiba. Tuwashirikishe wale ili angalau hili jambo la Bima ya Afya kwa Wote, liwe jambo la jamii badala ya kuwa jambo la Serikali. Tukitumia mfumo wetu wa kawaida ule wa elimu kwa umma, tutatumia TV na mifumo mingine, tunashusha kutoka juu kupeleka chini. Hii itakuwa ngumu kwa watu kuipokea. Tuanzie kule kwenye grassroots tupande juu, hii elimu itaenda kwa urahisi. Hilo ni eneo la kwanza ambalo mimi nataka nichangie. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni eneo la kuwatumia watumishi wetu sawa sawa ili watu waweze kutumia huduma za afya kwenye taasisi za Serikali, vituo vya afya vya Serikali, zahanati na hospitali za Serikali. Tuangalie namna ya kuwatumia wataalam wetu vizuri. Kama wataalam hawa ambao tunao kwenye sekta ya umma ndiyo wanaokwenda kufanya kazi sekta binafsi, tuangalie mechanism kuhakikisha kwamba yale wanayofuata sekta binafsi, wanayapata kwenye sekta ya umma. Kwa sababu, mwishoni aliyehudumiwa kwenye sekta ya umma na anaehudumiwa kwenye

sekta binafasi au kwenye hospitali binafsi, wote wana mfumo wa malipo sawa sawa.

Mhehimiwa Spika, kama kule wanaweza, Serikali inashindwa nini? Hebu tuboreshe, tuangalie kama kuna *incentives* zinazotakiwa, siyo kila wakati tu utaratibu, utaratibu, utaratibu, hii itatukwamisha. Tutafute namna ya kutoa *incentives* kwa watumishi. Badala ya kwenda kutumia muda wake kwenye sekta au hospitali binafsi, tuangalie namna ambavyo tunaweza kum-accommodate kwenye hospitali ya Serikali akafanya kazi ile. Wale wanaozalisha, kwa maana ya wale ambaao ni *productive*, tuone namna ya kuwapa tuzo (*incentives*) ili hatimaye huduma za afya ziwe nzuri kwenye sekta ya umma.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni eneo la bima za magari, namna ambavyo inaweza ikatibu watu wambao wanapata ajali. Tuna vijana wetu wengi, vijana wa bodaboda wanapata ajali sana kwa sababu ya aina ya vyombo wanavyovitumia. Tunapata ajali za magari na hii niseme tu nakushukuru sana, ulinipa nafasi ya kwenda kujifunza Ghana. Wenzetu wanatumia eneo hili la bima kama chanzo cha mapato ya bima. Kwa sababu, vyombo vyaa moto ni kweli wanalipia bima, sasa, badala ya mtu amepata ajali unahangaika namna gani anaweza kupata matibabu, wakati huo ambapo tunahangaika hangaika, hebu litumieni hili eneo ili tuhakikishe kwamba, wale amabao wanapata changamoto za ajali, mtu amevunjika badala ya kuhangaika.

Mheshimiwa Spika, natoa mfano wa Jimboni kwangu, kwa sababu ya mifumo tu migumu wanaenda kutibiwa kienyeji, wakati mwingine wanapata hasara kweli kweli, wanaumia. Hebu tutengeneze mfumo ambaao utaunganisha bima za vyombo vyaa moto na hii bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo mimi nataka nichangie jioni hii ya leo, ni upande wa teknolojia. Serikali imewekeza fedha nyingi sana kwenye vifaa na vifaatiba. Sasa,

teknolojia hizi nyingi zinatoka nje ya nchi, kwa sababu teknolojia zinatoka nje ya nchi, tunao wataalam ambao tayari tuweshawafundisha nchini lakini si wateknolojia mahsus. Ili tuboreshe huduma kwenye maeneo yetu hasa sekta za umma, maana yake hospitali zetu, tuone namna ya kuhakikisha kwamba zile *technology transfer* zinafanyika ipasavyo. Pia kunakuwa na *training proper* ya vifaa tunavyovinunua kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kuna maboresho mengi sana yamefanyika kwenye upande wa teknolojia-tiba lakini bado haitoshi kwa sababu, kila wakati teknolojia inabadilika. Serikali iweke mpango mahsus wa manunuzi ya teknolojia lakini wa mafunzo ya wataalam wa vifaa na vifaatiba. Hii itatusaidia kwamba, vifaa tutakavyovinunua vitatumika sawa sawa na hatimaye vitaleta tija ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme tu Mheshimiwa Waziri, pamoja na pongezi zangu zile za mwanzo, hiki ndicho tulikuwa tunakisubiri. Imefika wakati muafaka, ninaamini changamoto tulizokuwa tunazipata kwenye maeneo yetu kwamba, kwenye upande wa wazee kila mkuano unaokwenda Mheshimiwa Mbunge, bwana hili la wazee halieleweki. Ninaamini tukiwa na bima ya afya kwa wote itaeleweka.

Mheshimiwa Spika, akina mama wajawazito hilo nalo litaeleweka na ninaamini pia, matibabu ya watoto chini ya miaka mitano hili nalo litakaa sawa. Ninachoomba tu Mheshimiwa Waziri, utekelezaji uanze mapema. Tuanze taratibu, hakuna kinachoshindikana. Tukianza ndiyo tutajua sehemu gani ambako kuna mashimo na hatimaye mashimo haya tuyazibe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa nafasi. Ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Festo Richard Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mheshimiwa Eric James Shigongo ajiandae.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Muswada huu wa Bima kwa Wote.

Jambo la kwanza, niseme tu ninaunga mkono asilimia 100, kwa hili jambo kuja kufanyika wakati huu ambao ni wakati sahihi sana kwetu, tunaona kwa sababu ya yale ambayo nyuma tulikuwa tunaona ni changamoto lakini kwa sasa yamepatiwa ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mama Samia Suluhu Hassan. Kwa sababu, kwanza anaenda kuandika historia, kwa kulipitisha hili jambo kipindi ambacho yeye ni Rais akiwa madarakani. Pili, kwenye utekelezaji wa Ilani. Ujisoma kwenye Ibara ya 9 (d) "kutoa huduma kwa wote" na Ibara ya 83 "kuimarisha mfumo wa bima wa afya nchini". Kwa hiyo, kwetu sisi hili ni goli na ni ushindi kwenye Chama cha Mapinduzi, kwa sababu yale tulioandika kwenye Ilani sasa yanatekelezwa na yanaendelea kutekelezwa kwa kiwango cha juu sana. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Wizara na Mheshimiwa DKT. Mollel, kwa jinsi ambavyo wamekuwa wavumilivu licha ya maneno na kauli za hapa kwenda juu lakini amesimama imara kuhakikisha hili jambo hatimaye leo linafika hatua hii ambayo leo hii imefika. Pia, Wizara ya Fedha na wengine wote, baadhi ya Mawaziri kwa hatua hii ya kuleta hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo langu lingine niseme tu kwamba, Watanzania wanaotusikiliza, hili jambo kama Taifa kwanza tumechelewa. Hii ni ajenda ya Kidunia. Dunia nzima wanaenda kwenye Bima ya Afya kwa Wote. Kwa hiyo, kusiwepo na chama au

mtu au mpotoshaji yejote atakayewaambia Watanzania hili tumekosea. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo uso wa dunia unavyolitazama hili jambo kwa sasa. Wenzetu majirani zetu Kenya wameshapitisha huu Muswada. Zanzibar wameshapitisha huu Muswada. Tulibaki Tanzania na tulivyobaki tulikuwa na sababu za msingi, kwa sababu tulikuwa na vitu ambavyo watu wamepigia kelele na Serikali imeshachukua hatua. Jambo kubwa ilikuwa ni kufungamanisha bima ya afya na mambo ya vitambulisho na leseni na vitu vingine lakini Serikali imeona haja ya kuondoa hilo jambo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine kilikuwa ni *funding*. Kwa kweli watu tulikuwa na changamoto ya kuangalia *funding* itatoka wapi lakini niipongeze Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Wizara ya Afya, kwa kuoanisha hivi vyanzo vya mapato ambavyo vinakwenda kutusaidia kwenye utatuzi wa kero ya Bima kwa wote ambapo Watanzania wengi zaidi ya milioni 15 wanaenda kufaidika.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na wasi wasi hata upande wetu wa pili huko, wamezungumza kwamba tumekosea kuweka hivi vyanzo. Hivyo ndiyo vyanzo tulivyonavyo kwa sasa. Lazima tuanze kama Taifa kwenda mbele. Kuna mchangiaji alizungumza kutokea upande wa pili kwamba, tumekosea kufanya hili jambo. Mimi naona tuko sahihi. Hatua ya kwanza tumeianza, hatua ya pili itafuata. Hili ni Taifa letu sisi siyo kisiwa. Lazima tusonge mbele kwenye suala la Bima ya Afya kwa Wote, kwa sababu tofauti na hapo labda wangependekeza vyanzo gani ambavyo ni sahihi kuliko hivi ambavyo tuko navyo sasa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naona Serikali yangu iko imara na iko vizuri. Vyanzo hivi ndiyo vyanzo sahihi na ndivyo ambavyo tulikuwa tunavitafuta Watanzaia. Tuwe na uhakika pa kuanzia, haya mambo mengine yatakuja kufuata baadaye.

Mheshimiwa Soika, ombi langu ni moja; suala la Bima kwa Wote siyo suala la Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Suala la Bima kwa Wote siyo suala la Wizara ya Afya peke yake. Suala la Bima kwa Wote ni suala la Wizara zaidi ya tatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapo unamzungumzia Mheshimiwa Ummy Mwalimu leo lakini kuna TAMISEMI wanaokwenda kuajiri watumishi. Pia, kuna Wizara ya Fedha inayokwenda kukusanya haya mapato, kwa maana ya *betting* na hivyo vipodozi. Naomba tusilitazame hili suala kama ni la Mheshimiwa Ummy Mwalimu wa Wizara ya Afya peke yake. Mheshimiwa Ummy ameanza, sisi wengine na Wizara zingine wasimuachie mzigo huu Mheshimiwa Ummy Mwalimu peke yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili hili suala la Bima ya Afya kwa Wote lifanye kazi, lazima ajira ziwepo kwa sababu kuna changamoto. Ukienda Makete kule Uganga, unakuta mtumishi yuko mmoja kwenye kituo cha afya au kwenye zahanati. Tukiwa na huu mchakato wa kutokuwa na watumishi wa kutosha kwenye hivi vituo vya afya na zahanati, hili suala litaendelea kuonekana ni kero kwa wananchi. Kwa hiyo, ni vema Wizara ya TAMISEMI ikalichukua hili jambo, kwa sababu wao wana wajibu wa kuajiri watumishi. Wakaisaidia Wizara ya Afya, wakaisadia Serikali, wakamsaidia Mheshimiwa Rais kuwaajiri watumishi wengi ili waweze kulisaidia Taifa letu na baadaye uonekane umuhimu wa hili jambo ambalo tunalifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni suala la elimu. Taifa letu lina changamoto ya kupotosha Umma. Upotoshaji umekuwa ni mkubwa. Sijui changamoto ni kwamba mizani either haija-balance! Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mollel yeye anasema ana changamoto, watu wenye akili huwa wanateseka sana kwa pale wanapokutana na watu wenye changamoto ya kupotosha potosha mambo. Mheshimiwa Ummy, hili jambo sasa hivi kuna watu watajitokeza kuanza kulipotosha au kuonesha kwamba

haliwezekani au kuonekana kama Serikali imeamua kitu tofauti. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ni vema sasa Serikali ikachukua hatu kwenda huko chini *grassroot level* kabisa. Mikutano; sisi Wabunge tuna wajibu wa kuelimisha lakini watendaji wa Serikali, Wakurugenzi na Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata kuwaelimisha wananchi umuhimu wa hili jambo kama Taifa letu ili tuweze kuvuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ummy naomba kabisa kwamba, Wizara ina haja ya kuanza sasa kujenga na kutoa elimu kwa nguvu ili wapotoshaji wengine wasipate nafasi ya kudanganya Umma. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni upatikanaji wa madawa. Hili jambo ni lazima tuliboreshe. Mheshimiwa Ummy tunahitaji sana ili Bima ya Afya kwa wote iweze kufanya vizuri, ni lazima upatikanaji wa madawa uweze pia kuendana na kasi ya hili jambo linavyokwenda. Kumekuwa na changamoto MSD. Muda mwingine halmashauri zinatuma fedha kwa ajili ya kununua dawa, zinachelewa. Sasa, ili na sisi tupate kuzungumza na wananchi vizuri, ni vema dawa zikapatikana kwa wakati lakini zikapatikana kwa wingi ili hili jambo tunapokwenda kulijengea hoja kwa wananchi, liweze kupata baraka na liweze kupata muono wa pamoja na baadaye likawa na faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la kwamba, tumeona hapa vyanzo ni vingi kuna betting, kuna vipodozi, soft drinks na hard drinks, tumeziona hapa. Ni Wizara kuwa na account moja kwa ajili ya kusimamia hili jambo la bima ya afya. Hizi fedha zote zikiwa na account moja na ikipendeza, Wizara ya Afya yenewe kwa sababu mzigو wake siyo mkubwa sana, wakiisimamia itakuwa na tija ili tuweze kufanya suala la kujua maendeleo ya Mfuko wetu wa Bima ya Afya ukoje. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi sina mambo mengi lakini naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hili aliloliamua, kama Wabunge

tunaandika historia kwa wakati mwingine, kwenda kupitisha jambo lenye tija na maslahi kwa Taifa. Hii ni token ya ushindi wa Chama cha Mapinduzi kuelekea 2025. Hakuna mtu atasimama kinyume na hili jambo kwa sababau linakwenda kufanikiwa na kwa sababu pia limekuja katika mlengo mzuri. Kwa hiyo, naipongeza sana Wizara, nampongeza Mheshimiwa Rais lakini nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kuunga mkono. (Makof)

Mheshimiwa Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Makete na wote ambao wanatusikiliza, tunaunga mkono jitihada hizi za Serikali. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia jambo hili muhimu kwa ustawi wa wananchi wetu lakini kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kuipongeza sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. Jambo hili tulikuwa tunalishubiri sana sana, kwa muda mrefu Watanzania kama Taifa tulikuwa na kiu ya watu wetu wote wapate tiba. Utakumbuka siku za nyuma sisi sote tulikuwa tunakwenda hospitalini tunapata dawa bure, tunapata sindano bure. Sasa, lilituzoesha lakini ilivyokuja hatua hii ya kulipia huduma hizi za afya, shughuli ikawa kubwa kweli kweli. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ndipo hapo sasa baadhi ya Watanzania walikuwa wanawatumia viongozi wa nyanja tofauti tofauti kuomba ahueni. Kuomba namna ya kuweza kupata hizi huduma. Hivi leo Serikali hii ya Awamu ya Sita kulitekeleza hili, kwa kweli ni jambo la kuponbezwa sana sana na Watanzania wote. Hivyo, natumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi haya. Kwa sababau, ingewezekana kabisa, kwa namna jambo

lenyewe liliivyokua linaenda angekata tamaa. Lakini Mama huyu kwa mapenzi na mapendo makubwa ya Watanzania hakukatishwa tamaa, amelisimamia hatimaye leo limefikia katika hatua hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nawapongeza wasaidizi wake. Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, Mheshimiwa Dkt. Mollel lakini na wataalamu wote. Hawakukatishwa tamaa kwa namna yoyote ile. Jambo hili limekuja, limekuja, limekuja lakini watu hawa hawakukata tamaa. Wameenda kuboresha yale yote yaliyokuwa yanaonekana kwamba yanakwenda kukwamisha huu Muswada. Hatimaye leo tunaenda kujadili Muswada huu. Waswahili wanasema "kawia ufike" na leo tumefika. Ahsanteni sana Mheshimiwa Waziri na timu yako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kilichonisimamisha hapa pamoja na pongezi hizi, ni eneo lile la Vitita. Nimefarijika sana na suala hili la vitita na nimefarijika zaidi hasa kitita kile cha CHF kuingizwa kwenye huu Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote. Kwa sababu, nakumbuka pale nyuma ulikuwa na shida fulani kwa sababu huduma yake ilikuwa inatolewa kwa mipaka. Kwa maelezo ya Muswada huu, sasa hivi huduma yake inaenda kote. Binafsi lakini na wapigakura wangu wamenipigia simu, wamefarijika sana pale uliposema suala hili la Vitita vya CHF. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Pili, hapo katikati pia tulikuwa na Kitita cha Ushirika Afya. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo ilifanya jambo hili jema sana na wanaufaika hasa yale maeneo yaliyokuwa na AMCOS, walichangamkia sana. Bahati mbaya sana kwenye huu Muswada sijui tumesahau au imekuwaje, sijasikia. Sasa, wapigakura wangu wamenipigia simu, imekuwaje hili suala la Ushirika Afya? Mbona hatujaliskia? Mengine yote wanayaunga mkono kabisa kabisa lakini hili halijasikika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba hapa Mheshimiwa Waziri atolee ufanuzi ili wale wananchi wangu kule wapate kuelewa. Kwa

sababu, wako tayari kuchangia kupitia Ushirika Afya. Hii inaweza kupunguza mzigo mkubwa sana kwenye upande wa *funding*, kwa sababu mwisho wa siku wanaweza wakaongezeka kundi la watu lisiloweza kuchangia, kumbe lilikuwa na eneo ambalo lingeweza kuchangia vizuri mfuko huu. Kwa hiyo, naomba hapa Waziri atolee ufanuzi hili eneo la Ushirika Afya imekuwaje, kwa sababu limefanya vizuri maeneo ya kahawa, maeneo ya korosho na maeneo ya pamba. Limefanya vizuri sana, kwa hiyo lingekuwepo hapa lingeendelea kuboresha maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ninaomba yawezekana wakati huu tunapitisha Muswada huu pengine patakuwa na kipindi cha mpito. Watu hawa wa Ushirika Afya sasa hivi wana kadi lakini hawajaruhusiwa kuhuisha zile kadi. Hii inawapa shida sana. Sasa hivi mimi ni mhanga wa eneo hilo. Wako wagonjwa hospitalini wanashindwa kupata huduma, kwa sababu huduma ile sasa inahitaji fedha kwa asilimia 100, pale walipokuwa na Ushirika Afya walikuwa wanaweza kutibiwa na walikuwa wanaweza kabisa kupata huduma hizi pasipo hata kuomba msaada eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba sana kama kutakuwa na kipindi cha mpito, basi wale wenye kadi waruhusiwe pengine kuhuisha kadi zao hadi kufikia kipindi ambacho sasa hii Bima ya Afya kwa Wote itakapoanza kuchua hatua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwa sisi tunaotoka vijiji, wamesema wenzangu hapa, tuna shida kubwa sana ya maeneo haya ya kutolea huduma. Natambua ipo jitihada kubwa sana ya Serikali yetu hii ya kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali. Naomba sana jitihada hii iongezeke zaidi, kwa sababu kwa maeneo ya vijiji unaweza kukuta kata nzima haina hata kituo cha afya hata kimoja, hata zahanati ya kutolea huduma. Hili jambo linaweza kuleta tatizo kidogo katika utekelezaji wa huu Muswada. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake, naunga mkono sana, na wananchi wangu wamenipigia simu hapa, wanaunga mkono sana Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nakushukuru sana kwa nafasi hii. (Makofii)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, na Mheshimiwa Kilumbe Shabani N'genda, ajiandae.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kulitendea mema Taifa lake. Mara kadhaa nimezungumza, na leo tena nitasema na nitarudia kusema kila siku, *we have the most intelligent, most smart President in Africa.* Kwa hiyo, nimesimama hapa kukushukuru wewe pia kwa namna unavyoliongoza Bunge letu Tukufu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna tunavyofanya kazi yetu kwa uadilifu wa hali ya juu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunaismamia Serikali yetu vizuri sana. Mtakumbuka tulifanya kazi nzuri sana kwenye Mkataba wa DP World, tumefanya vizuri sana kwenye mkataba huu pia, tuendelee kulitumikia vizuri Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka mmoja uliopita nilimtembelea mtu mmoja amekaa hapa nyuma ofisini kwake, na hii ilikuja baada ya kuuguliwa na mama yangu. Nikampeleka hospitali moja pale Dar es Salaam, sitaki kuitaja jina, akapimwa kipimo kinaitwa MRI, baadaye tukapewa *referral* ya kwenda Muhimbili. Tulivyofika Muhimbili, akapimwa kipimo kile kile tena kwa sababu hawakuweza

kupata majibu ya hospitali tuliyotoka. Kwa hiyo, ikawa vipimo mara mbili.

Mheshimiwa Spika, hiyo inaitwa *duplication of care*. Kwa sababu hiyo NHIF ikalazimika kulipa mara mbili kwenye kipimo hicho hicho kimoja. Nilipotoka hapo, nilimfuata huyo mtu ofisini kwake, yupo hapa nyuma ananisikiliza. Nikapata muda wa kujadiliana naye ofisini kwake. Nikamwambia, ninauona Mfuko wa Bima ya Afya unakwenda kufa kwa sababu ya matibabu kufanyika mara mbili mbili. Tulizungumza pale akanipa *document* moja nikaenda kuisoma, ilikuwa ni ya *actuarial study* iliyofanyika na ILO, ikiwa inatabiri kwamba Bima ya Afya ingeendelea hivyo 2026 ingekufa. Sikuwa tayari ife, nikaanza safari ya kutaka kuuokoa huu mfuko. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa nimekutana na Mheshimiwa Waziri, nikamwambia ipo sababu ya kufanya kila tunachoweza kuuokoa mfuko huu kwani unasaidia Watanzania maskini. Mheshimiwa Waziri ni shahidi. Sasa katika hilo, naunga mkono kabisa sheria hii ipite, kabisa asilimia mia moja. Sina cha kusema marekebisho yamefanyika, nimeridhika kwa niaba ya wananchi wa Buchosa, sheria hii ipite. Hata hivyo nina mabo matatu ya kutoa angalizo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni mifumo. Mifumo haisomani. Hospitali moja hadi nyingine unarudia vipimo. Muhimbili pale pale, ndani ya Muhimbili kuna M NH na kuna MOI. Ukitoka M NH kwenda MOI mifumo haisomani. Hii inasababisha NHIF iingie hasara kubwa sana kwa kuwa na matibabu mara mbili mbili. Ikiendelea hivi, hata tukibadilisha sheria itakuja kufa. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mfumo wa kuendesha NHIF uboreshwe uwe ni mfumo unaosomana. Mheshimiwa Waziri ni shahidi, nilitafuta mpaka wawekezaji kutoka Marekani nikamletea ofisini kwake, wakakaa kikao, wakajadiliana wakakubaliana kwamba mfumo unaotumika unaitwa *Electronic Medical Record*

ambao kila hospitali una mfumo wake. Ili tufanye vizuri tunahitaji mfumo unaoitwa *Electronic Health Record System* ambao unakusanya zile *IMR* zote pamoja zinakuwa zinasomana. Mgonjwa akitoka Buchosa leo akifika hapa, majibu ni kuyaita tu yanakuja na mnayaona. Kwa kufanya hivyo, tutaokoa fedha nyingi sana na mfuko wetu hautakuwa na hasara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hilo ni la kwanza. La pili, ni wizi (*fraud*), sina kumbukumbu vizuri kama kuna kuna mfuko mwengine katika nchi hii unaibiwa kama *NHIF*, sina kumbukumbu. Ukweli ni kwamba kuna watu wamekuwa mabilionea kwenye Taifa hili kwa sababu ya *NHIF*, ninyi ni mashahidi. Lazima tupitishe sheria kifanyike kila kinachowezekana Mheshimiwa Waziri na wanao nimesikiliza huku nyuma, kudhibiti *fraud*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mmoja hai, huwezi kuamini. Kadi ya Bima ya Afya sikuhizi ni pesa. Mtu anaweza akaenda nayo mahali, akamwambia mwenye hospitali nipatie Shilingi 30,000/= hapo nikanunue chakula. Akampa Shilingi 30,000/=, aka-sign document akaondoka. Huku nyuma daktari anajaza anachotaka. Wanajua. Wiki iliyopita nimemkamata mtu Songea anafanya kitu cha namna hiyo hiyo. *That for*, hata kama tunapitisha sheria, lazima tu-control *fraud*. Tofauti na hapo, mfuko huu niliwahi kusema ulikuwa *ICU* wakati fulani, watu wakakasirika. Tofauti na hapo, utarudi *ICU* tena, sheria hii tulioiletia inautoa mfuko huu *ICU* unauleta *HDU*, wodi ya kawaida. Baadaye itakwenda wodi ya kawaida atapata *discharge*, lakini kama hatuwezi ku-control *fraud* kwa vyovoyote vile itakufa tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimesikiliza sana na nimeusoma Muswada huu, nahitaji kuona tunawekeza sana kwenye preventive medicine. Tuzuie watu wetu wasiugue. Badala ya kusema watu wauguwe tutawatibu, hatuna uwezo wa kuwatibu. Huko nyuma nilisema, narudia tena leo, ipo siku mtanielewa. Tufanye kila kinachowezekana kuzuia watu wetu wasiugue. Sisi tumejielekeza kwenye kutibu.

Mheshimiwa Spika, hapa tutakuja kusema aah, bajeti yetu ya dawa imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 200 mpaka 700, siyo sifa. Sifa iwe ni kupunguza watu wasiugue. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana dada yangu, wekeza kwenye kuzuia watu wasiugue. Kuna shida gani NHIF wakichukua sehemu ya fedha zao, asilimia mbili, asilimia moja, wakaanzisha hata open gyms za bure watu wakawa wanafanya mazoezi? Wawekeze kwenye elimu. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kinachotuua leo ni magonjwa ya mitindo ya maisha (*life style diseases*). Kisukari kimeongezeka nchi hii; watoto wa miaka miwili wanaugua kisukari, ilikuwa siyo jambo la kawaida zamani, lakini leo hii *life style diseases* zinatumaliza. Nataka Serikali yangu sikivu, Serikali hii ni sikivu sana, iwekeze fedha ya kutosha kwenye kuzuia magonjwa yasitokee. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, watu wanakufa na magonjwa ambayo tungeweza kuyazuia yasitokee. Kama tukifanya kampeni kubwa kabisa nchi hii, kama tulivyofanya kwenye sensa dhidi ya magonjwa haya, watu wataelewa na watu watakuwa salama. Zamani wakati mimi nakua, mtakumbuka wazee wenzangu mliopo hapa, ilikuwa ukifungua redio unasikia “kuleni chakula bora, mboga Samaki...” Mnakumbuka hizo nyimbo? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, redio zilikuwa zinatangaza kuhimiza watu wale chakula bora na pa kulala pawe safi. Leo hii ukifungua redio unachokisikia Nyama Choma Festival ukifungua tena upande mwingine, watu wanahimizwa kunywa, starehe bila mazoezi. Lazima sehemu ya fedha zinazopatikana zipelekwe kwenye kuzuia magonjwa yasitokee. Magonjwa ya Afrika ni biashara ya viwanda vya madawa duniani. Wanataka tuendelee kuugua, tuendelee kununua madawa. Hatuwezi kukubali, ndiyo maana tuna kiwanda chetu pale Kibaha cha kuzuia Malaria kile cha viuadudu. Cuba hawana Malaria kwa sababu ya kiwanda hicho hicho, lakini kimekuja nyumbani hapa kinatengeneza dawa lakini dawa hizo

hatuzinunui sisi wenyewe kuzuia watu wetu wasiugue Malaria. inasikitisha. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono sheria ipite, lakini maangalizo haya niliyoyasema yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyolitumikia Taifa lake. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tukitoka hapa, twende kwenye majimbo yetu, (alizungumza Mheshimiwa Dkt. Mnzava asubuhi) tukatangaze mema ya Rais wetu, tukazungumzie huu mfuko wa huduma ya afya na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema, ahsante kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. Mungu akubariki sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia. Muswada huu wa Bima ya Afya kwa Wote, ni Muswada ambao kwa kweli umenifurahisha sana na naamini kuwa umewafurahisha hata Wabunge waliomo humu ndani. Muswada huu ingawa umechelewa, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeuleta huu Muswada leo tarehe 01/11/2023 humu Bungeni, kusudi tuweze kuujadili. Kwa hiyo, umekuja kwa wakati muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya hasa kwenye nyanja hii ya afya. Amefanya mambo mengi ambayo siwezi nikayaeleza nikayamaliza ikiwemo vituo vyatya afya, zahanati, vifaa, watumishi ingawaje bado hawajatosha, lakini tunamshukuru

kwa jambo hili hasa kwa Muswada huu ambao ataupitisha najua tukishapitisha humu. Kwa hiyo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hilo. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel pamoja na Wizara nzima ya Afya, bila ya kuisahau Kamati iliyoshughulikia Muswada huu. Hongereni sana, mmetuletea Muswada mzuri sana. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa sababu huu Muswada unakwenda kuhudumia watu wote, hasa wale ambao hawana uwezo. Kwa kweli tunashukuru sana. Wewe ni shahidi, naamini hata watu wengine walikuwa wanakuja kwako kukuomba waweze kwenda hospitali, lakini sasa hiyo itaisha kwa sababu kila mmoja ataweza kupata Bima ya Afya na ataweza kutibiwa kwa mpango uliowekwa. Kwa hiyo, ni jambo zuri sana ambapo tunamshukuru Mheshimiwa Rais, pamoja na wewe na Mwenyezi Mungu ambaye yeeye ndio amefanya haya yote. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, naamini sana kuwa watu ambao hawana uwezo walikuwa wanakufa. Magonjwa sugu yalikuwa yanawaua watu wengi kwa sababu ya gharama nydingi. Sasa hivi kuna magonjwa sugu ikiwemo kisukari, kansa, na magonjwa mengine ya moyo; Sasa hivi mfuko utawekwa, ambao vyanzo vyake vimeainishwa tayari, ambapo watu wenyewe magonjwa haya wataweza kutibiwa. Naamini hata huko wagonjwa waliopo kama wanatusikiliza, wanafurahi sana kuwa suluhisho la uhai wao ni Bima ya Afya. Kwa kweli ni jambo la furaha sana kuona kuwa jambo hili linakuja kutendeka. Jambo nilaloomba, hivi vyanzo vyaa mfuko huu viwe endelevu, viangaliwe kwa makini viweze kuwa endelevu kusudi watu wetu waweze kuendelea kutibiwa bila ya ubaguzi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wakati wa kuwachambua hawa watu viangaliwe vigezo vyenyewe ambavyo ni kweli vinamhusu mtu ambaye hana uwezo ili aweze kutibiwa huyo huyo ambaye kama tulivyopanga, mfumo unavyokwenda uweze kuangaliwa isije ikawa kama TASAF. Ni kweli TASAF wakati mwingine walikuwa wanachukuliwa watu ambao wana uwezo lakini ndio

wanaopewa mambo hayo ya TASAF. Kwa hiyo, naamini juu yako Mheshimiwa Waziri, utaweza kuangalia vigezo na kanuni kusudi hao watu wenyе vigezo hivyo ndio waweze kutibiwa kwa kuwa hawana uwezo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kuwa vile viambatanisho vilivyokuwepo, kuwa ili uwe na Bima ya Afya ni mpaka uwe na TRA, mpaka uwe na leseni ya udereva, hiyo imetolewa. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa hilo, na Kamati pia naishukuru kwa hilo, kwa sababu mmeangalia na kuona kuwa ni jambo zuri kuondoa vigezo hivi ambavyo na watu wote waweze kupata Bima ya Afya na kutibiwa bila ya matatizo yoyote. Kwa kweli nimefurahi. Suluhisho la tatizo hili limekwisha, watu wote watapata Bima ya Afya ambayo hasa ni kurefusha maisha ya binadamu na kumtibia kila mmoja bila ya ubaguzi wowote. Kwa hiyo, nashukuru kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, bado kuna tatizo la dawa. Ingawa namshukuru Mheshimiwa Rais, lakini naomba hili la dawa mliangalie hasa dawa kutoka MSD kusudi dawa ziweze kutosheleza, kwani hii Bima ya Afya itafanya kazi vizuri kama dawa zitatosheleza.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni watumishi, hasa watumishi kwenye zahanati zetu na kwenye vituo vya afya. Wakati mwingine unakuta kituo cha afya kipo pembezoni na kina mtumishi mmoja au wawili. Mmoja akiugua, mwingine asipokuja au ni mjamzito inakuwa tatizo. Kwa hiyo, naomba nalo hilo muweze kuliangalia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni elimu. Elimu kwa wote iweze kufikika, watu wanapenda Bima ya Afya, lakini hawana elimu ya kutosha. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo na wengine tumeshaanza, naamini mnaongelea Bima ya Afya. Sasa tumepata elimu ya kutosha twende tukwaelimishe wananchi wetu kuwa wajiunge na Bima ya Afya na wale wa kuchangia lisiwepo

**1 NOVEMBA, 2023**

tatizo waweze kuchangia kwa hiyari kusudi twende kwa pamoja, tusimuache mtu yeyote nyuma. (Makof)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine utafiti. Naomba Mheshimiwa Waziri, kwenye utafiti uchunguze kwa nini haya magonjwa sugu yakiwemo kisukari, magonjwa ya ini, na kadhalika yanakuwa makubwa zaidi kwa sasa hivi? Nafikiri tuwekeze sana kwenye utafiti ili tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa mambo yote aliyoyafanya hasa kwa mkoa wangu wa Morogoro, ameo fedha nyingi sana. Jambo la kufurahisha, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, wameweza kutupatia oxygen plant au mtambo wa oxygen. Mnavyojua, pale Morogoro nililia sana humu na oxygen plant tumeweza kupatiwa na leo nimeweza kuongea na Daktari wa Mkoa, amesema unafanya kazi vizuri, unaendelea vizuri. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa jambo hilo Mheshimiwa Rais, nampongeza kwa sekta hii ya afya, amefanya mambo mazuri kama anavyofanya kwenye sekta nyingine. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nawaomba Wabunge wote waunge mkono hoja iweze kupita. Nami naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki na aendelee kukuinua zaidi na zaidi. Ahsante sana. (Makof)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Hamis Tabasam ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupa uhai na afya ili tuendelee kufanya kazi ya Taifa letu. Nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye jambo hili kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, napenda niseme kwamba kwa kweli Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Afya, Naibu wake, Katibu Mkuu na wote katika sekta ya afya, napenda niwape pongezi nyingi sana kwa kazi kubwa ambayo imeendelea kufanyika kwenye sekta hii na leo mnaongeza hatua nyingine kubwa sana katika kuzungumza suala la kusimamia afya za Watanzania kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ninyi nyote mtakumbuka kwamba mimi nilikuwa mionganini mwa watu ambao walikuwa wanachelea sana kukubali jambo hili, lakini msingi mkubwa ulikuwa ni mmoja, kwamba tunayo asilimia 26.4 ya Watanzania ambao hawana uwezo wakuchangia. Michango yao itatoka wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ikawa inakiri kabisa kweli lakini vyanzo vilivyokuwa vinazungumzwa vikawa bado havijaturidhisha sisi Wawakilishi wa wananchi. Leo ninafurahi kusimama hapa kusema kwa niaba ya wananchi, kwamba vyanzo mlivyoviweka na maboresho makubwa mliyoyafanya yanatupa matumani kwamba sasa tunakwenda kufanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (WHO), katika ile *Universal Health Coverage* inazungumzia mambo matatu makubwa. Moja ni huduma zinazofikika, pili huduma bora na tatu huduma zinazogharamiwa bila mtu kugusa mfukoni, yaani kwa maana ya kutumia Bima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana na watangulizi waliozungumza hapa kwamba kufanya jambo hili ni sisi kuendana na Dunia inavyokwenda. Sisi kama Tanzania ni sehemu ya Dunia hatuwezi kwenda kivyetu vyetu lazima twende kama Dunia inavyokwenda. Hapa kuwekuwa na wasiwasi ambao nitaomba nisaidie kuwaondoa wasiwasi wenzangu. Kuna mambo yanachanganywa juu ya Bima ya Afya kwa Wote na Maboresho ya Sekta ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kwamba leo hata kama kijiji kwako hakuna zahanati, ugonjwa hauwezi kuacha kuja kwa sababu kijijini kwako hakuna zahanati. Yaani ugonjwa haukuulizi ninataka kuja je, una zahanati kijiji kwako? Ninataka kuja je, una daktari kwenye zahanati yako? Ninataka kuja je, una dawa? Hapana! Ugonjwa unakuja hata kama zahanati ipo kilomita 100, ugonjwa unakuja. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapa tunachokifanya leo sambamba na kazi nzuri kubwa iliyofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kujenga zahanati, vituo vya afya na kuendelea kuviboresha na hospitali zetu. Tunachokifanya ni kwamba hata kama zahanati ipo mita tatu, kutoka nyumbani kwako utakapoumwa utakapokwenda pale utatakiwa kuchangia huduma. Kama huna unaweza ukapata madhara pamoja na kwamba kituo cha afya kipo mita tano, kutoka nyumbani kwako. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachokifanya ni kwamba kama mtu zahanati ipo mbali na kwake, kituo cha afya au hospitali ipo mbali na kwake, asipate mizigo miwili. Mzigo wa kuifuata na mzigo wa kwenda tena kulipia huduma za afya. Kwa hiyo, Bima ya Afya kwa Wote itakuwa ni jambo ambalo huyu mtu ambaye yupo mbali na huduma ya afya atabaki na mzigo mmoja tu wa ndugu zake kumbeba kumfikisha kwenye eneo la huduma akifika hapo anatibiwa bila gharama yoyote. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, katika hili niseme kwamba tutafaidika mambo mengi. Mimi niliwahi kupata bahati ya kuteuliwa na Boss wangu, wakati huo Katibu Mkuu wa Chama na bahati nzuri yupo humu ndani, Mheshimiwa Dkt. Balozi Bashiru Ally Kakurwa, aliniteua kwenye Kamati ndogo ya kwenda kuangalia hali ya Majimbo ya Mkoa wa Dar es Salaam. (Makofij)

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa katika kazi ile, alinipa hadidu za rejea kubwa tatu. Moja ni kero gani zinazowakera wananchi

**1 NOVEMBA, 2023**

kwenye eneo la Jimbo hilo unalo kwenda, pili, hali ya mshikamano wa viongozi wa chama na tatu ni watu gani wanaosemwa kwa wagombea wanaokubalika na watu kwenye eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa tulipokuwa katika suala la kero, lilitokea jambo moja hata lilinipa changamoto. Mtu mmoja aliuliza kwamba sisi tumefika mahala ambapo wagonjwa wetu wanaugua tunalipa gharama mpaka tunaishiwa. Halafu mgonjwa anaendelea kutibiwa tunadaiwa gharama halafu anafariki tunambiwa a maiti haitoki mpaka mlipe hizi fedha.

Mheshimiwa Spika, ni Serikali hii hii, tumeiona gari limeanguka la mafuta limemwaga mafuta watu wamekatazwa kwenda kuchukua mafuta wakaenda kwa kiburi na mafuta siyo yao wanaenda kuiba maana wao siyo wenyewe gari hilo lilioanguka. Moto ukawaka wakaungua, wakafa baada ya kufa Serikali ikatoa sanda, ikatoa sanduku, ikatoa magari na mkono wa pole kwa watu hao amba walikuwa wanenda kuiba mafuta. Sisi amba ndugu yetu ambaye hakuenda kuiba anaugua raia mwema yupo hospitali amekufa. Tunaambiwa hamtoi maiti mpaka kwanza mlipe gharama. Wema gani huu wa Serikali? Sasa wema wa Serikali unakuja kuonekana hakuna maiti itakayozuiliwa pale ambapo kutakuwa na Bima ya Afya kwa Wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. Naounga mkono hoja na ninasema kwa kweli jambo hili ni la manufaa kwa Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Tabasam, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi lakini nichukue nafasi hii pia na mimi

kuipongeza Serikali kwa juhudini kubwa ambayo inafanya kuimarisha huduma za afya katika Taifa letu. Pia, kuangalia mipango mbalimbali ambayo inaweza ikawakwamua watu wetu kutokana na matatizo ya afya ikiwepo mpango huu wa Bima ya Afya chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini bila kuwaacha Waziri wetu wa Afya na Naibu Waziri pamoja na Viongozi wetu Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru tumesoma tumeambiwa na Waziri tumepitia Muswada huu. Nitaongelea sehemu mbili tu, sehemu ya kwanza inahusu ufanuzi nitaomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama ujaribu kutushibisha, kwa sababu sisi pia tunataka tukawashibishe wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni Ibara ya 21, Mheshimiwa Waziri pale panakupa nafasi wewe na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kukaa na kuangalia viwango. Hilo ndilo suala kubwa ambalo tungetamani kuona namna gani mtafanya consideration, kwa sababu ibara inasema mtaangalia uhai wa mfuko na uendelevu wake. Natamani mngeangalia pia na vipato vya Watanzania kwa jinsi walivyo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 32, nitaomba ufanuzi sitaielezea. Kutokana na namna ambavyo Ibara ya 22, inasema lakini niwapongeze kwa sababu mmeshatoa yale masharti ambayo yalikuwa yanakwenda kutubana kidogo. Hasa ukuiona kwamba kwenye kutoa leseni, kupata *NIDA* lazima ifungamane na hii kidogo ingetupa changamoto.

Mheshimiwa Spika, nakwenda kuongelea sasa ibara nyingine. Ibara ya 22, watu wasiyojiweza namna ya kubaini watu wasiojiweza. Hapa lazima tuwaeleze Watanzania, Watanzania watambue kwamba bima siyo msaada. Bima ni kitu ambacho mwenyewe unawekeza, bima ni kama kibubu ni kibubu cha kuchangia afya yako, bima ni kama mchango wa msiba, ukichanga kwa wenzako

na wenzako wakichanga siku moja ukifiwa na wewe utanufaika. Mfuko huu ili uwe endelevu, lazima tuwaeleze, maana tunaposema hapa ni Bima kwa wote, watu wanafikiri sasa wote watakwenda kutibiwa bure bila ya kuwa na backup nyuma yake. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, *backup* yake ni kwamba kadiri wengi tutakavyochanga kwenye hicho kibubu cha Bima ya Afya, ndivyo tutakavyoweza kutibiwa wengi. Faida utakayopata ni kwamba unachanga kwenye msimba wa mwezako lakini wewe hufiwi leo unaweza ukafiwa miaka mitatu ijayo. Kwa hiyo, ukatumia fedha za mwenzako na wewe ukija kuwa hai, mwenzako atakapoumwa wewe pia fedha zako zitatumika kumtibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaombe Watanzania tuchukue kwamba hii ni njia itakayotusaidia siku usiyotarajia, utakayoumwa wewe kama ulichanga na wewe utanufaika kutibiwa kwa fedha uliyochanga. Inawezekana ulichanga fedha kidogo ukatumia gharama kubwa kwa ugonjwa wako. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivi, lazima tujue kwamba ni wajibu wa kuziangali afya zetu ni wajibu wetu sisi. Sisi tuna mtu mmoja Paulo kwenye kile Kitabu cha Biblia aliwaambia Wafilipi, Wafilipi sikilizeni, kufa kwa Mungu ni faida na kuishi ni Kristo. Kuishi wako unamtegemea Mungu na ukifa pia ni faida, kwa sababu Mungu amekupa wajibu wa kuiangalia afya yako wewe mwenyewe. Usipoiangalia anaweza akakuonea huruma kwamba mwanangu anapata tabu ngoja afe, aje akae na mimi huku Mbinguni. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, sasa ili afya hiyo uweze kuingalia lazima ulichangie. Hii ni sawa na Mkulima anavyolima mahindi yake, analima wakati akiwa na nguvu siyo wakati wa njaa anahifadhi mahindi wakati wa chakula kingi siyo wakati wa njaa. Tunatakiwa tukate Bima tukiwa wazima siyo wakati tunaumwa ili iweze kutusaidia ndio mwelekeo jinsi ulivyo. (*Makofij*)

Mheshimiwa Spika, tukate Bima hii tukiwa wazima kwa ajili ya siku tutakayoumwa. Mheshimiwa Waziri amesema hapa na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tunafahamu. Watu wengi wanapokuwa na changamoto ya kuumwa, ndio anaulizia ukimuuliza huna Bima anakwambia sina labda nikakate. Sasa ndio maana mfuko wetu una-suffocate unakuwa imeshindikana. Kwa hiyo, Watanzania tutambue kwamba tunatakiwa kuchangia kwenye mfuko huu ili utusaide siku tutakapokuwa na shida. Tusitegemee kwamba Serikali itachangia, jamani kwanza vyanzo vyenyewe tunesema kwenye *betting*, vyanzo vyenyewe tunasema kwenye pombe kali na sisi tulio Wahubiri tunaongeza mahubiri watu waache kulewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mfuko unaweza ukakosa michango, kwa sababu hatuna mpango wa kuruhusu watu waendelee kulewa kwenye nchi hii, ili wewe utibiwe kwa sababu huyo anayelewa naye ni mgonjwa mtarajiwa hatupo tayari. Kwa hiyo, tunachomba Watanzania usisubiri uumwe ili uwe na Bima ya Afya kata Bima yako mapema hiki ndio kibubu kwa ajili ya afya yako. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna Mheshimiwa mmoja amesema tuache tabia ya watu wakifa ndio tunawachangia, hapana. Ukifa ni jukumu letu kwa sababu wewe huna uwezo huwezi kujisema tutakusemea. Wewe mzima kwa nini tukuchangie jichangie mwenyewe Bima yako ila siku ukifa lazima tukuzike, kwa sababu hata tukikuacha sisi ndio tutakao pata matatizo, lazima tukuzike. Tutakuzika kwa namna yoyote ila kwa wakati huu unapohitaji matibabu weka utaratibu wako, watoto wako na wale wanaokutegemea kuhakikisha kwamba umejikatia Bima yako na unakaa kukiwa free.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye Bima nyingine ndivyo ilivyo hata ya magari, unakata Bima ya gari ili gari inapopata ajali usiapate stress, kupata kuchanganyikiwa, kupata matatizo ya afya ya akili, kwamba utapata wapi gari nyingine? Kwa sababu tayari ulisha ilipia Bima. Kwa hiyo, unapoumwa hauhitaji kupata stress

yoyote, kwa kuwa huitaji kupata stress yoyote kuwa na Bima ya Afya. Ukiwa na Bima yako unajua kabisa nina uhakika ninaweza nikatibiwa popote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapokwenda kukaa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha cha msingi ni kwenda kuangalia Watanzania wetu kwa uwezo wao. Vile vitita mtakavyo viweka tofauti tofauti, kila mtu apate fursa ya kuchangia. Tena mimi niliipenda vile mlivyo-ci average kwamba huwezi kupata hiki bila kuwa na Bima hii, kwa sababu sasa hivi kuumwa tunaumwa. Kuna magonjwa tunaanzisha wenyewe na mengine tuna ya-*import* kutoka nje kama corona. Wakati usiyodhani unaumwa na unaumwa vibaya.

Mheshimiwa Spika, suala la Bima ya Afya kwa sasa hivi haliepukiki ni la msingi. Kila Mtanzania ajue kama anavyoweka akiba ya mchele nyumbani kwake, unaweka akiba ya sukari, unaweka akiba ya fedha za ada, ujue una wajibu wa kuweka akiba kwa ajili ya afya yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali imekurahisishia kwamba itakutunzia hiyo akiba na utakwenda kutibiwa kwenye hospitali zetu ambazo watu wote ni mashuhuda tunaona namna Serikali inavyofanya kazi kubwa kuimarisha huduma za afya kwenye nchi hii. Ndugu zangu ninaomba Vitabu vya Mwenyezi Mungu vinasema masikini hawata koma kwenye nchi. Ni kweli lakini watu wengine na wenyewe wameshakaa hapa tayari tumeshajipanga.

Mheshimiwa Spika, walivyosikia Bima ya Afya bure, tayari ameshaanza kujipanga kuwa kwenye kundi la wasiyo na uwezo. Usijipange kuwa kwenye kundi la wasio na uwezo, kwa sababu hata Biblia inavyosema masikini hawatakoma kwenye nchi, anamwambia. Kwa hiyo, wewe mwenye kutoa endelea kutoa kusaidia masikini, kwa sababu mimi Mungu wako nitakubariki. Wewe unayeendela kujipanga kuwa kwenye kundi la masikini

hutabarikiwa. Hebu sema mimi nataka kutoka huko na mimi nibarikiwe na Mwenyezi Mungu, fikiria wewe kutoa. (Makofij)

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Msambatavangu, muda wako umekwisha. Ahsante.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru Sana. Naunga mkono hoja. (Makofij)

**SPIKA:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Hamis Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mtoa hoja, ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuchangia Muswada huu wa Sheria wa Bima ya Afya. Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuelekeza jambo hili limalizwe na lipate ufumbuzi. Pamoja na mimi kuunga mkono hoja hii, nina sehemu ambayo napata wasiwasi ambao wasiwasi huu Mheshimiwa Waziri akija katika majumuisho atakuwa kuwaeleza Watanzania wakiwemo wa Jimbo la Sengerema.

Mheshimiwa Spika, hii Bima ya Afya wasiwasi wangu mkubwa upo katika eneo ambalo sijaona mpango wa kina mama Wajawazito watahudumia wa namna gani katika mpango huu, kwa sababu Wajawazito na watoto tumeambiwa wanatibiwa bure. Lazima wawekwe kwenye mapango ili waweze kupata huduma iliyo sahihi, kwa sababu wapo akina mama ambao wanataka wakajifungulie labda katika hospitali kubwa. Hawa wanatakiwa wawekwe katika eneo gani?

Mheshimiwa Spika, la pili, suala la mpango wazee, kwa sababu hakuna yoyote ambaye amekubali yeye kuzeeka, yaani tunajikuta tu tunaenda kuzeeka. Sasa wazee sijaona mpango umekaaje katika Bima ya Afya. Je, wazee watawekwa katika kundi masikini au kundi la watu mafakiri? Ni vizuri Mheshimiwa Waziri akija hapa aje atueleze wazee watawekwa wapi kwa sababu wamelitumikia Taifa hili kwa nguvu kuwa hata ni Mkulima Mfugaji, amefanya kazi katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, siku moja mimi nilikuwa hotelini nilimuona power mmoja, sikutaka kutoa mfano huu lakini alikuwa ni power maarufu katika Afrika Mashariki na Kati, aliipa heshima sana Tanzania, lakini nikamkuta ni mgonjwa wali maharage sahani ndogo hawezi kuila akamaliza. Nikamuuliza vipi kaka? Akaniambia yeye mgonjwa. Sasa hii hali ya namna hii tayari ameshazeeka lakini kama angekuwa na Bima ya Afya angekuwa yupo vizuri sana katika uzee wake na sisi tunaelekea huko.

Mheshimiwa Spika, jingine ambalo wasiwasi wangu, kuna lugha imetumika watu masikini. Katika Kamusi ya Kiswahili, watu masikini wamekaa katika *angle* nyingine wapo katika sehemu ya ulemavu na watu wenyewe mahitaji maalum. Lugha nilikuwa naona ingetumika watu mafakiri. Sasa tungejua, kwamba hawa masikini na mafakiri watakuwa katika eneo lipi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri akija atakuja kutueleza.

Mheshimiwa Spika, jingine wasiwasi wangu upo katika vyanzo vya pesa. Vyanzo vya pesa hivi vilivyotumika nina imani baadaye tutakuja tupate upinzani mkubwa kwa viongozi wa dini, kwa sababu inaoneka pesa tunazitoa kwenye kamari, pesa tunazitoa kwenye vipodozi. Sasa tunataka hawa akinamama waongezewe kodi na wenyewe waache kujipodoe wawe kama wanaume haiwezekani. Lazima akinamama wajipodoe tuwapende. Sasa tukianza kuweka kodi hayo itakuwaje? Hili jambo halijakaa vizuri. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimuelekeze Waziri wa Fedha angalie vyanzo vingine. Jamani ni kwamba kwa mfano, natoa mfano tu ambao kidogo unaweza ukawa siyo mfano mzuri lakini ndivyo ilivyo. Tunakwenda kumaliza Miradi kama ya Bwawa la Mwalimu Nyerere kule kuna pesa tunatenga sisi zaidi ya shilingi 100, katika mafuta. Kwa nini pesa zile zisichukuliwe kwa sababu huu mfuko tunakwenda kuuanza Mwaka 2026.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, lazima tuandae vyanzo vilivyo sahihi. Tusileté ugomvi tena tunatoka katika ugomvi tunaleta

ugomvi, kwa sababu sisi tunatumia mafuta lita milioni 12 mpaka 13 kwa siku. Kule ikiweka shilingi moja tu, kwenye lita ya mafuta ni shilingi 12, kwa siku na kama tunaweka shilingi tano ni milioni 60 kwa siku. Kwa hiyo, ule mfuko unaweza ukatengeneza fedha zake kwa mifumo hiyo na tukaweka *ring fence* badala ya kwenda kuchukua pesa kwenye kamari tunamtibu raia, mcha Mungu kama Tabasam nikitibiwe na pesa ya kamari. Sasa hii inakuwa hatari. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine dogo sana, suala la zahanati. Hivi vipimo vyetu vya afya; kule kwenye zahanati kuna vipimo Mheshimiwa Waziri. Mtu anatumia bima ile katika vipimo katika zahanati, akipewa rufaa kwenda kituo cha afya, akifika kituo cha afya vipimo tena. Akitoka kituo cha afya anakwenda hospitali ya Rufaa ya Wilaya. Kule nako tena daktari atakuwa hana Imani, lazima ampime tena. Akitoka tena pale anahamishiwa hospitali ya Mkao, Sekou Toure tena, vipimo tena. Akitolewa tena Sekou Toure anapelekwa Bungando, kwa sisi watu wa Mwanza, hospitali ya rufaa vipimo tena, daktari ajiridhishe. Akitoka pale tena anahamishiwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, vipimo tena.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni lazima sheria ije; na mimi ninamuunga mkono sana Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni aliyesema kwamba hii lazima iundiwe authority, iwe ni mamlaka sasa zitengenezwe sheria.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la bei za matibabu katika hospitali zetu za Serikali zinajulikana, lakini unaweza ukafanyiwa operation hiyo hiyo ya henia kwenye Hospitali ya Wilaya ya Sengerema kwa shilingi laki moja, operation kama hiyo hiyo ya shilingi laki moja na elfu arobaini ukifanyiwa Aghakan ni shilingi milioni tatu na laki sita. Haiwezekani, huu mfuko utakufa hata kama tutapata fedha kutoka mbinguni, haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, lazima sasa tutengeneze mfuko wa matajiri na mfuko wetu sisi. Watakaokwenda kutibiwa katika Hospitali za

private wawe na mfuko wao na sisi tunaokuja kutibiwa kwenye Hospitali za Serikali tuwe tuna mfuko wetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, wasiwasi wangu ambao kidogo Mheshimiwa Waziri aje utusaidie; ni kuhusu haya magonjwa makubwa kama ya moyo, figo na kansa. Haya magonjwa yawekwe pia katika mfuko huu. Mfano, kama hawa wanaotibiwa kwa dialysis. Kila siku ya Mungu mtu anakwenda kutibiwa, sasa kama atakuwa hayupo kwenye mfuko huyu mtu si anakufa?

Mheshimiwa Spika, pia niongelee suala la kulipa bima ya afya. Tunashukuru wameitoa miezi mitatu mpaka mwezi mmoja. Lakini umelipia leo bima yako ya afya una shilingi laki tano au laki tatu, baada ya wiki ukaugua unashiria unaambiwa bwana bima yako ya afya ku-mature ni mpaka mwezi; na hili pia liangaliwe. Jamani sisi tuna watu masikini, akienda kuitoa fedha yake kama ni shilingi elfu sitini amemaliza ndani. Hili liangaliwe pia.

Mheshimiwa Spika, juzi nilifiwa na Diwani wangu kule Sengerema. Mheshimiwa Diwani yule nilikwenda kumchukua Bugando Hospital na alikuwa na bima ya afya ya halmashauri. Tumefika pale ninaambiwa kwamba mgonjwa wenu anadaiwa fedha za mochwari. Nikauliza vipi? Wakasema bima yake imekufa. Kwamba, alivyokufa tu na bima ikafa. Hii sasa inakuwaje? Mheshimiwa Waziri tuwekee hili jambo tuelewe vizuri, haiwezekani mimi nimekata bima ya shilingi laki tano nimeenda hospitali leo nikafa na bima yangu ife, nilipie tena, ndugu waanze kuchanga fedha badala ya kuchanga fedha ya sanduku wanaanza kuchanga fedha ya kunitoa mochwari ilhali nina bima; haiwezekani. Tukubaliane kwamba mpaka nitakapozikwa ndipo bima yangu ife. Hii tunaomba utusaidie sana Mheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kuhusu hivi vitita. Kwenye hivi vitita kuwepo na aina ya vitita vyta kutibiwa nje ya nchi kwa sababu kuna wagonjwa wanaopelekwa na Serikali nje ya nchi. Serikali inabeba mzigo mzito sana kutibu wagonjwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Waziri wa Afya anajua; leo kuna vibali pale vipo vingi na fedha nyingi zinatumika kwa ajili ya kutibu watu nje ya nchi. Sasa raia awe ana haki, kama kutakuwa kuna kitita cha shilingi milioni tano ili akiugua apate nchi mbili duniani. Nchi moja inaweza kuwa Asia, nyingine Afrika na na nyininge Ulaya. Kuwepo na kitita cha namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Tabasam, kwanza sisi wanawake tunakushukuru kwa kututetea kuhusu vipodozi, hivyo tuachie wenyewe. Vipodozi tuachiwe kwa mujibu wa Mheshimiwa Tabasam. Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel. Mtoa hoja ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kujali afya za Watanzania na hii ni mikakati ambayo kiukweli imeandikwa kwenye llani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Tuliahidi na sasa tunatekeleza.

Mheshimiwa Spika, la pili nimuombe dada yangu Mheshimiwa Waziri, jambo hili leo linafuatiliwa na Watanzania wengi sana hasa maskini na hasa wa vijiji. Leo tulivyoahirisha Bunge mchana hapa nilikuwa ninaangalia TBC, kulikuwa na kipindi kinaitwa waweke wazi, waweke wasikike kitu kama hicho, wape nafasi, kinaitwa wape nafasi. Nimekuta dada mmoja anahojiwa anaitwa Esther, amezungumza takriban saa nzima. Anasema ameugua figo huu mwaka wa 14. Ameanza kuugua akawa anatibiwa Hospitali ya Benjamin, ameenda pale akaanza matibabu kila siku ya Mungu analipa shilingi 150,000 na kwa wiki anaenda mara tatu. Akasema, kutohana na ndugu zangu wote wamefilisika inanilazimu niahirishe

mara mbili niende mara moja ninapopata fedha, na wakati mwingine ninakaa mpaka siku kumi. Nimeenda na hayo maumivu mpaka leo nipo hai. Lakini kizuri zaidi nilichokifanya kwa Watanzania sasa hivi mimi nimekuwa mgojwa wa mfano. Serikali ilipoanzisha matibabu haya Hospitali ya Mount Meru Wizara yako ilimbeba kumpeleka Mount Meru kama mgonjwa wa kufundishia. Yamezungumzwa leo mwende mkaaangalie TBC.

Mheshimiwa Spika, amekaa siku 14 katika hospitali ya mount Meru huku watu wanajifunzia kwake. Wanajifunza lakini si kwa ubaya, wanajifunza wakiwa na walimu wao lakini kwangu ninatibiwa bure na hivyo ninaona kama ni nafuu. Hii huduma lkafunguliwa Hospitali ya Amana akapelekwa tena, huko nako amekaa siku 14, suala ni hilo hilo. Anasema mpaka na mimi sasa wananiita doctor. Ikafunguliwa Hospitali ya Temeke, akapelekwa, na sasa hivi yupo Hospitali ya Tumbi. Hii ni story ya leo mchana kwenye TBC, mnawenza kwenda kuangalia, niwapongeze sana. Yule mama amezungumza story kwa mtu wa kawaida lazima utoe machozi.

Mheshimiwa Spika, mwishoni kabisa akasema, ningekuwa na bima ya afya huu umaskini wangu nisingekuwa natembezwa kiasi chote hiki, ninalazimika kutembea kwa sababu sina namna nyingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho akaweka picha ya Mheshimiwa Rais yule mtangazaji, unaweza kuangalia hicho kipindi TBC. Akasema kwa kuwa Mheshimiwa Ummy ni dada mwenye huruma na mimi ni mwanamke mwenzie ninaomba kwa huu mchango ambao na mimi nimejitolea kufundishiwa kwenye hizi hospitali wabebe hii gharama wanisaidie nitibiwe bure. Sasa Mheshimiwa Waziri inawezekana Mungu alipanga iwe hiyo neema na mimi ninaamini huu mzigo sio lazima apelekewe Mheshimiwa Rais maana mwishoni TBC wameweka Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais wakamuweka na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa Baraka ya Mungu, na kwa sababu ninaona upepo upo *fresh* kwa Waheshimiwa tunamwagika kumpitishia, Wizara ibebe dhamana ya huyu mwananchi ambaye wamemchukua kama mwalimu wa mfano wa kuhamasisha hawa watu wengine. Ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri ili amtibu huyo mama bure ili Watanzania waone maana ya moyo wake kama mwanamke. Nitampa namba ya simu.

Mheshimiwa Spika, la pili, mimi ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Kwanza amekuwa Waziri wa mfano sana. Mambo yote magumu humu ndani yeye unayavalia mabomu na ndiyo maana kuna kipindi watu husema yeye ni mwanaume, haya ni maneno ya wenzangu lakini kiukweli amekuwa ni Waziri wa mfano. Tumeona jitihada zake kwenye Ugonjwa wa Korona.

**SPIKA:** Ngoja ngoja Mheshimiwa, ya Waziri kuwa mwanaume ina uhusiano na kwamba wanawake hawawezi kazi wanaoweza ni wanaume ama?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba unisamehe Mheshimiwa Rais wa IPU. Ninaomba unisamehe sana lakini nichukulie mapungufu yangu...

**SPIKA:** Ngoja ngoja, ili sifa za Mheshimiwa Waziri ziendelee kuwepo hilo neno tu la kumlinganisha na wanaume, yanaweza kuzungumzwa huko nje lakini humu ndani tunatunza Taarifa Rasmi za Bunge, wanawake wana uwezo wa kufanya kazi vizuri kabisa na wakawa wa mfano. Kama ambavyo tunaye sasa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo tupo vizuri tukiwa wanawake hivi hivi wala hatuna haja ya kuwa wanaume, ahsante sana. (*Makofij*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninalitoa hilo neno na kwa kuwa muongozo umetolewa na mama na mimi nimezaliwa na mama, nimelelewa na mama ninakushukuru sana kwa kunirekebisha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ummy amekuwa ni Waziri ambaye kwa kweli tumembebesha kama Serikali mapigo makubwa makubwa. Mapigo yakinotea kule Bukoba kwa ndugu zangu wakina Mwijage yale ya hatari ya kujifunika mpaka na nailoni yeye yupo, imeingia Korona yupo. Sasa zigo hili mama, kwa kweli utakuwa umeacha heshima kubwa sana kwenye nchi hii hata kama utakuja kustaaafu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine. Sisi Wabunge tunaotoka vijijini kwanza tuna raha mno leo. Mimi ukiniuliza namba za madaktari wote wa hospitali kubwa kubwa hizi za rufaa ninazo kwa sababu ya kubembeleza msamaha. Watu wetu wanaoteseka na wenyewe magonjwa ya ajabu ajabu ni watu tunaotoka mazingira ya kijijini ambayo kwa kweli hata kuipata hiyo TBC wakati mwingine ili usikilize chakula bora hatuipati yaani tunakula chochote tu kinachokuja kwa siku hiyo. Tunakula mihogo, majani na vyovoyote vile. Tunakula kila kitu bila mpangilio kwa hiyo tunaongoza kwa mambo mengi. Mimi kwa niaba ya Jimbo langu la Geita, ninaunga mkono kwa asilimia 100, tunaisubiri kwa hamu.

Mheshimiwa Spika, na Wabunge wenzangu ninaomba hili suala tulichukulie kwa uzito wake, humu ndani ndiyo siasa ya nchi hii inatengenezwa, sisi ndio wasemaji wa Serikali. Tuliweza kufanya kampeni ya sensa, tuliweza kufanya kampeni ya NIDA ambayo ni hewa mpaka leo, hatuwezi kushidwa kutetea hili kwa ajili ya wananchi wetu. Niombe kabisa, hili tutakutetea kwa sababu tunaamini likifanyika wananchi wetu watakuwa wamepata mkombozi mkubwa sana; na ninamuomba hata Mheshimiwa Rais tukipisha leo kesho mpelekee atusainie maisha mengine yaendelee. Hatusubiri mbwambwambwa. Kama tulivyomaliza leo na Mheshimiwa Rais achukue kasi kama Bunge lake lilivyokuwa na kasi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri, na Waheshimiwa Wabunge; ninazungumza polepole kwa sababu ninayoyazungumza saa nydingine ndio hao hao nikiugua wanabitibu. Tumekuwa na mifuko mingi. Tumeanza na sijui tele kwa tele tukapiga

kampeni, tumekuja na CHF tukapiga kampeni, imekuja NHIF tukapiga kampeni. Ninaona kama zote haziendi vizuri ukisikiliza hata michango kwamba mwingine kasema 26 tulikuwa tunaenda kupotea; Hapana, huo ndio mfumo mzuri wa maisha, kwamba unakwenda unajirekebisha. Tulikoanza tulikosea tukajirekebisha, tumejirekebisha tena sasa tunapoenda ninadhani tumeshafika kwenye *level at least* ya madaktari au maprofesa. Tusitudi tena nyuma.

Mheshimiwa Spika, sasa mtusikilize tuwaambie kwa sababu sisi tunaishi maisha hayo ya kawaida. Mifuko hii inakosa usimamizi hasa kwenye matumizi ya usimamizi wa mifumo, hapo ndipo Serikali inapoteza mabilioni; na tunapisha matrilioni hapa Mheshimiwa Waziri lakini ninajua kuna watu sasa hivi wanapiga tu makofi hasa kwenye *private sector*. Mimi nimesema nizungumze polepole.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, na unajua inawaumiza watu wengi. Ukiufatilia upigaji mkubwa wa fedha za NHIF zimepigwa kwenye *private sector*. Sasa una fedha, una matrilioni na watu wote wataitika mfumo ule ule mwisho huyu Konga tutaenda kumfunga jela tu; huyu msimamizi. Kwa hiyo mimi ninaomba kama mtatusikiliza sisi Wabunge ambao ndio tuna wale wananchi tunaona; kama Mheshimiwa Tabasam ameeleza, Mheshimiwa mwingine ameeleza; kwamba unatibiwa hapa inaandikwa, unaenda pale inaandikwa; kwa siku moja anaweza kuingia mtu hata mara sita.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Serikali kwa kuwa Watanzania wanaenda kuwa na Imani na maneno tunayoyasema leo, biashara hii tukimaliza, sasa hivi kila kijiji, kila hatua 200 - 300 kuna zahanati na imeboreshwa. Mmetuletea vifaa vingine hata kufunga yanawashinda. Ukienda city scan kila mahala. Ninawaomba mtupatite hata mwaka mmoja au miwili hii biashara ifanyike kwenye Hospitali za Serikali halafu wale wengine waendelee huko kwenye NHIF; ili upigaji ukipigwa, zile fedha zikipotea tuumane nao maana hawa *at least* wana vetting huku mtaani ni biashara. Hata yeye

Mheshimiwa Waziri akigundua kuna dirisha la kuperomosha tu mabilioni hautapata nafasi ya kuhurumia.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri. Ni ukweli tunakushauri vizuri kwamba, hii Serikali kama imeamua kuleta sisi tumepokea na wananchi wetu kwa niaba yao wamepokea lakini *at least* mfanye majaribio miaka miwili, msituru dishe tena kwenye private sector.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho, Madaktari waliopo kwenye private sector ndio wale wale waliopo Serikalini lakini wenzenu wafanyabiashara wameazidi akili. Daktari yule yule anayemuona mgonjwa wa NHIF ile fedha yake ya kumuona mgonjwa analipwa. Sasa ninyi mnachukua hadi fedha ya daktari na yenyewe inakuwa chanzo cha mapato. Haiwezekani watu wanakimbilia kwenye private sector. Mkubaliane kabisa, nendeni mkajifunze JK Nyerere kwa Janabi pale, utafikiri upo London. Utaratibu ndio huo, hospitali ni biashara; hata kama ni bure mtu anatakiwa aende pale akute pasafi. Unakuta mate na uchafu mwingi kwa sababu watu hawana morale.

Mheshimiwa Spika, lakini mtu akienda private sector akiona wagonjwa 10 ana laki yake anaondoka nayo. Kwa nini msizitenge kuzitoa kwenye NHIF? Kwenye hiyo bima tunayopitisha, mtu akiona wagonjwa atoke na fedha yake kama motosha wanayopewa na hospitali za private.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na ninampongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Ummy pamoja na Wabunge wenzangu. Tumeona Dalili ya mvua, sisi tunasubiri utuhoji mambo yaende, Mheshimiwa Rais kesho asaini. Hakuna mtu anakuwa na bajeti kwenye ugonjwa jamani. Hayupo. Sisi tutawaambia watu wetu hata kama ni shilingi ngapi, weka bima utibiwe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa hili suala la kutuambia tunalipa bima leo Mheshimiwa Ummy, kama alivyosema mwenzangu, unaambiwa tena ni miezi mitatu. Mheshimiwa Hamis ameshusha. Ukienda pale unaambiwa haujaenda kwenye mfumo. Tukienda kulipia pale mnaingiza kwenye kompyuta, hivi kompyuta inachukua masaa mangapi kuchukuwa majina kuyapeleka huko kwa Mkurugenzi wa Bima mpaka yarudi. Miezi mitatu? Komyuta za aina gani? Pentium one au pentium four? Lazima tufanye mabadiliko. Hili ni Bunge la wajanja na Mheshimiwa Rais wetu ana nia nzuri, hivyo tusimwangushe, tupeleke mambo kisasa, ahsante sana. (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya. Mto Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye eneo la afya. Nikushuru wewe, lakini nimshukuru Waziri wetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu na kugongea aliyosema Mheshimiwa Musukuma kwamba kwa kweli amekuwa ni mtu ambaye anathubutu kufanya yale magumu ambayo hayawezekani lakini yamefanyika, na watumishi wote wa Wizara ya Afya wakiongozwa na Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashukuru Bunge lako tukufu, ahsanteni sana kwa sapoti mliyotupa lakini asanteneni sana kwa mawazo mazuri ambayo mmetupa leo. Mimi niwahakikishie chini ya dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kiongozi wetu. Mimi ninataka kuwaambia kila mlilolisema litakuwa accommodated. Niwatoe wasiwasi, leo mmeona jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu amewekeza kwenye miundombinu. Mmeona tukiwa Mtwara, tukiwa Lindi lakini leo hapa mna ushahidi kwamba vimejegwa vituo 3,181 kwa miaka miwili, sio kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa muda mfupi sana, emergence deperiment zimejegwa 111, zimejengwa sehemu za

watoto njiti 123; na leo tunapozungumza hapa kwenye eneo muhimu sana la wakina mama tumetoka kwenye vifo vya wakina mama 530 kati ya wakina mama 100,000 mpaka leo kwa muda mfupi sana tumefika vifo 104 chini ya 100,000 ni hatua kubwa sana na ni uwekezaji uliowekezwa kwenye miundombinu, teknolojia pamoja na uliwekezwa kwenye taaluma ya wataalamu wetu.

Mheshimiwa Spika, ukisikia kwenye taaluma ya wataalam wetu, kila mwaka shilingi 9,000,000,000 zinaenda kwa ajili ya kuboresha taaluma. Ukiona sasa hivi tumeambiwa teknolojia zote ambazo zimebekwa na Mheshimiwa Rais wetu kwenye eneo la afya, suala ni moja, teknolojia imewekezwa; leo Mheshimiwa Rais wetu ametufikisha mahali, sehemu ambayo Muhibili walikuwa wanakufungua kifua chote ili waweze kukutibu moyo, sasa hivi wanakutoboa sentimita mbili mpaka sentimita nne unatibiwa unarudi nyumbani. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, suala ni kwamba ili utibiwe, Mtanzania apate hiyo huduma, je, ni Watanzania wangapi wataweza kulipia na wao waweze kutibiwa kwa hiyo teknolojia ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameiweka.

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana leo mmeenda kupitisha na mnaenda kutoa njia ambayo itamfanya kila Mtanzania kwenye hizi teknolojia na miundombinu mizuri ambayo Rais wetu ameenda kuwekeza, Watanzania wote wataenda kupata hiyo huduma. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, ninachowea kuwaambia Wabunge wenzangu, ahsanteni sana, ahsanteni sana. Nataka kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwenye maeneo wanayayaona kwamba hatujafika. Ni lini wameweza kuona Mheshimiwa Rais anagawa magari 989 kwa wakati mmoja kwa ajili ya kuja kwenye majimbo yao. Kama haya yamewezekana, hayo mengine ni madogo sana.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaambia, mimi na wenzangu tumefuatilia kwa mwaka, exemption zinazofanyika ni bilioni 667, lakini ukifuatilia wengi waliofanyiwa exemption siyo kwamba hawana uwezo. Ila hawana uwezo wa kulipa kwa mara moja hizo fedha. Maana yake leo tukienda kwenye bima ya afya kwa wote wataweza kulipa bima yao. Hizi bilioni 667 zinazotumika kuwatibu Watanzania bure kwa sasa ambazo Serikali inazitoa, zitarudi kwa ajili ya kujenga vituo vya afya na zahanati kwenye maeneo yetu ambayo hakuna zahanati. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, leo tumeona teknolojia kubwa sana ambayo amewekeza Rais wetu. Kule kwenye maeneo yetu tunaambiwa kuna x-ray 199, tunaambiwa kuna ambulance 989, tunaambiwa kuna CT scan, kuna MRI na vitu vingine. Maana yake fedha zinazokuja kupatikana kwenye Mfuko wetu wa Bima ya Afya, maana yake wataalam kule watahakikisha hatutarudi tena hapa Bungeni kupitisha fedha kwa ajili ya kununua CT scan na x-ray. Hii ita-generate fedha na itarudi kwenye eneo hilo na vifaa hivyo vitahudumiwa vizuri na wakati mwingine vikihitajika vingine vitanunuliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hapa maana yake ni kwamba, tutapata fedha ya kuwekeza kwenye maeneo mengine ya kiuchumi *strategic* na kuongeza fedha kwenye Mfuko wetu na kumaliza matatizo mengine yaliyoko kwenye mfumo wetu. Ninachokisema ni kwamba, tukipitisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote, nataka kuwaambia hata fedha zinazotoka *direct* kutoka kwenye Bajeti ya Serikali kuelekea kwenye kutibu watu kwenye mahospitali na kwenye Wizara ya Afya zitapungua na fedha hizo zitaelekezwa kwenye miundombinu na vitu vingine ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Shigongo amezungumzia hapa suala la *preventive medicine*. Yote ambayo kaka yangu Mheshimiwa Shigongo amesema kwetu sisi tunayachukua, tunayapigia mstari kwa sababu tukitaka kweli

kulinda Mfuko wetu wa Bima ya Afya na kupunguza matumizi kwenye eneo hili, ni lazima twende kwenye mwelekeo huo.

Mheshimiwa Spika, nataka pia kuelezea ambacho amekizungumza Mzee wangu Mheshimiwa Sanga, amesema vizuri sana mzee wa mabilioni na mabilioni, lakini nataka nimwambie siyo mabilioni na mabilioni tena. Ni matrillioni na matrillioni. Tumeshatoka kwenye mabilioni na mabilioni, sasa hivi ni matrillioni na matrillioni. Mapinduzi wanayoyaona kwenye afya leo yamefanywa na Rais wetu kwa kutumia trilioni 6.7. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge na nataka kuwaambia chini ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na uongozi wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, sisi Sekta ya Afya yote mnayoyasema yanaenda kutekelezeka, ahsanteni sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana mtoa hoja. Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa ufanuzi wa hoja, maoni au ushauri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kipekee nakushukuru tena kwa uongozi wako mahiri, lakini pia kwa kuweza kutushauri, kutuelekeza na kutuhimiza tufanye kazi kwa karibu na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ili tuweze kuleta Muswada mzuri wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa maoni na ushauri mzuri ambao wametupatia. Kipekee nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametoa michango yao katika kuboresha Muswada huu, lakini pia katika kuboresha maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba, katika hatua hii tumepokea maoni na ushauri wao. Ushauri waliotupatia ni mzuri sana na wote tutaufanyia kazi au tutautekeleza. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kubwa tunawashukuru kwa kututia moyo na kutupongeza, kazi hii haikuwa kazi rahisi ilianza 2018. Tumekuja Bungeni mara tatu, tukarudi lakini tunaona amesema vizuri Mheshimiwa Kapinga, hatukukata tamaa, lakini Waswahili wanasema kawia ufile. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, sisi Waislam pia tunaamini kila shari ndani kuna kheri yake. Kwa hiyo, kuchelewa kukamilika kwa Muswada huu umetuwezesha sasa kutengeneza sheria nzuri, kumetuwezesha kuja na utaratibu mzuri wa Bima ya Afya kwa Wote. Ahsanteni sana sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kwamba Mkutano wa Kumi na Tatu leo endapo Wabunge watapitisha Muswada huu wanakwenda kuandika historia iliyotukuka kwa nchi yetu ya kuwawezesha Watanzania kupata huduma za afya bila ya kikwazo cha fedha. Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza ni jinsi gani wananchi wetu wanapata changamoto za kupata huduma za matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niseme mambo makubwa manne. La kwanza, Maoni ya Kamati kuhusu, vyanzo vya fedha, wanatuelekeza au wanashauri kabla ya kuanza utekelezaji wa sheria, tuweke utaratibu madhubuti wa uendeshaji wa Mfuko unaopendekezwa. Maoni haya yamepokelewa. Pia, tumepokea maoni kuhusu vitita vya mafao kwamba, tuongeze kitita cha mafao ili tuweze kuwakidhi watu wa kati, tumelipokea. Kifungu cha 8 kinampa mamlaka Waziri ya kuboresha Scheme za Bima ya Afya za Umma. Pia tumepokea maoni kuhusu utafiti wa kina, tufanye *actuarial study* kama Kamati ilivyotueleza kabla ya kuanza kutekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali hatukuona haja ya kuja na Taasisi ya Kudhibiti Bima ya Afya kwa Wote. Kwa hiyo, katika

Muswada huu tunaendelea tena kupeleka wazo kwamba, tuwatumie *TIRA* (*Tanzania Insurance Regulatory Authority*) ili waweze kufanya kazi hii, naamini wataifanya.

Mheshimiwa Spika, maoni ya mwisho ya jumla kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ni suala la elimu kwa umma. Hili tunalipokea na tutalizingatia, kwa sababu ni kweli kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengi, elimu kwa jamii, elimu kwa jamii, elimu kwa jamii ndiyo itawezesha Muswada huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na elimu kwa jamii, kama Serikali tunatambua kwamba utayari wa wananchi kuijiunga na scheme mbalimbali za Bima ya Afya kwa kiasi kikubwa pia utategemea ubora wa huduma. Suala hili tumelipokea na tumepokea pia changamoto tuliyopewa na Waheshimiwa Wabunge, mbona wenzenu private sector wanafanya vizuri. Ni kweli kama walivyosema Mheshimiwa Msukuma na Mheshimiwa Tabasamu, wanaokwenda kutibu wagonjwa ni Madaktari wetu hao hao walioko katika hospitali za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaweka utaratibu mzuri wa motisha na mazingira wezeshi ili kuweza pia kuvutia. Ndiyo maana leo kwa mfano, Jakaya Kikwete, Madaktari wengi wanajitolea kufanya kazi kwa sababu upo utaratibu mzuri wa motisha. Tunaenda vizuri pia kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, tumeanza vizuri, Profesa Makubi baada ya kumpeleka MOI. MOI imeanza kubadilika sana. Kwa hiyo, tunaamini kabisa hospitali zitabadilika.

Mheshimiwa Spika, tumemsikia Mheshimiwa Getere, sasa tushuke mpaka ngazi ya zahanati, vituo vyta afya na hospitali za wilaya ili kuboresha huduma za afya. Hili nalo tumelipokea.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya TEHAMA, kaka yangu Mheshimiwa Shigongo nakubaliana na yeye, *duplication of care*. Unatoka Bombo Hospital, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga, umefanya *CT scan*, unapelekwa Muhimbili unarudia tena kufanya

CT scan. Kwa kweli mfuko lazima uanguke, lazima utikisike. Kwa hiyo, tunakubaliana naye kuondoka kwenye *Electronic Medical Records*, kwenda kwenye kitu kinaitwa *Electronic Health Record*. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ukifanya CT Scan Bombo, Tanga umeenda Muhimbili, umeenda *MOI* hakuna haja ya kurudia. Unless kuwe na sababu ya msingi ya kurudia kipimo hiko.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeelezwa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile ni kwamba lazima tuweke mfumo wa motisha kwa watumishi wa afya. Tunalipokea na hili tumeanza kama tulivyosema, tumetoa mwongozo, mapato yatokanayo na bima tumeruhusu asilimia 40 zigawanywe kati ya watumishi wa afya ambao wametoa huduma ikiwemo Madaktari.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwe na hela ya kulipia umeme, kulipia maji na masuala mengine ya dawa. Haya yote pia tutayafanya kazi. Pia limetoka wazo, kwa nini tusitoe motisha kwa wananchi kujunga na Bima ya Afya. tumelipokea wazo hili, tumeanza mazungumzo na Wizara ya Fedha. Kama kuna mtu amelipia kwa mfano amedai risiti ya VAT, atapata point hela yake itaenda kuchangia mchango wake wa kulipia bima ya afya. Kwa hiyo, tunaamini suala hili pia tutaweza kulikamilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utambuzi wa watu wasio na uwezo, tumelipokea na nimeona Waheshimiwa Wabunge, mna wasiwasi na TASAF. Tutakaa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Utumishi wa Umma wanaohusika na TASAF ili kuja na mfumo mzuri wa kutambua wasio na uwezo. Mheshimiwa Jesca, nakushukuru sana na Mheshimiwa Benaya Kapinga, kwamba, siyo kila mtu tu attingia katika mfumo huu. Wenzetu Rwanda, uliruhusu twende na Kamati, wamem-profile kila mtu mapato yake na *income* yake. Kwa hiyo, tunaweza na sisi kidogo kidogo tukafikia hapo. Kila mtu atachangia kwa kadri ambavyo ataweza.

Mheshimiwa Spika, kipekee na sisi tunarudia tena kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua na kuridhia kwamba kwanza tuendelee na Muswada huu. Pili, kuturuhusu kutumia vyanzo vyaa mapato kwa ajili ya kulipia wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, umekuwa ni Rais wa Mabunge Duniani, hakika sasa utakapoyanyooshea au utakapokaa katika Mabunge mengine, unayo sababu ya kusema Tanzania tumefanya *26 point something percent* ya Watanzania. Tunawapa matibabu kupitia bima ya afya. Hakika umeacha *legacy* kubwa ndani ya Bunge lako. Waheshimiwa Wabunge wameacha *legacy* kubwa katika maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kipekee tunamshukuru Waziri wa Fedha. Kuna maoni yametoka, wanawake wajawazito, Mheshimiwa Ritta Kabati, tuanze na wasio na uwezo kwanza. *Under five*, chini ya miaka mitano wasio na uwezo. Wazee pia ni wale wasio na uwezo. Tuna wazee humu ndani ya Bunge, hawa wazee wana uwezo. Siyo kila mzee sasa ata-*qualify* katika kundi hili la watu wasio na uwezo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mheshimiwa Deo Sanga, amesema tutatue kero. Samahani, kuhusu vyanzo Mheshimiwa Festo Sanga, amezungumza vizuri. Tuanze na hivi vilivyopo. Nafahamu lakini uzuri ni vyanzo tayari viro, kwa hiyo, tunapewa asilimia ya vyanzo hivi. Siyo kwamba tunaenda ku-introduce mambo mapya. Tusinunue mawigi, tusibandike kope za macho, tukose vipodozi. Kwa hiyo, ni yale yale.

Mheshimiwa Spika, amesema vizuri Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Tumejikita katika kile kitu kinaitwa syntaxes. Ndugu zangu sasa hivi asilimia 25 ya Watanzania, wana magonjwa, wana Shinikizo la Juu la Damu, linawapelekea kwenye kisukari na kwenye magonjwa ya moyo. Asilimia 12 ya Watanzania wana kisukari. Kwa hiyo, ndiyo maana tumechukua kwenye vyanzo vilevile iliwa ni sehemu ya ku-

discourage pia matumizi ya baadhi ya vitu ambavyo vinasababisha magonjwa.

Mheshimiwa Spika, Ushirika Afya tumesikia, lakini changamoto ni ile ile kama Toto Afya Kadi. Ushirika Afya tulitegemea wakulima wote Mheshimiwa Kapinga, wangejiunga, wakajiunga wagonjwa tu. Kwa hiyo, mwisho wa siku *sustainability* ya NHIF ikawa ni changamoto. Viwango vya kuchangia tuta-take *into consideration* hali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, kuna moja limeulizwa kwamba, NHIF tumesema imechoka, je, tuna majibu gani sasa hivi? Muswada huu ni moja pia ya, kwanza kulifanyika *actuarial study*. Ika sema msipochukua hatua, Mfuko huu hautafika kule mnakotaka kufika, ndio maana tukasimamisha baadhi ya vifurushi, Ushirika Afya, Toto Afya Card na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea pia kuchukua hatua kwa ajili ya wizi na ubadhirifu. Muswada huu unakwenda kutibu changamoto ya wizi na udanganyifu unaofanywa kwanza na wanachama wa NHIF.

Pili, watumishi wa NHIF; na tatu, watumishi wa vituo vya kutoa huduma za afya. Tumefungia hospitali lakini unakuta kosa siyo la mwenye hospitali, kosa ni watumishi wataalam ambao wamefanya udanganyifu. Leo hapa mtu anapata maambukizi ya UTI, anaandikiwa anti-biotic tano au sita. Kwa nini? Tumeshamwelekeza, jana nimemwelekeza Mganga Mkuu wa Serikali, lazima tutoe mwongozo wa matumizi sahihi ya dawa na matumizi mengine ya matibabu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mzuri ambao wametupatia kwa kutuvumilia, kwa kutuelewa, kwa kutushauri na kutuhimiza yapi tunayopaswa kuyafanya. Namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa upendo wake, kwa huruma

yake na utu wake kwa Watanzania, zaidi Mheshimiwa Rais Samia, ameonyesha uthubutu, hili jambo siyo rahisi. Muda hautoshi, bima ya afya kokote duniani unapopitishwa Muswada kuna kuwa na kelele, kunakuwa na maneno na kunakuwa na mingongano. Mheshimiwa Rais Samia amesimama kidete kwa masilahi ya Watanzania na kwa maslahi ya nchi yake, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa; Mawaziri wenzangu wote, hususani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama; Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba; pamoja na Wataalam wa Sekta ya Afya, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Jingu; Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Grace Magembe; na Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nyagu. Tunashukuru taasisi zote, *NHIF, TIRA, NSSF*, Ofisi ya Rais TAMISEMI, MBS, TASAF, AFTA, TEA na kampuni binafsi za bima.

Mheshimiwa Spika, kipekee narudia tena kukushukuru wewe. Umeonyesha kwa vitendo wanawake wanaweza. Wanawake wanaweza kusimamia masuala makubwa yenyе maslahi kwa Watanzania. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Nyongo na Waheshimiwa Wabunge wote, wametuvumilia sana, lakini naamini sasa wameona jambo letu. Hatukuwa tunapigania jambo hili kwa maslahi binafsi, tulikuwa tunalipigania jambo hili kwa sababu tunaamini kwa dhati ndiyo moja ya mikakati madhubuti na endelevu ya kuwawezesha Watanzania wote kupata huduma bora za afya bila ya kikwazo cha fedha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Msukuma ameonyesha *dialysis* laki na nusu. Wakifanya mara tatu, ni laki nne na nusu kwa wiki. Kwa mwezi milioni moja na laki nane. Kwa mfano, leo tukiwaambia bima ya afya ni 340,000, hii 340,000 kwa watu sita kwa mwaka mzima kulinganisha na 1,800,000. Tunaweza tukaiona bima ya afya ni ghali endapo huna mgonjwa au hujaugua, lakini bima ya afya ni rahisi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimshukuru tena Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa ushirikiano mzuri. Kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa ni mtu mwema sana. Wakati wowote ninapomtuma na kumwelekeza kufanya kazi amekuwa akinisikiliza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa Watanzania tunawashukuru sana. Tutaendelea kutoa elimu na hamasa kuhusu bima ya afya. Bima ya afya ni kuchangiana. Siyo mtu aumwe ndiyo akakate bima ya afya, Mheshimiwa Jesca amelisema vizuri sana. Watanzania, tutakapoanza utekelezaji, lazima tujichangie. Tutaweka utaratibu wa watu kudunduliza kidogo kidogo badala ya kutoa fedha yote. Nimesema hapa kwamba ni vizuri tukaanza na sisi lakini tunaomba pia tufanye maandalizi mazuri. Hatutaki tuanze vibaya. Tunataka tuanze vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana tena kwa kunipa fursa hii kuweza kuwasilisha Muswada huu. Waheshimiwa Wabunge kwa michango mliyoitoa, leo nadhani nitalala usingizi mnono. Ahsanteni sana sana. Tunafahamu kwamba Muswada huu unapita na majina ya Wabunge yataandikwa kwa wino wa dhahabu kwamba, nyie ndiyo chachu ya kuwafikishia Watanzania huduma bora za afya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kutoa hoja. (Makofi)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa tutaendelea na utaratibu wetu lakini kabla sijamuita Katibu, wapo wageni hapa ndani. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, ambaye Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, ambao ni familia yake kutoka Zanzibar, yupo Ahmed Ally Sharif na Said Nassir Said, karibuni sana. (Makofi)

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako sasa ijielekeze katika Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote wa Mwaka 2022.

Jina Refu la Muswada

(Jina refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 4

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 5

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 6

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila  
mabadiliko yoyote)

Ibara ya 7

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 8

Ibara ya 9

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila  
mabadiliko yoyote)

Ibara ya 10

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 11

Ibara ya 12

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila  
mabadiliko yoyote)

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16  
Ibara ya 17

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisheso yake)

Ibara ya 18

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila  
mabadiliko yoyote)

Ibara ya 19

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisheso yake)

Ibara ya 20

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila  
mabadiliko yoyote)

Ibara ya 21

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisheso yake)

Ibara ya 22

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hiki kifungu cha 22 naona kwenye jedwali la marekebisheso kuna sehemu ya kufuta Ibara ndogo ya tatu na kubadili mpangilio wa Ibara ndogo ya nne kuwa Ibara ndogo ya tano, halafu kuna kuongezeka kifungu cha 22A ambayo inahusu mfuko wa kugharamia wasio na uwezo, tuko hapo sote? Mheshimiwa Waziri, tuko hapo wote? Ukurasa wa nne wa marekebisheso ya jedwali la marekebisheso.

Hapa hebu mtusaidie kidogo, kwenye hiki kifungu cha 22A(3) umeshafika hapo?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali naamini unayo hiyo pia. Hapa kwenye tatu mmeeleza kuhusu mapato, kwa kuzingatia masharti ya Sheria za Fedha, fedha zinazolipwa katika Mfuko wa kugharamia Bima ya Afya, kwa watu wasio na uwezo zitatokana na vyanzo vifuatavyo:-

- (a) Mapato yatokanayo na miamala ya kielektroniki kwa kiwango kitakachoainishwa katika Sheria za Fedha.
- (b) Kwa namna itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha, hii kiswahili sijui inaitwaje
  - (i) (i) au (e), utungaji wa sheria kwa Kiswahili, unanipa changamoto kidogo, lakini sawa, mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za vinywaji vyenye Kaboni, vinywaji vyenye vimeo na bidhaa za vipodozi.
  - (ii) Kodi kwenye michezo ya kubahatisha.
  - (iii) Ada ya Bima ya vyombo vy'a moto.

Sasa nisaidie tu maelezo, hii (a) na (b) halafu tofauti yake na (c) ni nini? Kwa sababu mimi nawaza haya mapato yote tuliyoyataja hapo juu ni yale ambayo Wizara yako wakati inaleta bajeti itakuwa inaeleza kwenye fedha zitakazotengwa na Bunge, kwa sababu Sheria yetu tukiitunga kwa sura hivi vifungu vikiwa vinasomeka hivi; Je, ni fedha zote zitakazokusanywa kwenye miamala ya kielektroniki vitaenda kwenye Bima.

Pili, hii tuliyosema Waziri wa Fedha atasema mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vyenye kaboni,

vinakuja tu kwenye mfuko huu na vinywaji vyenye vimeo vinakuja hapa pekee na bidhaa za vipodozi vitakuja hapa pekee, halafu kuna kodi kwenye michezo ya kubahatisha vitakuja vyote hapa ama kutakuwa na asilimia kadhaa.

Pia kuna hii ada ya Bima ya Vyombo vya Moto itakuja hapa pekee au na mahali kwingine, kama itakuja hapa pekee hivi vyanzo viro sawasawa kuainishwa kwenye Sheria kwa namna ilivyoainishwa, lakini kama kutakuwa na kwenda sehemu nyingine halafu tukaviweka hapa tutakuwa kidogo hii Sheria sijui tutakuwa tumeitunga kwa sura gani, tutakuwa tunajipa wenyewe changamoto.

Mheshimiwa Waziri, toa maelezo halafu watakusaidia, nadhani Waziri wa Fedha, anataka kutoa maelezo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, karibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi tulivyoshauriana na Wizara ya Afya, Serikali ilitengeneza timu ya wataalam wakapitia vigezo vingi, moja ikiwepo ya mahitaji na mbili ikawepo kukuwa kwa mahitaji. Kwamba mahitaji yaliyobainishwa leo yanaweza yasiwe mahitaji yanayotakiwa mwaka 2026 au mahitaji yanayotakiwa mwaka 2027/2028 na kuendelea, kwa hiyo, tulichoweka kwanza tulitaja vyanzo ambavyo vinaelekezwa kwenye Mfuko, chanzo kikubwa ambacho ni *main* kwa sasa hivi ukienda kwenye takwimu za makusanyo tunayoyapata ni kile cha kielektroniki, kwa sababu mpaka sasa ndiyo *substantial, amount* yake ni kubwa ambayo inapatikana, vile vyanzo vingine makusanyo yake ni madogo madogo.

**MWENYEKITI:** Sawa, ngoja tuende kidogo kidogo. Kwa hiyo, yale mapato yanayopatikana kwa hii miamala ya kielektroniki zile kazi zinazofanyika kule sasa yatahamia kwenye huu Mfuko.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yatahamia kwenye mfuko.

**MWENYEKITI:** Sehemu ama yote? Naona hapa naambiwa sehemu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tumesema mahitaji yanaenda yanabadilika kwa hiyo tulikuwa tunatamani tubainishe vyanzo *then evaluation* hiyo inafanyika kila mwaka wa fedha, kwenye *Finance Bill* inabainisha ni kiwango gani. Kingine tulichoongelea kwenye *commitment* yetu tuliyopeleka kwenye Wizara ya Afya, barua ambayo nimeisaini tumeelezea pia kwamba Wizara yetu itaendelea kabainisha vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbuka wakati huu tunavyotunga hivi tumesema tutaanza na wale amba wako kwenye *extreme poverty*, wale amba wapo kwenye mstari wa chini kabisa wa umaskini, lakini tutakapokwenda kwenye *full package* ni dhahiri kabisa hivi vyanzo tulivyovitaja huenda visitosheleze, kwa hiyo ndiyo maana tumewe fursa ya kuvitaja lakini pia tukasema na vyanzo vingine vinavyoendelea kufanyiwa kazi, pia tukasema itakuwa inabainishwa kila mwaka wa fedha unapoendelea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Naona, Mheshimiwa Waziri wa Afya.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri wa Fedha, ni kweli timu imekaa na tuna *calculations* ni sehemu kwa mfano ya mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa, labda tuongeze neno ni sehemu ya, kwa sababu kama alivyo sema Waziri wa Fedha, sasa hivi kazi imefanyika tumeangalia percentage ndogo lakini kama mahitaji yakiwa makubwa inaweza ikawa asilimia zaidi ya hiyo. Kwa hiyo, nadhani kama itakupendeza tuseme sehemu ya mapato.

**MWENYEKITI:** Wasiwasi wangu, uzuri Waziri wa Afya naye ni Mwanasheria, wasiwasi wangu ni kwamba hiki Kifungu Bunge likikipitisha namna kilivyo kinamaanisha nini. Kinatofauti na hii tuliyosema kwamba; (c) Je, fedha zitakazotengwa na Bunge

ambazo ni Serikali ndiyo mnaleta kwamba Mfuko huu una mahitaji ya fedha kiasi hiki, kwa hiyo sisi kwenye bajeti yenu yaani si ndiyo mtakavyoeleza kwamba tutakavyowahudumia hawa wasiojiweza kiasi cha bilioni 40 zinahitajika au bilioni 400 mwaka huu zinahitajika na ndiyo tumetenga. Kuliko hivi mlivyoainisha humu kama vyanzo vya mapato wakati tunajua huwa vinaelekea na kwingine huko vinadaiwa ni hivi hivi. Mheshimiwa Waziri naona una jambo la kusema.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi wakati tumekuja kama Serikali tulisema tu, fedha ambayo itapitishwa na Bunge kwenye bajeti ya Wizara ilikuwa ni maoni na ushauri wa Kamati, lazima viwe *ring fenced*, tuwe na vyanzo mahsus. Kwa hiyo, ukisema kwenye bajeti bado Wizara ya Afya inaweza ikatenga bajeti yake lakini hii unakuwa na uhakika kwamba fedha itakayokusanya kwenye miamala ya elektroniki basi asilimia fulani itaweza kugharamia Bima ya Afya kwa wasio na uwezo, fedha itakayokusanya kwenye mapato ya kodi kwenye michezo ya kielektroniki. Kwa hiyo, hii inakuwa na uhakika chanzo cha uhakika kuliko tukiacha (c) ikibaki tu fedha zitakazotengwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo bado tulidhani Serikali tu-maintain kama ilivyo.

**MWENYEKITI:** Sawa. Sasa hapo kwenye *ku-ring fence*, sheria yetu hii itawezaje *ku-ring fence* kitu ambacho haikijui? Maana hatujui tunaenda *ku-ring fence* nini, hatuwezi *ku-ring fence* miamala ya kielektroniki kwa nini? kwa sababu ni sehemu ndiyo inakuja hapa na nyingine inaenda kule, labda kama Serikali inataka kusema kwenye hii miamala ya kielektroniki, kama mifuko ambayo imewahi kuanzishwa na Sheria na ikawa *ring fenced* ni kama ule Mfuko wa REA. Mfuko wa REA umetaja mahsus ndiyo maana ni rahisi *ku-ring fence*. Hapa tunavyo vyanzo vingi na vyote tunasema sehemu tunar-ing fence vipi hizi fedha za mfuko?

Mheshimiwa Waziri, samahani utakuwa wa mwisho kuna Mheshimiwa Katambi, alisimama hapo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira hayo nami nakuelewa katika kutunga Sheria ambayo ni principle, kutakuwa na shida katika kuitafsiri ili kuondoa changamoto hiyo, nafikiri kwamba ningeweza kupendekeza au kuishauri kwamba sasa kile kiwango au kiasi kikaelezwe kwenye Kanuni kwamba Sheria hii ieleze tu kwamba vyanzo ni hivi, kiasi cha fedha hizo. Lakini kutakuwa kuna kanuni ambayo itatungwa kila Mwaka wa Fedha katika utekelezaji wa hiyo. Nadhani itakuwa rahisi zaidi katika kuondoa ile generality kwenda kwenye deductive badala ya inductive.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chief Whip, naona kuna Wabunge humu wanataka kusaidia kwenye hoja hii Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa sentensi chache kwa sababu tumekubaliana na Waziri wa Fedha ili aweze kuimalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunasema hivi, ukiangalia kwenye (q) kifungu cha 22A pale ulipoanza kusoma ukienda pale kwenye (a) imeeleza kabisa: "mapato yatokanayo na miamala ya kielektroniki kwa kiwango kitakachoainishwa katika Sheria za Fedha, lakini (b) kwa namna itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha" Kwa sababu tayari tumeshakubaliana kwamba hivyo ndivyo vitakuwa vyanzo lakini tutakapofika kwenye bajeti ni lazima masuala yale ya fedha, mgawanyo, Sheria za Fedha zitaongozwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale pia tumesema kwa namna itakavyopendekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha ndiyo tunasema hivyo itakavyopendekezwa wakati huo wa bajeti; (i) Mapato yatokanayo na ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa na vinywaji na kadha wa kadha. Sasa ninapofika hapo ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sasa atuwekee ule utaratibu kwa kadri hiyo ambayo tunaimaanisha sasa tunapofika hapo wakati wa bajeti.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi unaooneshwa pamoja na hoja zinazotolewa zote ni za msingi, lakini kitu kimoja tu ambacho nilitaka niliombe Bunge lako Tukufu lizingatie, ambacho kimezingatiwa na wataalam wetu wa Serikali. Iko namna hii, leo hii hapa tunatunga Sheria, Bunge lako likishatunga kama ambavyo *Chief Whip*, alivyosema hapa kitakacholindwa ni pale ambapo Sheria ya Fedha ya mwaka husika itakapotaja kutoka kwenye kile chanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo umekuwa utaratibu hata kwenye maji, REA, TANROADS, kila mwaka wa fedha pamoja na kwamba Mfuko wa Barabara unasema chanzo itakuwa ni mafuta, pamoja na kwamba Mfuko wa REA unasema chanzo itakuwa ni mafuta, pamoja na kwamba Mfuko wa Maji unasema chanzo itakuwa ni mafuta, kwenye mwaka wa fedha husika huwa tunakuja kusema hapa kwamba tunapendekeza shilingi 100 iende kwenye TARURA, hiyo tumeshaisema shilingi 100 inaenda kwenye TARURA ndiyo inayolindwa kwamba inatakiwa iende kwenye mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuweka tu moja kwa moja kwenye Sheria wakati inatungwa kwamba kutakuwa na shilingi 100 ya maji, tunaweka tunapokwenda kwenye *Finance Bill*. Kwa maana hiyo tunabainisha chanzo kama tulivyofanya kwenye mifuko mingine tumetaja vyanzo vile, lakini kila *Finance Bill* tutakuwa tunataja kwamba sasa hivi kwenye chanzo hiki asilimia 100 itakuwa

**1 NOVEMBA, 2023**

inaenda kwenye Bima ya Afya, ama asilimia 80 itakuwa inaenda kwenye Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye mafuta tuliweka kwenye Road Fund, lakini bado tukagawanya asilimia na zote zikalindwa. Tukasema asilimia 70 itaenda kwenye barabara za TANROADS, asilimia 30 itaenda TARURA, hivyo ndivyo ambavyo tunaenda lakini Sheria inabainisha tu chanzo asilimia ngapi Mheshimiwa, Bunge lako Tukufu litakuwa linaweka kufuatana na mahitaji ya mwaka husika kutoka kwenye hicho chanzo tulichotaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuliona hili. Kusema ukweli mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na hili ndilo lilikuwa kikwazo kikubwa sana ndani ya Kamati, tumevutana sana kuhusu hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia ni kwamba sisi kama Kamati tulichoambiwa kwamba hii miamala ya kielektroniki hichi chanzo chote kinakwenda kwenye huu Mfuko, tukaambiwa mpaka sasa hivi kuna bilioni 58 zipo, wakatupa projection kwamba hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa fedha kutakuwa na bilioni 218, ndio maana tukaridhia baada ya kuhakikishiwa kwamba fedha zote za hiki chanzo cha kielektroniki kinakwenda kuingia kwenye Mfuko wa Afya na siyo sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona Serikali iridhie tu kama ambavyo Kamati tulikubaliana kwamba chote hiki chanzo kiende kwenye Mfuko wa Afya kama ambavyo Mheshimiwa Waziri aliji-commit kwenye barua kwa Kamati nasi kama Kamati tulivyoambiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Sanga ameahirisha. Mwenyekiti wa Kamati, tumalizie hapo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tulihakikishiwa kwamba vyanzo hivi ndivyo vyanzo vya mapato ambavyo vitakwenda kuingiza fedha kwenye Mfuko wa Afya. Sasa kanitoa wasiwasi kama kweli kila mwaka wa fedha chanzo kile lazima tukipitishe kwa kiwango fulani, mpaka hapo mimi naona hakuna wasiwasi. Pengine labda atusaidie tu, kwa sababu katika moja ya vyanzo, kuna chanzo kingine ambacho kinasema, mapato yanayotokana na uwekezaji wa mfuko. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa labda atuhakikishie kwamba, na lenyewe mtaliwekea percent na litakuwa linapitishwa kila mwaka kwenye mwaka wa fedha, au ni fedha zote zinazotokana na mapato ya mfuko wa bima? Kama vyanzo hivi viro protected na tunavipitisha kwenye *Finance Bill* kila mwaka, mpaka hapo nadhani haina wasiwasi, ahsante sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, amenipata vizuri kwenye *spirit* ya *discussion* tuliyofanya. Ile ambayo ni ya uwekezaji wa kutoka ndani ya chanzo chenyewe ni jambo ambalo litakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawakumbushia tu kupitia experience ya ile mifuko mingine. Baada ya kuwa tumeshapitisha kwa mwaka wa kwanza tutakapokuwa tunaanza, tukapishisha vile viwango, kama mwaka husika hatubadilishi, inaendelea kuwa ile ile ambayo ilikubalika. Kwa hiyo, kwenye *Finance Bill* tutakuwa tunasema tu, ile amount tunaendelea, tunapendekeza kuibakiza kama ilivyokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo kwenye TANROADS hata mwaka ambao hatuibadilishi, kwenye *Finance Bill* huwa tunasema napendekeza kuendelea kutoza kiwango hiki hiki kwa ajili

ya mfuko a, b, c. Kwa maana hiyo, bado jambo hili litakuwa kwenye mikono ya Bunge kuhusu kuamulia aidha ni chote ama asilimia 90, ama asilimia kadhaa. Hii ni *spirit* tu ya utungaji wa sheria unaozingatia mambo yanayobadilika badilika. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano leo hii, miamala tumeifikisha katika kiwango cha bilioni 200 ama mia mbili kumi na ngapi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini utakumbuka kuna mwaka mmoja miamala ya simu tulipigia kwenye kadirio la shilingi trilioni 1.2. Sekta zinakua, ikitokea tumeiweka kwenye sheria, na yenewe iko labda shilingi trilioni tatu, halafu mahitaji, ukijumlisha na vyanzo vingine vyote vimekua labda ikawa iko kwenye makadirio ambayo inameza kiwango kikubwa sana cha bajeti, ndiyo maana tunabainisha vyanzo. Kwenye *commitment* tuliyomwandikia Waziri wa Afya ni kwamba tutaendelea kuchambua na vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakubaliana na Mwenyekiti wa Kamati, na ninawaomba na Waheshimiwa Wabunge wengine, hivi ilivyo imekaa vizuri na *commitment* yetu ni kwamba kwenye *Finance Bill* itakuwa inasema na kama haibadilishi, itakuwa inasema kwa mwaka huu hatubadilishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii pia italipa fursa Bunge kuendela na Kamati yenewe ambayo ndiyo inachambua hivi vitu kuanzia kwenye ngazi ya Kamati kwa niaba ya Bunge kuendelea kwenda kwa undani zaidi kuweza kujiridhisha zaidi kuhusu uendelevu wa vyanzo vyenyewe, lakini vyote viro *protected*. Kwa hiyo, kipaumbele ni mfuko. (Makof)

**MWENYEKITI:** Sawa. Unajua pale mwanzo nilikuwa nimemtaja AG kwa sababu hizi sheria tunavyozitunga, Bunge ndiyo hili hili. Ukihatunga sheria lazima iwe na uhakika, hakuna kudhani ama kufikiri ama kuwa na nia njema. Sasa nilikuwa naangalia hapa ile Sheria ya REA, imetaja viwango na Bunge hili hili ndiyo lilitunga inataja 5% of..., inataja hii. Sasa hii ya kwetu leo tunataka tuitunge

na tukiwa tumesema kila kimojawapo halafu asilimia hatuisemi. Wakati huo huo tunaagiza zikawe *ringfenced*.

Sisi ndio watunga sheria hapa, na sio mimi jamani natunga. Kwa hiyo, tunakubaliana wote hapa ndiyo tunatunga. Kwa hiyo, tukikubaliana kwamba tunataka iende kwa sura hii, ni kazi yetu sisi wote ile *finance* inapokuja, tuanze kuangalia kimoja kimoja ni asilimia ngapi zimetenga huko?

Katika utungaji wa sheria, Bunge hili linapoanzisha fund fulani huwa inataja hizo sources kama zinaenda zote, kama zinaenda kwa sehemu inataja kiasi kinachoenda. Sehemu ile ambayo Waziri ametoa ufanuzi kwamba ikitaja mafuta, baadaye mnagundua kwamba pengine iende 80%, kwingine 20% ni sawa, lakini inakuwa imetaja kwa sura ambayo siyo kama hii ya kuwa umetaja maalumu. Kwa mfano, hapa ukisema miamala ya kieletroniki, asilimia ngapi ya hiyo miamala? Kwa sababu fedha zinajulikana zinakusanywaga ngapi kwa mwaka? Huu mfuko unahitaji kiasi gani?

Upo uwezekano vyanzo hapa vilivyotajwa na Serikali imeweke wazi jambo ambalo ni zuri, kwamba imeweke vyanzo vingi kwa maana ya kwamba zitakusanywa fedha lazima zitoshe huu Mfuko wa Bima ya Afya kwa wote hasa kwa kuanza na wasiojiweza, lakini mazingira ambayo tunaitungia, maana hii ni sheria; sisi hatuangalii kanuni hapa, wala hii siyo sheria ndogo. Hii ni Sheria Mama tunaitunga leo, kwa hiyo, ni kazi yetu sisi sote hiki kifungu kama tunakipitisha, wakati wa Bajeti lazima tuanze kufuatilia vilivyotajwa hapa, kule zimetajwa asilimia ngapi? Kwa kuwa hapa hatujasema, kule hata wakisema 0.03, lazima turidhie kwa sababu tumejitisha sheria ambayo haisemi. Kwa hiyo, mazingira ni hayo na lazima tuwe tunazitazama sheria zote kwa sijui inaitwa urari au uwiano! Sawa, nadhani hoja imeeleweka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Dkt. Ndugulile naona umesimama muda mrefu. Atakuwa wa mwisho huyu kuzungumza halafu tuendelee. (*Kicheko*)

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe katika Kamati hii ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Hii ilikuwa ndiyo hoja ambayo ilizungumzwa kabla ya huu Muswada kurejea katika Bunge hili. Uelewa wangu mimi, commitment ya Serikali ni kwamba chanzo hiki cha miamala ni moja ya chanzo ambacho kitatumika katika Bima ya Afya, na ni chote. Jana walituambia kwamba mpaka sasa hivi walikuwa wana-project kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 200 na mpaka sasa hivi wamekusanya kama shilingi bilioni hamsini na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, my understanding ambayo ilisababisha na sisi kukubaliana na hilo ni kwamba hiki kitakuwa ni chanzo mahususi kwa ajili ya Bima ya Afya. Ndiyo maana katika ripoti yetu ya Kamati ikasema, sasa tuki-ringfence kwa ajili ya shughuli hiyo; sasa naona maelezo hapa kidogo yanakinzana, lakini sisi tulisema kwamba hiki ni chanzo mahususi kwa jambo hili. Nami nawaomba Waheshimiwa Wabunge twende na msimamo huo. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Sasa hatuwezi kwa sababu huenda mahitaji ya huu mfuko yanawezakuwa hayahitaji zile pesa zote na Serikali ikishazikusanya lazima iweze kutumia kwenye maeneo mengine. Kama hesabu ilikuwa imeshapigwa tukajua hapa asilimia hizi na hizi na hizi zinatosheleza, tungeishia hapo, lakini sasa tumetaja vyanzo vingi hapa, halafu asilimia hatuzijui, na hatujui kama zinatosheleza ama vipi. Kwa hiyo, hiyo kidogo ndiyo inayoleta changamoto ikiwa ni pamoja na haya mengine. Mawigi jamani si huwa hata Finance Act inayotekelizwa sasa hivi tumo mle na humu namo tumetajwa. Sasa yataongezewa bei kidogo kwa ajili ya kuwekewa kwenye bima au ile ile itagawiwa? Kwa hiyo, ni mambo kama hayo. Nimetaja wigi kama mfano. (Makofij)

Nadhani hoja ya msingi imeelewaka na kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hili jambo tunalolifanya leo ni la muhimu sana kwa wananchi ambao kwa kweli wanapata taabu kwenye matibabu, nadhani kwa sababu ndiyo mara ya kwanza nchi yetu

inapitisha jambo kama hili; kwa kuwa Kamati yetu ililitazama hili kwa urefu, sisi tuwape tena hii kazi Kamati kwa sababu sheria zetu hata tukitunga huwa kuna uwezekano wa kubadilisha; tuseme Bunge kazi yetu ni kutunga sheria, kwa hiyo, hatupangiwi kwamba lini tutafanya haya marekebisco; nafikiri kwa hapa tulipofika na mjadala huu, hoja imeelewka.

Kwa hiyo, tutapitisha hiki Kifungu, Kamati ikafuatilie ikitazama na sheria nyingine zinasemaje zinapoanzisha mifuko? Kwa sababu la sivyo utaanzisha mfuko ambao hauna fedha, maana huna uhakika utapewa kiasi gani? Maana viwango vyote hapa tumesema Waziri wa Fedha ataamua. Sasa akiamua 0.009 itakuwaje?

Kwa hiyo, mambo kama hayo nadhani Kamati mllichukue hilo, na uzuri mwezi wa Kwanza mtakuwa mnawasilisha taarifa yenu, nadhani mlitazame hili kwa undani sana ili kifungu hiki tuweze kukifanyia marekebisco yanayostahili kuliko hapa. Nadhani hoja mmezielewa na hapa tukisema tunataka kubadilisha, hata Waziri wa Fedha hawezi kutaja asilimia kwa sababu lazima wawe wamepiga hesabu. Hata hivi vyanzo vingine haviwezi kutajwa asilimia. Ila sheria zinazoanzisha mifuko, tumeangaria hii moja ya REA inataja fedha zitakuwa kiasi gani, zinatokea wapi?

Waheshimiwa Wabunge, nadhani baada ya maelezo hayo tumeelewana.

Ibara ya 22

Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisco yake)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

## 1 NOVEMBA, 2023

Ibara ya 25

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 25 hakijaafikiwa eeh?

Waheshimiwa Wabunge tuko kutunga sheria hapa.

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 26

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 27

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na Marekebisho yake)

Ibara ya 28

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila Mabadiliko yoyote)

Ibara ya 29

Ibara ya 30

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 31

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)

**1 NOVEMBA, 2023**

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Ibara ya 32 kina marekebisho ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja, ngoja. Kifungu cha 32 kinafutwa nafikiri. Siyo kwamba kina marekebisho, kinafutwa hebu tazama vizuri.

**NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 32 kinafutwa na Serikali.

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilifutwa na Serikali)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 34

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 34 Waheshimiwa Wabunge kina marekebisho ya Serikali.

Sasa marekebisho yamefanywa mara mbili, sina uhakika sana kama wote tumepeata marekebisho mengine yaliyoongezeka. Kwa sababu kwenye hiki kifungu kulikuwa hakuna uwiano wa adhabu zilizotolewa kwenye lile jedwali la mwanzo, kwenye adhabu linasema, kipindi kisichopungua miezi sita na na kisichoziidie miezi 12, halafu adhabu ya kifedha ni kuanzia shilingi 500,000 mpaka shilingi 5,000,000. Kwa hiyo, wamejaribu kuyatazama hayo yote hapo, wameleta marekebisho mengine. Kwa hiyo, kuna marekebisho ya nyongeza hapo kwenye hicho kifungu chote cha 34.

Mheshimiwa Waziri kifungu cha 34A, umeshafika hapo? Kifungu 34A(2) sehemu ya mwisho kabisa hapo inasema, “anaweza kutoa

msamaha wa ulipwaji wa riba kwa watu au kundi lolote lenye wajibu wa kujunga na Skimu ya Bima ya Afya chini ya Sheria hii. Sasa hapa sina uhakika kama ni wewe au Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Huu ni msamaha wa bima ambao siyo msamaha wa kujunga, lakini huyu mtu si ni kwamba hii riba anayodaiwa ni kwamba hakujunga kwa wakati aliotakiwa? Sasa akisamehewa hiyo riba inamaanisha nini? Ni kwamba Waziri anatoa nafasi ya watu kutokujunga halafu atasamehewa? Hebu hapo tuelezee vizuri, yaani namna kilivyoandikwa, na uzuri ni Kiswahili kwa hiyo, kidogo inakuwa mtihani wakati mwingine. Naweza kuwa tu sijaelewa mimi mwenyewe kwa Kiswahili change. Karibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru sana. Baada ya kwamba tumefuta kifungu cha 32 ambacho kilikuwa kinafungamanisha Bima za Afya na huduma za kijamii, lakini katika kuifanya ile bima kuwa mandatory tukaja kama na assumptions fulani kwamba baada ya miaka mitatu toka sheria imetungwa hujakata bima, angalau kuwe na adhabu kidogo, utachajiwa asilimia 10. Labda kama bima ni shilingi 50,000 utachangia asilimia 10 ya shilingi 50,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunatambua mazingira ya wananchi wetu. Tunataka kutoa fursa kwa Waziri, anaweza akasema miaka mitatu imepita hamjakata bima, lakini nasamehe hii riba labda ya miaka mitatu, miaka minne ili kuvutia tena wananchi kujunga na bima. Kwa hiyo, tunaamini ilivyobaki hapa ni sahihi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri unawaza wananchi milioni 40, tuwaache wale 20 waandike kwako maombi ya kusamehewa ile riba?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, litatoka tu tamko kama kwenye Sheria za Ardhi sasa hivi, unatakiwa kulipa *annual rate*, lakini kwa mamlaka ya Waziri wa Ardhi anaweza akatangaza tu kwamba natoa tangazo mtu ambaye hajalipa kodi ya ardhi,

**1 NOVEMBA, 2023**

tunasamehe riba, unalipa tu *principal amount*. Ndiyo tunakwenda kwa mtazamo huo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumepewa ufanuzi huo. Katibu tuendelee.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 35

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 36

**MWENYEKITI:** Kifungu cha 36, ngoja nione vizuri hapa. Haya, kifungu hiki nacho kilikuwa hakina uwiano, Serikali imeleta marekebisho ya ziada ili ile adhabu iwe na uwiano na kifungu.

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 37

Ibara ya 38

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 39

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 40

Ibara ya 41

Ibara ya 42  
Ibara ya 43  
Ibara ya 44  
Ibara ya 45  
Ibara ya 46  
Ibara ya 47  
Ibara ya 48

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 49

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 50  
Ibara ya 51  
Ibara ya 52

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 53  
Ibara ya 54  
Ibara ya 55  
Ibara ya 56

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 57

**MWENYEKITI:** Sasa hivi vinavyofutwa, Kifungu cha 57 mpaka  
cha 60 vinafutwa na Serikali.

Ibara ya 57  
Ibara ya 58  
Ibara ya 59  
Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa na Serikali)*

Ibara ya 61

**MWENYEKITI:** Namba tutazirekebisha mwishoni.

Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 63  
Ibara ya 64  
Ibara ya 65  
Ibara ya 66

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa na Serikali)*

Ibara ya 67  
Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69  
Ibara ya 70  
Ibara ya 71  
Ibara ya 72

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilifutwa na Serikali)*

Ibara ya 73  
Ibara ya 74

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
bila mabadiliko yoyote)

**NDG. NEEMA MSANGI- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko yaliyofanyika na Serikali, kuna mabadiliko ya renumbering vifungu vya 11 mpaka 74 kuwa kifungu cha 10 mpaka 67 mtawaliya.

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima  
pamoja na marekebisho ya yake)

**MWENYEKITI:** Katibu, ngoja hili Jedwali ambalo liko kwenye Jedwali la Marekebisho la Mheshimiwa Waziri, liko sehemu?

Waheshimiwa Wabunge, kuna Jedwali ambalo Serikali imeliweka kwenye haya marekebisho ambayo yameletwa na hili jedwali halikuwa sehemu ya ule Muswada. Jedwali hili limekuja baada ya kuwa kuna baadhi ya vile vifungu vilivyofutwa, kufutwa kwa vile vifungu kunasababisha lazima wa kuwa na jedwali la hizi huduma zitakazokuwa zinatolewa.

Sasa kwa kuwa yale marekebisho yamegawiwa kwenye vishikwambi vyenu, ninaamini na hili Jedwali mnalo. Mheshimiwa Waziri pia si unalo hilo jedwali?

Sasa kabla sijawahoji kwenye hili jedwali, hebu tusaidie ufanuzi wa hii "A" zimetolewa huduma hapo na "B" zimetolewa huduma. Kwenye "B" huduma ambayo inakosekana ni huduma ya kibingwa na ubingwa bobesi kwenye hawa "B." Je, hiyo tofauti inatokana na nini? Yaani, hawa wote wana bima, halafu huyu mwenye bima mmoja anaweza kuonana na bingwa na bingwa mbobezi lakini huyu mwagine hawezo.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante...

**MWENYEKITI:** Nikuletee, uko nalo?

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko nalo. Kwenye Jedwali A ni kitita cha mafao ya huduma muhimu, *standard benefit package*, inakadiriwa itakuwa kama ile ya laki tatu na arobaini. Ndio maana, hii utakuta anapata na huduma kidogo ambazo ziko bingwa na ubingwa bobazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jedwali B ndio kile kitita cha huduma za msingi cha jamii, kwa hiyo nayo basically itakuwa ni zile huduma za msingi kwenye *primary health care facilities*, kwa hiyo ndio maana tumetofautisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baada ya kupokea maoni na ushauri wa kamati, tumeongeza pale kwamba kutakuwepo na kanuni za kufafanua vizuri huduma hizi ni zippi, kwa hiyo, itategemea pia na *premium*, michango ambayo mwanachama amechangia, lakini *at least* kila mtu atapata huduma zile za msingi na muhimu.

**MWENYEKITI:** Sawa, mimi sio daktari kwa hiyo sijui, lakini huyu anayemuona huyu wa kibingwa sio kwamba kuna aina fulani za magonjwa lazima zitibiwe na huyu bingwa au bingwa mbobezi au ni kwamba huwa tunaenda tu kule kwa sababu ya uwezo wetu? Ili tuwe tumeelewa hilo.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema vizuri, kwenye Muswada huu na kwenye Jedwali la Marekebisho, tumesisitiza kuzingatiwa kwa taratibu za rufaa. Kwa hiyo, huwezi tu kusikia homa unaenda kumuona *specialist*, kwa hiyo, hilo ni jambo ambalo tumezingatia kwenye marekebisho.

**MWENYEKITI:** Nilichotaka kuelewa ni huyu ambaye naye yupo kwenye bima lakini kitita chake hakitamruhusu. Swali langu; kitaalam, (madaktari) anayeenda kumuona Daktari Bingwa ni

kwamba ugonjwa wake unahitaji ubingwa fulani au ule ubingwa huwa hauhitajiki, na kwamba hata huyu wa kawaida akikutibu uko sawa tu ila huwa tunahitaji huduma za ziada? Hilo ndio swalilangu.

Mfano, mtu kama anahitaji upasuaji wa ubongo atahitaji huyu wa ubobezi au hata huyu wa kawaida tu anaweza kufanya hiyo kazi? Yaani, hilo ndio swalilangu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, unapozungumzia zile package za *primary health* maana yake anakuwa amelipa kulingana na *primary health* na hakuna namna utakuwa kwenye zahanati, kituo cha afya au hospitali ya Wilaya ukakutana na Daktari Bingwa Mbobezi. Daktari Bingwa Mbobezi utakutana naye huku juu kuanzia Kanda, mara chache Mkoani na Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunachosema ni kwamba utakapolipa kile kitita kidogo cha *primary health* utapata hizo huduma, lakini utakapoongeza ina uwezo wa kukulipia mpaka juu. Kwa wale waliolipa basic bima ya kawaida ya *primary health* wataishia chini kwa sababu ndio watakao kutana nao so far ni asilimia kubwa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi kuna mtoto anapata kifua unakuta anakoroma, anafanya nini lakini unakuta mwananchi ameondoka moja kwa moja kwa sababu bima yake inalipa, akaamua kumwona *specialist*, lakini mara nyingi hawahitaji. Kuna wengi wanaenda kwa *specialists*, lakini mara nyingi hawahitaji ma-*specialists*.

**MWENYEKITI:** Ngoja, nirahishe swalilangu, mwenye kitita cha B anahitaji upasuaji wa ubongo, Muhimbili...

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, linapofika suala la upasuaji wa ubongo...

**MWENYEKITI:** Na amefuata utaratibu wala hayuko kwenye zahanati yaani ndio ameshapewa rufaa ya kwenda Muhimbili lakini kitita chake hapa hakina. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika suala la upasuaji wa ubongo inahitaji...

**MWENYEKITI:** Nimetoa tu mfano anaweza kuwa anahitaji upasuaji mwingine ambao ni wa huyu mbobezi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli unahitaji daktari gani wakati gani inategemeana na unahitaji *intervention* gani na ya kitu gani, hiyo ipo, lakini mara nyingi, umetoa mfano wa ubongo hiyo inahitaji daktari bobezii.

**MWENYEKITI:** Hapo hapo, huyu mwenye "B" atawezza kupata hiyo huduma? Kwa sababu yeye hizi huduma za kibingwa hazipo, na huduma za kibingwa zimeishia yule wa juu, sasa huyu mwananchi ambaye ndiye lengo, si unajua wale wanao waomba Wabunge wawasaidie ndio ambao wamefika huko na wale wa zahanati hawawapigii Wabunge? (*Makofii*)

Wale wanaoomba ndio mjadala mkubwa umetokea hapa, wale wanaoomba usaidizi wa Serikali ni wale ambao wameshafika huko, sasa hiki kitita cha pili atawezza kupata hizo huduma pamoja na kwamba hapa hili halipo? Hilo, ndilo swalii langu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumekubaliana kwamba kuna package mbalimbali, kwa hiyo, utatibiwa kulingana na package yako, kwa maana umelipia shilingi ngapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiondoi kwamba, wewe umelipia huduma ambayo ni package ndogo, lakini ikitokea umepata ajali au umepata tatizo ambalo linahitaji rufaa, bado zile taratibu

**1 NOVEMBA, 2023**

ambazo zinazotumika mpaka sasa kumsaidia huyu mtu akihitajika ghafla kwenda juu zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana utaona kuna package iliyowekwa huku ya yale magonjwa mengine na emergency ambazo zinatokea, lakini kuna namna ya kumsaidia huyo asiyeweza kulipia hiyo rufaa kubwa. Ameweza hiki kidogo lakini hawezi kulipa ile ya juu.

**MWENYEKITI:** Sasa si ndio tunataka kuondoka kwenye huo msaada ili bima yake ilipe au mimi ndio sielewi? Kwa sababu huu Muswada unahu *Universal Health Insurance* au unaitwaje? Maana Kiingereza na nimeomba radhi tangu mwanzo. Huu Muswada wetu unaitwaje?

Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, kama hivyo ndivyo, huyu mwingine, chochote atakacholipa si umemwekeea kwa kiwango kile alichoweza kulipa? Sasa kwa nini asipate hizo huduma? Na hawa ndio ambao huwa tunawasumbua kwa simu. Mheshimiwa Waziri, hawa ndio huwa tunasema jamani upasuaji. Anyway, kwa kweli nendeni mkalitazame kwa sababu tukifika mahali tukawa tunahitaji msaada sasa tena tutakuwa tuna...

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, concern yako ni nzuri, mwanzoni tulipokuja na Muswada tulikuja na kitita kimoja tu ambacho kinamfikisha mtu mpaka Muhimbili, MOI, mpaka JKCI lakini tukasikiliza maoni na ushauri wa kamati, kwamba pia, tuje na kitita cha huduma ya ngazi ya msingi. Asilimia 70 ya watanzania wanatibiwa katika ngazi ya msingi, kwa hiyo, ndio maana tukaja na hiki kitita ambacho kinakuwa chini ya Jedwali B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulitambua hilo kitita hiki hakitafika mbali, tumekuja na marekebisho kwenye 22(A) sambamba na mfuko huu kugharamia bima ya afya kwa watu

wasio na uwezo. Tumesema bila kuathiri kifungu kidogo cha kwanza, mfuko unaweza kutumika kugharamia huduma za matibabu ya magonjwa sugu, ya muda mrefu na huduma za afya za dharula kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tulivyosema, inawezekana huyu mwenye kitita kidogo hana uwezo lakini kwa kutumia sheria hii ataweza pia kupata huduma za magonjwa ambayo Wizara ya Afya tutatoa kwenye kanuni, kwa hiyo, concern yako nisahihi lakini Muswada huu unakwenda kutibu jambo ambalo umelieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeangalia experience ya wenzetu Kenya, sambamba na wasio na uwezo lakini wame-establish kinaitwa *Chronic Illness and Accident and Injuries Fund*, kwa hiyo, na sisi tukatumia ubunifu huu tukasema kuna watanzania wataishia bima ya elfu hamsini lakini watashindwa kufika, ndio maana tumekiweka hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wasiwasi wako utatibiwa na sheria hii.

**MWENYEKITI:** Hili naomba niongee na Mwenyekiti, haya naona Mwenyekiti amesimama. Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla hujaongea naona kuna mjumbe hapo. Mheshimiwa Musukuma halafu Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kwa kuwa makini na unatuongoza vizuri. Wananchi wetu kule vijijini, chanzo kikubwa hata cha kuwa na kukatika morali ya kujunga na bima ni pamoja na haya maelezo. Siyo, wote wanaelewa kwamba, tumeenda na bima halafu ukifika pale unaambiwa wewe kitita chako kiko huku na mwingine akaambiwa kitita chako kiko huku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora kwa ushauri wako wakaliangalie upya kwa sababu watanzania wengi wanaotusumbua ni wale wenye matatizo makubwa. Ni bora tukaenda na kile kifungu ambacho mtu anaumwa kuanzia mwanzo mpaka mwisho anatibiwa. Kulikoni kwenda kuchagua yaani wewe leo unaishia ukienda tenda huku uanze kusumbua Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu kwamba ni bora tukahamasisha tukaenda kwenye kile kitita kinachoona matibabu yote na Waziri alivyoeleza alieleza vizuri kwamba utatoa room ya watu kulipa kwa awamu. Ni vizuri zaidi kuliko kuwa na ubaguzi wengine wataishia hapa wengine wakipata matatizo ya daktari bingwa unaambiwa kitita kimeishia hapa anarudi nyumba. Kwa sisi wasukuma kule kijini wanasema agenayo ghete gakale, ni yale yale kama ya zamani, kwa hiyo ni vizuri tujipange.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi huo ulionao hata sisi tulikuwa nao kwenye kamati. Kwanza kabisa tumependekeza, kile kitita cha A na B ikiwezekana kianzishwe kitita kingine cha katikati. Tumetoa mapendekezo mapendekezo kwenye kamati na Serikali imeridhia na kwa sababu tumempa Mheshimiwa Waziri, mamlaka ya kuanzisha kitita kingine atakwenda kulijali hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitita cha msingi tulikiangalia kwa mapana na marefu sana. Kwanza tuliangalia unafuu wa bei, lakini tuliangalia uwezo wa wananchi wetu na tuliangalia huduma zinazotolewa kwenye kitita hiki. Ujisoma kitita cha msingi unaangalia na unaona kabisa hapa kuna huduma ya kujifungua ina maana mama atapata huduma bure kwa kutumia kitita hicho cha chini lakini bado kuna huduma ya upasuaji. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, atatoa ufanuzi kwenye kanuni. Upasuaji ni kitu kipana na hapa kuna mambo mengi maana upasuaji uko wa aina nyingi kuna head oral, kutoa mambo ya *hernia* na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ulichokihoji kwamba zile huduma bobezi; Mheshimiwa Waziri, tumempa *room* uwezo wa kufungua ule mfuko. Mfuko huo hautakuwa kwa ajili ya kugharamia watu maskini tu kwa maana ya kulipia vitita badala yake ni pamoja na kumhudumia mwananchi kwenye gharama ambazo anahitaji huduma bobezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa, kile kitita namba B, mwananchi wa kawaida akiwa na kile kitita na akahitajika kupata huduma ya kibobezi uliyoihoji...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, umetupeleka kwenye 22A; "A" inazungumzia magonjwa sugu na ya muda mrefu na huduma za afya za dharula zitokanazo na ajali. Huyu anayetakiwa kupewa huduma ambayo kwenye kitita chake kile alicholipia haipo hapa haipo kwenye hii 22. Hapa 22 ilitakiwa iwe (a), (b) na (c).

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli palitakiwa pawe na (a), (b) na (c) yaani tuwe na (b) kwa maana ya kifungu kingine. Tulitazama kwamba wananchi wengi wanakosa huduma hata hizi za msingi na tungesema kama anavyozungumza Mheshimiwa Musukuma kwamba tungeweka kitita kimoja ambacho mtu anapata huduma zote hadi bobezi, gharama yake ingekuwa kwenye laki tatu na elfu themanini hakuna Mbunge angekubali hapa.

**MWENYEKITI:** Ni sawa tukubaliane kwamba Mheshimiwa Waziri, kama tulivyokubaliana kamati Mwenyekiti, kama tulivyokubaliana

kwenye vyanzao kwamba mkapaangalie, hapa napo mkapaangalie kwanini? Kwa sababu watu ambao tunawazungumzia kwamba huwa tunapiga simu za kuomba msamaha ni wale wasiojiweza ambao hata kwenye vitita hivi watakuwa hawajiwezi, kwa hiyo atakata cha chini na atakajikuta yuko Muhimbili unatakiwa umtafute Waziri kwa sababu huduma anayoihitaji kule ni ya mbobezi. Huduma anayoihitaji ni ya kibingwa na yeze bima yake haimfikishi kwenye kumuona bingwa wala huyo mbobezi. (Makofij)

Ndio hoja ilipo hapo, na kwa sababu tunayehitaji kushughulika naye ni yule maskini, basi huyu maskini basi asaidiwe kwa ngazi zote madam amejipinda kwa hiki kidogo alichochangia akawa na uradhi. Mheshimiwa Waziri, apewe nguvu kisheria kama alivyopewa huku kwenye hii 22A.

Mheshimiwa Waziri, kwa ufanuzi, huku kwenye magonjwa sugu yaendelee kuwepo, yale ya ajali yaendelee kuwepo, awekwe na huyo ambaye anakitita ambacho hakimwezeshi kuwaona wale lakini sasa huduma anayohitaji inamwitaji awaone wale. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, hilo nalo linearudi kwako kama lile lingine, kwa hiyo, naamini kwa ushirikiano ambao Serikali imeutoa hili pia mtashirikiana ili mliweke vizuri. Kwa sababu kwa ngazi hii hiki kifungu hatuwezi kukiongeza lakini ni muhimu sana kiwepo, ili wote wapate huduma, maadam tunesema hii ni bima ya afya kwa wote, hivyo wote wapate huduma zote.

Japokuwa Mheshimiwa Musukuma, ameenda mbali kidogo, lakini sio kwa namna ile. Watu lazima watatofautiana lakini wote wapate huduma hata kama wanatofautiana. Nadhani hilo limeeleweka, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, kwa hiyo, una hizo kazi mbili na kwa ushirikiano ambao Serikali iliouonesha bila shaka haya mawili pia mtayafanya kazi vizuri, ahsante sana. Katibu!

**1 NOVEMBA, 2023**

Samahani ilikuwa ni hoji sasa hili jedwali ambalo limeongezwa kwenye marekebisho, halikuwa sehemu ya Muswada.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jedwali hapa ambalo limeletwa, tunaliafiki?

(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana, katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge linarejea.

(Bunge Lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja, taarifa. Waheshimiwa Wabunge, ambaye amewasha kisemeo azime.

## **TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Bunge zima imekaa na kupitia kifungu kwa kifungu na kupitisha Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na. 8 wa Mwaka 2022 pamoja na Marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liridhie kupitisha Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja llitolewa lamuliwe)

**1 NOVEMBA, 2023**

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote kwa ajili ya kuweka Masharti ya Kuwezesha Upatikanaji wa Huduma za Afya kwa Wananchi Kupitia Bima ya Afya.

Kuanzisha Mfumo wa Bima ya Afya kwa Wote, Kuweka Masharti ya Kupanua Wigo wa Huduma Mbalimbali za Afya pamoja na Masuala Mengine yanayohusiana na hayo.

*(Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote wa Mwaka 2022)*

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada umeshasomwa kwa Mara ya Tatu. Muswada wetu kwa kuwa umesomwa kwa mara ya tatu, maana yake kama Bunge tumemaliza kazi yetu ya kutunga Sheria hii na kwa hiyo, nitangaze rasmi kwamba Bunge limeshapitisha Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa Wote wa mwaka 2022. (Makofii)

Kama ilivyo ada utapelekwa kwa Mheshimiwa Rais ili aweze kuupitia na kuona kama atatoa kibali chake basi utaweza kuanza kazi kwa wakati ule ambao utatangazwa.

Nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote chini yenu kwa ushirikiano wenu mzuri ambao mnao huko Serikalini mpaka mmeefika mahali ambapo yale mambo yote yaliyokuwa yanazungumzwa na Wabunge, lakini pia na wananchi mkayakusanya hayo yote, mkayafanya kazi na mkaleta marekebisho ambayo yanaufanya Muswada wetu uwe katika hali bora zaidi. Kwa hiyo ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. (Makofii)

Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Kamati yetu yote, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana ya kusikiliza wadau mbalimbali na kupeleka mawazo yao na ya wadau Serikalini na Serikali imeweza kuyafanya kazi. Tunawashukuru sana kwa umakini mliouonesha kwenye Muswada huu, na sasa nafikiri unaweza kuanza kufanya kazi vizuri kwa namna ambavyo wananchi wengi wataweza kufaidika, kwa hiyo nawapongeza sana Kamati ya Bunge. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, wengi mmeshiriki katika ngazi mbalimbali. Sio wote mmepata nafasi ya kuchangia leo, lakini mlischachangia huko katika maeneo mbalimbali kuhusu Maboresho ya Muswada huu. Leo nimefurahi kusikia hata wengine waliokuwa wanapinga, kwa marekebisho yaliyofanywa na Serikali nao wameafiki Muswada huu, kwa hiyo ni hatua nzuri sana. (Makof)

Ninawapongeza Wabunge wote kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge na imewachukua muda kurejea tena lakini muda mliouchukua ilikuwa na nia njema ya kuhakikisha mnayafanya kazi maoni ya Wabunge na maoni ya wananchi. Kwa hiyo, ahsanteni sana kwa kazi hii nzuri mliyoifanya katika kutunga sheria hii. (Makof)

Baada ya kusema hayo, nawatakia kila laheri katika utekelezaji wa yale yote ambayo mmeyazungumza. Baadhi ya mambo mmezungumza kwenye ngazi ya kamati, mengine mmeyazungumza hapa Bungeni, mengine mmeyazungumza kwa sura ya utendaji ambayo hayapo kwenye vifungu vya sheria, lakini tunawatakia kila la heri katika utekelezaji wa hayo yote. Na yale ambayo tukiwa kwenye Kamati ya Bunge zima tumekubaliana yakafanyiwe kazi, basi yafanyiwe kazi kwa haraka ili Muswada huu utakapoanza kazi basi maeneo yote uwe uko sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, tunawatakia kila la kheri, ahsanteni sana kwa ushiriki wetu kwenye kutunga sheria hii.

## **1 NOVEMBA, 2023**

Baada ya kusema hayo naahairisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.01 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 2 Novemba, 2023 Saa Tatu Kamili Asubuhi)*